

**UCHAWI NA MAZINGAOMBWE KATIKA RIWAYA ZA
SHAABAN ROBERT NA ZA EUPHRASE KEZILAHABI**

**NA
CHARLES NYANDURU MAGGATI
C82/27820/2013**

**TASNIFU IMEWASILISHWA ILI KUTOSHELEZA MAHITAJI YA
SHAHADA YA UZAMIFU KATIKA IDARA YA KISWAHILI
CHUO KIKUU CHA KENYATTA**

MEI, 2022

UNGAMO

Tasniifu hii ni kazi yangu binafsi na haijatolewa kwa mahitaji ya shahada katika Chuo Kikuu kingine.

Sakibi 

Tarehe 27/05/2022

Charles Nyanduru Maggati -- C82/27820/2013
Idara ya Kiswahili

WASIMAMIZI

Tasniifu hii imetolewa kwa Chuo Kikuu cha Kenyatta kwa idhini yetu kama wasimamizi.

Sakibi 

Tarehe 25/5/2022

DKT. Richard. M. Wafuta
Idara ya Kiswahili

Sakibi 

Tarehe 25/5/2022

DKT. Miriam. K. Osore
Idara ya Kiswahili

TABARUKU

Kazi hii naitabarukia mke wangu Milisent Akinyi Gryson, Mama yangu Yunes Otulo Achar na watoto wangu: Immanuel, Amosi, Maombi, Mark, Glory, Yunistar, Davis na Mikaeli.

SHUKRANI

Nafurahi kutoa shukrani za dhati kwa uongozi wa Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Mkwawa kwa kunipa kibali cha kwenda kusoma na kunilipia gharama zote za masomo. Bila kunilipia gharama hizo zote za masomo nisingeweza hata kidogo kumudu kujisomesha. Wasimamizi wangu: Dkt. Richard Wafula na Dkt. Miriam Osore wamekuwa msaada mkubwa sana kwangu kwa muda wote wa uandishi wa tasnifu hii. Muda wote nilipohitaji msaada wao hawakusita kunielekeza kwa upendo na uvumilivu mwingi kutoka hatua za mwanzo mpaka kukamilika kwa tasnifu hii.

Profesa Ndashao, ndiye aliyenishawishi na pia kunisaidia mpaka nikapata nafasi na kusajiliwa katika Chuo Kikuu cha Kenyatta, Mungu ambariki. Zaidi ya yote namshukuru mke wangu na familia yangu kwa maombi yao yasiyokoma kwa ajili yangu kwa muda wote niliokuwa masomoni. Katika hayo yote shukrani zimwendee Mungu muumba kwa kunipa uzima na afya na pia kuwawezesha hao wote walionisaidia kufanya yote hayo kwa mapenzi yake.

YALIYOMO

UNGAMO	Error! Bookmark not defined.
TABARUKU	\ii
SHUKRANI	iv
YALIYOMO	v
ORODHA YA MAJEDWALI	x
UFAFANUZI WA ISTILAHI MUHIMU	xi
IKISIRI	xiii
ABSTRACT	xiv
SURA YA KWANZA	1
UTANGULIZI WA JUMLA	1
1.1 Usuli.....	1
1.1.1 Riwaya Teule	2
1.1.2 Uchawi na Mazingaombwe	3
1.2 Suala la utafiti	6
1.3 Malengo ya utafiti.....	7
1.4 Maswali ya utafiti	8
1.5 Sababu za Kuchagua mada	8
1.6 Upeo na Mipaka.....	10
1.7 Yaliyoandikwa Kuhusu Mada	11
1.7.1 Yaliyoandikwa Kuhusu Uchawi na Mazingaombwe katika Kazi za Fasihi.....	12
1.7.2 Yaliyoandikwa Kuhusu Uhusiano wa Mazingira Asilia ya Mtunzi na Kazi Yake ya Fasihi	24
1.7.3 Yaliyoandikwa Kuhusu Kazi Teule za Shaaban Robert na Euphrase Kezilahabi.....	29
1.8 Misingi ya Nadharia	34
1.8.1 Nadharia ya Uhalisiamazingaombwe	35
1.8.1.1 Matukio ya Kichawi na ya Kimazingaombwe Yanaonekana ya Kawaida Lakini Yenye Hali za Kuogofya na Kuduwaza.....	39
1.8.1.2 Uhalisi na Ndoto Vinaingiliana.....	39

1.8.1.3 Matukio Yanakosa Mtiririko wa Kawaida	40
1.8.1.4 Uvunjivu wa Kaida za Uasililia na za Uhalisia	41
1.8.1.5 Wakati na Mahali Vina Uhusiano wa Kiduara na si wa Kiufuatano	41
1.8.2 Nadharia ya Kiwewe cha Kuathiriwa	41
1.8.2.1 Kusoma na Kuvutiwa na Kazi	43
1.8.2.2 Kumwiga.....	43
1.8.2.3 Upotoshaji	43
1.8.2.4 Kubadili Mada	44
1.8.2.5 Upekee na Uasililia	44
1.8.2.6 Kufufuka kwa Kazi.....	44
1.9 Mbinu za Utafiti.....	46
1.9.1 Muundo wa Utafiti.....	46
1.9.2 Kundi Lengwa	47
1.9.3 Mahali pa Utafiti.....	47
1.9.4 Uteuzi wa Sampuli.....	49
1.9.5 Ukusanyaji wa Data.....	51
1.9.6 Uchanganuzi wa Data	53
1.9.7 Mbinu za Kuwasilisha Matokeo	54
1.9.8 Maadili ya Utafiti.....	54
1.10 Kiishilio	55
SURA YA PILI	57
UCHAWI NA MAZINGAOMBWE KATIKA MAZINGIRA ASILIA YA	
WATUNZI WA RIWAYA TEULE	57
2.0 Utangulizi	57
2.1 Uchawi na Mazingaombwe katika Mazingira Asilia ya Shaaban Robert	58
2.1.1 Uchawi na Mazingaombwe katika Ukoo wa Shaaban Robert.....	59
2.1.2 Watu na Viumbe wa Ajabu.....	60
2.1.2.1 Kisa cha Mrefu	60
2.1.2.2 Miujiza ya Kibwana Jafari.....	61
2.1.2.3 Kisa cha Nondo Mla Vyote	64
2.1.3 Matukio ya Ajabuajabu.....	65
2.1.3.1 Kisa cha Mtu wa Bara Aliyemwoa Mdigo.	65
2.1.3.2 Kisa cha Dereva na Jini	69

2.1.3.3 Kungonga Jini kwa Baiskeli na Jini Kusonya	70
2.1.4 Uvunjivu wa Kaida za Uhalisia	73
2.1.4.1 Uvunjivu wa Kaida na Kisasili cha Mawe Mawili ya Jafari Kibwana Pamoja na Sherehe za Mwaka Chumbagama.....	73
2.1.4.2 Kisa cha Osale Otango cha Uvunjivu wa Kaida ya Mahali.....	76
2.1.4.3 Kupotea kwa Mgonjwa Chumbani na Wanawake Wanaosukana Chini ya Bahari Pamoja na Kutia Nanga Katika Mji wa Wachawi Katikati mwa Bahari.....	78
2.1.4.4 Kujibadilisha Kimazingaombwe Chumbageni.....	80
2.1.4.5 Shukrani ya Bundi	82
2.1.4.6 Kuachwa Uchi Juu ya Mbuyu Mwaka 1967 Barabara ya 18 Tanga Mjini.....	83
2.2 Uchawi na Mazingaombwe katika Kisiwa cha Ukerewe, Mazingira Asilia ya Euphrase Kezilahabi.....	84
2.2.1 Matukio ya Ajabuajabu katika Kisiwa cha Ukerewe	84
2.2.1.1 Matukio ya Ajabuajabu katika Historia ya Ukoo wa Euphrase Kezilahabi	85
2.2.1.2 Kuchukuliwa Matunu Aloyce Euphrase.....	88
2.2.1.3 Ebiaro Nyabatesho, Kichaka Kinachotembea	91
2.2.1.4 Kupondwa na Watu Wasioonekana.....	93
2.2.2 Uvunjivu wa Kaida za Uhalisia	94
2.2.2.1 Kuzika Shina la Mgomba na Mechi ya Wafu.....	94
2.2.2.2 Kunigwa na Matunu Mwaka 1989	96
2.2.2.3 Kusafirishwa na Mamba: Uvunjivu wa Kaida ya Mahali au Mazingira..	97
2.2.2.4 Mamba Kama Kijiti na Kujibadilisha na Kusafirishwa Kama Samaki	98
2.2.2.5 Kutumia Sura ya Mtu Mwingine Kufanyia Uchawi.....	100
2.2.3 Visasili	102
2.2.3.1 Nyabulebeka Jiwe Linalocheza	102
2.3 Kiishilio.....	103

SURA YA TATU.....	105
ATHARI YA MAZINGIRA ASILIA YA WATUNZI KATIKA USAWIRI WA WAHUSIKA WA AJABU KATIKA RIWAYA TEULE ZA SHAABAN ROBERT NA ZA EUPHRASE KEZILAHABI.....	105
3.0 Utangulizi	105
3.1 Wahusika wa Ajabu.....	106
3.2 Wahusika wa Ajabu katika Riwaya Teule.....	109
3.2.1 Wahusika Wenye Uwezo wa Kujibadilisha Kimazingaombwe na Wanaoishi Kati ya Uhai na Kifo na Kutoweka Kimiujiza na Wenye Kufahamu Mawazo ya Mtu.....	109
3.2.2 Wahusika kama Majitu na Wenye Matendo na Nguvu za Ajabu.....	128
3.2.3 Wahusika Jumui na Wenye Nafsi Mbili na Wahusika Wenye Hali ya Kiungu Isiyo Bayana.....	146
3.3 Kiishilio	158
SURA YA NNE	161
ATHARI YA MAZINGIRA ASILIA YA WATUNZI KATIKA MSUKO WA MATUKIO YA AJABUJABU KATIKA RIWAYA TEULE ZA SHAABAN ROBERT NA ZA EUPHRASE KEZILAHABI	161
4.0 Utangulizi	161
4.1 Matukio ya Ajabuajabu.....	162
4.2 Matukio ya Ajabuajabu Katika Riwaya Teule.....	165
4.2.1 Matukio ya Ajabuajabu Yanayotendwa na Watu na Viumbe wa Kufikirika kama Majini, Mizimu na Majitu.....	165
4.2.2 Matukio ya Ajabuajabu Yanayotendwa na Ndege na Wanyama	184
4.2.3 Matukio ya Ajabuajabu Yanayotendeka Yenyewe Kutokana na Ukiamaumbile.....	199
4.3 Kiishilio	204
SURA YA TANO	208
ATHARI YA MAZINGIRA ASILIA YA WATUNZI KATIKA UVUNJIVU WA KAIDA ZA UHALISIA KATIKA RIWAYA TEULE ZA SHAABAN ROBERT NA ZA EUPHRASE KEZILAHABI.....	208
5.0 Utangulizi	208
5.1 Uvunjivu wa kaida.....	209

5.2 Uvunjivu wa kaida katika riwaya teule	211
5.2.1 Uvunjivu wa Kaida za Mahali au Mazingira na wa Mbali na Karibu	211
5.2.3 Uvunjivu wa Kaida Kati ya Uhai na Kifo.	242
5.2.4 Uvunjivu wa Kaida Kati ya Ndoto na Uhalisia	251
5.2.5 Uvunjivu wa Kaida za Kuhesabu Wakati	261
5.2.5.1 Wakati wa Kiufuatano	263
5.2.5.2 Wakati tuamavu	264
5.2.5.3 Uduara wa Wakati	272
5.3 Kiishilio	289
SURA YA SITA	292
ATHARI YA MAZINGIRA ASILIA YA WATUNZI KATIKA MATUMIZI YA VISASILI NA ISTIARA KATIKA RIWAYA TEULE ZA SHAABAN ROBERT NA ZA EUPHRASE KEZILAHABI.....	292
6.0 Utangulizi	292
6.1 Visasili	292
6.2 Istiara	303
6.3 Kiishilio	318
SURA YA SABA	321
MUHTASARI, MATOKEO NA MAPENDEKEZO.....	321
7.0 Utangulizi	321
7.1 Muhtasari wa Utafiti	322
7.2 Matokeo ya Utafiti	326
7.3 Mchango wa Utafiti	331
7.4 Matatizo	333
7.5 Mapendekezo	334
7.5.1 Mapendekezo kwa Ajili ya Tafiti Zaidi	334
7.5.2 Mapendekezo kwa Wasomaji na Wahakiki wa Kazi za Fasihi	336
7.5.3 Mapendekezo kwa Watunga Sera.....	336
MAREJELEO	338
VIAMBATISHO	349
KIAMBATISHO A: Mwongozo wa Usaili, Mijadala na Ushuhudiaji kwa Wenyeji wa Tanga/Ukerewe.....	349
KIAMBATISHO B: Vibali vya kufanya utafiti	351

ORODHA YA MAJEDWALI

Jedwali na. 7.1 Uwiano wa Matumizi ya Uvunjivu wa Kaida katika Riwaya Teule
.....330

UFAFANUZI WA ISTILAHU MUHIMU

Uchawi na mazingaombwe: Sanaa bunifu ambapo uwepo wa nguvu zilizofichika kama mizungu, sihiri, mizimu, mashetani, majini, majitu na roho zisizoonekana huathiri matukio katika mazingira asilia kwa kufanya matukio ya kushangaza, ya ajabu, yanayoteka usikivu, ya kuhadaisha, yasiyo ya kawaida na yasiyoeleweka wala kufumbuka kwa akili ya kawaida.

Uhalisiafifi: Nadharia inayomwezesha mwandishi kuyachunguza na kuyasawiri matukio au hali za kindoto au za kisaikolojia zinazotokea katika ung'amuzibwete wa akili.

Uhalisiajabu: Dhana inayotumiwa kuyaeleza matukio ya kichawi na ya kimazingaombwe kwa namna inayoyafanya yaonekane ya kawaida kwa kuvunja mpaka kati ya mambo yanayoweza kupatikana katika ulimwengu halisi na yasiyowezekana ambapo msomaji anaamini kuwa ulimwengu wa sanaa ni tofauti na ulimwengu wao asilia wanapoishi.

Uhalisiamazingaombwe: Nadharia ya fasihi inayokutanisha uhalisi na mambo ya ajabu au ya kuogofya ambayo si ya kiuhalisia, au namna ya kuangalia vitu vya kawaida kwa namna isiyo ya kawaida ambapo msomaji na mwandishi wanaamini kuwa hakuna tofauti yoyote kati ya ulimwengu wa sanaa na ulimwengu wao wa kawaida wanapoishi.

Ndoto: Mfululizo wa picha , mawazo, mihemko na hisia ambazo hutokea akilini mwa mtu awapo usingizini.

Wakati tuamavu: Wakati tuamavu au wakati uliotuama ni wakati ambao hausongi mbele, ni wakati uliosimama. Hutumika kuelezea maisha katika jamii ambapo mambo na maisha hayasongi wala hakuna mabadiliko yoyote ingawa siku na tarehe zinasonga mbele.

Ngano: Hadithi za kimapokeo zitumiazo wahusika kama watu, wanyama, miti, miungu, mizimu na viumbe visivyo na uhai kama mawe na miamba kueleza au kuonya juu ya maisha.

Visasili: Hadithi za kale zinazohusisha matukio ya ajabuajabu yasiyotarajiwa kutokea katika maisha ya kawaida zinazopatikana katika imani zilizopo katika jamii fulani.

Istiara: Hadithi ambayo maana yake ya wazi inawakilisha maana nyingine iliyofichika.

IKISIRI

Utafiti huu ulichunguza na kulinganisha matumizi ya uchawi na mazingaombwe kati ya vipindi viwili tofauti: kipindi cha riwaya za Kiswahili kabla ya uandishi wa usasabaadaye na kipindi cha usasabaadaye kwa kutumia riwaya za Shaaban Robert na za Euphrase Kezilahabi kwa kuzihusisha na mazingira asilia ya watunzi hao. Lengo la kuhusisha mazingira asilia yaliyowalea na kuwakuza watunzi hao lilikuwa ni kutaka kubaini mchango wa mazingira asilia ya mtunzi katika matumizi ya mbinu ya uchawi na mazingaombwe katika riwaya teule. Riwaya za *Adili na Nduguze* (1952), *Kusadikika* (1951) na *Kufikirika* (1946) za Shaaban Robert ziliteuliwa kimaksudi kuwakilisha kipindi cha uandishi wa riwaya za Kiswahili kabla ya usasabaadaye (uandishi unaotumia nduni za fasihi simulizi katika fasihi andishi). Riwaya za *Nagona* (1990) na *Mzingile* (1991) za Euphrase Kezilahabi ziliteuliwa kuwakilisha kipindi cha uandishi cha usasabaadaye (kipindi cha utandawazi). Madhumuni ya utafiti huu yalikuwa ni kubainisha uchawi na mazingaombwe katika mazingira asilia ya watunzi wa riwaya teule. Kuchunguza athari ya mazingira asilia ya watunzi katika matumizi ya mbinu ya uchawi na mazingaombwe katika riwaya teule, na kulinganisha matumizi ya mbinu ya uchawi na mazingaombwe kati ya watunzi Shaaban Robert na Euphrase Kezilahabi. Uchambuzi wa data katika utafiti huu uliongozwa na nadharia mbili: Nadharia ya uhalisiamazingaombwe iliyoasisiwa na Franz Roh mwaka 1925 na nadharia ya kiwewe cha kuathiriwa iliyoasisiwa mwaka 1973 na Harold Bloom. Uhalisiamazingaombwe ulitumika kubainisha matumizi ya uchawi na mazingaombwe katika riwaya teule na kuchunguza uhalisia wake katika mazingira asilia ya watunzi wa riwaya husika. Hii ni kwa sababu matumizi hayo hayawezi kufumbuliwa kwa kutegemea mbinu za kisayansi na nadharia za kihalisia. Nadharia ya kiwewe cha kuathiriwa ilitumika kulinganisha na kulinganua matumizi ya uchawi na mazingaombwe kati ya waandishi hao wawili katika riwaya teule. Utafiti umefanyika katika maktaba na nyanjani. Katika maktaba, riwaya teule zilisomwa na data za uchawi na mazingaombwe zilibainishwa na kulinganishwa. Nyanjani utafiti ulifanyika kwa njia za mahojiano, madodoso na ushuhudaji. Utafiti ulihusisha matumizi ya uchawi na mazingaombwe kutoka mazingira asilia ya watunzi husika na kutoka riwaya teule. Hii ni kwa sababu hakuna utafiti wa kina uliokwishinganisha matumizi ya uchawi na mazingaombwe kati ya kipindi kabla na kipindi cha usasabaadaye katika fasihi ya Kiswahili uliohusisha matumizi ya uchawi na mazingaombwe kutoka mazingira asilia ya watunzi na kazi zao za fasihi. Data zilizokusanywa na kuchambuliwa kwa kuongozwa na mkabala wa kitaamuli ni pamoja na: matumizi ya wahusika wa kichawi na wa kimazingaombwe, matukio ya ajabuajabu, uvunjivu wa kaida za uhalisia, na visasili na istihara. Matokeo yaliwasilishwa kwa njia ya maelezo na ufafanuzi kwa maandishi. Iltarajiwa kuwa kazi hii itawasaidia wasomaji, waandishi na wahakiki wa kazi za fasihi, kubaini mchango wa mazingira asilia ya mtunzi katika kuelezea na kukuza kazi za fasihi. Kutambua kuwa uchawi na mazingaombwe ni mtindo mwafaka wa kifasihi unaoweza kutumiwa kuelezea matukio halisi yanayomkabili binadamu katika mazingira yake kwa namna isiyo ya kawaida kwa kufumbata ujumbe katika matukio ya ajabu yanayojenga taharuki ili kumteka msomaji, huku ukifaulisha kueleza masuala ya kisiasa, kiuchumi, kijamii, kidini na ya kitamaduni kwa namna inayokwepa kudhibitiwa na tabaka tawala.

ABSTRACT

This study investigated the use of magic and enchantment in two time frames, the pre postmodernist and the postmodernist periods. Specifically, the study focused on the context that produced the works of Shaaban Robert and Euphrase Kezilahabi respectively. The purpose of relating of context of the writers and their literary works was to demonstrate that the writers were influenced by enchantment and magic to write their works. Both writers' works were selected purposively. *Adili na Nduguze* (1952), *Kusadikika* (1951) and *Kufikirika* (1946) by Shaaban Robert and *Nagona* (1990) and *Mzingile* (1991) by Kezilahabi were selected for this study. The objectives of the study were: to demonstrate the existence of enchantment and magic in the environments in which the novels were written, to analyze the influence of the original context of the writers on the use of enchantment and magic and to compare and contrast the use of enchantment and magic in Shaaban Robert and Euphrase Kezilahabi. The analysis applied two theories: Magical realism that was initiated by Franz Roh in 1925 and anxiety of influence that was propounded by Harold Bloom in 1973. Magical realism was applied to analyze enchantment and magic in the home environments from which the author emerged. The use of magic and enchantment can not be fully understood through conventional scientific methods and realistic theories. The anxiety of influence was used to compare and to contrast how magic and enchantment emerged in the works of the two respective writers. This study was undertaken through the library research and fieldwork. In the library, the selected works were read and data relating to magic and enchantment was isolated and analyzed. Fieldwork involved interviews, questionnaire and participatory observations. The research related the use of magic and enchantment in the lived experiences of the authors and this manifested itself in the selected novels. No detailed study has hitherto been done to compare the use of magic and enchantment in pre postmodern and postmodern in Kiswahili literature. The data that was collected and analyzed included enchanted and magical characters, marvelous happenings, breakage of conventions of realism, the use of myths and metaphor. The results of the analysis were reported through elaborate description. It is expected that this work will assist readers, writers and critics to understand the contribution of the context to the production of a literary work by recognizing that enchantment and magic is a suitable literary device that can be used by writers to depict realistic problems that face human beings. Moreover, enchantment and magic portray, through extraordinary means marvelous events that are build on suspense for the purpose of arresting the readers' attention thereby succeeding to explain political, economic, social, religious and cultural issues in ways that are undecipherable to the ruling classes.

SURA YA KWANZA

UTANGULIZI WA JUMLA

1.1 Usuli

Kumekuwa na mawazo yanayokinzana kuhusu dhana za uchawi na mazingaombwe katika fasihi ya Kiswahili. Kuna wanaodai kuwa uchawi na mazingaombwe ni mtindo mpya katika fasihi ya Kiswahili na kuuhusisha na waanzilishi kutoka nchi za Magharibi (Mohamed, 2003; 2005). Tofauti na hao, kuna wanaodai kuwa licha ya uchawi na mazingaombwe kuwepo tangu zamani katika fasihi simulizi za jamii nyingi duniani, katika fasihi ya Kiswahili uchawi na mazingaombwe umetokana na tajriba ya maisha ya jamii za Waafrika, na kuwa umekuwepo toka mwanzo katika fasihi ya Kiswahili (Madumulla, 1993; Senkoro, 2007). Senkoro (2007) anasisitiza kuwa, uchawi na mazingaombwe ni istilahi mpya lakini ni mtindo mkongwe.

Mulokozi (1996) anasema kwamba, mbinu ya uchawi na mazingaombwe ilitumiwa awali katika fasihi simulizi ya Kiswahili kutoa mafunzo katika jamii husika kwa kutumia wahusika wa ajabu, mandhari ya kuogofya na visa pamoja na matukio yenye kuvunja kaida za uhalisia. Katika fasihi andishi ya Kiswahili kabla ya usasabaadaye, katikati ya miaka ya 1945 na 1980, mbinu ya uchawi na mazingaombwe ilijitokeza katika baadhi ya riwaya kama vile, *Adili na Nduguze* (1952), *Kusadikika* (1951) na *Kufikirika* (1946) za Shaaban Robert; *Mzimu wa Watu wa Kale* (1960) ya Muhamed, S. Abdulla, *Kurwa na Doto* (1960) ya Salehe Farsy na *Mirathi ya Hatari* (1977) ya C. G. Mung'ong'o. Kipindi cha usasabaadaye katika fasihi ya Kiswahili, hasa kuanzia mwaka 1990, kumekuwa

na kasi kubwa ya utunzi wa riwaya zilizosheheni visa na matukio ya uchawi na mazingaombwe. Miongoni mwazo ni *Nagona* (1990) na *Mzingile* (1991) za Euphrase Kezilahabi, *Walenisi* (1995) ya K. Mkangi, *Ziraili na Zirani* (1999) ya W. E. Mkufya na *Babu Alipofufuka* (2001) na *Dunia Yao* (2006) za S. A. Khamis. Riwaya zingine ni *Bina-Adamu!* (2002), *Zimwi la Leo* (2002) na *Musaleo* (2004) za Kyallo Wamitila pamoja na *Mafamba* (2008) na *Watu wa Gehenna* za Tom Olali. Watunzi wa riwaya zilizotajwa wametumia mbinu ya uchawi na mazingaombwe kusimulia visa na matukio ya ajabu yasiyotarajiwa kutokea katika uhalisia yaonekane ya kawaida na kama sehemu ya uhalisia wa kila siku katika maisha ya jamii husika (Wimitila, 2003).

1.1.1 Riwaya Teule

Shaaban Robert katika riwaya ya *Adili na Nduguze* anazungumzia wahusika wanaofanya matukio ya ajabu yanayovunja kaida za uhalisia. Kuna majini wanaozungumza na wanadamu, wanaobadilika sura mbalimbali, wanaoweza kumbadilisha binadamu kuwa nyani na wanaoweza kuingia popote. Kuna wahusika warefu na wenye nguvu kiasi cha kumkamata nyangumi baharini na kumwoka kwa jua angani na kuzunguka dunia kwa dakika tano. Riwaya ya *Kusadikika* inazungumzia wahusika wa ajabu wanaoweza kula tani milioni za chuma bila kushiba. Kuna uvunjivu wa kaida za kimawasiliano ambapo binadamu wanazungumza na malaika na mashetani. Hakuna kizuizi cha umbali wala mazingira ambapo binadamu anaweza kusafiri mpaka mbinguni na kuingia katika nchi ya ardhi. Riwaya ya *Kufikirika* nayo inazungumzia uchawi wa mizizi, utabiri, hirizi, mashetani na mazingaombwe ya viumbe wakubwa kama tembo na nyangumi kuingia na kutoka ndani ya chupa ndogo bila kizuizi chochote.

Kezilahabi katika riwaya za *Nagona* na *Mzingile* anawasawiri wahusika wanaofanya matukio ya ajabu na kuna uvunjivu mkubwa wa kaida za uhalisia na uasilia. Kuna wahusika wanaoweza kubeba na kuhamisha milima. Wanaoweza kunywa maji yote ya mto na kuyatapika ili kuloanisha ardhi kavu. Wanaoweza kukunja na kukunjua mguu kufuata kitu kilicho umbali wa kilomita nyingi kwa muda mfupi. Vile vile, kuna wanaoweza kujibadilisha katika sura mbalimbali, wenye nafsi mbili na wanaoweza kuishi mamilioni ya miaka. Kuna wenye uwezo wa kuongea wakiwa tumboni kabla ya kuzaliwa. Kuna wafu wanaoongea na walio hai, wenye uwezo wa kufufuka, kutapika, kuzungumza na kusafisha roho zao na roho zao kupotea lakini wakaendelea kuishi. Pia kuna matukio yanayotendwa na watu wasioonekana pamoja na miili inayotoa mwanga na wanyama wanaweza kuongea na wanadamu.

1.1.2 Uchawi na Mazingaombwe

Maana ya uchawi na mazingaombwe imezua utata mkubwa sana. Utata huo unasababishwa na kuwepo kwa aina na makundi mbalimbali ya uchawi na mazingaombwe pamoja na mitazamo tofauti ya watu kulingana na imani, elimu na tamaduni zao (Parrinder,1963; Thonya,1974; Spindler, 1993). Kwa mfano, waandishi wa Kiajemi wa zama za Kati (1100-1500 BK) waligawa matumizi ya uchawi na mazingaombwe katika makundi mawili makubwa. Kundi la kwanza ni la miujiza, mazingara, ulozi na uaguzi. Kundi la pili ni lile linalotokana na matokeo ya nguvu zilizo nje ya ulimwengu wa kawaida, mfano, kuingiliana na pepo, mizuka na mizimu.

Marwick (1970) na Bronowski (1978) pamoja na Lucius (1974) wanadai kuwa uchawi na mazingaombwe pamoja na dini na sayansi vilifungamana sana zamani kiasi cha kupata ugumu kuvitenganisha na hivyo kuhitimisha kuwa uchawi na mazingaombwe ndiyo iliyokuwa dini na sayansi ya jadi. Strassberg (2005) akijibu mawazo hayo anasema kwamba, uchawi na mazingaombwe hauwezi kuitwa kuwa ni sayansi katika usasa wake. Hii ni kwa sababu, tofauti na sayansi inayoangalia uhalisia kwa namna moja tu ya mantiki, uchawi na mazingaombwe hutazama uhalisia kwa namna mbili tofauti. Namna ya kawaida ya maisha ya kila siku katika ulimwengu halisi na mazingira asilia na namna nyingine ni ile ya kimiujiza, inayopita akili ya kawaida ya mwanadamu.

Katika sanaa neno uchawi na mazingaombwe mwanzoni lilitumiwa na Mjerumani Franz Roh likiwahusu wachoraji na wachongaji katika miaka ya 1920 (Zamora 1995). Franz Roh (1925) anaeleza uchawi na mazingaombwe kama matukio ya kifantasia au ya kiajabu ambayo yanaelezwa kwa namna inayoyafanya yaonekane ni ya kawaida tu. Mpaka kati ya mambo yanayoweza kupatikana katika ulimwengu halisi na yale yasiyowezekana huwa mdogo sana. Roh alitumia uchawi na mazingaombwe katika muktadha wa sanaa kama mbinu fulani maalum ya kudhihirisha usiri ulioko katika maisha ya kila siku bila kuwa na shaka lolote juu ya uhalisia huo.

Katika fasihi dhana ya uchawi na mazingaombwe imeingizwa kwa mara ya kwanza mwaka 1949 na mwandishi wa riwaya kutoka Cuba, Alejo Carpentier. Carpentier alitumia neno uchawi na mazingaombwe katika fasihi ili kueleza uhalisia uliosukwa kwa namna maalum katika ruwaza inayobadilikabadilika

daima, huku ikiwakilisha matukio ya kawaida kwa maelezo ya kina pamoja na vipengele vya kifantasia na ndoto na kutumia mambo yanayotokana na hekaya na visasili (Abrams 1999).

Baada ya dhana za uchawi na mazingaombwe kutoka katika matumizi yake ya awali ya uchoraji huko Ujerumani miaka ya 1920 na kuingia katika uwanja wa fasihi miaka ya 1960, kumekuwa na tafsiri tofauti kati ya Roh na wahakiki wa kazi za fasihi wa wakati huo. Kwa mfano Hegerfeldt (2005) anasema, uchawi na mazingaombwe ni mbinu mpya na mwafaka ya kuelezea uhalisia kwa namna ya undani zaidi ambao sayansi na uhalisia pekee haziwezi. Anasisitiza kuwa maana ya uchawi na mazingaombwe iangaliwe si kwa mwono wa Roh pekee bali pia kwa kutegemea utamaduni wa jamii na maendeleo yaliyofikiwa na jamii husika kwa wakati huo.

Cooper (1998) akizungumzia uchawi na mazingaombwe ya Afrika Magharibi, anawatenga waandishi wa riwaya za uchawi na mazingaombwe katika makundi mawili. Wale wenye mtazamo uliofungamana na utamaduni wa nchi zao kama katika riwaya za Amos Tutuola na za D.O. Fagunwa, na wale ambao wanasawiri matukio ya uchawi na mazingaombwe kwa mtazamo mpana wa kiulimwengu ambao hawajafungwa na utamaduni finyu wa jamii zao bali wana uzoefu mkubwa wa sehemu mbalimbali duniani. Anawataja waandishi wa kundi la pili kuwa ni pamoja na Ben Okri katika riwaya yake ya *The Famished Road* (1991) na wengine ni Syl Cheney-Coker na Kojo Laing. Kwa kusisitiza mgawanyo wake huo, Cooper anasema kwamba kazi ya Tutuola iliwaathiri sana waandishi waliotajwa hapo juu kutumia mbinu ya uchawi na mazingaombwe katika utunzi

wao. Hata hivyo, bado itahesabika katika kundi la riwaya za kizalendo na za kitamaduni zilizokuwa zinapigania uhuru wa nchi zao. Cooper anajaribu kuelezea na kupanua ufahamu wetu juu ya matumizi ya uchawi na mazingaombwe katika muktadha wa fasihi ya Kiafrika.

Kwa ujumla tafsili hizo zinachanganya maana na matumizi ya maneno "uchawi" na "mazingombwe", hivyo kusababisha utata katika kufasili kila kimoja peke yake. Kwa maana hiyo, katika utafiti huu uchawi na mazingaombwe imetumiwa kama neno moja. Hata hivyo, pale palipobidi kutenganishwa, uchawi imetumiwa kama sanaa bunifu ambapo uwepo wa nguvu zilizofichika kama mizimu, mashetani, majini na roho zisizoonekana huathiri matukio katika mazingira asilia, kwa kufanya matukio ya ajabu yasiyoeleweka wala kufumbuka kwa akili ya kawaida. Kinyume chake mazingaombwe imetumika kama sanaa au kitendo cha kuhadaisha kinachozalisha matokeo ya kichawi yanayoshangaza na kuteka usikivu.

1.2 Suala la utafiti

Matumizi ya uchawi na mazingaombwe yameshughulikiwa na kutafitiwa na wataalamu mbalimbali wa kazi za fasihi (Cooper, 1998; Magaju, 2004; Nyabunga, 2005; Vutagwa, 2013; Wanjiru, 2013; Faustine, 2017; Mturo, 2018). Hata hivyo, kwa mujibu wa uchunguzi uliofanywa na mtafiti katika kupitia kazi mbalimbali za fasihi, ilionekana kuwa hakuna kazi ya kiutafiti iliyo zamia katika kuchunguza athari ya mazingira asilia ya mtunzi katika matumizi ya wahusika wa ajabu, matukio ya ajabuajabu na uvunjivu wa kaida za uhalisia na za uasilia pamoja na visasili na istiara katika riwaya ya Kiswahili kwa kulinganisha

matumizi ya vipengele hivyo vya uchawi na mazingaombwe kati ya kipindi kabla na kipindi cha usasabaadaye katika riwaya ya Kiswahili.

Utafiti huu ulifanywa ili kuziba pengo lililobainishwa hapo juu kwa kubainisha vipengele vya uchawi na mazingaombwe vilivyotajwa hapo juu katika riwaya teule za Shaaban Robert na za Euphrase Kezilahabi na kuchunguza uwepo wake katika mazingira asilia ya watunzi hao. Aidha, utafiti ulichunguza athari ya mazingira asilia ya watunzi katika matumizi ya mbinu ya uchawi na mazingaombwe katika riwaya teule. Si hivyo tu, pia utafiti umeziba pengo hilo kwa kulinganisha matumizi ya mbinu ya uchawi na mazingaombwe kati ya watunzi Shaaban Robert na Euphrase Kezilahabi. Riwaya zilizoteuliwa ni *Adili* na *Nduguze* (1952), *Kusadikika* (1951) na *Kufikirika* (1946) za Shaaban Robert ambazo zimewakilisha kipindi kabla ya usasabaadaye. Riwaya za Euphrase Kezilahabi zilizoteuliwa ni *Nagona* (1990) na *Mzingile* (1991) nazo zimewakilisha kipindi cha usasabaadaye. Riwaya hizo zimeteuliwa kimakusudi kwa sababu ndizo riwaya zilizosheheni matumizi mengi ya uchawi na mazingaombwe yanayosadifu vipindi tajwa.

1.3 Malengo ya utafiti

Utafiti huu uliangazia malengo yafuatayo:

1. Kubainisha uchawi na mazingaombwe katika mazingira asilia ya watunzi wa riwaya teule.
2. Kuchunguza athari ya mazingira asilia ya watunzi katika matumizi ya mbinu ya uchawi na mazingaombwe katika riwaya teule.

3. Kulinganisha matumizi ya mbinu ya uchawi na mazingaombwe kati ya watunzi Shaaban Robert na Euphrase Kezilahabi.

1.4 Maswali ya utafiti

Kutokana na malengo yaliyotajwa hapo juu, utafiti huu ulikusudiwa kujibu maswali yafuatayo:

1. Uchawi na mazingaombwe umebainishwa vipi katika mazingira asilia ya watunzi wa riwaya teule?
2. Mazingira asilia ya watunzi yameathiri vipi matumizi ya mbinu ya uchawi na mazingaombwe katika riwaya teule?
3. Matumizi ya mbinu ya uchawi na mazingaombwe yamelinganishwa vipi kati ya watunzi Shaaban Robert na Euphrase Kezilahabi?

1.5 Sababu za Kuchagua mada

Sababu mojawapo ya kuchaguliwa kwa mada hii ilikuwa ni kushamiri kwa matumizi ya mbinu ya uchawi na mazingaombwe ndani na nje ya fasihi andishi. Katika fasihi andishi ya Kiswahili hasa katika utanzu wa riwaya, baada ya Kezilahabi kuandika riwaya ya *Nagona* (1990) na *Mzingile* (1991) kumeibuka riwaya nyingi zinazoandikwa kwa kutumia mbinu ya uchawi na mazingaombwe. Miongoni mwazo ni *Walenisi* (1995) ya K. Mkangi, *Ziraili na Zirani* (1999) ya W. E. Mkufya na *Babu Alipofufuka* (2001) na *Dunia Yao* (2006) za S. A. Khamis. Riwaya zingine ni *Bina-Adamu!* (2002), *Zimwi la Leo* (2002) na *Musaleo* (2004) za Kyallo Wamitila pamoja na *Mafamba* (2008) na *Watu wa Gehenna* za Tom Olali. Nje ya fasihi andishi matumizi ya mbinu ya uchawi na mazingaombwe yamejidhihirisha katika nyanja mbalimbali, kwa mfano, uchawi umekuwa motifu

maarufu katika utengenezaji wa filamu, mfano mzuri ni filamu za ki-Nigeria ambazo zimekuwa maarufu sana siku hizi. Uchawi unatumika katika mahubiri ya uponyaji wa kimiujiza ambayo yameshika kasi kubwa sana siku hizi. Si hivyo tu, bali pia kumekuwa na matangazo mengi katika vyombo vya habari juu ya matukio katika jamii yanayohusishwa na uchawi na mazingaombwe. Hivyo, kulikuwa na haja ya kuchunguza sababu ya kuibuka kwa kasi ya matumizi ya mbinu ya uchawi na mazingaombwe katika fasihi andishi, hasa katika utanzu wa riwaya ambapo matumizi ya uchawi na mazingaombwe yamejidhihirisha kwa kiwango kikubwa.

Ili kutimiliza sababu tajwa hapo juu, riwaya za *Adili na Nduguze*, *Kufikirika* na *Kusadikika* za Shaaban Robert na *Nagona* na *Mzingile* za Euphrase Kezilahabi ziliteuliwa. Riwaya hizo licha ya kuwa na matumizi mengi ya mbinu ya uchawi na mazingaombwe (Ohly, 1981; Wamitila, 1991; Mohamed, 1998; Khamis, 1999), pia zinatoshleza hitaji la kulinganisha matumizi ya uchawi na mazingaombwe kabla na kipindi cha usasabaadaye katika riwaya ya Kiswahili ambalo ni lengo mojawapo la utafiti huu.

Sababu nyingine ya kuchaguliwa kwa mada hii ilikuwa ni kukusudia kuwasaidia watunzi na wasomaji wa kazi za fasihi kufahamu dhana za uchawi na mazingaombwe na matumizi yake katika kazi mbalimbali za fasihi. Pia wafahamu umuhimu wake kama mtindo muhimu katika uwasilishaji wa maudhui mahsusi kama vile: uongozi mbaya katika nchi za Kiafrika, ufisadi, ukoloni na ukoloni mamboleo pamoja na utandaridhi na athari zake.

Zaidi ya yote, sababu nyingine ya kuchagua mada hii ilikuwa ni mwono hasi wa jamii juu ya uchawi na mazingaombwe. Watu wengi wamekuwa na mtazamo hasi neno uchawi na mazingaombwe linapotajwa. Wanachukulia uchawi na mazingaombwe kwa maana moja tu, kuwa ni nguvu za ajabu azitumiazo mtu kudhuru watu wengine bila sababu. Kwao hakuna jema lolote katika uchawi na mazingaombwe. Kinyume na mawazo hayo hasi, imedhihirika kuwa kuna mazuri mengi pia katika matumizi ya uchawi na mazingaombwe (Makula, 2010). Hivyo, mada hii ilichaguliwa ili kubaini pia matumizi chanya ya uchawi na mazingaombwe na kuyaweka wazi kwa jamii. Kwa sababu hiyo, mada hii ilikusudiwa pia kuwahamasisha watunzi wa kazi za fasihi kubadilisha mwelekeo wao katika utunzi kwa kuandika namna chanya ya matumizi ya uchawi na mazingaombwe kwa nia ya kutumiwa kwa ajili ya kuleta maendeleo katika jamii na siyo kuididimiza.

1.6 Upeo na Mipaka

Utafiti huu ulishughulikia riwaya za *Kufikirika* (1946), *Kusadikika* (1951), na *Adili na Nduguze* (1951) za Shaaban Robert na *Nagona* (1990) na *Mzingile* (1991) za Euphrase Kezilahabi. Waandishi hawa wameandika kazi nyingi sana za fasihi zikiwemo riwaya, mashairi na tamthilia. Hata hivyo, riwaya zilizoteuliwa ndizo ambazo zimesheheni matumizi ya uchawi na mazingaombwe kwa kiwango kikubwa.

Riwaya tatu za Shaaban Robert na riwaya mbili tu za Kezilahabi ziliteuliwa kwa sababu riwaya za Shaaban Robert zilizoteuliwa ndizo zenye data za kutosha zinazosadifu matumizi ya uchawi na mazingaombwe kabla ya kipindi cha

usasabaadaye. Riwaya za Kezilahabi ziliteuliwa mbili tu kwa sababu, licha ya kuwa zina matumizi mengi sana ya uchawi na mazingaombwe kuliko riwaya zake zingine, ndizo riwaya pekee alizoandika katika kipindi cha usasabaadaye katika historia ya riwaya ya Kiswahili (Senkoro, 2011).

Zaidi ya riwaya hizo teule, utafiti ulilinganisha matumizi ya uchawi na mazingaombwe yaliyoko katika riwaya hizo na hali ilivyo katika mazingira asilia yaliyowalea na kuwakuza waandishi hao. Lengo lilikuwa ni kuchunguza kama matumizi ya mbinu ya uchawi na mazingaombwe katika riwaya teule imeathiriwa na mazingira asilia ya watunzi wa riwaya hizo. Hivyo, mkoa wa Tanga na kisiwa cha Ukerewe ilitumika kama maeneo ya kufanyia utafiti huu. Maeneo hayo yalizingatiwa kwa sababu Shaaban Robert asili yake ni mkoa wa Tanga ilhali Kezilahabi asili yake ni kisiwa cha Ukerewe. Mkoani Tanga utafiti ulifanywa Machui Kibambani, Machui Hospitalini, Chumbageni, Neema na Tanga mjini katika ofisi ya mkuu wa mkoa. Kisiwani Ukerewe utafiti ulifanywa kata ya Namagondo, Nansio mjini na eneo la jiwe la Nyabulebeka katika kisiwa cha Ukara.

1.7 Yaliyoandikwa Kuhusu Mada

Sehemu hii imebainisha maandiko mbalimbali yanayohusiana na matumizi ya uchawi na mazingaombwe. Maandiko hayo yamegawanywa katika makundi makubwa matatu. Kundi la kwanza ni yaliyoandikwa kuhusu uchawi na mazingaombwe katika kazi za fasihi. Kundi la pili linahusu yaliyoandikwa juu ya uhusiano wa mazingira asilia ya mtunzi na kazi yake ya fasihi. Na, la tatu ni yaliyoandikwa kuhusu kazi teule za Shaaban Robert na za Euphrase Kezilahabi.

1.7.1 Yaliyoandikwa Kuhusu Uchawi na Mazingaombwe katika Kazi za Fasihi

Uchawi na mazingaombwe umeelezwa na wataalamu mbalimbali ndani na nje ya uwanja wa fasihi. Wako wanaodai kuwa uchawi na mazingaombwe ni uwezo na nguvu za ajabu anazozaliwa nazo mtu na anazoitumia kudhuru wengine bila sababu kwa lengo tu la kujifurahisha au pengine kwa kujinufaisha binafsi (Shorter, 1998). Mawazo hayo hasi ya maana ya uchawi na mazingaombwe yanaungwa mkono na *Merriam-Webster Learner's Dictionary* (2006) kuwa uchawi ni mambo ya kimiujiza yanayofanywa na wachawi, matumizi ya nguvu za kiroho zilizochukuliwa toka kwa roho waovu kwa lengo la kusababisha madhara kwa watu. Ni nguvu inayowawezesha watu kama vile wachawi kufanya mambo ya ajabu yasiyowezekana kwa hali ya kawaida. Ni ujanja au viinimacho ambavyo kwa hali ya kawaida haviwezekani lakini hufanywa na mtu fulani kwa lengo la kufurahisha na kuwaburudisha watu. Nayo *Kamusi ya Kiswahili Sanifu* (1981) inasisitiza kuwa uchawi ni ufundi wa kutumia dawa au vitabu maalum vya uganga ili kuleta madhara kwa viumbwe, au juju. *Kamusi ya Kiarabu Lisanul Arab* (1924) inashadidia kuwa uchawi ni kitendo cha kujikurubisha na shetani na kwa msaada wa shetani, uchawi ni kulibadilisha jambo mbali na uhakika wake, ni kuwadhihirishia watu jambo lisilo la kweli wakaliona kuwa ni la kweli.

The New Century Dictionary of the English Language (1957) na *Webster's Revised Unabridged Dictionary* (2003) zinaeleza mazingaombwe kuwa ni sanaa ya kuhadaisha inayowezesha jambo fulani kusudiwa kufanyika kwa kuomba kwa Mungu au kwa msaada wa mashetani. Ni matumizi ya manuizo ya kichawi au mbinu ya kuvuta na kuteka akili, ni kile kinachozalisha matokeo ya kichawi. Ni

kitendo cha kufurahisha, uzalishaji wa tukio fulani la ajabu la kimiujiza kwa kutumia nguvu za roho waovu. Ni kile kinachokoga mioyo, ni nguvu fulani au uwezo mkubwa wa kuvutia, kushawishi na kupumbaza kwa kukazia macho. *Kamusi ya Kiswahili Sanifu* (1981) nayo inaeleza mazingaombwe kuwa ni mambo yanayofanywa kudanganya macho ya mtu ili aone kinyume na kisichokuwepo; mauzauza, kiinimacho.

Kinyume cha hao, kuna wanadai kuwa, zaidi ya kudhuru uchawi na mazingaombwe unaweza kutumika kuponya, kuadhibu waovu, kuelimisha na kurahisisha maendeleo (Makundi, 2010). Mawazo ya Makundi ni kuwa uchawi na mazingaombwe isitazamwe tu kwa mtazamo hasi, uliotuama, wa kizamani na uliopitwa na wakati, bali iangaliwe pia kwa mtazamo mpya kwa lengo la kuleta mabadiliko na maendeleo katika jamii husika.

Maoni ya wataalamu hao yamesaidia sana katika utafiti huu, hasa katika kulinganisha namna uchawi na mazingaombwe ilivyotumiwa katika riwaya teule na katika mazingira asilia ya watunzi wa riwaya hizo. Kwa mfano, katika tamthiliya ya *Ngoma ya Ng'wanamalundi*, mtunzi Emmanuel Mbogo ameonesha aina zote mbili za matumizi ya uchawi na mazingaombwe (hasi na chanya). Mhusika Chidama katika tamthilia hiyo anatumia uchawi kudhuru kwa kuwabadilisha watu vizuu kwa lengo la kuwatumikisha katika biashara zake za kinyonyaji. Kinyume chake, Ng'wanamalundi anatumia uchawi na mazingaombwe kuwaokoa vizuu, kuwatibu, kuwafundisha na kuwarudisha katika urazini pamoja na kumwadhibu Chidama. Usomaji wa tamthiliya hiyo pia ulimsaidia mtafiti katika kubainisha matumizi hasi na chanya ya uchawi na

mazingaombwe katika riwaya teule na katika mazingira asilia ya watunzi wa riwaya hizo.

Cooper (1998) kama alivyokwishaelezwa awali kuwa katika kuzungumzia uchawi na mazingaombwe ya Afrika Magharibi, amewatenga waandishi wa riwaya za uchawi na mazingaombwe katika makundi mawili. Wale wenye mtazamo uliofungamana na utamaduni wa nchi zao. Na wale wanaosawiri matukio ya uchawi na mazingaombwe kwa mtazamo mpana wa kiulimwengu, ambao hawajafungwa na utamaduni finyu wa jamii zao, bali wana uzoefu mkubwa wa sehemu mbalimbali duniani. Kwa kusisitiza mgawanyo wake huo, Cooper anajaribu kuelezea na kupanua ufahamu wetu juu ya matumizi ya uchawi na mazingaombwe katika muktadha wa fasihi ya Kiafrika.

Cooper ameeleza kwa mapana jinsi waandishi hao walivyojaribu kuunganisha uzoefu wao wa matukio ya uchawi na mazingaombwe wa kiwango cha kimataifa na ule wa tamaduni zao kuelezea masuala ya kijamii, kisiasa na ya kiuchumi katika muktadha wa Kiafrika. Anasema kuwa kwa kutumia mbinu kama za kejeli, mafumbo, ubeuzi, mwigo wa sanaa, vitendawili na vidokezo vya visasili, hawa waandishi wameandika kazi zinazosawiri maisha kwa namna mbalimbali. Wamesawiri maisha yanayoonekana na yasiyoonekana, halisi na ya kimazingaombwe, huku wakihoji umuhimu wa utamaduni na kushutumu ubepari na hivyo kufagilia mabadiliko.

Uchambuzi huo wa Cooper umekuwa na manufaa katika utafiti huu kwa sababu umejaribu kuwatenga waandishi wa riwaya wanaotumia mbinu ya uchawi na mazingaombwe katika makundi mawili: wale wenye mtazamo wa ulimwengu

mpana kama Kezilahabi katika *Nagona* na *Mzingile* na wale waliofungamana na utamaduni wa nchi zao kama Shaaban Robert katika *Adili na Nduguze*, *Kusadikika* na *Kufikirika*. Tofauti na cooper, utafiti huu umepiga hatua mbele zaidi na kuchunguza tofauti za matumizi ya uchawi na mazingaombwe zilizosababishwa na athari ya mazingira asilia kati ya watunzi wa riwaya zilizoandikwa kabla na zilizoandikwa kipindi cha usasabaadaye katika historia ya riwaya ya Kiswahili.

Sanchez (2000) katika uchambuzi wake wa riwaya ya Tom Morrison, aliangazia jinsi wanawake weusi wa Marekani wanavyopigania mabadiliko ya kitamaduni. Aligundua kuwa riwaya hiyo imetumia mbinu ya uchawi na mazingaombwe kuelezea historia ya Waafrika jinsi wanavyodunisha utamaduni wao kwa kuiga na kung'ang'ania tamaduni za wazungu. Ingawa Sanchez alitumia mbinu ya uchawi na mazingaombwe kupamba lugha, hata hivyo, utafiti wake huo nao umetusaidia katika kutumia uchawi na mazingaombwe kuwabainisha wahusika wa ajabu na uajabu wao katika riwaya teule na katika mazingira asilia ya watunzi wa riwaya hizo.

Gromov (2004), D'Haen (2005) na Walibora (2010) wanataja uchawi na mazingaombwe kuwa ni tawi mahususi la usasabaadaye. Wanaeleza historia ya usasabaadaye kama njia mojawapo ya kubuni kazi za fasihi kuwa, ulianza mapema tokea miaka ya 1950 baada ya kuporomoka kwa uhalisia na usasa. Hata hivyo, ni katika miaka ya 1980 ndipo usasabaadaye ulipopata upana wa matumizi katika nyanja za falsafa na utamaduni na pia katika fasihi na uhakiki wa kifasihi. Katika fasihi ya Kiswahili usasabaadaye umezuka mwanzoni mwa miaka ya 1990 hasa baada ya uandishi wa riwaya za *Nagona* (1990) na *Mzingile* (1991) za

Euphrase Kezilahabi. Wanaendelea kueleza kuwa lengo kuu la usasabaadaye ni kuonesha kutoweza kwa mwanadamu kufahamu ulimwengu, kwa sababu urazini wa mwanadamu hauwezi tena kuutambua utata wa ulimwengu. Kile kinachowezekana labda ni kuchunguza picha au alama za vitu. Mwanadamu haufahamu ulimwengu wake kwa sababu tu umekuwa ni uwanja wa fujo. Pia haufahamu ulimwengu wake kwa sababu ni kama matini. Yaani, ni mlimbikizo usiokuwa na mwisho wa alama zinazobuniwa na mwanadamu. Kwa hiyo, uzoefu wa mwanadamu, historia yake, utamaduni wake, kila kitu ni mkondo wa alama, ambazo zile zilizo tata hutokana na zile sahili zilizokuwepo hapo awali.

Wataalamu hao wanazidi kusesitiza kuwa usasabaadaye kama mbinu fulani ya fasihi na sanaa kwa ujumla unakwenda sambamba na utandawazi au ubepari mpevu, kuonesha mkinzano mkubwa uliomo ndani ya mfumo wake. Usasabaadaye kama mfumo una sifa ya kuvunja kanuni zote za kijadi, kaida na namna ya kutumia lugha kisanaa. Sifa nyingine ya usasabaadaye ni utouzoefu. Yaani, kuichangamsha na kuitia lugha uvuguvu ili ionekane mpya au ngeni kuliko ilivyokuwa. Lengo likiwa ni kubadilisha mtazamo wa msomaji kwa kumwonesha ujumi wa lugha ambao utachukua makini ya msomaji, kumvuta kisanaa na kumfanya afikiri zaidi. Sifa nyingine ni mvutogubi. Yaani, mjazo wa jazanda zenye fumbo, nguvu na mapigo ya muziki. Mchanganyo ndimi ni sifa nyingine ya usasabaadaye, hii ni kwa sababu mara nyingi husomba na kujaza kila kitu katika matini yake: historia, uchumi, siasa, utamaduni, dini, muziki, saikolojia na sosholojia. Pia mna mchanganyiko wa visasili, maghani na hurafa (Mogha, 2012).

Maelezo ya wataalamu waliotajwa hapo juu yamekuwa na manufaa makubwa sana katika utafiti huu. Yamemwezesha mtafiti kuweka mpaka kati ya kipindi kabla na kipindi cha usasabaadaye katika fasihi ya Kiswahili. Pia yalitoa mwanya kwa mtafiti kuchunguza sifa za kazi za fasihi zilizoandikwa kipindi kabla ya usasabaadaye. Hivyo, kurahisisha ulinganisho kati ya riwaya za Shaaban Robert na za Kezilahabi.

Osore (2008) amechunguza usadikivu na uelewekaji wa riwaya za Euphrase Kezilahabi na za Said Ahmed Mohamed. Riwaya za Kezilahabi alizochunguza ni *Rosa Mistika* (1971), *Kichwa Maji* (1974) na *Gamba la Nyoka* (1978). Katika utafiti wake amechunguza tamathali mbalimbali kama mtindo uliotumiwa na waandishi hao na hivyo kufanya kazi zao zisieleweke kwa urahisi kwa wasomaji wao. Madhumuni ya utafiti wake yalikuwa kutafuta maana fiche katika tamathali hizo ili kutatua utata wa maana na kujaribu kuleta usadikivu wa kazi za waandishi hao. Osore amegundua kuwa waandishi tajwa wametumia tamathali hizo ili kusisitiza na kuweka wazi maana kusudiwa.

Osore ametaja ndoto na kubadilika kimazingaombwe kama mbinu mojawapo zilizotumiwa na Euphrase Kezilahabi na Said Ahmed Mohamed katika kuzifanya kazi zao zisieleweke au kusadikiwa na hadhira lengwa. Utafiti huo umekuwa muhimu sana katika utafiti huu kwa sababu umefafanua sifa za ndoto na kujibadilisha kimazingaombwe; vipengele ambavyo vimeshughulikiwa pia katika utafiti huu.

Olali (2010) amechunguza riwaya ya *Babu Alipofufuka* (2001) ya Said Ahmed Mohamed. Anasema uchawi na mazingaombwe unajitokeza katika riwaya hiyo

kwa namna mbalimbali. Kwa mfano, mzuka (babu yake K aliyefariki zamani) anajitokeza ghafla kwa K akiwa nyumbani, ofisini, kwa dereva wake na hata kuchukua chakula cha mbwa wake kimiujiza. Pia K anabadilishwa kuwa mchwa kwa namna ya ajabu. Olali anakusudia kutujaza kuwa Mohamed ametumia uchawi na mazingaombwe kuonyesha kuwa matukio hayo ingawa ni ya ajabu lakini ni ya kweli na yanatokea katika maisha ya jamii husika. Olali amezidi kupanua uelewa wetu kuhusu vipengele vya uchawi na mazingaombwe kama vile, uvunjivu wa kaida kati ya uhai na kifo na kujibadilisha kimazingaombwe. Vipengele hivyo ni miongoni mwa vipengele vilivyochunguzwa katika utafiti huu.

Walibora (2010), katika Kiswahili Forum, analinganisha na kulinganua uhalisia na uhalisiamazingaombwe kati ya *Dunia Yao* (2006) ya Said, A. Mohamed na *The Tin Drum* (1962) ya Grass Die Blechtrommel ambazo zimeandikwa katika mtindo wa usasabaadaye. Walibora ametumia nadharia ya uhalisiamazingaombwe kwa madhumuni ya kuhakiki uhusiano wa kiuandishi kati ya waandishi hao waliotengana mbali sana kijiografia. Mbinu aliyotumia ni ya maktaba kwa kusoma riwaya teule na vipengele alivyovilinganisha ni: mkakati wa usimulizi, maana ya maisha, nguvu za dini na ngono. Katika uhakiki huo, Walibora amegundua kuwa ingawa waandishi hao wako mbali kijiografia (Mohamed Zanzibar na Blechtrommel Ujerumani), kazi zao zimewiana kwa kiasi kikubwa.

Tofauti ya utafiti wa Walibora na utafiti huu ni katika vipindi vya utafiti. Uhakiki wa Walibora umeshughulikia kipindi kimoja tu cha usasabaadaye kwa kutumia nadharia moja tu na tena kwa waandishi wanaotoka bara mbili tofuti. Utafiti huu unalinganisha matumizi ya uchawi na mazingaombwe katika vipindi viwili tofauti

katika fasihi ya Kiswahili: kipindi kabla na kipindi cha usasabaadaye. Hata hivyo mbinu na nadharia aliyotumia ni muhimu sana kwa utafiti huu.

Makulla (2012) amechunguza athari za uchawi na mazingaombwe kwa msomaji katika kuzielewa kazi za Said, A. Mohamed. Katika uchunguzi wake aligundua kuwa uchawi na mazingaombwe ni mbinu ya kifasihi inayochanganya uhalisi na matukio ya ajabuajabu ambayo hayazoeleki wala kuaminika kwa hadhira. Hali hii huzua taharuki na hivyo kutaka kujua nini maana yake. Athari hiyo inajitokeza pale ambapo mwandishi ametumia mbinu hii kwa kuchanganya matukio na wahusika wa ajabuajabu pamoja na mandhari ambapo humtaka msomaji kuwa makini na kutumia upembuzi wa hali ya juu kufahamu makusudi ya mtunzi. Utafiti huo wa Makulla ulitufaa katika utafiti huu kwa sababu amejaribu kuorodhesha baadhi ya vipengele vya uchawi na mazingaombwe vinavyotafitiwa katika utafiti huu. Tofauti na utafiti huu ni kuwa, Makulla (2012) alikuwa akichunguza mabadiliko ya vionjo vya uandishi katika riwaya ya Kiswahili; ilhali utafiti huu umetumia vipengele tajwa vya uchawi na mazingaombwe kuchunguza athari ya mazingira asilia ya mtunzi katika matumizi ya mbinu ya uchawi na mazingaombwe katika riwaya ya Kiswahili.

Srikanth (2014) amelinganisha matumizi ya uchawi na mazingaombwe katika riwaya za waandishi wawili tofuti, *One Hundred Years of Solitude* (1967) ya Garcia Marquez kutoka Kolombia Amerika Kusini na *Midnight's Children* (1981) ya Salman Rushdie Mhindi aliyezaliwa Uingereza. Lengo la utafiti wake lilikuwa ni kubainisha na kulinganisha sifa na vipengele vya uchawi na mazingaombwe vilivyomo katika riwaya za waandishi hao wawili waliotoka katika mazingira yaliyotofautiana sana. Alitumia nadharia ya uhalisiamazingaombwe na mbinu ya

maktaba kwa kusoma riwaya tajwa. Vipengele alivyochunguza kwa kutumia nadharia ya uhalisiamazingaombwe ni pamoja na: kujitokeza kwa wafu kuwasiliana na walio hai, matumizi ya visasili na uduara wa wakati. Katika uchunguzi wake aligundua kuwa waandishi wote wawili wametumia mbinu ya uchawi na mazingaombwe kuwasilisha masuala halisi ya kisiasa, kiuchumi, kijamii na ya kidini yaliyokuwa yakikabili jamii zao.

Tofauti ya utafiti wa Srikanth na utafiti huu ni kuwa licha ya kulinganisha matumizi ya uchawi na mazingaombwe katika vipindi viwili tofauti: kipindi kabla ya usasabaadaye na kipindi cha usasabaadaye, utafiti huu umechunguza matumizi ya uchawi na mazingaombwe katika mazingira ya fasihi ya Kiswahili. Hata hivyo uhakiki wa Srikanth umechangia pakubwa katika utafiti huu hasa upande wa nadharia na jinsi vipengele vya uchawi na mazingaombwe vinavyotumika katika kueleza uhalisia wa mambo katika maisha ya mwanadamu katika jamii mbalimbali duniani.

Kwa mujibu wa uchunguzi uliofanywa na mtafiti katika kupitia kazi mbalimbali za fasihi, ilionekana kuwa kazi za kiutafiti zilizofanywa katika fasihi ya Kiswahili zilizogusia kwa kiwango kikubwa suala la uchawi na mazingaombwe hasa upande wa nadharia ya uhalisiamazingaombwe ni zile za Magaju (2004), Nyabunga (2005), Vutagwa (2013), Wanjiru (2013) na Mturo (2018). Kazi hizo zimejaribu kutoa ufafanuzi wa baadhi ya mihimili ya nadharia ya uhalisiamazingombwe na matumizi ya uchawi na mazingaombwe ambayo yametumiwa katika utafiti huu.

Uchunguzi wa Magaju kwa mfano, ulishughulikia riwaya mbili (*Babu Alipofufuka* S.A. Mohamed, 2001 na *Bina-Adamu!* K.W. Wamitila, 2002) zote za kipindi cha usasabaadaye. Madhumuni ya utafiti wa Magaju yalikuwa kuchunguza jinsi uhalisiamazingaombwe ulivyotumiwa katika riwaya hizo na kubainisha ni kwa namna gani uhalisiamazingaombwe unavyoashiria na kuzungumzia uhalisia wa matukio ya nyakati zetu. Ili kufaulisha madhumuni hayo, Magaju ametumia nadharia ya uhalisiamazingaombwe. Alitumia mbinu ya maktaba kwa kusoma riwaya tajwa na kuhojiana na waandishi wa riwaya hizo. Matokeo ya utafiti huo yanaonesha kuwa uhalisiamazingaombwe umo kwa kiwango kikubwa katika riwaya zote mbili. Zaidi ya yote, utafiti huo umebaini kuwa Mohamed katika riwaya ya *Babu Alipofufuka* anajadili kwa kiwango kikubwa uongozi mbaya katika nchi za Afrika. Wamitila naye katika *Bina-Adamu!* anazungumzia utandaridhi hasa athari zake kwa mataifa ya Afrika.

Utafiti wa Magaju umetufaa hasa katika kufafanua matumizi ya nadharia ya uhalisiamazingaombwe katika kazi za fasihi. Pia, umetoa mwanya wa kimaarifa ambao ulimsukuma mtafiti kulinganisha matumizi ya nadharia ya uhalisiamazingaombwe na nadharia ya kiwewe cha kuathiriwa katika kuchanganua kazi za fasihi zenye kutumia mbinu ya uchawi na mazingaombwe.

Nadharia ya uhalisiamazingaombwe imetumiwa na Nyabunga (2005) kuhakiki riwaya za *Bina-Damu!* (2002) na *Musaleo!* (2004) za Wamitila. Madhumuni ya utafiti huo yalikuwa ni kuchunguza jinsi vipengele vya uhalisiajabu vinavyojidhihirisha katika riwaya tajwa na jinsi uhalisiamazingaombwe unavyoshughulikia kadhia zinazohusu maisha ya wahusika katika riwaya hizo. Nyabunga ametumia mbinu ya maktaba kwa kusoma na kuchambua riwaya teule.

Matokeo ya utafiti huo yanaonesha kuwa uhalisiamazingaombwe umetumiwa katika riwaya tajwa kutalii masuala nyeti yanayosibu ujirani wetu kama ya uongozi mbaya katika nchi za Afrika, ufisadi, ukoloni mamboleo na utandaridhi na athari zake kwa mataifa ya Kiafrika.

Utafiti wa Nyabunga pia umeufaidia utafiti huu kwa kufafanua zaidi matumizi ya nadharia ya uhalisiamazingaombwe na kutoa mwanya wa tafiti zaidi. Mwanya huo umesababishwa na hitimisho analotoa kuwa uhalisiamazingaombwe umetumiwa katika riwaya tajwa kutalii masuala nyeti yanayosibu ujirani wetu. Hivyo, kuibua swali kuwa, ni kwa nini mwandishi aachague kutumia uhalisiamazingaombwe badala ya mbinu zingine za utunzi wa kazi za fasihi? Mwanya huo umezibwa na utafiti huu kwa kulinganisha matumizi ya mbinu ya uchawi na mazingaombwe katika riwaya teule na uhalisia wake katika mazingira asilia ya watunzi wa riwaya hizo.

Katika *Utenzi wa Mwanafatuma*, Vutagwa (2013) ameshughulikia sifa za uhalisiamazingaombwe. Madhumuni yalikuwa kuchunguza maudhui ya kidini tu katika utenzi huo. Nadharia aliyotumia ni nadharia ya uhalisiamazingaombwe. Alitumia mbinu moja tu ya maktaba kwa kusoma utenzi tajwa na miswada mbalimbali inayozungumzia uhalisiamazingaombwe. Matokeo ya utafiti wake yanaonesha kuwa uhalisiamazingaombwe umetumiwa kwa kiwango kikubwa kuendeleza dini ya Kiislamu.

Utafiti wa Vutagwa umezidi kutoa mwanga kwa kutoa ufafanuzi zaidi wa kinadharia. Hata hivyo, Tofauti na Vutagwa aliyeshughulikia dhamira moja tu ya kidini, utafiti huu licha ya kutumia nadharia mbili na kulinganisha riwaya tano za

waandishi wawili tofauti, umetumia mbinu za uchawi na mazingaombwe kuangazia masuala ya kijamii, ya kisiasa, ya kidini, na ya kitamaduni katika riwaya hizo.

Nadharia ya uhalisiamazingaombwe imetumiwa na Wanjiru (2013) kwa madhumuni ya kuchunguza na kubainisha dhana ya uhalisiamazingaombwe na uhalisia katika vipengele vya wahusika na mandhari katika riwaya mbili: *Babu Alipofufuka* (2001) ya Said A. Mohamed na *Watu wa Gehenna* (2012) ya Tom Olali. Matokeo ya utafiti huo yanaonesha kuwa waandishi wa riwaya tajwa wametumia wahusika wa kiajabu na mandhari yenye matukio ya kiajabu. Hivyo, utafiti huo umebainisha kuwa uhalisiajabu umejitokeza katika viwango vya mandhari na wahusika.

Utafiti huo wa Wanjiru nao umezidi kupanua uelewa wetu juu ya nadharia ya uhalisiamazingaombwe na matumizi yake katika kuhakiki kazi za fasihi. Wanjiru ametumia nadharia ya uhalisiamazingaombwe kuchunguza vipengele viwili tu (mandhari na wahusika). Utafiti huo haukushughulia vipengele vingine vya uchawi na mazingaombwe kama vile, matukio ya ajabu, uvunjivu wa kaida pamoja na visasili na istiara. Pengo hilo limezibwa katika utafiti huu.

Mturo (2018) amechunguza Jiniuchawi na Ushirikina kama mkakati wa uchimuzi katika riwaya teule za Maundu Mwingizi. Licha ya utafiti wa Mturo kupanua uelewa wetu juu ya nadharia ya uhalisiamazingaombwe na aina mbalimbali za uchawi na mazingaombwe; hajahusisha mchango wa mazingira asilia ya mtunzi katika matumizi ya uchawi na mazingaombwe katika riwaya alizokuwa akizichunguza. Pengo hilo pia limezibwa na utafiti huu.

1.7.2 Yaliyoandikwa Kuhusu Uhusiano wa Mazingira Asilia ya Mtunzi na Kazi Yake ya Fasihi

Barthes (1967) katika makala yake ya ‘Death of the Author’ anasema kuwa mawazo ya mwandishi, wasifu wake pamoja na mazingira yake ya kijamii, kidini, kisiasa na hata ya kitamaduni hayana mchango wowote katika kuifahamu na kuihakiki kazi yake. Anasema mwandishi habuni kitu kipya bali ni nyenzo tu ya kupitishia historia ambayo tayari ipo. Mawazo hayo ya Barthes yanashadidiwa na Syambo na Mazrui (1992) kuwa, utungo wa kazi ya fasihi ni dunia ya kubuni inayojitegemea na kujitosheleza yenyewe bila kuhusishwa na jambo lolote katika ulimwengu wetu huu wa kawaida. Katika kutafiti mahusiano ya utungo na nafsi yake basi, maswali yanayohusu mtunzi, jumua ambayo utungo huo umetokana nayo, hadhira iliyodhamiriwa, tungo nyingine za wakati huo, yote huwa si muhimu. Wanasisitiza kuwa dunia ya sanaa ni ulimwengu kamili unaojitegemea kivyake wala hauhitaji kuhusishwa na jambo lolote lililo nje yake. Kwa maoni yao, mandhari, wahusika na hata matukio katika kazi za kubuni yasihusishwe na hali ilivyo katika jamii.

Tofauti na mawazo hayo ya Barthes, Hirsch (1967) anakubaliana na nafasi ya mazingira yaliyomlea na kumkuza mtunzi kuchangia kwa kiwango kikubwa katika utunzi wake. Anasema:

Hakuna ubunaji ambao hautegemei mambo yaliyomo kwenye uzoefu na tajriba zetu au za jamii zetu. Ubunaji hautokani na ombwe, bali unatokana na hali halisi, hali ya mambo ambayo msanii ameyaona, ameyasikia, ameyanusa, ameyaonja, ameyahisi au ameyasoma pahali. Kwa kutumia kipawa chake cha kubuni msanii atayafinyanga upya mambo hayo ili kuunda umbo la kisanaa (Hirsch1967: 16).

Mawazo hayo ya Hirsch kuwa ili msanii aweze kuandika kazi yake kuna masuala yaliyoko katika jamii yaliyomgusa, yakamtekenya na kumsukuma kuyazungumzia kwa namna ya ubunifu wa pekee, yanadhihirisha kuwa ubunifu unatokana na uhalisia wa mazingira yaliyomzaa na kumlea msanii. Ubunifu ni uwezo wa kuunda dunia mpya kutokana na dunia tuliyomo, ni uwezo wa kuanzisha kitu ambacho hakipo kabisa kutokana na kitu ambacho tayari kipo. Maoni hayo ya Hirsch yanashadidia mawazo ya Candwell (1947) na Brecht (1964). Candwell (1947) anasema ulimwengu huu wa kisanaa ni ulimwengu wa hisia za kijamii, ulimwengu wa maneno na picha ambao umejengwa kutokana na tajriba ya maisha ya wote, hisia za utangamano kwa wote. Pia Brecht (1964) anasema kwamba ni kwa maslahi ya jamii ambapo fasihi inatakiwa kutoa vielelezo kwa ukweli wa maisha, vielelezo ambavyo vina maslahi kwa umma.

Kwa mawazo hayo ya Candwell (1947), Brecht (1964) na Hirsch (1967), inaweza kusemwa kuwa matumizi ya uchawi na mazingaombwe katika kazi za fasihi ni ubunaji wa kazi ya binadamu anayetokana na jamii fulani, inayoakisi au yenye kuiga uhalisi unakubaliana na wakati, mazingira na mfumo wa jamii husika. Kazi bora ya fasihi ni ile inayohusiana na utamaduni, siasa, dini, elimu na saikolojia pamoja na jinsi mtunzi aonavyo mambo mbalimbali ya nje na ya ndani ya nafsi yake pamoja na nguvu zote zisizoonekana kama miungu, malaika na mashetani, ambazo ziko nje ya uwezo wa kawaida wa binadamu (Maggati na Wenzake, 2021).

Kupishana kwa maoni ya Barthes (1967) na Hirsch (1967) juu ya mazingira ya mtunzi kuathiri au kutoathiri utunzi wake yametufaa sana katika utafiti huu hasa

kama kichocheo cha kuchunguza ili kubaini kama mazingira asilia ya mtunzi yana mchango wote au la katika utunzi wake wa kazi ya fasihi.

Nochlin (1971) anasema kuwa kutumia mafumbo na mifano kutoka katika mazingira halisi ni kama kuondoa shuka la njozi lililofunika uhalisi kwenye mambo yanayozungumzwa. Maoni hayo ya Nochlin (1971) yanafafanuliwa na Levinson (1983) anayesema kwamba, kazi yoyote ya sanaa hutungwa katika muktadha fulani na uelewaji wa muktadha ni muhimu sana katika kuelewa maana alizokusudia mwandishi. Nyawira (2016) anashadidia mawazo hayo kwa kusema kuwa, mtunzi ni zao la mazingira na utamaduni wa jamii anamolelewa na kukulia humpa mwongozo bora wa maisha yake hasa kama mtunzi. Anaendelea kusema kwamba watunzi wengi waliopata elimu ya kimagharibi hadi vyuo vikuu wameathiriwa hivi kwamba wamejiunga na kundi la washahiri wanamapinduzi ambao wanaongozwa na muasisi mkuu wa kundi hili ambaye ni Kezilahabi.

Mawazo hayo yanasisitizwa na Ayiera (2017) kuwa mazingira ya mwandishi hayana budi yaoane na yale anayoandika. Hivyo, fasihi haina budi ichunguzwe katika muktadha wa kumhusisha binadamu sio tu na nguvu za kimaumbile, bali pia na nguvu zinazotokana na jamii yake ambazo huweza kuathiri mawazo na mielekeo yake. Mawazo hayo yamekuwa na manufaa katika utafiti huu kwa sababu yalimhamasisha mtafiti kuchunguza kama matumizi ya uchawi na mazingaombwe katika riwaya teule yameathiriwa na mazingira asilia ya watunzi au la. Pia yamepanua uelewa wetu kuhusu mazingira ya mtunzi, kuwa mazingira ya mtunzi siyo pale alipozaliwa na kukulia tu, bali kuna mazingira ya shuleni,

kazini, mazingira ya kidini pamoja na mwingiliano au uigilizaji wa tamaduni za kigeni.

Momanyi (1991) anasema kuwa, mwandishi anayeandika kutokana na uhalisia wa mambo anachota maudhui yake kutoka kwa watu halisi na mazingira halisi. Mawazo hayo yanafafanuliwa na Oka (2002) akielezea riwaya ya Okri ya *The Famished Road* (1991). Anasema kwamba, Okri anachunguza kwa undani mkubwa historia ya maisha ya wananchi wa Nigeria kuanzia wakati wa ukoloni hadi wakati wa uhuru na utawala wa kijeshi. Kuzaliwa na kufa kwa Azaro mara tano kunaonyesha vipindi vitano vya utawala nchini Nigeria. Oka anabainisha kuwa hadithi ya uchawi na mazingaombwe ya kufa na kufufuka mara tano kwa Azaro ni dhihirisho la hali ya umaskini na siasa za nchi ya Nigeria. Okri anasema kuwa aliandika kutokana na hasira, umaskini uliomzunguka na mwelekeo hasi wa serikali na mateso kwa wananchi. Ulikuwa wakati wa ufisadi mwingi nchini Nigeria (Okri, 1990).

Maelezo hayo ya Oka juu ya utunzi wa Okri yanaonesha kuwa Okri alitumia mtindo wa uchawi na mazingaombwe kuelezea hali halisi ya maisha katika mazingira halisi ya jamii yake. Okri kutumia uchawi na mazingaombwe ni kutokana na mazingira yake asilia kugubikwa na matumizi ya uchawi na mazingaombwe kiasi cha matumizi hayo kuwa sehemu ya uhalisia wa kawaida katika jamii yake. Matumizi hayo ya uchawi yanajidhihirisha hata katika picha nyingi za filamu za ki-Nigeria ambazo zinatumia uchawi na mazingaombwe kwa kiasi kikubwa. Uchunguzi huo wa Oka umepanua mawazo yetu katika utafiti huu juu ya mchango wa mazingira asilia ya mtunzi katika utunzi wa kazi ya fasihi.

Utafiti wa Oka ulifanyika nchini Nigeria, Afrika Magharibi, kwa kutumia riwaya moja tu. Tofauti na Oka, utafiti huu ulimakinia kuchunguza athari ya mazingira asilia kati ya watunzi wawili walioandika katika vipindi viwili tofauti. Mmoja aliyeandika kipindi kabla na mwingine kipindi cha usasabaadaye katika riwaya ya Kiswahili.

Senkoro (1995) anasema kwamba hakuna ubunifu ambao hautegemei mambo yaliyomo kwenye uzoefu na mazingira yaliyomzaa na kumlea msanii. Ayiera, Ontieri na Ayodi (2017) wanashadidia kuwa mazingira anamotungia kazi mwandishi huathiri sana uchaguzi wake wa lugha na jinsi anavyoenda maudhui yake. Wanaendelea kusema kuwa kufahamu mazingira asilia kunamsaidia msomaji kutambua kama palikuwa na mshawasha wa namna fulani uliomfanya mwandishi kuandika hivi na sio vile na pengine kutambua ni kwa nini kaandika. Maelezo hayo yameufaidia utafiti huu, hasa kwa kumhamasisha mtafiti kuchunguza kwa kina athari ya mazingira asilia ya watunzi katika matumizi ya mbinu ya uchawi na mazingaombwe katika riwaya teule. Kwa hiyo, kuchunguza mazingira asilia ya Shabaan Robert na ya Euphrase Kezilahabi kuhusiana na matumizi ya uchawi na mazingaombwe ilikuwa ni suala la muhimu katika uchambuzi wa riwaya zao zinazoshughulikiwa katika utafiti huu. Historia ya maisha ya mwandishi na mazingira asilia yaliyomlea na kumkuza mwandishi ni kama kurunzi inayotumika kumulikia kazi yake.

Kutokana na maoni ya wataalamu hao ni muhimu kuchunguza mazingira asilia ya mtunzi ili kuielewa vizuri kazi yake. Hivyo kuchunguza mazingira asilia yaliyomlea na kumkuza mtunzi ni mbinu ya msingi na ya muhimu katika

kuchunguza kazi ya sanaa. Ubunifu chanzo chake ni uhalisi na bila uhalisi wa mazingira asilia yaliyomlea na kumkuza msanii hakuna ubunifu (Austin Warren, 1949; Whimsatt and Beardsley, 1946; Hirsch, 1967; Senkoro, 1995; Mohamed, 1995; Chuachua, 2016).

1.7.3 Yaliyoandikwa Kuhusu Kazi Teule za Shaaban Robert na Euphrase Kezilahabi

Kwa upande wa fasihi ya Kiswahili, Wafula (1989 na 2014), amechunguza majazi katika nathari za Shaaban Robert. Madhumuni ya utafiti huo yalikuwa ni kuchunguza kwa nini Shaaban Robert alitumia majazi katika kazi zake. Mbinu aliyotumia katika utafiti huo ilikuwa ni ya maktaba kwa kusoma nathari teule za Shaaban Robert. Katika uchunguzi wake amegundua kuwa Shaaban Robert ametumia majazi katika riwaya alizokuwa akizichunguza za *Adili na Nduguze*, *Kusadikika*, *Kufikirika*, *Utu Bora Mkulima* na *Siku ya Watenzi Wote* kwa makusudi mbalimbali yakiwa ni pamoja na kuonesha tabia au hali ya mhusika, mji au kazi za kitu. Zaidi ya yote, ameitumia kama masimulizi yatumiayo ishara ambayo maana yake hujitokeza pia katika masimulizi. Ameonesha, kwa mfano, kitendo cha nduguze Adili kugeuzwa manyani kama ni mwendelezo wa masimulizi yanayothibitisha matokeo ya maana ya majina ya kimajazi, ikionesha jinsi waovu wanavyopatilizwa na kuvuna matokeo ya matendo yao. Utafiti huo wa wafula umetufaa katika utafiti huu, hasa kama kichocheo cha kufanya uchunguzi wa uwezekano wa matukio ya ajabu kama ya binadamu kugeuzwa nyani kutokea katika mazingira halisi katika jamii. Hii ni kwa sababu katika kanuni za kimaumbile, ni muujiza kwa binadamu kujibadilisha au kubadilishwa kuwa nyani.

Wamitila (2003) anaeleza kuwa maudhui ya *Nagona* (1990) na *Mzingile* (1991) za Euphrase Kezilahabi hayako wazi kutokana na ubunifu wa hali ya juu uliotumiwa hasa katika usawiri wa wahusika, ukiukwaji wa kanuni za kijadi za utunzi na namna ya usimulizi wake. Uchunguzi wa Wamitila umeufaa utafiti huu kwa kufafanua baadhi ya vipengele vya uchawi na mazingaombwe kama vile, wahusika wa ajabu na uvunjivu wa kaida ambavyo vilikuwa sehemu ya utafiti huu. Pia uchunguzi huo ulizidi kutoa mwanya zaidi wa utafiti. Hivyo, kumtia hamasa mtafiti kuchunguza sababu zilizomsukuma Kezilahabi kusawiri wahusika kwa namna ya ajabu na kukiuka kaida za kijadi zilizozoeleka katika utunzi wa kazi za fasihi.

Rettova (2004) amechunguza riwaya za *Nagona* na *Mzingile* za Euphrase Kezilahabi kwa kuangazia jinsi falsafa ya nchi za Magharibi inavyoakisiwa katika riwaya hizo. Katika utafiti wake amebaini kuwa Kezilahabi anaamini kuwa falsafa ya nchi za Magharibi inaweza kufaa na kutofaa katika vipengele fulani katika kuelezea falsafa na maisha ya Waafrika. Utafiti wa Rettova umechangia utafiti huu hasa katika kulinganisha athari ya mazingira asilia ya mtunzi (Euphrase Kezilahabi) katika utunzi wa kazi ya fasihi. Hii ni kwa sababu Kezilahabi licha ya mazingira yake asilia ya Ukerewe alikozaliwa kuna mazingira mengine nje ya hapo ambayo yameathiri utunzi wake. Hata hivyo, utafiti wa Rettova ni tofauti na utafiti huu kwa sababu Rettova amechunguza tu kipengele cha kifalsafa na kushughulikia riwaya za mwandishi mmoja na za kipindi kimoja tu cha usasabaadaye. Utafiti huu umepiga hatua zaidi kwa kuangazia athari za mazingira asilia ya mtunzi katika kutumia uchawi na mazingaombwe kwa kulinganisha matumizi ya uchawi na mazingaombwe katika vipindi viwili tofauti

katika fasihi ya Kiswahili: kipindi kabla ya usasabaadaye na kipindi cha usasabaadaye.

Khamis (2007) anapoeleza mwanzo wa uibukaji wa riwaya za uchawi na mazingaombwe katika riwaya ya Kiswahili anataja kazi za Shaaban Robert za *Adili na Nduguze* (1952), *Kusadikika* (1951) na *Kufikirika* (1946). Anasema kwamba, ingawa mbinu hii ilianza kutumiwa na Shaaban Robert katika riwaya zake tajwa, lakini sasa imeshika hatamu na kukua kwa kasi na kutumiwa na waandishi wengi kama Kezilahabi, Mohamed, Wamitila na wengine. Si hivyo tu, bali pia anataja riwaya za *Nagona* (1990) na *Mzingile* (1991) kama riwaya za kipindi cha usasabaadaye zilizoandikwa kwa kutumia mbinu ya uchawi na mazingaombwe. Anasema kuna utata mkubwa sana katika fani na maudhui ya riwaya hizo unaosababishwa na mbinu ya uchawi na mazingaombwe iliyotumiwa na mwandishi kwa lengo la kutaka kumwezesha mwanadamu kutambua utata uliomo katika ulimwengu anamoishi. Anasisitiza kuwa Kezilahabi ametumia mbinu ya uchawi na mazingaombwe pamoja na fantasia katika riwaya hizo kwa makusudi maalumu. Lengo ni kumfanya msomaji afikirie kwa makini juu ya uhalisia mpya wenye ukweli fulani maalumu uliosimikwa katika miingiliano ya masimulizi na mpangilio wa matukio ambao si wa moja kwa moja.

Mawazo hayo ya Khamis yametufaa kwa namna nyingi katika utafiti huu. Kwanza, kwa kueleza kuwa uchawi na mazingaombwe umo katika riwaya teule za Shaaban Robert na za Euphrase Kezilahabi zinazochunguzwa katika utafiti huu. Manufaa ya pili ni kuwa yameuwezesha utafiti huu kupata riwaya zilizotumia mbinu ya uchawi na mazingaombwe zilizoandikwa kipindi kabla na kipindi cha usasabaadaye katika fasihi ya Kiswahili. Manufaa ya tatu ni kueleza

kuwa kuna utata katika kuzielewa kazi zilizoandikwa kwa kutumia mbinu ya uchawi na mazingaombwe kwa sababu kazi hizo zinatafsiri utata uliomo katika maisha halisi. Khamis aliishia tu kutaja riwaya za uchawi na mazingaombwe zilizoandikwa katika vipindi hivyo viwili tofauti katika historia ya riwaya ya Kiswahili na kusema tu kuwa kuna utata katika uchambuzi wake. Mtafiti alichochewa kuchunguza uhalali wa maoni hayo ya Khamis kwa kulinganisha matumizi ya mbinu ya uchawi na mazingaombwe katika vipindi hivyo viwili tofauti katika historia ya riwaya ya Kiswahili na kuhusisha na uhalisia wake katika mazingira asilia ya watunzi wa riwaya teule.

Madumulla (2009) ana maoni sawa na Khamis (2007). Anasema kuwa riwaya za *Nagona* na *Mzingile* zilizotumia mbinu ya uchawi na mazingaombwe ni riwaya fupi lakini tata kuliko riwaya zote katika fasihi ya Kiswahili. Anasisitiza kuwa riwaya hizi ni zao la kazi za kifasihi linalotokana na visasili mamboleo vinavyoonesha kifalsafa mzunguko unaofanywa na mwanadamu pasipokufika katikati ya mzunguko huo panapofikiriwa kuwa ndipo penye ukweli wa maisha. Maoni hayo ya madumulla juu ya utata wa kueleweka kwa riwaya mamboleo zinazotumia mbinu ya uchawi na mazingaombwe yalizidi kutoa mwanga juu ya mada yetu ya utafiti na hivyo kuzidi kupanua wigo wetu wa kulielewa mada ipasavyo. Hata hivyo Madumulla hasemi lolote juu ya namna ya kutatua huo utata wa kutoeleweka kwa riwaya za *Nagona* na *Mzingile* na hivyo kutoa mwanya na utafiti zaidi. Hii ni kwa sababu lengo la Madumulla lilikuwa ni kubainisha aina za riwaya na sio kufumbua utata au kutafsiri kile kinachoelezwa katika riwaya hizo. Hivyo utafiti huu ulikusudia kuliziba pengo hilo kwa kuhusisha vipengele vya uchawi na mazingaombwe vilivyokuwa sehemu ya

utafiti huu vilivyoko katika riwaya husika na uhalisia wake katika mazingira asilia ya Euphrase Kezilahabi.

Ponera (2014), amechunguza ufutuhi katika nathari za Shaaban Robert na za Euphrase Kezilahabi. Katika utafiti wake amegundua kuwa waandishi hao wametumia vichekesho, kinaya na dhahaka siyo kwa lengo tu la kuifurahisha hadhira bali pia kufichua uovu au ujinga fulani uliotawala katika jamii kwa namna inayowafanya wasemwao kutoelewa kuwa wanasemwa na pia kuwafanya wasomaji wanapogundua hukerwa na kuchukizwa na maovu hayo. Katika utafiti huo Ponera ametumia mbinu ya ufutuhi kuelezea ulafi wa mfalme Jeta wa nchi ya Majuju katika riwaya ya *Kusadikika*. Mwandishi anasema:

Kabuli alipopelekwa mbele ya Jeta alimkuta amepanua midomo na mto mrefu na mpana ulikuwa ukimiminika katika kinywa chake kikubwa sana. Tone la maji hata moja halikupata nafasi ya kukiepa kinywa hicho. Tani milioni za miamba, za chuma, za magogo, na za samaki zilimiminika pamoja na mkondo wa maji humo kinywani pia kila dakika tano. Lakini kila dakika moja Jeta alilia: kiu njaa, kiu njaa (uk.23).

Utafiti wa Ponera umechangia pakubwa katika utafiti huu hasa kwa upande wa nadharia. Ponera ametumia nadharia ya kiwewe cha kuathiriwa ya Harold Boom kwa kulinganisha ufutuhi katika nathari za Shaaban Robert na za Euphrase Kezilahabi, nadharia ambayo pia imetumika katika utafiti huu. Utafiti wa Ponera ulilenga katika ufutuhi (vichekesho). Hivyo, mtu anaweza kuucheka ulafi wa Jeta hasa pale anapoendelea kulia kiu njaa, kiu njaa, baada ya kubugia tani hizo zote. Hata hivyo, ni ajabu na si rahisi katika hali ya kawaida ya kimaumbile na kiuhalisia mtu kupanua mdomo na maji ya mto kuingia kinywani pamoja na tani nyingi za chuma, magogo na samaki. Kwa nini Shaaban Robert atumie matukio yanayokiuka uhalisia wa kawaida katika utunzi wake? Ni miongoni mwa maswali

ambayo hayakujibiwa na utafiti wa Ponera. Pengo hilo limezibwa na utafiti huu kwa kuchunguza athari ya mazingira asilia ya mtunzi katika kutumia wahusika na matukio ya ajabu katika riwaya teule.

1.8 Misingi ya Nadharia

Uchaguzi wa nadharia inayofaa kutumika katika utafiti wowote inategemeana na utafiti wenyewe. Hii ni kwa sababu hakuna nadharia inayoweza kuihakiki kazi fulani ya fasihi kwa ukamilifu na utoshelevu. Kinachozingatiwa ni kile kinachotarajiwa kuchunguzwa na mhakiki na vigezo anavyovitumia katika uhakiki huo (Ntarangwi, 2004).

Utafiti huu umeongozwa na nadharia mbili kwa pamoja ili kuweza kutimiza malengo yaliyokusudiwa. Nadharia hizo ni nadharia ya uhalisiamazingaombwe na nadharia ya kiwewe cha kuathiriwa. Nadharia ya uhalisiamazingaombwe ni miongoni mwa nadharia za uhakiki wa kazi za fasihi zinazojumuishwa katika tapo la nadharia ya usasaleo (Zamora, 1995). Nadharia hii iliasisiwa mwaka 1925 na mhakiki wa kazi za sanaa, Franz Roh kutoka Ujerumani. Waitifaki wa nadharia hii ni pamoja na Zamora (1995), Abrams (1999) na Hegerfeldt (2005). Ilhali, Nadharia ya kiwewe cha kuathiriwa iliasisiwa mwaka 1973 na Mmarekani Harold Bloom. Waitifaki wa nadharia hii ni pamoja na Moh (1991).

Nadharia ya uhalisiamazingaombwe ilitumiwa kwa sababu inatumika kuyaelezea matukio ya kifantasia, ya kiajabuajabu au ya kichawi kwa namna inayoyafanya yaonekane kama ya kawaida tu. Mpaka uliopo kati ya mambo yanayoweza kupatikana katika ulimwengu halisi na yasiyowezekana huwa mdogo sana (Wamitila: 2003). Sababu hasa ya kutumia nadharia hii ilikuwa ni kutaka kudhihirisha sifa za kichawi na za kimazingaombwe zilizopo katika riwaya teule

na kuonesha kuwa matumizi ya uchawi na mazingaombwe hupatikana katika maisha ya kawaida katika jamii zinazohusika.

Nadharia ya Kiwewe cha Kuathiriwa ilitumiwa kwa sababu inatumika kulinganisha na kulinganua kazi mbalimbali za sanaa. Hivyo, katika utafiti huu, nadharia hii ilikuwa muhimu kwa sababu nadharia ya uhalisiamazingaombwe haiwezi kutumika kulinganisha na kulinganua kazi za waandishi wawili tofauti na za vipindi tofauti kama ilivyokusudiwa katika utafiti huu. Kwa hiyo, nadharia hii imetumika kulinganisha na kulinganua matumizi ya uchawi na mazingaombwe yaliyoko katika riwaya teule za Shaaban Robert na za Euphrase Kezilahabi. Pia imetumika kulinganisha miktadha iliyowasukuma waandishi tajwa kutumia mbinu za uchawi na mazingaombwe katika riwaya zao. Zaidi ya yote imetumika kulinganisha uhusiano uliopo kati ya matumizi ya uchawi na mazingaombwe yaliyoko katika riwaya teule na hali ilivyo katika mazingira halisi ambapo kazi hizo zimechotwa.

1.8.1 Nadharia ya Uhalisiamazingaombwe

Ingawa dhana ya uhalisiamazingaombwe ilianza kutumika zaidi mwishoni mwa miaka ya 1940, dhana hii ilitumiwa kwa mara ya kwanza na mchoraji na mpiga picha wa Kijerumani Franz Roh mwaka 1925. Roh alitumia dhana hii akirejelea mtindo wa uchoraji uliojulikana kwa Kijerumani kama 'Neuer Sachlichkeit' au 'the new objectivity' kwa Kiingereza kama kabadala cha uhalisiafifi 'surrealism' ya Andre' Breton iliyokuwa ikisisitizwa na Mjerumani mwenzake Gustav Hartlaub aliyekuwa mkurugenzi wa jumba la makumbusho.

Roh alitambulisha uhalisiamazingaombwe kama picha au sanamu iliyochorwa au kutengenezwa kwa umakini mkubwa na kwa uwazi wa pekee ikisawiri uasilia wa uchawi na mazingaombwe katika ulimwengu halisi. Na wakati huo huo ikitafsiri uajabu wa watu katika ulimwengu wa sayansi na ufundi au teknolojia ya kisasa.

Baadaye uhalisiamazingaombwe ulitumiwa kuelezea mambo ya ajabuajabu yanayosawiri uhalisia na wachoraji wa Amerika Kusini kama vile: Ivan Albright, Paulo Cadmus na George Tooker kati ya miaka ya 1940 na 1950. Miongoni mwa waandishi wa fasihi waliovutiwa na sanaa hii ya uchoraji wa Wajerumani ni pamoja na Massimo Bentempelli wa Itali, Hubert Lampo wa Ubelgiji na Arturo Uslar-Pietri wa Venezuela. Leal (2009) anasema kuwa Pietri ni miongoni mwa walioanza kutumia neno 'realismo magico' yaani uhalisiamazingaombwe mwaka 1948. Ilhali Alejo Carpentier kutoka Cuba kwa kutofurahia istilahi ya uhalisiamazingaombwe ya Roh, mwaka 1949 alizuka na dhana ya 'marvelous realism' uhalisiajabu. Bowes akiandika juu ya hili anasema, fasihi na sanaa ya uhalisiamazingaombwe ambayo kisemantiki inaonekana kuwa na maana inayokinzana (uhalisia na mazingaombwe) hueleza mambo ya kweli, halisi, yanayoonekana na kugusika na wakati huo huo uingiza ushetani, umizimu na mazingaombwe katika mazingira halisia kutegemeana na utamaduni wa jamii husika (Bowes, 2004).

Roh aliamini kuwa uhalisiamazingaombwe ulihusiana na kuhitilafiana na uhalisiafifi ya Andre' Breton ya 1924 ambayo wengine wameufananisha na Uhalisiamazingaombwe. Hii ni kwa sababu wakati uhalisiamazingaombwe ukilenga katika vitu halisi na uhakika wa kuwapo na kuishi kwa vitu au viumbe hivyo katika ulimwengu halisi; uhalisiafifi hueleza mambo yaliyobanwa katika

ung'amuzi wa akili ya binadamu na kwa njia ya ndoto. Uhalisiafifi ni mkondo wa uwazaji unaomwezesha mwandishi kuyachunguza na kuyasawiri matukio au hali za kindoto au za kisaikolojia zinazotokea katika ung'amuzibwete wa akili. Ung'amuzibwete ni sehemu ya akili ya binadamu ambapo mambo ya kibinafsi ubanwa na kuzuiliwa yasitoke. Lengo hasa la Breton kutumia mkondo huu ni kusawiri uhalisi tofauti na mkondo wa uhalisia wa kimantiki uliozoeleka.

Ingawa uhalisiafifi umepiga hatua moja mbele katika kuleta mwono mpya katika kuutazama uhalisia lakini hauwezi kufaa katika utafiti huu na ni tofauti kabisa na nadharia ya uhalisiamazingaombwe iliopendekezwa kutumika katika utafiti huu. Hii ni kwa sababu yale yanayoshughulikiwa kwa kutumia uhalisiafifi hayahusiani na vitu halisi au maisha katika uhalisi wake bali ni ya kufikirika, ya kuwazika, ya akilini na hivyo yanataka kueleza maisha ya ndani na saikolojia ya binadamu kupitia Sanaa. Unakusudia kuelezea ung'amuzi, ung'amuzibwete na mambo yaliyobanwa akilini ambayo hayatakiwi kutoka na ambayo hayakubaliki kiuhalisia. Uhalisiamazingaombwe, kwa upande mwingine, ni mara chache sana kuelezea mambo yasiyo ya kawaida kwa njia ya ndoto au uzoefu wa kisaikolojia. Kufanya hivyo Bowers (2004) anasema, "Ni kuchukua vitu halisi kabisa vinavyotambulika kichawi na kimazingaombwe na kuviingiza katika ulimwengu usiofahamika vizuri wa kufikirika. Ukawaida au kuzoeleka kwa mizungu ya uchawi na mazingaombwe hutokana na matokeo au kutokea kwake katika vitu vinavyoonekana na kugusika, vinavyokubalika na kupokelewa kama hali ya kila siku, ya kawaida na vilivyozoeleka bila kutiliwa shaka lolote.

Kwa mujibu wa Franz Roh, nadharia ya uhalisiamazingaombwe hutumika katika sanaa kusawiri matukio ya kichawi na ya kimazingaombwe yaani maajabu na

miujiza iliyomo katika mazingira halisi na inayotokana na uzoefu wa maisha ya watu katika jamii husika. Hayo maelezo yanakubaliana na mawazo ya Amaryll katika Michelle (1993) anayesema kuwa, “Uhalisiamazingaombwe una mitazamo miwili inayokinzana na kukubaliana. Mtazamo mmoja ni ule wenye msingi wa uhalisi (ukweli jinsi unavyoonekana) na wa pili una msingi wake katika imani kuwa mazingaombwe ni kiungo muhimu cha ulimwengu wa kila siku (wa kawaida).

Hegerfeldt (2005) katika makala yake ya “Uchawi na Mazingaombwe Yaingia Uingereza”, akilenga mifano yake kutoka Uingereza ya wakati huo anasema, waandishi wa riwaya wanaofuata nadharia ya Uhalisiamazingaombwe wanazungumzia mabadiliko sio katika nchi zilizojipatia huru kutoka minyororo ya ukoloni tu, bali hata katika nchi zilizotawala kama Uingereza. Anasema kuwa matumizi ya uhalisiamazingaombwe yamepanuka na yanatumika katika taaluma mbalimbali za kijamii. Akichunguza jinsi mtu mmoja mmoja na jamii mbalimbali wanavyoiangalia dunia, anasema waandishi wa kimazingaombwe wanadhihirisha jinsi uhalisia na sayansi pekee zisivyoweza kueleza uhalisia wa maisha ya mwanadamu.

Kama mojawapo wa waitifaki wa nadharia ya uhalisiamazingaombwe, Hegerfeldt anapanua maana na matumizi ya nadharia ya uhalisiamazingaombwe katika fasihi. Anasema, uhalisiamazingaombwe husisitiza uhalisia wa kazi za ubunifu kwa kutumia mbinu mbalimbali ambazo msingi wake uko katika uvunjivu wa kaida za isimu ya lugha na mantiki zaidi ya ukiushi wa utanzu. Anasema mifano ya mbinu hizo ni pamoja na uhalisishaji wa sitiari, ambapo maana ya kisitiari hugeuzwa katika maana yake hasa, halisi na ya kawaida. Mbinu nyingine ni

majina dhahania huchukua hali ya kuishi na kutendewa kama viumbe hai. Zaidi ya yote ni uhalisishaji wa kisaikolojia ambapo viumbe vya kufikirika kama mizimu, majini na mashetani hupewa urazini na kuishi na kutenda matendo sawa na watu wa kawaida kana kwamba ni watu halisi.

Zamora (2005) akiunganisha mawazo ya Roh, na wahakiki wa baadaye anasema kwa ujumla, uhalisiamazingaombwe hutambulishwa kwa sifa yake ya kuunda maana ya kimazingaombwe kwa kuangalia vitu vya kawaida kwa namna isiyo ya kawaida.

Nadharia hii ilitumiwa kwa sababu mihimili yake inatosheleza kuchambua riwaya zilizohakikiwa katika utafiti huu. Mihimili ifuatayo ya Uhalisiamazingaombwe ilitumiwa katika utafiti huu.

1.8.1.1 Matukio ya Kichawi na ya Kimazingaombwe Yanaonekana ya Kawaida Lakini Yenye Hali za Kuogofya na Kuduwaza

Mhimili huu umesaidia katika kuchunguza matumizi ya uchawi na mazingaombwe katika riwaya za Shaaban Robert na za Euphrase Kezilahabi kama matukio ya kawaida yanayotokea katika jamii na kuhusisha matukio hayo na kile yanachokisawiri katika maisha ya kawaida katika jamii husika (Wamitila, 2003).

1.8.1.2 Uhalisi na Ndoti Vinaingiliana

Inawezekana mtu anapoota ndipo yupo katika uhalisi na wakati yu uhalisini ndipo yu ndotoni. Hii ni kwa sababu katika uhalisiamazingaombwe hakuna mpaka kati ya uhalisi na utohalisi. Hii inadhihirisha kuwa uhalisiamazingaombwe haukubaliani na uhusiano wa kadhia zinazotendeka katika maisha ya mtu kiutengano. Hali kama za uhalisi na ndoto, usasa na ukale, uhai na kifo, mbali na

karibu, ugeni na uwenyeji na tamaduni zinaingiliana. Mhimili huu umetumika katika riwaya teule kwa sababu waandishi wametoa mawazo yao kwa namna mbalimbali kama vile kwa njia ya ndoto, kama majini, malaika, mashetani, kama vichaa na hata kama wafu. Hivyo kwa kutumia mhimili huu mawazo na maoni ya wahusika yamepewa uzito stahiki bila kujali kuwa yametoka kwa njia ya ndoto, au yametolewa na mfu, jini, malaika au mnyama. Kwa kukubaliana na mhimili huu Flores (1988) anasema, “Uhalisiamazingaombwe unajumuisha uchanganyaji wa uhalisia na fantasia. Unakusudia kuunganisha na kuvunja mpaka kati ya kweli na uongo, ndoto na urazini, uhai na kifo, sasa na zamani (usasa na ukale), utoto na utu uzima na mbali na karibu. Kwa maana hiyo lengo la uhalisiamazingaombwe katika fasihi ni msisitizo wa umoja kati ya mazingaombwe na uhalisia.

1.8.1.3 Matukio Yanakosa Mtiririko wa Kawaida

Wasanii hutumia mtindo wa ukumbushaji, mbinu rejeshi na ujenzi wa wahusika wenye nafsi mbili (nafsi tulivu na nafsi inayotembea ndotoni kichawi na kimazingaombwe). Pia mazingira hupewa kipaumbele na viumbe wa ajabuajabu kama mazimwi, mashetani, mizuka, mizimu, majini pamoja na misitu mikubwa, wanyama, mito na bahari hurejelewa. Na baadhi ya tanzu za fasihi simulizi kama visasili, istiara na hurafa hutumika kwa kupeleka hadhira katika safari ya hali na matukio ya kweli na yanayowezekana. Mhimili huu ni faafu kwa sababu umeuwezesha utafiti huu kuchungunguza mazingira ya kuogofya, viumbe wa ajabu na wa kufikirika kama mazimwi, malaika, majini na mashetani kama watu wa kawaida wanaopatika katika mazingira halisi katika jamii.

1.8.1.4 Uvunjivu wa Kaida za Uasilia na za Uhalisia

Hakuna mpaka kati ya jamii na jamii, nchi na nchi au mbali na karibu, kaida za uasilia na za uhalisia huvunjwa, hivyo, binadamu anaweza kujibadilisha sura na kuwa kitu kingine, kuingia popote bila kizuizi, kuzungumza na viumbe wengine na kufa na kuishi kwa wakati mmoja. Wana uhalisiamazingaombwe hushughulikia masuala ya ulimwengu kwa upana wake bila kujifunga katika mazingira finyu kama vile jamii, taifa au bara moja. Mhimili huu umetumika hasa katika kuchunguza mawazo yaliyoibushwa na waandishi wa riwaya teule ambayo hayakufungamana na utamaduni wa jamii finyu kama masuala ya kisiasa, kiuchumi na ya kidini.

1.8.1.5 Wakati na Mahali Vina Uhusiano wa Kiduara na si wa Kiufuatano

Mhimili huu unasisitiza kuwa jambo linaweza kutokea wakati mmoja, ambalo linaweza lisiwe la kwanza, na kuweza kujirudia pahali pengine kwa namna nyingine. Mhimili huu ni faafu kwa sababu wakati na muda wa matukio katika vipengele fulani katika baadhi ya riwaya teule hautabiriki, kuna mduara mkubwa na unaomchanganya msomaji wa riwaya hizo. Hii ni kwa sababu nyakati zote, yaani wakati wa kiufuatano, wakati tuamavu na wakati wa kiduara zinaweza kujitokeza katika riwaya moja na kwa wakati moja. Hivyo, kwa kutumia mhimili huo utafiti umezingatia zaidi ujumbe uliokusudiwa na mwandishi katika uduara, utuamavu na ufuatano huo wa wakati.

1.8.2 Nadharia ya Kiwewe cha Kuathiriwa

Kiwewe cha kuathiriwa ni nadharia inayotumiwa kuelezea sifa za sanaa, muziki, siasa, falsafa na fasihi. Nadharia hii hutilia mkazo na kutukuza mtu binafsi katika

ngazi za kijamii, kisiasa na kiakili. Sifa hii inajitokeza katika fasihi kwa msisitizo mkubwa kwenye mada zinazoakisi uwiano wa kibinadamu pamoja na uhuru wa kujieleza kibinafsi kwa mitindo na mikabala yao (Bloom,1973; Brahms, 1988; Wamitila, 2003).

Harold Bloom aliibuka na nadharia hii mwaka 1973 baada ya kuonekana uwepo wa utata wa kimahusiano kati ya waandishi wakongwe wa kazi za fasihi na waandishi wapya hasa katika ‘Utanzi wa Ushairi’. Waandishi wapya walionekana kukabiliwa na kiwewe cha kuathiriwa na kazi za watangulizi wao na hivyo kazi zao kuonekana dhaifu na kutothaminiwa. Hivyo, kuzidi kuwa na kiwewe kuwa kazi zao haziwezi kudumu au kutambulika hata kwa kizazi kimoja. Hali hii ilimlazimu Bloom kujaribu kuchunguza mchakato ambao umewawezesha waandishi wengi mashuhuri wa kazi za fasihi kutoa kazi za msingi licha ya kuwepo kwa nguvu ya kuathiriwa na kazi za waandishi tangulizi. Katika uchunguzi wake aligundua kuwa katika uandishi wa kazi za fasihi, karibu waandishi wote wameathiriwa kwa namna moja au nyingine na waandishi tangulizi. Katika kitabu cha *The Anxiety of Influence* (1973) anasema kuwa hii hutokea kwa sababu waandishi wa kazi za fasihi huvutiwa kuandika kwa kusoma kazi za waandishi tangulizi na hivyo huwa na hatari ya kuathiriwa. Anasema kuwa hata mwandishi mashuhuri wa kazi za fasihi William Shakespeare katika kazi zake za mwanzo aliathiriwa kwa kiasi fulani na Christopher Marlowe. Bloom anasema kuwa kuna hatua (mihimili) sita ambazo mwandishi fuatishi hupitia ili kutoa kazi bora. Hatua hizo ni:

1.8.2.1 Kusoma na Kuvutiwa na Kazi

Kabla ya kuandika kazi yenye kuathiri ni lazima msanii asome na kuvutiwa na kazi au mwandishi wa kazi tangulizi. Kuathiriwa au ushawishi huo unakuwa mkubwa kiasi kwamba msanii fuatishi huandika kwa namna inayokaribia kuwa sawa na msanii tangulizi, ila kufikia hatua fulani anachepuka na kuonekana kuwa msanii tangulizi alikuwa na ushawishi mpaka kiwango fulani au katika vipengele fulani. Kutoka hapo mwandishi fuatishi huandika kwa namna na mtindo wake ingawa bado kwa juu juu au kidogo kidogo bado anaonekana kuathiriwa na msanii tangulizi.

1.8.2.2 Kumwiga

Bloom anasema kuwa kwa kuiga, msanii fuatishi huendeleza mada na mawazo ya msanii tangulizi lakini siyo kwa mwigo sisizi bali anayakamilisha kwa namna nyingine inayoonesha kuwa msanii tangulizi inawezekana alishindwa kuyakamilisha. Hapa msanii fuatishi mara nyingi anatumia “tabaini” kuendeleza mawazo hayo ya msanii tangulizi.

1.8.2.3 Upotoshaji

Hapa msanii fuatishi hujaribu kujiengua kutoka kwa athari za msanii tangulizi kwa kutumia mbinu za kiisimu ili kuleta athari au fikra mpya katika kazi za fasihi kwa kujitenga na athari za msanii tangulizi. Msanii fuatishi hufanya hivyo kwa kutumia mbinu tano za upotoshaji za kiisimu ambazo ni: udondoshaji, uhamishaji, udunishaji, ujalizaji na ugeuzaji.

1.8.2.4 Kubadili Mada

Bloom anasema kuwa hapa msanii fuatishi anajitahidi kubuni kwa ufundi wa hali ya juu mada nyingine tofauti kabisa na mada ya msanii tangulizi. Msanii fuatishi anafanya hivyo kwa kujitahidi kujitenga au kuachana na mada ya msingi ya msanii tangulizi ili kuonesha dhahiri kuwa kazi yake ina nguvu kuliko ya mtangulizi wake. Lengo la msanii fuatishi likiwa ni kujijengea utukufu au jina binafsi mbali na msanii tangulizi.

1.8.2.5 Upekee na Uasilia

Hapa mwandishi fuatishi hujitenga kabisa na namna ya uandishi wa msanii tangulizi na hata namna yake mwenyewe. Lengo la msanii fuatishi hapa ni kujitenga na aina yoyote ya mabaki au masalio (masazo) ya athari kwa nia ya kuwa na uhuru kamili au mafanikio binafsi.

1.8.2.6 Kufufuka kwa Kazi

Hapa mwandishi baada ya kuelemea na hali ya upekee wa uandishi, kazi yake sasa inakuwa wazi kwa uhakiki na uchunguzi na kuwa na nguvu kuliko kazi ya msanii tangulizi kiasi cha kazi ya msanii tangulizi kusomwa au kuhakikiwa kwa kutumia kazi ya msanii fuatishi. Kazi za msanii tangulizi zinaonekana kuwa sasa zinaathiriwa na kazi za msanii fuatishi. Hapo ndipo dhana ya kufufuka au kuzaliwa kwa kazi inapojitokeza. Hii hutokana na hali ya msanii fuatishi kuwa na hamu ya kutunga kazi yenye kiwango cha juu kuliko kazi zile za msanii tangulizi.

Mawazo ya msingi ya nadharia ya Kiwewe cha Kuathiriwa ni pamoja na: kila kazi ya sanaa iliyotangulia lazima iwe na mchango wa aina fulani katika

kupatikana kwa kazi za sanaa zinazofuata. Kazi nzuri ya sanaa ni ile inayozingatia upekee na uasilia na wala si ile yenye mwigo sisisi wa kazi tangulizi. Kazi za sanaa huigwa au hutafsiriwa, haziundwi hivyo hakuna awezaye kuunda au kuzaa kazi mpya ya sanaa. Hata hivyo uwazaji au utafutaji wa namna ya kazi za sanaa ni sawa na kuiunda kazi nyingine.

Kutokana na hatua sita ambazo mwandishi wa kazi za fasihi hupitia ili kutoa kazi yenye kushawishi na misingi ya nadharia ya Kiwewe cha Kuathiriwa zilizelezwa hapo juu, nadharia hii imetumiwa katika utafiti huu kulinganisha na kulinganua kazi za Shaaban Robert na za Euphrase Kezilahabi. Katika kufanya ulinganisho na ulinganuzi huo kati ya waandishi teule, Shaaban Robert ametumiwa kama mtangulizi na Kezilahabi kama mfuasi. Hivyo, katika kulinganisha na kulinganua kazi zao mambo ya muhimu yaliyozingatiwa kama anavyobaini (Maho, 1999) ni: ubainishaji wa sampuli ya vitu vya kulinganisha, ufafanuzi wa dhana inayolinganishwa, ukusanyaji wa data, ubainishaji wa kanuni za ulinganisho na ulinganuzi, ubainishaji wa ulinganisho na ulinganuzi wenyewe na ufafanuzi wa matokeo ya ulinganisho.

Hatua namba moja na namba mbili hapo juu zimetumika kuchunguza matumizi ya uchawi na mazingaombwe ambapo Euphrase Kezilahabi amemwiga Shaaban Robert moja kwa moja yaani kwa kuandika kwa namna inayofanana au kwa kuendeleza mada au mawazo ya Shaaban Robert. Kwa kufuata hatua namba tatu, utafiti umechunguza kama Kezilahabi amejaribu kujiengua kutoka kwa athari za Shaaban Robert kwa kujaribu kudondosha, kuhamisha, kudunisha, kujaliza, au kugeuza baadhi ya vipengele vya uchawi na mazingaombwe vilivyotumiwa na Shaaban Robert. Kwa kutumia hatua namba nne na namba tano, utafiti

umechunguza kama Kezilahabi anaandika mada tofauti na ya kipekee juu ya uchawi na mazingaombwe, tofauti kabisa na Shaaban Robert. Na kwa kutumia hatua namba sita, utafiti umechunguza kama kazi za Kezilahabi juu ya uchawi na mazingaombwe zina nguvu na mvuto mkubwa kuliko za Shaaban Robert na kufikia hatua kazi za Shaaban Robert kuhakikiwa kwa kutumia kazi za Kezilahabi.

Kwa kufuata hatua hizo sita kazi hii imefanikiwa kuchunguza iwapo Shaaban Robert na Euphrase Kezilahabi wanawiana na kutofautiana katika matumizi ya mbinu ya uchawi na mazingaombwe katika riwaya zao teule.

1.9 Mbinu za Utafiti

Mbinu za utafiti ni njia mbalimbali zinazotumiwa na mtafiti ili kupata taarifa sahihi juu ya suala analolichunguza. Mbinu za utafiti hujumuisha: muundo wa utafiti, mahali pa utafiti, uteuzi wa sampuli, ukusanyaji na uchanganuzi wa data pamoja na mbinu za kuwasilisha matokeo ya utafiti.

1.9.1 Muundo wa Utafiti

Muundo uliotumiwa katika utafiti huu ni wa kimaelezo. Utafiti wa kimaelezo ni mtazamo ambao huchunguza sifa zinazobainika katika jambo linalochunguzwa. Kusudi lake lilikuwa ni kuchunguza jinsi mambo yalivyo katika mazingira fulani. Lengo kuu la kutumia muundo huu lilikuwa ni kukusanya data na kueleza uhusiano wa vipengele mbalimbali vya data hiyo. Kwa kutumia muundo huu matumizi mbalimbali kuhusu uchawi na mazingaombwe kutoka riwaya teule na katika jamii husika yalipitiwa. Mwisho, maelezo juu ya utafiti kwa ujumla yametolewa.

1.9.2 Kundi Lengwa

Kundi lengwa katika utafiti huu ni riwaya za *Adili na Nduguze* (1952), *Kusadikika* (1951) na *Kufikirika* (1946) za Shaaban Robert pamoja na *Nagona* (1990) na *Mzingile* (1991) za Euphrase Kezilahabi.

1.9.3 Mahali pa Utafiti

Utafiti huu ulifanyika maktabani na nyanjani. Maktabani, utafiti wa kina ulifanyika kwa kudurusu vitabu, makala na majarida mbalimbali pamoja na magazeti na katika mtandao. Aidha, data kutoka riwaya teule za Shaaban Robert na za Euphrase Kezilahabi pamoja na machapisho na tasnifu zilizotangulia pia zilisomwa. Lengo lilikuwa ni kupata taarifa za kina kuhusu masuala ya uchawi na mazingaombwe pamoja na nadharia zilizotumika katika utafiti huu.

Utafiti wa nyanjani ulifanyika katika mkoa wa Tanga na kisiwa cha Ukerewe. Maeneo hayo yaliteuliwa kwa sababu iliyofafanuliwa awali kuwa mkoa wa Tanga ni mazingira asilia alikozaliwa Shaaban Robert na kisiwa cha Ukerewe pia ni mazingira asilia alikozaliwa Euphrase Kezilahabi. Mtafiti alizuru mazingira asilia ya watunzi wa riwaya teule ili kuhojiana na wenyeji 20 wenye umri wa miaka kuanzia 60 na kuendelea (kwa upande wa Shaaban Robert), pia wenyeji 20 wenye miaka 60 na kuendelea (kwa upande wa Kezilahabi).

Ilitarajiwa na mtafiti kuwa wazee wenye miaka 60 na kuendelea wanataarifa nyingi zinazohusiana na uchawi na mazingaombwe zaidi ya vijana. Sababu hasa ya kufanya hivyo ilikuwa ni kutaka kulinganisha kama matumizi ya uchawi na mazingaombwe yanayopatikana katika riwaya teule yanahusiana na hali ilivyo katika mazingira asilia ambako ndiko chimbuko la watunzi wa riwaya hizo au

hakuna uhusiano wowote au kuna tofauti kulingana na mabadiliko kiwakati. Kwa hiyo, mtafiti alizuru mkoa wa Tanga alikozaliwa Shaaban Robert na kisiwa cha Ukerewe alikozaliwa Euphrase Kezilahabi. Changamoto ilikuwa kuwapata wazee wenye miaka 60 na kuendelea hasa upande wa Shaaban Robert. Hata hivyo, maelezo kutoka kwa jamaa wa karibu katika ukoo wa Shaaban Robert na mahojiano na wazee wa mkahawani karibu na Machui hospitalini yalitua changamoto hiyo.

Mkoani Tanga maeneo yaliyoteuliwa ni Machui Kibambani, Machui Hospitalini, Chumbageni, Neema na Tanga mjini katika ofisi ya mkuu wa mkoa. Maeneo hayo yaliteuliwa kimaksudi kwa sababu ya uwezekano mkubwa wa upatikanaji wa data zinazohusiana na utafiti huu. Shaaban Robert alizaliwa Machui Kibambani na wengi katika ukoo wake wanaishi Machui Kibambani. Mtafiti baada ya kufika Machui Kibambani alielekezwa kuwa baadhi ya wazee wenye umri wa miaka sitini na wenye kufahamu masimulizi mengi ya uchawi na mazingaombwe wanapatikana Machui Hospitalini. Pia alielekezwa kuwa matukio mengi yanayohusiana na uchawi na mazingaombwe yanapatikana Chumbageni. Aidha, alielezwa na Ikibali, mtoto wa Shaaban Robert kwenda mtaa wa Neema kumhoji Hatibu Kibwana. Hatibu anafahamu habari zote za ukoo wa Shaaban Robert na ndiye kiongozi wa shughuli za ibada za asili za ukoo huo. Zaidi ya yote, katika ofisi ya mkuu wa mkoa wa Tanga kuna kitengo maalum kinachoshughulika na nyaraka zenye matukio ya asili ya jamii za mkoa wa Tanga. Hivyo, maeneo hayo yalikuwa mwafaka kwa ajili ya hupatikanaji wa data kwa ajili ya utafiti huu.

Kisiwani Ukerewe, maeneo yaliyoteuliwa ni kata ya Namagondo, Nansio mjini na eneo la jiwe la Nyabulebeka katika kisiwa cha Ukara. Maeneo hayo yaliteuliwa kimaksudi baada ya mtafiti kufika kijijini Namagondo nyumbani kwao Euphrase Kezilahabi. Mtafiti alielekezwa na mtendaji wa kata ya Namagondo mji wa Pantaleo Nagano ambaye ni kaka yake Kezilahabi. Pantaleo ndiye aliyemwelekeza mtafiti kwa watu wengine ambao wangempatia taarifa zaidi. Watu hao ni pamoja na Erenestina Nakahozya, ambaye ni dada yake Kezilahabi na Veneranda Muyanga ambaye ni binti yake Pantaleo Nagano. Erenestina na Veneranda wanaishi Nanzio mjini. Pia Veneranda Muyanga ndiye aliyemwelekeza mtafiti kwa Kakulu Makorokoto. Kakulu anaishi katika kisiwa kidogo cha Ukara na ndiye mrithi, msimamizi na mchezeshaji wa jiwe la Nyabulebeka. Hivyo, kila mtafiti alivyokuwa akihojiana na mtafitiwa mmoja, mtafitiwa huyo alimwelekeza kwa mtafitiwa mwingine mpaka alipofanikiwa kupata data zote alizohitaji.

1.9.4 Uteuzi wa Sampuli

Utafiti ulitumia mtindo wa sampuli lengwa na mbinu ya usampulishaji iliyotumika ni mbinu ya kimaksudi. Sampuli lengwa hufaa kadhia zinazopatikana katika makundi au sehemu inayoaminika kuwa ina data mwafaka inayofaa malengo ya utafiti. Hii inamaanisha kuwa kilichozingatiwa ni kama sampuli yenyewe ilimwezesha mtafiti kupata data za kutosha iliyomwezesha kushughulikia kikamilifu suala lake la utafiti (Kombo na Tromp, 2006; Lune, 2010; Ngugi, 2014).

Sampuli iliyotumika katika utafiti huu ni ya kutoka riwaya teule na ya kutoka nyanjani. Riwaya zilizoteuliwa ni *Kufikirika* (1946) *Kusadikika* (1948) na *Adili na Nduguze* (1952) za Shaaban Robert na *Nagona* (1990) na *Mzingile* (1991) za Euphrase Kezilahabi. Riwaya hizo ziliteuliwa kimakusudi baada ya usomaji wa awali wa riwaya zote za waandishi tajwa. Mtafiti alisoma riwaya zote za waandishi hao na kubaini kuwa zilizoteuliwa ndizo zenye data toshelevu za uchawi na mazingaombwe na kwa kuzingatia vipindi tajwa. Kwanza, Shaaban Robert alizaliwa na kuandika riwaya zake kabla ya kipindi cha usasaleo katika fasihi ya Kiswahili. Hivyo, riwaya zake zilizoteuliwa zilikuwa na data toshelevu zinazohusu uchawi na mazingaombwe zenye mwelekeo wa kifasihi simulizi kama vile visasili, istiara na hurafa. Kwa upande mwingine Euphrase Kezilahabi ameandika riwaya nyingi zilizosheheni matukio ya uchawi na mazingaombwe. Hata hivyo, riwaya zake za mwanzo ingawa zina matukio ya uchawi na mazingaombwe, ziliandikwa kabla ya usasabaadaye katika fasihi ya Kiswahili. Kutokana na kubadilisha uandishi wake na kwa kuzingatia malengo ya utafiti huu, riwaya zake za *Nagona* na *Mzingile* ndizo zilizoandikwa kwa mtazamo wa usasabaadaye, na ndizo zenye data toshelevu za uchawi na mazingaombwe zilizosadifu ulinganisho dhidi ya zile za Shaaban Robert zilizoteuliwa. Riwaya hizo kwa pamoja zimesheheni matumizi ya uchawi na mazingaombwe kama vile: wahusika wa kichawi na wa kimazingaombwe, matukio ya ajabuajabu, uvunjivu wa kaida za uhalisia pamoja na matumizi ya visasili na istiara.

Kutoka nyanjani kulikuwa na sampuli ya kimaeneo, sampuli ya wenyeji wenye umri wa miaka 60 na kuendelea na sampuli ya visa na matukio ya uchawi na mazingaombwe. Kutoka maeneo ni mkoa wa Tanga na Kisiwa cha Ukerewe

ambapo sampuli ya wenyeji 20 wenye umri wa miaka 60 na kuendelea walihusishwa. Wenyeji 20 wenye miaka 60 walioteuliwa ni wale waliofikiriwa kuwa na huelewa kuhusu matukio na visa vya uchawi na mazingaombwe vinavyohusiana na jamii yao. Mkoa wa Tanga na Kisiwa cha Ukerewe ziliteuliwa makusudi kwa sababu ni maeneo walikozaliwa waandishi wa riwaya teule, na hivyo data zinazowahusu waandishi hao zilipatikana huko kwa urahisi zaidi. Pia wenyeji wenye miaka 60 na kuendelea walifikiriwa kuwa na ufahamu au maelezo zaidi ya uchawi na mazingaombwe kuliko wenye miaka chini ya hapo. Hata hivyo, baada ya mtafiti kufika nyanjani kuna data zilizopatikana kwa wenyeji wenye umri chini ya miaka 60 waliokuwa na ujuzi na uelewa mpana kuhusu uchawi na mazingaombwe katika jamii husika. Kwa hiyo, licha ya kigezo cha umri, mtafiti alizingatia upatikanaji wa data ya kuaminika na inayosadifu malengo ya utafiti huu. Zaidi ya yote, sampuli ya matukio na visa vya uchawi na mazingaombwe vilivyohusishwa katika mahojiano ni matukio ya uchawi na mazingaombwe, wahusika wa ajabuajabu, uvunjivu wa kaida za uhalisia na za uasilia pamoja na visasili na istiara.

1.9.5 Ukusanyaji wa Data

Mbinu tatu zilitumika kukusanya data kutoka maktabani na kutoka nyanjani katika utafiti huu. Mbinu hizo ni upitiaji wa nyaraka, usaili na ushuhudiaji. Mtafiti alisoma riwaya teule ili kubainisha na kuorodhesha vipengele vinavyohusiana na uchawi na mazingaombwe vilivyokuwa vikitafitiwa. Vipengele hivyo ni wahusika wa ajabu, matukio ya ajabuajabu, uvunjivu wa kaida za uhalisia na za uasilia pamoja na visasili na istiara. Nyanjani Mtafiti alionana ana kwa ana na watafitiwa na kuwauliza maswali yanayohusiana na data

husika za utafiti huu. Kisiwani Ukerewe mtafiti alifanikiwa kukutana ana kwa ana na wasailiwa 20 na kuhojiana nao juu ya masuala yanayohusiana na uchawi na mazingaombwe. Aidha, mtafiti alifanikiwa kufika kisiwa cha Ukara na kushuhudia maajabu ya Nyabulebeka (jiwe linalocheza).

Mkoani Tanga, mtafiti alifanikiwa kukutana ana kwa ana na wasailiwa 19 kati ya 20 aliotarajia kuhojiana nao. Msailiwa mmoja (Ikibali Shaaban Robert), alikuwa safarini Dar es Salaam. Hata hivyo, mtafiti alihojiana naye kwa njia ya simu. Aidha, mtafiti alitembelea kisiwa cha Chumbagama ili kushuhudia mahali ukoo wa Shaaban Robert wanapofanyia ibada za kutoa kafara kwa majini. Zaidi ya hapo, mtafiti alitembelea mawe mawili ya Jafari Kibwana yaliko ndani ya bahari ili kushuhudia maajabu ya mawe hayo, kwani yakipigwa picha hayapigiki.

Lengo la mtafiti kufanya mahojiano na ushuhudiaji katika mazingira asilia ya watunzi wa riwaya teule lilikuwa ni kutaka kuhakikisha kama kuna uhusiano kati uchawi na mazingaombwe uliotumiwa katika riwaya teule na hali halisi katika mazingira asilia ya watunzi husika. Mohamed akinukuliwa na Senkoro (1995: 86) anakiri kuwa hakuna ubunifu ambao hautegemei mambo yaliyomo kwenye uzoefu na mazingira yaliyomzaa na kumlea msanii. Anasema:

Hakuna ubunaji ambao hautegemei mambo yaliyomo kwenye uzoefu na tajriba zetu au za jamii zetu. Ubunaji hautokani na hali tupu (ombwe), bali unatokana na hali halisi, hali ya mambo ambayo msanii ameyaona, ameyasikia, ameyanusa, ameyaonja, ameyahisi au ameyasoma pahali. Kwa kutumia kipawa chake cha kubuni msanii atayafinyanga upya mambo hayo ili kuunda umbo la kisanaa.

Mawazo hayo ya Mohamed kuwa ili msanii aweze kubuni kazi yake kuna masuala yaliyoko katika jamii yaliyomgusa, yakamtekenya na kumshawishi

kuyazungumzia kwa namna ya ubunifu wa pekee, yanakubaliana na Senkoro (1995:87) anayesema kuwa:

Ubunifu unatokana na uhalisi, bila kuwepo kwa uhalisi wa mazingira yaliyomzaa na kumlea msanii hakuna ubunifu. Ndiyo maana tunaweza kusema kuwa ubunifu ni uwezo wa kuunda dunia mpya kutokana na dunia tuliyomo, ni uwezo wa kuanzisha kitu ambacho hakipo kabisa kutokana na kitu ambacho tayari kipo.

Mahojiano yalifanyika kwa kufuata maswali yaliyotayarishwa juu ya uchawi na mazingaombwe (taz. kiambatisho A, uk. 349). Mahojiano hayo yote yalirekodiwa kwa ajili ya uchanganuzi.

1.9.6 Uchanganuzi wa Data

Mtafiti alipitia hatua mbalimbali katika uchanganuzi wa data. Katika hatua ya kwanza, mtafiti alihariri masimulizi juu ya uchawi na mazingaombwe yaliyopatikana nyanjani kwa kuyaweka katika maandishi. Hatua ya pili, mtafiti alichambua masimulizi hayo ya uchawi na mazingaombwe kwa kuyagawa katika makundi anuwai. Mtafiti aligawanya masimulizi hayo katika makundi makuu manne yafuatayo: masimulizi juu ya wahusika wa ajabu, matukio ya ajabuajabu, uvunjivu wa kaida za uhalisia na za uasilia, pamoja na masumbulizi yanayohusiana na visasili na istiara. Aidha, baada ya mgawanyo huo, katika hatua ya tatu, mtafiti alitafsiri data kwa kuhusisha malengo na maswali ya utafiti. Katika hatua hii, kila lengo na swali lake lilitafutiwa data zinazolitimiza na kujibu swali lake. Mwisho, data zilizopatikana nyanjani katika mazingira asilia ya Shaaban Robert na ya Euphrase Kezilahabi zililinganishwa na data zilizotokana na usomaji wa riwaya teule za watunzi hao ili kupima na kutathmini athari ya mazingira asilia ya mtunzi katika matumizi ya uchawi na mazingaombwe katika riwaya teule. Uchanganuzi huo uliohusisha ubainishaji, ulinganishaji na

ulinganuzi ulifanywa kwa kuegemea mihimili ya nadharia ya uhalisiamazingaombwe na kiwewe cha kuathiriwa.

1.9.7 Mbinu za Kuwasilisha Matokeo

Data yote iliyokusanywa na kuchanganuliwa imewasilishwa kwa njia ya maelezo na ufafanuzi kwa maandishi.

1.9.8 Maadili ya Utafiti

Maadili ya utafiti ni uwajibikaji na uelekevu kitabia kuhusiana na wale wote tunaotangamana nao katika utafiti, uwelekevu katika nia na malengo ya utafiti na jinsi ya kutumia matokeo kwa uadilifu ili yaweze kuwa na faida kwa jamii ya binadamu (Mathooko na Wenzake, 2007; Mukuthuria, 2009). Utafiti huu ulizingatia masuala yote ya maadili ya utafiti wa kitaaluma.

Kabla ya kuanza utafiti, mtafiti aliomba na kupewa kibali cha kufanya utafiti katika mikoa ya Tanga na Mwanza. Kwa mujibu wa sheria za utafiti nchini Tanzania kibali cha kufanya utafiti hutolewa na mamlaka husika katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Mtafiti aliwasilisha kibali kwa makatibu tawala wa mikoa hiyo ambao pia walitoa kipali cha kukusanya data katika maeneo mbalimbali ndani ya wilaya zilizohusishwa katika utafiti huu (nakala za vibali zimeambatishwa, taz. Kiambatisho B, uk. 351).

Vile vile, watoa taarifa wote walitoa taarifa kwa uhuru wao bila kulazimishwa na mtafiti. Hii ilifanyika baada ya mtafiti kuwaeleza sababu na malengo ya utafiti pamoja na utunzaji wa siri kwa taarifa ambazo watoaji hawakutaka majina yao

yatambulike kuwa taarifa hizo zimetoka kwao. Zaidi ya yote mtafiti alizingatia maadili ya kijamii ya watoa taarifa katika utafiti huu.

1.10 Kiishilio

Sura hii imefafanua vipengele muhimu vinavyohalalisha kufanyika kwa utafiti huu. Vipengele hivyo ni pamoja na usuli wa tatizo la utafiti, suala la utafiti, maswali na malengo ya utafiti, sababu za kuchaguliwa kwa mada ya utafiti, upeo na mipaka ya utafiti, yaliyoandikwa kuhusu mada, misingi ya nadharia pamoja na mbinu za utafiti.

Katika kupitia maandiko mbalimbali yanahusiana na mada ya utafiti huu, imebainika kuwa kuna historia ya muda mrefu ya kuwapo kwa matumizi ya uchawi na mazingaombwe katika jamii mbalimbali duniani. Matumizi hayo yamewashughulisha waandishi mbalimbali wa kazi za fasihi ikiwa ni pamoja na waandishi wa riwaya ya Kiswahili. Imedhihirika kuwa kuna utata mkubwa katika kueleza maana ya uchawi na mazingaombwe kama istilahi zinazojitegemea. Hii inatokana na kuingiliana kwa kiasi kikubwa kwa istilahi hizo katika matumizi. Mwingiliano huo unasababishwa na tofauti za kijamii, za kitamaduni, kidini na miktadha mbalimbali inayohusika katika matumizi ya istilahi: uchawi na mazingaombwe. Imebainika kuwa licha ya kuwepo kwa matumizi mengi sana ya uchawi na mazingaombwe katika riwaya za Shaaban Robert na za Euphrase Kezilahabi, lakini hakuna uchunguzi wa kina uliokwishafanywa ili kuweka bayana sababu zilizowasukuma waandishi hao kutumia kwa kiwango kikubwa uchawi na mazingaombwe katika kazi zao za sanaa. Ili kuziba pengo hilo utafiti ulijikita katika kuchunguza nafasi ya mazingira asilia ya watunzi hao katika

kutumia kwao uchawi na mazingaombwe katika riwaya zao teule za *Adili na Nduguze, Kusadikika, Kufikirika* na *Nagona* na *Mzingile*.

Nadharia za Uhalisiamazingaombwe na Kiwewe cha Kuathiriwa ndizo zilizotumiwa katika utafiti huu. Nadharia ya Uhalisiamazingaombwe imetumiwa kutokana na uwezo wake wa kuhakiki kazi za sanaa zinazokiuka kanuni au kaida za uhalisia wa kawaida unaofahamika. Kazi hizo, kwa mfano, zenye matumizi mengi ya uchawi na mazingaombwe haziwezi kuhakikiwa kwa kutumia nadharia za kihalisia na za kisayansi pekee bali kwa kutumia nadharia ya Uhalisiamazingaombwe. Nadharia ya Kiwewe cha Kuathiriwa imetumiwa kulinganisha na kulinganua athari ya mazingira asilia ya watunzi katika matumizi ya mbinu ya uchawi na mazingaombwe katika riwaya teule. Sura ya pili imebainisha matumizi ya uchawi na mazingaombwe katika mazingira asilia ya watunzi hao.

SURA YA PILI

UCHAWI NA MAZINGAOMBWE KATIKA MAZINGIRA ASILIA YA WATUNZI WA RIWAYA TEULE

2. 0 Utangulizi

Sura ya kwanza imeiwekea msingi utafiti huu. Imechunguza suala la utafiti, malengo ya utafiti, maandiko mbalimbali yanayohusiana na utafiti huu, na nadharia zilizoongoza utafiti huu pamoja na mbinu za utafiti. Maandiko yaliyopitiwa yameonesha kuwa hakuna utafiti wa kina ulioshafanyika kwa kutumia nadharia za uhalisiamazingaombwe na kiwewe cha kuathiriwa kuchunguza athari za mazingira asilia ya watunzi katika matumizi ya uchawi na mazingaombwe; unaolinganisha matumizi ya uchawi na mazingaombwe kati ya watunzi wawili tofauti katika fasihi ya Kiswahili.

Lengo la sura hii lilikuwa kubainisha hali ya uchawi na mazingaombwe katika mazingira asilia ya watunzi wa riwaya teule. Vipengele vilivyotarajiwa kubainishwa ni: matukio ya ajabuajabu, watu na viumbe wa ajabuajabu, uvunjivu wa kaida za uasilia na za uhalisia pamoja na visasili na istiara. Kusudi la kufanya hivyo lilikuwa ni kutaka kuthibitisha wazo la kuwa Shaaban Robert na Euphrase Kezilahabi wametumia mtindo wa uchawi na mazingaombwe katika riwaya zao teule kwa sababu ya kuathiriwa na mazingira yao asilia au la.

Data za sura hii zilitokana na mahojiano na wasailiwa kutoka nyanjani (mazingira asilia ya Shaaban Robert na ya Euphrase Kezilahabi). Wasailiwa walisimulia visa au matukio ya ajabuajabu yakiwa ni pamoja na watu au viumbe wanaotenda

mambo yasiyo ya kawaida ikiwa ni pamoja na kuvunja kaida za uhalisia pamoja na visasili na istiara. Sura hii imejenga msingi wa uchanganuzi katika sura zinazofuata, yaani sura ya tatu hadi ya sita. Hii ni kwa sababu wahusika wa kimazingaombwe, visa na matukio ya ajabuajabu, uvunjivu wa kaida za uhalisia pamoja na visasili na istiara vilivyoko katika mazingira asilia ya watunzi wa riwaya teule vimechunguzwa athari zake katika utunzi wa waandishi wa riwaya teule katika sura hizo.

Sura hii imegawanyika katika sehemu kuu mbili. Sehemu ya kwanza imebainisha watu na viumbe wanaofanya mambo ya ajabu, matukio ya ajabuajabu, uvunjivu wa kaida pamoja na visasili na istiara katika mazingira asilia ya Shaaban Robert. Sehemu ya pili nayo imebaini watu na viumbe wanaofanya mambo ya ajabu, matukio ya ajabuajabu, uvunjivu wa kaida za uhalisia pamoja na visasili na istiara katika mazingira asilia ya Euphrase Kezilahabi.

2.1 Uchawi na Mazingaombwe katika Mazingira Asilia ya Shaaban Robert

Kuna matumizi mengi ya uchawi na mazingaombwe yaliyotokea na mengine yanaendelea kutokea katika mazingira asilia aliyokulia Shaaban Robert. Matukio hayo yameelezwa hapa kwa njia ya visa vilivyotokea au kama matukio yaliyotendwa au kutendewa watu fulani katika mazingira asilia aliyozaliwa Shaaban Robert. Matumizi yanayojidhihirisha kwa kiwango kikubwa ni pamoja na watu na viumbe wanaofanya mambo ya ajabu, matukio ya ajabuajabu pamoja na uvunjivu wa kaida.

2.1.1 Uchawi na Mazingaombwe katika Ukoo wa Shaaban Robert

Ukoo wa Shaaban Robert na jamaa zake wa pande zote (yaani upande wa mama na upande wa baba) kwa ujumla wamegubikwa kwa kiasi kikubwa na matukio ya uchawi na mazingaombwe ikiwa ni pamoja na uaguzi, utabiri, kupiga ramli, sihiri na mwingiliano na majini. Karibu familia nzima ya kwao Shaaban Robert iliyokuwa inaishi Machui ilifahamu masuala ya uganga na hata uchawi na mazingaombwe kwa namna moja au nyingine. Kutokana na masimulizi aliyopata mtafiti nyanjani, hata Shaaban Robert mwenyewe, ingawa hakushughulika na uaguzi kwa sababu ya dini au kutokana na kukosa nafasi kwa sababu ya kazi yake serikalini, lakini kazi hii aliifahamu vizuri.

Mwishehe Ulenge, ndugu yake Shaaban Robert, mama mmoja baba tofauti; alimwendea Shaaban Robert na kumwomba amwagulie kama safari yake kwenda Unguja kutokea Tanga itakuwa shwari au itakuwa na nuksi. Shaaban alimwambia atandaze mikono yake mezani. Shaaban aliangalia mistari katika mikono yake na kutoa utabiri. Utabiri ulisema kuwa safari itakuwa salama wakati wa kwenda lakini wakati wa kurudi atapata taabu sana baharini. Shaaban pia alimwagulia kuwa katika maisha yake atachelewa sana kupata watoto.

Mwishehe alisafiri salama wakati wa kwenda. Wakati wa kurudi walipatwa na taabu sana na mtumbwi wao ulipasuka wakatumbukia baharini. Walikata tamaa ya kuishi ingawa waliokolewa mwishoni. Zaidi ya yote, Mwishehe hakupata

kuzaa watoto mpaka alipokuwa mzee ndipo alipofanikiwa kupata watoto. Hivyo, utabiri wa Shaaban Robert ukatokea vile vile alivyosema¹.

Kisa hiki cha Shaaban kumtabiria Mwishehe yatakayomtokea kwa kutazama alama kwenye mikono yake ni sawa na utabiri wa Mrefu kwa Mwelekevu katika riwaya ya *Adili na Nduguze*. Mrefu, kiumbe wa ajabu, alimtabiria Mwelekevu kuwa siku atakapoona mti wa mkomamanga umezaa matunda mawili ajue Adili, mwokozi wake amefika. Hilo ndilo lililomjulisha siku ile kuwa mgeni wake si mwingine ila Adili (*Adili na Nduguze*, uk. 30).

2.1.2 Watu na Viumbe wa Ajabu

Katika mazingira asilia ya Shaaban Robert kuna masimulizi mengi juu ya watu mbalimbali waliojijhusisha na matukio ya ajabuajabu ambayo si rahisi kufanywa na watu wa kawaida katika hali ya kawaida.

2.1.2.1 Kisa cha Mrefu

Inaelezwa na mzee Bakari Renge kuwa kijana mmoja kwa jina la Salehe Zongo alitoka kitongoji cha Mkindani, mahali ambapo sasa ni makaburi yao Shaaban Robert, kwenda Taviera. Njiani wakati anarudi nyumbani alimkuta mtu mrefu kupindukia amesimama njiani kwa kuziba njia kwa miguu yake. Urefu wake ulikuwa haukadiriki kwa sababu alishindwa kuona mwisho wa kimo chake.

Zongo alitimua mbio na kupitia chini ya magoti katikati ya mapaja ya jitu hilo refu kupindukia akipiga kelele na kilio cha woga kuelekea nyumbani. Alipiga

¹Utabiri wa Shaaban kwa Mwishehe ulielezwa tarehe 16/04/2019 na Jafari Mhunzi Kibwana, miaka 40, ni mjukuu wa Jafari Kibwana kaka yake Shaaban Robert

kelele akisema mrefu! mre-fu, m-re---fu nimemwona mre--fu. Alipiga teke mlango wa nyumba ya mama yake na kuingia nao ndani. Alifululiza na kujificha uvunguni mwa kitanda akiendelea na maneno yake: mrefu, mre—fu, nimemwona mrefu².

Mrefu, kiumbe wa ajabu aliyemwona Zongo ni sawa kabisa na Mrefu aliyetumiwa na Shaaban Robert katika Riwaya ya *Adili na Nduguze*. Hivyo, hapa Shaaban ametumia kisa cha Mrefu katika mazingira yake asilia katika riwaya ya *Adili na Nduguze* kwa mwigo sisisi. Bloom (1973) anasema, kazi ya sanaa huigwa, hakuna anayeweza kuunda kazi mpya ya fasihi. Ingawa Shaaban Robert katika *Adili na Nduguze* amelitumia jina la Mrefu vile vile lilivyotumika katika mazingira asilia, lakini maudhui na matendo ya mrefu wa hadithini na wa mazingira asilia ni tofauti.

2.1.2.2 Miujiza ya Kibwana Jafari

Tofauti na Shaaban Robert, matumizi ya uchawi na mazingaombwe pia yalionekana kwa mzee Kibwana Jafari mume wa kwanza wa binti Mwema Mwidau mama yake Shaaban Robert. Kibwana aliweza kujibadilisha sura mbalimbali, kuruka angani kwa ungo na kuwasiliana na majini. Mzee Kibwana Jafari aliweza kujibadilisha kama kinyonga kulingana na mazingira. Kama anataka kupita msituni palipo na wanyama wakali aliweza kujibadilisha simba ili kupita. Akitaka kuvuka mto mkubwa na unaoenda kwa kasi aliweza kujibadilisha mamba ili avuke.

²Mzee Bakari Renge, miaka 70. Ni mume wa Swaumu Mhunzi mjukuu wa Jafari Kibwana ambaye ni kakake Shaaban Robert (Utafiti, Aprili 2019).

Kibwana alikuwa anafahamu miti mbalimbali na magonjwa yanayoponywa na miti hiyo. Kwa mfano, akijiwa na mgonjwa, Kibwana alikuwa na uwezo wa kunusa harufu ya ugonjwa alionao mgonjwa wake na kuhusisha harufu hiyo na mti unaofaa kutibu ugonjwa huo. Aliweza kutafuta mti porini kwa ajili ya dawa kama atajiwa na mgonjwa hata usiku wa manane na kuupata kwa kunusa harufu yake. Alifahamu miti ambayo akiitafuna anaweza kujibadilisha kile alichotaka kuwa. Mara nyingine aliweza kujibadilisha na kutoonekana kabisa kama utatazama kwa kutumia macho ya kawaida.

Siku moja mzee Kibwana alitaka kutoka Taviera kwenda Pemba, akamwomba mwenye mtumbwi kumbeba bure bila malipo yoyote. Mwenye mtumbwi alikataa na mzee Kibwana akamwambia upende usipende utanipakia na tutakuwa pemba wote leo. Kwa vile kulikuwa na mtumbwi moja tu hapo ‘Taviera’, mwenye mtumbwi alisema kwa dharau, “We rudi tu nyumbani kwako hutapanda mtumbwi wangu”. Kibwana alijibu kuwa ingawa nina uwezo wa kwenda Pemba hata bila kutumia mtumbwi lakini sasa ni lazima nipande mtumbwi wako na nitakuwa wa kwanza kwa wote watakaopanda mtumbwi huu kukanyaga ardhi ya Pemba.

Safari ya kwenda Pemba ilianza bila Kibwana na mwenye mtumbwi akawa na uhakika kuwa Kibwana amebaki Tanga. Walipofika Pemba Kibwana aliinuka jirani kabisa na mwenye mtumbwi. Alipokuwa akimshangaa, Kibwana alisema “Asante sana kutufikisha salama”. Baada ya kusema hivyo, alishuka mtumbwini akiwa wa kwanza wakati wasafiri wengine wakiwa wameshikwa na mshangao.

Mzee Kibwana alikuwa na matukio mengi ya kichawi na kimazingaombwe kiasi cha kuwashangaza watu. Mara nyingine angeweza kuomba ashushwe katikati mwa bahari wakiwa safarini kwenda Pemba au Unguja kwa madai kuwa amefika mwisho wa safari yake na kituo chake ni hapo katikati mwa bahari. Wenye mtumbwi walipokataa aliweza kushuka kwa nguvu na kutembea juu ya maji bila kuzama na kisha kupotea machoni pao wasimwone tena. Mzee Kibwana aliweza, kwa mfano, kumwambia mtu achore mstari mbele yake ardhini kwa kutumia kijiti na kumwambia mtu huyo afumbe macho na kuruka mstari huo kwa kutaja mahali anapotaka kwenda. Kuruka tu mstari huo mhusika kwa dakika sifuri alijikuta amefika pale alipotaka kwenda hata kama ni mbali kiasi gani.

Kisa kingine cha mzee Kibwana Jafari ni cha usafiri wa ungo na kitanga. Ili kutumia usafiri huu ulifanyiwa uganga, kupewa dawa na kusomewa dua. Kabla ya kuanza safari unatakiwa kusoma dua kisha unafumba macho mpaka mwisho wa safari. Ukifungua macho katikati ya safari utapatwa na madhara makubwa ikiwa ni pamoja na kujikuta pale pale ulipoanzia safari au kuanguka kutoka angani na mara nyingine hata kufa. Kitu kingine cha kujiadhari ni kutonyeshewa hata na tone moja la mvua wakati wa safari hii ya kimazingaombwe.

Mzee kibwana kama mtaalamu na fundi wa mazingaombwe haya alisafiri mara kadhaa kutoka Tanga kwenda Kongo kwa kutumia usafiri huu. Alikuwa akitoka Tanga na kutua mikoa ya kati mwa Tanganyika na siku ya pili aliweza kuruka mpaka Kigoma na siku ya tatu alifika Kongo. Inasemekana alikuwa na uwezo wa kusafiri kwa siku moja au muda mfupi zaidi hadi Kongo, lakini kwa kuhofia

tofauti za hali ya hewa katika mazingira hayo tofauti; aliogopa kukutana na mvua angani na kujisababishia matatizo.³

Shaaban Robert ametumia visa na matendo ya Kibwana karibu katika riwaya zake zote teule. Katika *Adili na Ndunguze* ametumia visa vya jini, Huria binti Kisasi kujibadilisha kulingana na mazingira (*Adili na Nduguze*, uk.36,40) sawa kabisa na alivyo Kibwana katika mazingira yake asilia. Katika riwaya ya *Kufikirika* waganga wa mizizi kama alivyo Kibwana wa mazingira asilia ya Shaaban Robert; waliweza kunusa kama mbwa miti iliyotakiwa kwa kutibu ugonjwa fulani hata katika usiku wa manane maporini (*Kufikirika*, uk. 8). Na katika riwaya ya *Kusadikika* kama Kibwana alivyokuwa na uwezo wa kusafiri kimiujiza na kufika popote kwa muda mfupi ndivyo Ridhaa anavyoweza kufika mbinguni kimiujiza (*Kusadikika*, uk. 34)

2.1.2.3 Kisa cha Nondo Mla Vyote

Katika eneo linaloitwa kwa sasa Machui Hospitalini, aliishi mtu mmoja aliyetitwa Nondo. Nondo alijulikana kote kwa sifa ya kula kwa kupitiliza. Aliweza kula kilo 20 za wali, mikungu 10 ya ndizi, mbuzi mzima peke yake na kunywa ndoo 5 za maji mara moja bila kushiba. Nondo alikuwa na shamba kubwa alipokuwa akiitumikisha familia yake kulima kama watumwa. La ajabu mazao yote ya shamba yalipofika nyumbani Nondo alikuwa akitumia karibu asilimia 95 peke yake. Hata akiisha kula hivyo nyumbani kwake, lakini popote pale atakapokuta watu wakila, Nondo atavamia chakula hicho na kuwaacha waliokuwa wakila na njaa. Mwisho ilifikia hatua watu wakitaka kula walikuwa wakifunga milango.

³Jafari Mhunzi Jafari mjukuu wa Jafari Kibwana (Utafiti, Aprili 2019).

Watoto walifundishwa lugha mbalimbali za kuwaita baba zao wakiwa katika makusanyiko ya watu. Wengine walitumia maneno kama, “Baba kuku ametaga”. Hapo baba atafahamu kuwa anaitwa kula. Haya yote yalifanywa ili kumkwepa Nondo. Mwisho ilikuja kujulikana kuwa Nondo amerushiwa majini ya kula kupindukia⁴

Kisa cha Nondo mla vyote katika mazingira asilia ya Shaaban Robert ni sawa na kisa cha mfalme Jeta wa nchi ya Majuju katika riwaya ya *Kusadikika*. Tofauti kati ya visa hivi iko katika kiwango cha ulaji, aina ya vyakula na majukumu ya watu hao. Nondo ni mtu wa kawaida asiye na madaraka katika jamii anakula vyakula vya kawaida vinavyoliwa na binadamu ingawa ni kwa kiwango kikubwa tofauti na watu wengine. Jeta ni mfalme na anakula kila kitu: chuma, magogo, hata binadamu (*Kusadikika*, uk. 23). Hii inadhihirisha kuwa ingawa Shaaban Robert ameathiriwa na mazingira yake asilia kutumia kisa cha Nondo kwa kumpa jina la Jeta katika riwaya ya *Kusadikika*, lakini alikusudia kutumia kisa hiki kwa maana pana zaidi.

2.1.3 Matukio ya Ajabuajabu

Kuna matukio mengi ya ajabuajabu katika mazingira asilia ya Shaaban Robert ambayo ni ya kutisha na ya kuogofya. Kwa wenyeji wa mazingira hayo matukio hayo yanaonekana ni ya kawaida na ni matukio ya kila siku na hivyo yamekuwa sehemu ya mwono halisi wa maisha yao.

⁴wazee 6 wa Mkahawani karibu na Machui Hospitalini, miaka 60-85 (Mahojiano, Aprili 2019).

2.1.3.1 Kisa cha Mtu wa Bara Aliyemwoa Mdigo.

Kijana mmoja wa bara alienda kukaa Udigoni Tanga na kukubaliana kuoana na binti mmoja wa Kidigo wa kijiji cha Kwale. Taratibu zote za ndoa zilifanyika vizuri kwa ridhaa ya wazazi wa binti bila pingamizi lolote. Kijana alioa na kumchukua mkewe bara kwa wazazi wake. Kitendo hiki cha msichana huyu kuolewa na mtu wa bara hakikuwafurahisha vijana wa kidigo. Vijana hao walidai kuwa huyo jamaa wa bara ana nini cha kuwazidi kiasi cha kukubaliwa na huyo msichana na kuwaacha wao. Pia wasichana wa kijiji hicho wa Kidigo nao wakawa na wivu kuwa huyo msichana mwenzao ana uzuri gani kuwazidi kiasi cha huyo mtu wa bara kumwona yeye na kuwaacha wao. Vijana hao wa Kidigo wakapania kumshikisha adabu huyo mtu wa bara. Siku mmoja mtu huyo wa bara alimchukua mkewe wakarudi Kwale Tanga ili kuwasalimia wakweze. Vijana wale wa Kidigo walipomwona wakasemezana kuwa huo ulikuwa ni wakati mwafaka wa kumshikisha adabu mtu wa bara. Vijana hao wakaenda Machui kwa ‘mtaalamu’ ili awafanyie uchawi wapate kumfundisha mtu wa bara.

Siku ya pili mtu wa bara aliwaaga wakweze kwenda kumsalimia mjomba wa mkewe aliyeko kijiji cha Mtimbwani. Njiani alikutana na mwanamke aliyevaa baibui nyeupe. Mwanamke huyo alimsalimia kwa kutaja kabisa jina lake na kuonyesha kuwa anamfahamu wakati mtu wa bara hakumbuki popote alipowahi kukutana na mwanamke huyo. Mwanamke huyo alipopita hatua kama mbili hivi mtu wa bara akawaza kumtazama mtu ambaye amemsalimia vizuri tena kwa kumtaja kwa jina ili aweze naye kumwuliza jina lake na ni wapi wamewahi kukutana. Kugeuka, hakumwona mtu wala nyayo zake. Mtu wa bara alishikwa na wasiwasi na kujiuliza alikopotelea huyo mwanamke wakati eneo ni la wazi na

hakuchukua hata sekunde tano toka kusalimiwa na kupotea kwa huyo mwanamke. Akiwa katika mawazo hayo alihisi kizunguzungu na kupotelewa na fahamu.

Mtu wa bara alijikuta anarudiwa kidogo na fahamu akiwa porini chini ya mbuyu mkubwa. Hakujua hapo ni wapi na alifikafikaje hapo. Akiwa katika kuwaza na kuwazua ghafla alijitokeza yule mwanamke akamwamrisha amshike mkono. Mwanamke akaunyoshea mbuyu mkono wa kushoto na mbuyu ukapasuka na wakaingia ndani na mbuyu ukajifunga tena na mtu wa bara akapotelewa na fahamu tena. Aliporudiwa na fahamu alikuta wako katikati mwa bahari lakini juu ya maji. Mwanamke akamwambia apande mgongoni mwake kisha afumbe macho.

Alipoambiwa kufungua macho alikuta wako chini kabisa mwa bahari katika mji mkubwa na mzuri sana wenye watu wengi, watanashati na wanawake wazuri sana wanaoendelea na shughuli zao kama kawaida. Alikaribishwa na kupewa bakuli lililojaa damu ili anywe. Yule mwanamke aliyempeleka akamkataza asinywe. Wenyeji wakamuuliza kwa nini unakataa, akajibu kuwa huyu nimemleta ili ajionee tu maisha ya huku ili ajue kuwa dunia siyo tu ile anayoifahamu yeye. Wenyeji wakakasirika na kushika ulimi wa mtu wa bara na kuuvuta kwa nguvu tayari kuukata ili asije kuongea milele. Hapo napo mwanamke akamwokoza kwa nguvu waking'ang'aniana kisu na jitu la kutisha lililotaka kumkata ulimi. Aliokolewa kwa sharti kuwa asije kuyasema aliyoyaona huko chini ya bahari. Hata hivyo kwa kuona ukali wa kisu na jinsi ulimi wake

ulivyovutwa mtu wa bara alipotelewa na fahamu tena. Alizinduka akiwa chini ya mbuyu ule ule uliopasuka wakaingia na mwanamke wa ajabu.

Nyumbani kwa wakwe watu walikuwa wamekusanyika na taarifa za kupotea kwa mtu wa bara sasa ikiwa ni siku ya nne tangu aage kwenda kwa mjomba wa mkewe zikawa zimeenea kote. Watu walitawanyika kila kona kumtafuta. Akiwa chini ya mbuyu akili ilimrudia kidogo na kufikiria kutafuta popote penye njia wanayopita watu ili aweze kuwauliza njia ya kwenda kwa wakweze. Kwa bahati nzuri alifika njiani pale pale alipokutana na yule mwanamke.

Mtu wa kwanza kukutana naye alikuwa ni mjomba wa mkewe ambaye alikuwa pia katika kumtafuta. Alipopelekwa kwa wakweze alieleza habari yote ilivyokuwa mwanzo hadi mwisho. Wakamwambia ulichukuliwa na jini na kupelekwa ujinini. Baada ya kusimulia kisa chote alipelekwa kuoga katika bafu iliyokuwa mbali kidogo na nyumba. Akiwa bafuni alishtukia watu wasioonekana wanavuta ndoo na nguo alizokuwa ametundika bafuni. Alipiga kelele aking'ang'ania nguo zake lakini kabla ya wenyeji wake kufika watu hao wakaondoka mbio na nguo hizo.

Baba mkwe alipoenda Machui kwa mtaalamu au mganga aliwakuta vijana wawili wa kiume ndio nao wanafika kwa mganga wakiwa na nguo za mkwe wake mkononi. Sababu ya kuchukua nguo na kumfanyia vituko mtu wa bara

walipoulizwa wakajibu kuwa tulitaka kumwonyesha kuwa pwani si bara, wanawake wa pwani wana wenyewe⁵.

Kitendo cha mtu kunyooshea mti mkono nao unapasuka na watu kuingia kisha unajifunga sawia, kinafanana na kisa cha jini, Huria binti Kisasi kuelekeza kidole chini na ardhi kupasua na Huria kuingia ardhini (*Adili na Nduguze*, uk. 18). Visa kama hivi ni vingi katika mazingira asilia ya Shaaban Robert. Hivyo, Shaaban Robert kutumia visa vya uchawi na mazingaombwe katika riwaya teule ni kutokana na kuchota katika hazina ya mazingira yake asilia. Whimsatt na Beardsley (1946) wanasema kwamba, ubunifu chanzo chake ni uhalisia, na bila uhalisia wa mazingira yaliyomlea na kumkuza msanii hakuna ubunifu.

2.1.3.2 Kisa cha Dereva na Jini

Dereva mmoja alikuwa anaendesha gari na alipofika katika daraja karibu na gereza la Maweni alimkuta msichana mmoja na kumpakia katika gari lake. Msichana aliposhuka dereva alipomchunguza alishtuka kuona ana miguu kama kwato ya ng'ombe. Alipoendelea mbele alikutana na mtu waliyekuwa wanafahamiana naye na kumpakia vile vile. Katika kuzungumza, dereva akamwelezea kuwa alikuwa amempakia kwenye gari msichana ambaye alihisi ni jini kwa sababu alikuwa ana kwato kama ya ng'ombe. Yule mtu aliinua miguu akimwonyesha dereva kuwa alikuwa na kwato kama hizi zangu? Dereva alichanganyikiwa na ghafla huyo mtu akapotea. Kumbe alikuwa ni yule yule jini

⁵Muhamed Balozi Miaka 60, Masijala ofisi ya mkuu wa mkoa Tanga. Tarehe 26/04/2019

msichana ndiye alijibadilisha akachukua sura ya mtu anayemfahamu⁶. Kisa hiki ni sawa na visa vya jini, Huria binti Kisasi na jini, Hunde mfalme wa Ngazi kujibadilisha sura mbalimbali katika riwaya ya *Adili na Nduguze (Adili na Nduguze, uk. 18, 34, 40)*.

2.1.3.3 Kumgonga Jini kwa Baiskeli na Jini Kusonya

Katika mazingira asilia ya Shaaban Robert kuna matukio mengi ya ajabuajabu yanayofanywa na viumbe wanaoweza kujibadilisha sura mbalimbali. Miongoni mwa viumbe hao ni majini ambao wanaweza kujibadilisha na kuchukua sura ya binadamu au ya kiumbe kingine chochote.

Kisa kinasimuliwa na Shaaban Mwidau Ulenge cha kijana mmoja aliyekuwa akiendesha baiskeli kwa kasi sana kutoka Tanga Mjini kuelekea Machui. Alipofika karibu na mti mkubwa wa mbuyu uliokuwa kando ya barabara alitokewa ghafla na kiumbe mfano wa paka. Kwa kasi aliyokuwa nayo hakuweza kumkwepa wala kusimama. Alimgonga yule kiumbe na yeye kutupwa porini kando ya barabara. Kiumbe aliyegongwa alitoa sauti kali na kubwa kama radi. Sauti hiyo ilisikika na kutetemesha miji katika vitongoji vya karibu kama vile Neema. Sauti hiyo ilisikika mpaka Machui karibu kilomita 6 kutoka eneo la tukio.

⁶Jafari Mhunzi miaka 58, ni mjukuu wa Jafari Kibwana kaka yake Shaaban Robert (Utafiti, Aprili 2019).

Kwa vile sauti hiyo haikuwa ya kawaida watu wengi kutoka maeneo ya Neema na hata Machui walikimbilia eneo la tukio hili kujionea wenyewe. Walichoshuhudia ni shuka jeupe lililokuwa likipiga kelele huku likiruka huku na huku barabarani. Hata hivyo jini lenyewe lilikuwa halionekani. Walipotazama kando ya barabara walimwona mtu amelala chini na baiskeli imeanguka karibu yake. Mara wazee wakatambua kuwa kijana amemgonga jini, na jini litakapoamuka litataka kulipiza kisasi.

Wazee waliofika pale kwa sababu wengi wao walikuwa na utaalumu wa elimu ya majini, walisoma dua ya kuomba msamaha. Walimbembeleza jini kwa maneno ya upole ili amsamehe kijana. Walisema kijana huyo bado ni mtoto, hana jicho la tatu na hajui kitu chochote na pia hakumgonga kwa makusudi. Ghafla kilio cha jini kilikoma, shuka ikatulia. Ukaja upepo ukachukua na kupeperusha shuka kusikojulikana. Hiyo ilikuwa ni ishara kuwa kijana amesamehewa.⁷

Kisa kingine cha ajabu kinachotaka kufanana na cha kumgonga jini na baiskeli ni cha jini kusonya kinachosimuliwa na Hatibu M Kibwana. Ni tukio lililomtokea yeye mwenyewe, Hatibu. Hatibu alitoka Machui Vibambani kumsalimia mama yake bi Asha Jafari. Akiwa njiani kurudi nyumbani kwake, Neema, aliona moto ukiwaka karibu na mti mkubwa wa mwembe uliokuwa kama mita 30 kutoka nyumbani kwake. Moto ule ulikuwa ukiwaka lakini hakuna kilichokuwa kikiungua. Hatibu kwa sababu alikuwa na utaalumu au uchawi na mazingaombwe ya majini, akafahamu kuwa moto ule haukuwa wa kawaida bali ulikuwa ni jini.

⁷Shaaban Mwidau Ulenge, miaka 70, ni mjukuu wa Ulenge mume wa tatu wa mamake Shaaban Robert (Utafiti, Aprili 2019).

Hatibu akaanza kusoma dua ya kukemea majini. Jini likarusha kwa hasira cheche za moto ambazo hazikufanikiwa kumpata Hatibu kwa sababu Hatibu aliendelea kusoma dua kwa nguvu zaidi. Jini lilipoona kuwa linabughudhiwa lilisonya kwa hasira na kukatokea upepo na moshi mwingi uliopaa na kutokomea angani. Hatibu alipogeuka ili kuangalia upepo huo unavyopaa shingo lake likabaki hivyo hivyo limepinda upande.

Hatibu alifika nyumbani kwake shingo linauma, limepinda na anatembea upande upande. Mke wake alipomwona katika hali hiyo alimhimiza Hatibu waende hospitalini. Hatibu ingawa alikuwa na maumivu makali lakini alicheka kicheko cha kuonesha hali ya kutojali na ya kudharau maneno ya mkewe. Akajigeuza mwili wote kumtazama mkewe, akasema: si kila ugonjwa unapelekwa hospitalini, subiri nitawaita madaktari wangu sasa hivi.

Hatibu alinuiza maneno fulani yasiyoeleweka wala kusikika vizuri. Baada ya maneno hayo walijitokeza majini watano wenye sura zinazotisha na ndevu ndefu zinazovuta ardhi. Walimkandakanda na kugeuza shingo taratibu taratibu na baada ya muda mfupi Hatibu akawa sawasawa na maumivu yakakoma. Hatibu alijighamba kuwa hao majini watano ni walinzi wake imara na hakuna mtu anaeweza kumchezea. Akamtishia mtafiti kama anabisha au kama aamini basi awaite mara moja ili awaone. Mtafiti alibaki kucheka tu na kumwomba aeleze tukio lingine⁸.

⁸ Hatibu M Kibwana, miaka 75- ni Mjukuu wa Jafari Kibwana kakake Shaaban Robert. Ni mtoto wa Asha Jafari (Mahojiano, Aprili 2019).

Matukio yote mawili, la kumgonga jini kwa baiskeli na la jini kusonya yanafanana na tukio la kuwaka moto na kuwa majivu kwa jini, Hunde mfalme wa Ngazi katika riwaya ya *Adili na Nduguze*. Jinsi kijana alivyomgonga jini kwa baiskeli akidhani ni paka ni sawa na jinsi Adili alivyompiga kwa jiwe jini, Hunde mfalme wa Ngazi akidhani ni nyoka. Tofauti iko tu katika sababu za vitendo hivyo. Kijana alimgonga paka kwa bahati mbaya wakati Adili alimpiga nyoka kwa kukusudia kumwoka tandu. Katika kisa cha jini kusonya Hatibu anaona moto unaowaka bila kitu chochote kuungua. Moto huo ni jini. Katika riwaya ya *Adili na Nduguze* pia mwili wa nyoka unawaka moto na kuwa majivu. Hatibu katika kisa cha jini kusonya anapambana na jini (moto) kwa kufahamu wakati Adili anampiga jiwe jini (nyoka) bila kufahamu kuwa huyo ni jini. Visa hivi vinazidi kuthibitisha kuwa kuna uchawi na mazingaombwe katika mazingira asilia ya Shaaban Robert.

2.1.4 Uvunjivu wa Kaida za Uhalisia

Katika mazingira asilia ya Shaaban Robert kuna matumizi mengi ya uvunjivu wa kaida. Kuna mawasiliano kati ya watu na majini. Majini yanaongea na watu bila kizuizi cha tofauti ya lugha kati ya jini na binadamu. Pia majini au watu fulani wanaofanya matukio yasiyo ya kawaida kuweza kuingia mahali popote bila kizuizi chochote. Kwa mfano, kuingia ndani ya nyumba hata kama milango imefungwa.

2.1.4.1 Uvunjivu wa Kaida na Kisasili cha Mawe Mawili ya Jafari Kibwana Pamoja na Sherehe za Mwaka Chumbagama

Mtu mwingine aliyejikusisha na uchawi na mazingaombwe katika familia yao Shaaban Robert ni Jafari Kibwana. Jafari Kibwana ndiye mtoto wa kwanza kwa

mamake Shaaban Robert. Jafari alikuwa mganga na aliwafuga majini. Majini hao walikuwa wakimpa taarifa ya mambo mbalimbali na madawa yanayofaa kutibu magonjwa mbalimbali. Majini baada ya kumpa Jafari taarifa ya mambo fulani yanayoweza kutokea, yeye naye aliwaelezea wananchi. Aliweza kuwaambia watu, kwa mfano, kesho msiende pwani kuvua au kuogelea kwa sababu kutakuwa na kimbuga au watoto wasiende porini kutakuwa na mnyama mkali.

Kuna kisa cha watu wawili walioenda kuvua baharini siku ya Idi ingawa Jafari alikataza siku hiyo watu wasiende kuvua. Alikataza kwa sababu aliishatabiri kuwa kutakuwa na tukio baya baharini siku hiyo. Alisema watu wakienda kuvua siku hiyo kuna hatari ya kuzama na kufa. Matokeo yake watu hao walipokuwa wakivua karibu na mawe fulani mawili makubwa walizama na hawakupatikana mpaka leo. Mawe hayo yakabadilika na kuvaa sura ya binadamu, moja limesimama na lingine limeinama na yanafanana kabisa na sura za binadamu. La ajabu ni kuwa mawe hayo hata yakipigwa picha hayapigiki.

Jafari aliongea na majini kama mtu anavyoweza kuongea na rafiki zake. Yeye alikuwa anawaona ingawa watu wa kawaida walikuwa hawawezi kuwaona. Jafari aliyatumia majini kama walinzi na kama chanzo cha mapato. Aliweza pia kuwatumia kuwadhuru maadui zake na hata kuwarushia magonjwa ingawa mara nyingi aliwatumia kuwasaidia watu wenye shida na kutibu magonjwa mbalimbali. Watu waliweza kusikia nyakati fulani akiwafukuza hao majini akiwaambia, “Ninyi mnakuja kufanya nini hapa kwenye makazi ya watu bila kuitwa, rudini kwenye makazi yenu”. Makazi ya majini yanaaminika kuwa ni baharini, kwenye miti mikubwa kama mibuyu au mapangoni.

Hatibu anaendelea kusimulia kuwa Jafari aliwatumia majini pia kuendesha sherehe za ibada ya kutoa makafara kwa mizimu. Ibada hii ilikuwa ikifanyika mara moja kila mwaka na bado inaendeshwa na ukoo wake mpaka leo. Ibada hii ilikuwa ikifanyika katika mwamba mkubwa katika kisiwa cha Chumbagama na Kichibweni. Wakati wa ibada hii ikifika watu walipiga ngoma kualikana na kwenda kisiwani kutambikia majini. Katika ibada hii wanyama walichinjwa, ngoma zilichezwa na vyakula vingi sana vililiwa na hakuna kilichosazwa. Inaaminika kuwa karibu nusu ya mazao yaliyopatikana baada ya mavuno yalitumika katika sherehe hizi za kimizimu. Wenye shida na matatizo mbalimbali kama vile: kukosa watoto, magonjwa na hata wenye mikosi walipeleka shida zao na walifanikiwa.

Kama ilitokea mwaka kupita bila watu kwenda kutambika, majini yenyewe yalipiga ngoma kwa nguvu sana huko pwani kuwaita watu kama kuwakumbusha kuwa mbona hawaji kufanya matambiko? Watu waliposikia ngoma hiyo ya majini walijua maana yake na mara moja taratibu za matambiko zilifanyika. Watu walipofika hapo Kisiwani Chumbagama, walikaribishwa na ndege weupe waliorukaruka na kuchezeza kwa furaha. Baada ya matambiko pia ndege hao walirudia tena kucheza na kurukaruka kwa furaha. Hii ilikuwa ishara tosha kuwa majini yamefurahishwa na matambiko hayo na kuwa ibada yao imepokelewa na mizimu⁹.

⁹Hatibu M Kibwana, miaka 75. Hatibu ni mjukuu wa Jafari Kibwana. Mama yake anaitwa Asha binti Jafari. Hatibu ndiye amerithishwa uganga wa majini, mizizi, kitabu na utabiri na ndiye anayesimamia matambiko yanayofanyika Chumbagama na Kijibweni (Mahojiano, Aprili 2019).

Shaaban Robert katika riwaya ya *Adili na Nduguze* ametumia visa vingi sana vya mawasiliano yanayotumia lugha za wanadamu kati ya binadamu na majini. Kwa mfano, Adili anaongea na wazazi wa Huria, yaani Kisasi mfalme wa majini na Mjeledi malkia wa majini bila kizuizi cha tofauti ya lugha kati yao (*Adili na Nduguze*, uk. 36). Pia tukio la watu wawili kugeuka mawe kwa sababu ya kukaa onyo la Jafari Kibwana, ni sawa na kisa cha watu wa mji wa Fahari kugeuka mawe kwa sababu ya Tukufu, mfalme wa mji huo kukataa onyo la Mrefu (*Adili na Nduguze*, uk. 21). Hii inazidi kudhihirisha kuwa Shaaban Robert ametumia mbinu ya uchawi na mazingaombwe kwa sababu ya kuwepo kwa uchawi na mazingaombwe katika mazingira yake asilia.

Tukio la majini kupiga ngoma kuwaalika watu kwenye sherehe za Chumbagama na ndege weupe kuhudhuria na kufurahia sherehe hizo, limetumiwa pia na Kezilahabi katika riwaya ya *Nagona*. Katika riwaya ya *Nagona* kuna sherehe za matumaini ya mwezi ujao zinazosherehekewa kwa vicheko vya wanadamu na wanyama (*Nagona*, uk. 6). Namna Kezilahabi anavyoelezea sherehe hizo inaonekana kuwa amechota masimulizi hayo kutoka (sherehe za Chumbagama) mazingira asilia ya Shaaban Robert na kuyaeleza kwa namna nyingine. Hapa, Kezilahabi ametumia mbinu mbili (ujalizaji na ugeuzaji) miongoni mwa mbinu tano za upotoshaji ili kujiengua kutoka kwa athari za Shaaban Robert (Bloom, 1973).

2.1.4.2 Kisa cha Osale Otango cha Uvunjivu wa Kaida ya Mahali

Katika mazingira asilia ya Shaaban Robert visa vya uvunjivu wa kaida ya mahali hutokea sana na wenyeji huyachukulia kama matukio ya kawaida ingawa ni ya

kushangaza. Katika matukio hayo mtu anaweza kuingia na kutoka, kwa mfano, ndani ya nyumba ingawa milango yote imefungwa. Mfano ni kisa cha Osale Otango kilichosimuliwa na Abdalah Mwachaka. Osale alikuwa ni mpigania uhuru aliyesakwa na kukamatwa na serikali ya kikoloni ya Mwingereza mwaka 1958 mkoani Tanga. Waingereza walimtia gerezani katika gereza la Maweni. Gereza hilo lilikuwa imara na Osale alifungwa pingu mikono na miguu na kuwekwa katika chumba maalum peke yake. Asubuhi ya siku iliyofuata mkuu wa gereza aliyekuwa Mwingereza alipofungua ofisi yake alikuta karatasi mezani yenye maandishi ‘Kwa heri, tutaonana tena. Osale Otango.’ Mkuu wa gereza alikimbilia rumande, huko aliwakuta walinzi nje wakiwa kwenye lindo na chumba kiko salama lakini Osale Otango hayumo. Hakuna aliyeiba funguo za rumande wala za ofisi ya mkuu wa gereza na hakuna sehemu iliyovunjwa. Namna Osale alivyotoka rumande hakujulikani mpaka leo¹⁰.

Kisa cha Osale Otango kutoka gerezani kimiujiza ni sawa na kisa cha jini, Huria binti Kisasi, kuingia kwa Adili na kutoka milango ikiwa imefungwa (*Adili na Nduguze*, uk. 41, 47). Tofauti ya visa hivi viwili iko katika makusudio yake. Osale anatumia uvunjivu wa kaida ya mahali kujiokoa kutoka gerezani wakati Shaaban Robert anatumia uvunjivu huo kwa kumtumia Huria kuingia kwa Adili ili kumuadhibu.

¹⁰Abdalah Mwachaka, miaka 79, Binamu yake Shaaban (Mahojiano, Aprili 2019).

2.1.4.3 Kupotea kwa Mgonjwa Chumbani na Wanawake Wanaosukana Chini ya Bahari Pamoja na Kutia Nanga Katika Mji wa Wachawi Katikati mwa Bahari

Kupotea kwa mgonjwa chumbani ni kisa kilichotokea mwezi Machi mwaka 2019 katika kitongoji cha Machui Hospitali. Kijana mmoja alikuwa mgonjwa taabani. Mama yake pamoja na ndugu zake waliotoka sehemu mbalimbali kuja kumjulia hali walikuwa wakiongea sebuleni usiku. Mgonjwa alikuwa chumbani amelazwa kitandani. Mganga aliyeitwa kuja kumtibu mgonjwa alifika na dawa tayari kuanza matibabu yake. Mama akaenda chumbani kumwandaa mgonjwa kwa ajili ya matibabu. Kitandani hakumkuta mtu, akaangalia uvunguni hakuna mtu, chumbani kote mwanaye haonekani. Wakapiga yowe, wakatafuta kila kona lakini hakupatikana mpaka leo. Kinachowachanganya mpaka leo ni kuwa licha ya kijana huyo kuwa mgonjwa kiasi cha kutoweza hata kujikuna lakini nyumba hiyo ni ya mlango moja tu ambao ili mtu atoke nje ni lazima apitie sebuleni. Sebuleni kulikuwa na watu, sasa kapitia wapi? Mwisho habari zikaenea kuwa alichukuliwa na majini¹¹.

Kisa kingine cha uvunjivu wa kaida ya mahali kinasimuliwa na Abdallah Mwachaka juu ya Jafari kibwana na wanawake wanaosukana chini ya bahari. Siku moja Jafari Kibwana alienda kuvua samaki baharini na mtoto wake aliyeitwa Mhunzi Jafari Kibwana. Katika kuvua kwao Jafari alimtuma mwanaye azamie ndani ya maji ili kuinua ‘malema’ ili wapate kuwatoa samaki walionaswa. Alipofika huko chini alirudi kwenye mtumbwi haraka akitetemeka. Jafari alipomuuliza amekutwa na nini huko, Mhunzi alijibu akitetemeka kuwa

¹¹ Wazee sita wa Kahawani Machui Hospitali(Mahojiano na Mtafiti, Aprili, 2019).

amewakuta wanawake wawili chini ya bahari wamekaa kitako wanasukana bila wasiwasi.

Jafari kwa kuwa alikuwa na uganga wa majini na kwa kuwa alifahamu kuwa hao wanawake walikuwa ni majini, hakuonyesha dalili yoyote ya kushtushwa na tukio hilo. Alichanja kidole chake na kudondosha damu kwenye maji. Baada ya kufanya hivyo alimwamurisha Mhunzi arudi tena huko chini ya bahari. Aliporudi hakuwakuta majini hao na wakaendelea na kazi ya kuvua. Hii ni kwa sababu majini yanapenda sana kunywa damu. Damu aliyonyunyiza Jafari ndani ya maji ilikuwa ishara ya kuwafurahisha na kuwafanya waondoke pale kumwacha Jafari na mwanaye Mhunzi kuvua kwa amani na kupata samaki wengi sana siku hiyo¹².

Kisa kingine cha uvunjivu wa kaida za mahali kinachofanana na cha wanawake wanaosukana chini ya bahari ni cha kutia nanga katikati mwa bahari. Wavuvi walikuwa wametia nanga katikati mwa bahari ili kupumzika baada ya kazi kubwa ya kuvua usiku. Asubuhi walipojaribu kung'oa nanga ili waondoke nanga iligoma ikionesha kuwa imekwama sehemu fulani huko chini ya bahari. Ilimlazimu mvuvi mojawapo kushuka huko chini ili kuangalia tatizo ni nini. La ajabu aliposhuka huko chini alifika ghafla katika mji wenye watu wengi wanaoendelea na shughuli zao za kila siku bila wasiwasi. Jambo hili lilimshtusha na kumwogopesha sana. Mvuvi alijiwa na mzee mmoja wa mji huo na kumkaripia kuwa waache tabia yao mbaya ya kutia nanga popote bila kuzingatia usalama wa watu wengine. Mzee huyo alimwonyesha nanga yao iliyokwama katika paa ya

¹² Abdallah Mwachaka, miaka 79 ni binamu yake Shaaban Robert (Utafiti, Aprili 2019)

nyumba fulani karibu na watoto waliokuwa wakicheza bila wasiwasi. Mzee alimwambia mvuvi kuwa kama hiyo nanga yao ingeshuka chini kidogo ingeweza kuwaumiza watoto hao. Mvuvi aliomba sana asamehewe kwa sababu hawakujua kuwa kulikuwa na makazi ya watu chini ya maji katikati mwa bahari. Mvuvi alisamehewa baada ya kunyolewa upaa na kupigwa ububu. Wavuvi waliokuwa katika jahazi walipoona mwenzao harudi walianza kuwa na wasiwasi kuwa amepatwa na tatizo huko chini na yawezekana amekufa. Ghafla aliibuka akiwa amenyolewa na pia haongei. Mambo haya yaliwashangaza sana wenzake. Hata hivyo nanga yao ilitoka na wakaanza safari ya kurudi pwani. Walipofika nchi kavu mwenzao alirudiwa na uwezo wa kuongea na kuwaeleza yote yaliyompa huko chini ya maji katikati mwa bahari¹³.

2.1.4.4 Kujibadilisha Kimazingaombwe Chumbageni

Maajabu ya uchawi na mazingaombwe yanayohusiana zaidi na familia ya Shaaban Robert ni pamoja na kujibadilisha kichawi na kimazingaombwe chumbageni. Baada ya kufariki mke wa kwanza, Shaaban Robert alioa mke wa pili, Sharifa binti Husein wa Chumbageni Tanga. Chumbageni kulikuwa kunasifika na hata sasa kwa uchawi na mazingaombwe kuliko maeneo mengine yote mkoani Tanga. Hivyo Shaaban Robert kuoia Chumbageni pia kuliongeza uelewa na ushuhudiaji wake wa matumizi ya uchawi na mazingaombwe.

Chumbageni watu waliishi kwa tahadhari kubwa wasije kuwaudhi wachawi au majini. Ukitembea njiani unaweza, kwa mfano, kukanyaga gogo au kupiga teke kokwa la nazi. Kokwa au gogo hilo linaweza kukujia usiku katika sura nyingine

¹³ Abdalla Mwachaka (Utafiti, Machi 2019)

na kukuuliza kwa nini ulinipiga teke mchana? Ukimwona paka usimpige anaweza kuwa jini aliyevaa sura ya paka. Katika biashara unaweza kukuta mtu amepanga samaki kumbe samaki wengine ni vipande vya mbao. Ukikuta vikombe vimewekwa porini chini ya mti mkubwa mfano mbuyu usivichukue vyaweza kuwa vya majini wanavyonywea chai. Ukivichukua usiku watakuja na kukuuliza mbona unaingia katika miji ya watu na kuchukua vitu vyao bila kuwaomba au hata bila kubisha hodi?

Watu walionywa wasile chakula wakitembea. Ukila unapotembea njiani, jini angeweza kukupiga kofi na kupatwa na homa ya kufisha.

Mwalimu mmoja kutoka Ubena Somozi mkoani Morogoro alienda kufundisha huko Chumbageni. Paka wengi wakawa wanamsumbua sana ikiwa ni pamoja na kula chakula chake chote kila akitoka kwenda darasani. Namna paka hao walivyokuwa wakiingia na kutoka chumbani mwake hata kama mlango na madirisha ikiwa imefungwa hakufahamu.

Siku moja aliamua kuwatega paka hao. Aliporudi usiku kama yapata saa nne alikuta paka moja amenaswa. Mwalimu alichukua gongo ili kumpiga huyo paka. Paka alilia kwa sauti akisema usiniue, usiniue, usiniue. Mwalimu kusikia paka anasema alikimbia kutoka Tanga mpaka kwao Morogoro bila kusimama njiani. Alisema kazi kwaheri, na hakurudi Chumbageni hadi leo¹⁴.

¹⁴ Christopher Mkabenga, miaka 58, mapokezi ofisi ya Mkuu wa Mkoa Tanga (Mahojiano, Aprili 2019).

Tofauti na majini kuongea na binadamu wakiwa wamevaa sura ya ubinadamu, Shaaban Robert hakutumia wanyama kuongea na binadamu moja kwa moja katika riwaya zake teule. Hata Hasidi na Mwivu walipobadilishwa manyani hawakuongea lugha ya kutamkwa mpaka walipoondolewa uhayawani. Badala yake, Kezilahabi ametumia matukio hayo yaliyoko katika mazingira asilia ya Shaaban Robert katika riwaya ya *Mzingile* (uk. 126). Hapa Kezilahabi ametumia ujalizaji kama mbinu mojawapo ya upotoshaji ili kuleta athari na fikra mpya katika utunzi wa kazi ya fasihi (Bloom, 1973).

2.1.4.5 Shukrani ya Bundi

Kisa kinasimuliwa na Bi Asha Jafari cha mtu mmoja wa bara aliyeajiriwa kazi ya ualimu maeneo ya karibu na Chumbageni Tanga. Siku moja mwalimu huyu aliyekuwa mlevi alikuwa akitoka shambani, njiani alikuta ndege wawili aina ya bundi wakipigana. Ndege hao hawakushtuka licha ya mwalimu huyu kuwafikia karibu kama hatua moja tu kutoka hapo walipokuwa wakipigana. Bundi moja alilemewa karibu ya kufa. Mwalimu alimhurumia na kuwaachanisha na bundi aliyemlelea mwenzake kuruka na kutoweka. Jioni mwalimu alienda kilabuni kunywa pombe kama kawaida yake. Mtu mmoja miongoni mwa wanywaji alimwagizia mwalimu pombe nyingi na kumwambia hii ni shukrani kwa kile ulichonifanyia mchana. Mwalimu hakujua ni kitu gani alichomfanyia mchana mtu ambaye hajawahi kumwona. Mtu huyo alimwambia kuwa yeye ndiye bundi aliyemsaidia mchana katika ugomvi wa bundi wawili. Mwalimu alishtuka, pombe ikamwisha kichwani, na akaondoka kurudi kwake.

Katikati ya usiku ingawa milango ilifungwa lakini alishtukia kuna mwanga wa aina yake chumbani. Kuangalia vizuri akamwona mtu amesimama karibu na kitanda chake. Hakufahamu namna mtu huyo alivyoingia chumbani mwake wakati milango yote ilikuwa imefungwa. Mtu huyo alimwonya na kumwambia ugomvi usiomhusu kwa nini aingilie kuamua? Mtu huyo alijitambulisha kuwa yeye ndiye bundi yule aliyekuwa anampiga mwenzake. Kesho yake mwalimu huyu aliomba uhamisho kurudi kwao bara¹⁵.

Shaaban Robert ametumia visa mbalimbali vinavyofanana na kisa hicho hapo juu katika riwaya zake teule. Kwa mfano, uvunjivu wa kaida za mahali na kujibadilisha kimazingaombwe kwa jini, Hunde mfalme wa Ngazi na jini, Huria binti Kisasi (*Adili na Nduguze*, uk. 18, 34, 41).

2.1.4.6 Kuachwa Uchi Juu ya Mbuyu Mwaka 1967 Barabara ya 18 Tanga Mjini

Katika mazingira asilia ya Shaaban Robert kuna matukio mbalimbali ya majini kujigeuza na kuchukua sura za binadamu. Mwaka 1967 mtu mmoja alimtongoza msichana fulani aliyekutana naye barabarani akiwa katika matembezi yake. Katika kuzungumza kwao wakakubaliana kwenda magorofani alikoeleza msichana kuwa ni kwao ili kupitisha usiku huo. Walienda, na mtu huyo aliona kabisa kuwa wamepanda ngazi na kuingia chumbani. Jambo la ajabu ni mtu huyo kukutwa kesho yake asubuhi barabara ya 18 akiwa amelala fofofu juu ya mti wa mbuyu akiwa uchi wa mnyama. Watu wakafahamu kuwa alidanganywa na jini aliyejigeuza msichana na kumpeleka juu ya mti akiona mti kuwa ni nyumba ya

¹⁵Bi Asha Jafari, miaka 89, binti wa Jafari Kibwana ambaye ni kaka yake Shaaban Robert (Simulizi, Aprili 2019).

gorofa. Habari zilifika polisi na baadaye akachukuliwa na gari ya wagonjwa maututi kupelekwa hospitalini akiwa hajitambui¹⁶.

Kisa hiki cha kujibadilisha kwa jini na kuwa msichana mzuri kinafanana na kisa cha jini, Huria binti Kisasi katika riwaya ya *Adili na Nduguze* (uk. 18). Huria aliweza kujibadilisha katika sura mbalimbali na hata kuwa msichana mzuri pale Adili alipomwokoza asiawe na jini Hunde mfalme wa Ngazi. Hii inathibitisha kuwa uchawi na mazingombwe uliotumiwa na Shaaban Robert katika riwaya zake teule upo katika mazingira yake asilia.

2.2 Uchawi na Mazingaombwe katika Kisiwa cha Ukerewe, Mazingira Asilia ya Euphrase Kezilahabi

Kuna matumizi mengi ya uchawi na mazingaombwe katika mazingira ya Ukerewe ambayo kwa kiwango fulani yameathiri uandishi wa Kezilahabi. Matumizi hayo yameelezwa kama visa au kwa njia ya masimulizi ya mambo ya kweli yaliyotokea katika mazingira yaliyomlea na kumkuza Kezilahabi. Hapa chini yameelezwa baadhi ya visa halisi alivyosimuliwa mtafiti vinayohusishwa na uchawi na mazingaombwe. Matumizi yanayojidhihirisha kwa kiwango kikubwa ni pamoja na matukio ya ajabuajabu, uvunjivu wa kaida za uhalisia pamoja na visasili.

¹⁶Kisa kilisimuliwa tarehe 23/04/ 2019 na Musa Salim dereva ofisi ya Mkuu wa Mkoa Tanga, miaka 55

2.2.1 Matukio ya Ajabuajabu katika Kisiwa cha Ukerewe

Kuna matukio mengi sana yanayohusishwa na uchawi na mazingaombwe katika kisiwa cha Ukerewe. Mengi ya matukio hayo yanatendwa na watu wasioonekana ingawa yanawaathiri watu kiuhalisia.

2.2.1.1 Matukio ya Ajabuajabu katika Historia ya Ukoo wa Euphrase Kezilahabi

Euphrase Kezilahabi alizaliwa siku ya manjozi makubwa kwa familia yao. Siku hiyo alifariki mjomba wake aliyetitwa Karaba. Familia yao ilipopata habari za msiba walisafiri kwenda msibani na kumwacha Edina Bilenjo yaani mama yake Kezilahabi nyumbani kwa sababu alikuwa mjamzito na siku za kujifungua kwake zilikaribia. Siku hiyo hiyo alipatwa na uchungu wa kujifungua akiwa hapo nyumbani na binti yake mdogo wa miaka tisa tu anayetitwa Erenestina Nakahozya. Alipomtuma Erenestina kuwaita majirani kuja kumsaidia, Erenestina aliogopa akarudia njiani na kumdanganya mamake kuwa hakuwakuta majirani. Erenestina aliogopa kupita vichaka vilivyokuwa kati ya mji wao na miji ya jirani kwa sababu ya masimulizi yaliyokuwa kuwa wachawi walikuwa wakiwaficha matunu, yaani vizuu au misukule, katika vichaka hivyo. Mama alijifungua bila msaada wowote na kukata kitovu cha mtoto peke yake. Kwa sababu ya matukio hayo mtoto aliyezaliwa akaitwa Kezilahabi. Kezilahabi maana yake ni mtu au kitu kilichokuja kwa shida, bahati mbaya, kuponea chupuchupu au kuzaliwa wakati wa shida au huzuni. Hivyo Kezilahabi, kwa sababu ya kuzaliwa wakati

familia yao iko katika huzuni au majonzi ya kufiwa na mjomba wao akaitwa Kezilahabi yaani huzuni¹⁷.

Babake Kezilahabi, Vincent Tilibuzya alikuwa manangwa (msimamizi wa kijiji au kata ya Namagondo kwa sasa). Ukoo wa Kezilahabi ni wa asili ya kitemi. Asili yao ni Butiliti Hangunga kata ya Ngoma tarafa ya Mumbuga. Babu yake Kezilahabi, mzee Nfunzi Magaza ndiye aliyehamishiwa Namagondo na mtemi Ruhumbika kwenda kuwa manangwa wa eneo hilo. Mzee huyu alikuwa mpinzani mkubwa wa imani ya Kikristo. Matendo yake na mawazo yake yameathiri pia kwa kiwango fulani matumizi ya mambo ya ajabuajabu katika uandishi wa Kezilahabi. Nfunzi, kwa mfano, kama watoto wake wangefumba macho kuombea chakula angeweza kuchukua chakula hicho na kukificha akidai kuwa chakula hicho kimechukuliwa na mizimu ya Kikerewe kimiujiza. Alidai kuwa kufanya maombi kwa kutumia jina la Yesu ni ukafiri na ni kinyume cha utamaduni wa Kikerewe.

Siku mmoja alienda kanisani akakuta picha na sanamu za watakatifu mbalimbali zimetundikwa ukutani, akatoka amekasirika kuwa Mapadri wanaleta kanisani ‘mitunge’ yaani watu walichukuliwa vizuu. Vizuu ni watu wanaofikiriwa kuwa wamechukuliwa kichawi na wachawi kwa lengo la kuwatumikisha katika shughuli mbalimbali ingawa katika uhalisia wanaonekana kuwa wamekufa. Usiku mmoja mjukuu wake anayelitwa Florensia Mkwaya (dada yake Kezilahabi), aliumwa na ng’e. Binti huyo alilia sana kutokana na maumivu ya

¹⁷Masimulizi yalitolewa tarehe 17/03/2019 na Erenestina Nakahozya miaka 84-dada yake Kezilahabi, **yeye** ndiye aliyebaki nyumbani na mama yake siku ya kuzaliwa Kezilahabi.

sumu ya ng'e. Mzee Nfunzi badala ya kuangalia ni kitu gani kilichomtokea mjukuu wake, yeye alihitimisha kuwa analizwa na ndoto za picha za ajabuajabu za wafu wanazozabudu kanisani. Ikitangazwa kuwa kutakuwa na ekaristi takatifu kanisani, siku hiyo mzee Nfunzi ataleta matunda matamu kama ndizi, maembe na mipapai ili kuwatamanisha watoto wake na wajukuu zake kula akijua kuwa ni mwiko kula chakula kingine siku ya ekaristi takatifu kwa imani za dhehebu la Katoliki¹⁸.

Mtemi Lukonge, yaani baba yake mtemi Ruhumbika aliyemhamishia Nfunzi Namagondo, alimfuga chatu, nyoka anayeweza kumeza wanyama kama mbuzi, kondoo na hata binadamu. Mtemi alimpenda nyoka huyu kupindukia. Siku moja bila kutegemewa nyoka huyo alimmeza mtoto wa mfanyakazi wa mtemi. Habari hizi zilikuwa za kuhuzunisha kwa mtemi na kwa watu wote. Mtemi kwa kumpenda sana nyoka wake, hakutaka nyoka auawe badala yake alipitisha sheria kuwa chatu akikamata kitu chochote hata binadamu hawezi kuuawa. Hiyo imekuwa ni mwiko kwa Wakerewe hata leo. Kwa wakerewe chatu ni nyoka anayeheshimiwa sana, na hata akimkamata mtu watu watafanya jitihada za kumwokoza mtu huyo bila kumdhuru chatu huyo.

Kitendo hicho cha mtemi kutokubali nyoka auawe kinaweza kuonekana kuwa ni cha kikatili na cha ajabu, lakini katika historia ya Wakerewe watemi walitakiwa kuwa na mioyo mkuu na mara nyingine kutakiwa kuwa tayari kutoa maamuzi mazito na yasiyotarajiwa. Kwa Wakerewe ilikuwa ni sheria kuwa mtemi baada

¹⁸Veneranda Muyanga, Nesi mstaafu miaka70. Ni binti wa Pantaleo Nagano ambaye ni kaka yake Kezilahabi (Utafiti, Machi 2019)

ya kuteuliwa alitakiwa atende jambo fulani la kijasiri kabla ya kusimikwa kwenye kiti. Tendo lenyewe lilikuwa ni kufanya ngono na mama yake mzazi na bila kufanya hivyo ilikuwa hawezi kusimikwa. Mtemi mteule akionesha kukataa atabembelezwa mpaka akubali, na zaidi ya yote mama yake naye atamshauri zaidi kufanya hivyo kwa sababu walipenda heshima ya kuwa mama yake mtemi. Siku mtemi mteule anapofaulu mtihani huu ngoma zitapigwa kwa furaha na watu watasikika wakisema “Mtemi amepanda kwenye ngoma”¹⁹.

Kisa mojawapo cha uchawi na mazingaombwe katika familia yao Kezilahabi ni kisa cha bundi wa Deonatus Ninarwo. Deonatus Ninarwo ni kaka yake Kezilahabi. Kipindi fulani aliporudi nyumbani kutoka shule wakati wa likizo, alikuta kuna bundi wengi sana katika mti mkubwa uliokuwa uwanjani hapo nyumbani kwao Namagondo. Usiku bundi hao walikuwa wakilia sana na kumwogopesha mama yake Kezilahabi. Ninarwo alitafuta mti mrefu na kufungia kitambaa chenye mafuta ya taa. Aliwasha moto kwenye kitambaa na kuunguza viota vya bundi. Aliwaua bundi wengi sana kwa moto huo. Alipowaangalia bundi wale aliwaua alikuta karibu wote wamevishwa shanga shingoni. Usiku uliofuata walikuja bundi wengi tena na kulia kilio kilichoashiria kuwa walikuwa wanawalilia wenzao waliouawa na Ninarwo. Mama yake aliogopa sana kwa kuhofia kuwa mwanae amewaua bundi wa wachawi na wachawi watamdhuru. Hata hivyo hakuna kilichomtokea Ninarwo²⁰.

¹⁹Edmund Makaranga miaka 67, mpwa wake Kezilahabi na Jeremia Magafu Mwenyekiti wa kamati ya shule ya msingi Nakasahenge (Utafiti, Machi 2019).

²⁰Erenestina Nakahozya, dadake Kezilahabi (Utafiti, Machi 2019)

2.2.1.2 Kuchukuliwa Matunu Aloyce Euphrase

Tukio hili lililotokea kijijini Namagondo linaelezwa na Erenestina Nakahozya na Veneranda Muyanga. Aloyce alikuwa ni kijana mwenye nguvu nyingi na juhudi katika kilimo. Wachawi walitamani kumchukua ili wamtumikishe kulima katika mashamba yao. Siku moja, mwaka 1971 Aloyce alienda shambani kupalilia pamba. Akiwa shambani alijiwa na mwanamke mmoja na kumzunguka mara tatu. Baada ya kumzunguka, Aloyce akapotelewa na akili na kumfuata huyo mama hadi nyumbani kwake. Mama huyo alimwingiza Aloyce katika ghala la mawele na kufunika mlango wa ghala.

Aloyce hakurudi nyumbani. Wazazi wake walipoenda shambani walikuta jembe na panga, lakini mwanao hakuonekana. Walipomtafuta bila mafanikio filimbi ilipigwa na watu wote wa Namagondo na vijiji vya jirani walikusanyika kumtafuta Aloyce. Katika kumtafuta huko ndipo alipojitokeza mganga mmoja aliyekuwa akiishi hapo hapo Namagondo. Mganga alisema kuwa Aloyce amechukuliwa ‘matunge’ na anawafahamu waliomchukua kwa sababu aliwaona kichawi ila hawezi kuwataja mpaka apate ulinzi wa polisi.

Polisi walipoitwa, mganga akasema kuwa kwa kutumia jicho la kiganga, alimwona Aloyce akifuatana na watu watatu mvua ikiwa inanyesha sana. Watu hao walikuwa ni wanaume wawili na mwanamke mmoja. Wanaume hao mojawapo alikuwa anaitwa Malezo. Watu hao watatu walikamatwa na polisi na kufungiwa katika stoo ya pamba pahali penye joto kali sana ili waseme kama kweli wamemchukua Aloyce kichawi au hapana. Mwanamke aliyekamatwa

alikuwa na mtoto na alipoona kama joto linataka kumwua na mtoto wake alipiga kelele ya kufunguliwa ili aseme ukweli wote.

Alisema kuwa Aloyce wamemchukua matunge, na yeye alitumwa kumchukua Aloyce kwa sababu huwa wanapeana matunge kwa zamu na pia kubadilishana matunge na wachawi wa vijiji vya mbali. Alieleza kuwa mwaka jana ilikuwa zamu yake na alimtoa mtoto wake. Huyo mtoto, watu walidhani amekufa na kuzikwa lakini alikuwa amechukuliwa matunge. Kwa hiyo mwaka huo ilikuwa ni zamu ya baba yake Aloyce mdogo, ambaye wako naye katika chama cha wachawi, kumtoa mtu. Kwa hiyo Aloyce ametolewa na baba yake mdogo na yeye, yaani huyo mwanamke, alitumwa tu kumchukua. Hata hivyo kwa kuwa Aloyce alikuwa analima sana lengo lao lilikuwa kumtumikisha tu katika mashamba yao lakini siyo kumwua.

Walipoenda katika ghala alikofichwa Aloyce, Aloyce aliisha safirishwa hadi kijiji cha Bulamba kwa lengo la kusafirishwa kwenda Gambosh mji wa wachawi kwa Wasukuma mkoani Mwanza. Walipofuatilia Bulamba Aloyce alikuwa ameshavushwa kwa meli kwenda Gambosh. Watu waliamua kuwaua hao wachawi lakini wakashauriana kuwa wakiwaua Aloyce atakuwa ndio amepotea milele. Hivyo, kwa amri ya polisi hao wachawi wakaamurishwa kuwa lazima wamlete Aloyce.

Baada ya wiki moja tangia siku ya tukio, Aloyce alipatikana Gambosh akiwa hajitambui. Aloyce alitibiwa na mganga na wanakijiji cha Namagongo walichangia gharama za matibabu. Baada ya matibabu Aloyce alirudiwa na fahamu na kujitambua. Hata hivyo Aloyce alipoulizwa alikuwa wapi, hakuweza

kukumbuka na kuona kana kwamba alikuwa ndotoni. Alichokumbuka ni kuzungukwa mara tatu na mwanamke aliyekuwa anamfahamu na baada ya hapo hakujua kilichotokea mpaka aliporudiwa na fahamu akiwa kwa mganga. Wale wachawi walichomewa nyumba zao na kulazimishwa kuhama Namagondo. Ilisemekana kuwa walihamia Uzinza. Aloyce aliendelea kuishi kwa muda mrefu akiwa na akili timamu na kuendelea na shughuli zake kama mwanzo.

Baada ya muda kupita Aloyce alitaka kuo. Ili apate mahari, alijiunga na shughuli za uvuvi. Alivua salama mara mbili. Mara ya tatu walipatwa na zahama ya upepo mkali na mtumbwi wao ukapinduka. La ajabu, wanasema wavuvi wenzake kuwa mahali ulipozamia mtumbwi wao hapakuwa na kina kirefu na hapakuwa mahali ambapo mtu anaweza kufa maji. Hata hivyo Aloyce alizama na kupotea na mwili wake haukupertikana mpaka leo. Kwa tukio hili waliamini kuwa Aloyce amechukuliwa tena na wachawi.

2.2.1.3 Ebiaro Nyabatesho, Kichaka Kinachotembea

Inaelezwa na Kakulu Makorokoro²¹ kuwa Wakerewe wengi wanaamini kuwa kuna matukio mengi ya ajabu yanayotokea ziwani hasa kwa wavuvi wa samaki. Miongoni mwa matukio hayo ni: kumwona mtu ziwani anakuja na mtumbwi na anapoukaribia mtumbwi wenu anapotea ghafla na mtumbwi wake na msimwone tena au kuona meli yenye taa zinazowaka sana inawajia na inapopita mbele ya mtumbwi wenu inapotea. Mnaweza kuona wavuvi wengine wamepanga taa zao pale pale kwenye mitego yenu na kusikia sauti za maongezi yao na baadaye wakapotea. Pia mnaweza kumwona mtu hasa mwanamke ameibuka ghafla mbele

²¹ Kakulu Makorokoro miaka 59, ndiye mrithi, msimamizi na mchezeshaji wa jiwe la nyabulebeka katika kisiwa cha Ukara (Utafiti, Machi 2019)

yenu ndani ya maji na kupotea tena au jabali kubwa linajitokeza mahali pasipo na jabali.

Siku moja Kakulu (Msimuliaji wa kisa hiki) alienda kuvua samaki na wenziwe sehemu za Yozi katika kisiwa cha Ukara. Wakiwa katika kutega ghafla mwenzao mmoja akaona meli inakuja kwa kasi kubwa sana kuwaelekea kama kutaka kuwagonga. Wakamsikia akiita Athumani, Athumani. Athumani ni jina maalumu la maajabu kama hayo yanapotokea ziwani. Meli hiyo ilipowakaribia ilitoweka ghafla na kutoonekana tena. Siku nyingine walipoenda tena kutega waliona kichaka kinatembea kikiwaelekea. Walisikia sauti kama za watu wanaozungumza zikitoka kwenye miti iliyokuwa katika kichaka hicho cha ajabu. Kichaka kama hicho wanakiita Nyabatesho, yaani muujiza au Ebiaro, yaani kichaka kinachotembea. Kichaka hicho cha kutisha kilitembea na kilipofika karibu na mtumbwi wao kilipotea.

Kukiwatokea matukio kama hayo ziwani bila ninyi kuvunja masharti yake, kwa mfano kusema unaiona hiyo meli au wale ni watu gani au kupiga kelele kwa woga; mtapata samaki wengi siku hiyo. Lakini mkivunja masharti kuna hatari ya chombo chenu kuzama.

Visa vya watu wanaojitokeza na kutoweka ghafla pamoja na vichaka au miti inayoongea imetumiwa sana na Kezilahabi katika riwaya zake teule. Kwa mfano, kuna kisa cha mwanamke anayejitokezana na kutoweka ghafla peupe kama mzuka (*Mzingile*, uk. 15). Pia Kezilahabi ametumia miti inayocheke na yenye uwezo wa kumzomea mtu (*Nagona*, uk. 1, 13). kupigwa wasioonekana

2.2.1.4 Kupondwa na Watu Wasioonekana

Inaelezwa na Silvanus Malimi kuwa katika kijiji cha Maregea kati ya mwaka 1974-76, kipindi cha Operesheni Vijiji kulitokea matukio ya ajabu. Tukio mojawapo lilikuwa ni kupondwa na limau na watu wasioonekana. Maaskari au wanamgambo waliokuwa katika operesheni ya kuwahamisha watu vijijini walipondwa na limau na watu wasioonekana katika kijiji hicho. Wanamgambo hao walikimbia na kuhairisha zoezi hilo kwa muda.

Matukio ya kuchapwa au kupigwa makofi na watu wasioonekana inasemekana ni ya mara kwa mara kisiwani Ukerewe. Kwa mfano, mwaka 2001 katika nyumba ya kulala wageni la ‘Peace Land’ mjini Nansio wateja na wahudumu wa nyumba hiyo walishtukia wakichapwa na kupigwa makofi na watu wasioonekana. Tukio kama hilo lilijirudia mara nyingi mpaka nyumba hiyo kufungwa kwa kukosa wateja na wahudumu.

Tukio lingine la kuchapwa na watu wasioonekana lilitokea katika kijiji cha Irondo. Kijana mmoja mgeni alipita karibu na kichaka fulani usiku kama saa mbili hivi akiendesha baiskeli. Ghafila akaanza kuchapwa na watu wasioonekana. Aliruka kutoka juu ya baiskeli akakimbia akipiga kelele. Alipofika kwa wenyeji wake wakamwambia mahali hapo watu hawapiti usiku, ukipita lazima utachapwa au kupigwa makofi na watu wasioonekana²².

Visa vya kupigwa kofi, kuchapwa, kupondwa na mayai viza na watu wasiooneka vimetumiwa sana na Kezilahabi katika riwaya teule. Kwa mfano, Msaka paa

²²Silvanus Malimi Clement, miaka 74, jirani na rafiki yake Kezilahabi, walianza darasa la kwanza pamoja mwaka 1953 shule ya msingi Nakasahenge (Utafiti, Machi 2019).

anapigwa kofi na mtu asiyeonekana alipojaribu kukalia jiwe kando ya mto, pia anapondwa na yai viza katika mji wa watu wasioonekana (*Nagona*, uk. 1, 5).

2.2.2 Uvunjivu wa Kaida za Uhalisia

Wachawi katika mazingira asilia ya Kezilahabi wana uwezo wa kuvunja kaida za uhalisia ikiwa ni pamoja na uwezo wa kuingia ndani ya nyumba hata kama milango imefungwa, kumsafirisha mtu ndani ya maji kwa kutumia mamba pamoja na kufanya mazingaombwe na kuwafanya watu waone kama mtu fulani amekufa kumbe amechukuliwa msukule na wachawi.

2.2.2.1 Kuzika Shina la Mgomba na Mechi ya Wafu

Kisa kingine kinachotaka kufanana na kisa cha Aloyce ni cha Jefta Masota. Kisa hiki kilitokea Buswelu Mwanza mwaka 1977. Jefta alikufa akazikwa na kupita miaka zaidi ya kumi. Siku moja watu walishtuka walipomwona Jefta amerudi nyumbani kwao. Alipoulizwa, alisema yeye hakufa na siku ya mazishi yake alikuwa akiwaona wazazi wake walivyokuwa wakilia na kuomboleza. Aliwaona watu walivyokuwa wakirudisha udongo katika kaburi lake na kuwataja baadhi kwa majina yao. Alisema, kilichozikwa kilikuwa ni shina la mgomba.

Jefta aliendelea kueleza kuwa alikuwa amechukuliwa na watu fulani alioogopa kuwataja. Watu hao walimpeleka Ukerewe na kumbadilisha na mtu mwingine wa aina yake. Akiwa Ukerewe walikuwa wanatumikishwa hasa usiku kama wafanyakazi katika mashamba ya mabwana zao ambao alijua kuwa walikuwa ni wachawi. Kilichomshangaza ni kuwa yeye alikuwa akiwaona watu na alikuwa na akili timamu lakini watu wa kawaida walikuwa hawamwoni na hata akiwaita walikuwa hawasikii. Mwisho kulitokea njaa, na usiku kabla ya siku hiyo

aliyofika nyumbani kwao, bwana wake, mchawi, alimchukua na kumsafirisha kichawi mpaka nyumbani kwao Buswelu. Bwana huyo alimpulizia dawa na kutoweka. Watu walipoamka walishtushwa kumwona tena mtu aliyefariki miaka zaidi ya kumi iliyopita²³.

Kisa cha Jefta kinafanana na kisa cha mechi ya wafu kilichotokea kati ya mwaka 1987 na 1989. Inasimuliwa kuwa siku moja kati ya miaka hiyo katika kijiji cha Bugorora, lilisikika tangazo likitangazwa na mchezaji mmoja wa mpira wa miguu ambaye alikuwa amefariki miaka kama mitatu kabla ya tangazo hilo kuwa kutakuwa na mechi ya mpira wa miguu kati ya wafu katika uwanja wa mpira wa kijijini hapo. Baada ya tangazo hilo majina ya wafu watakaoshiriki katika mechi hiyo yalikutwa yamebandikwa uwanjani hapo na namba watakazocheza ziliwekwa mbele ya majina yao. Siku ya mechi ilipofika watu wengi sana walihudhuria kushuhudia mechi ya wafu. Watazamaji walisikia kelele za kushangilia, sauti ya mdundo wa mpira lakini wachezaji hawakuonekana kwa macho²⁴.

Kisa cha Jefta kinafanana kabisa na kisa cha kipofu katika riwaya ya *Mzingile*. Kipofu alikufa kwa ajali ya gari na kuzikwa. Hata hivyo, alikuwa anawaona wote waliohudhuria katika mazishi yake. Msimuliaji anaongea na kipofu bila kujua kuwa anaongea na mfu mpaka kipofu anampomweleza kuwa amekuja kumshukuru kwa sababu yeye, yaani msimuliaji ndiye aliyekuwa wa kwanza kutupa udongo katika kaburi lake. Kwa maelezo hayo ndipo msimuliaji

²³Kisa kimesimuliwa na Erenestina Nakahozya na Veneranda Muyanga Machi 2019 (Inaaminika Jefta bado anaishi maeneo ya Buswelu mjini Mwanza).

²⁴ Shirebero Mathias, miaka 55 Jirani na Pantaleo kaka yake Kezilahabi(Utafiti, Machi 2019).

anashtuka kuwa anaongea a mfu (*Mzingile*, uk. 52). Kufanana kwa visa hivi kunazidi kudhihisha uchawi na mazingaombwe katika mazingira asilia ya Euphrase Kezilahabi.

2.2.2.2 Kunigwa na Matunu Mwaka 1989

Tukio hili lilitokea kata ya Namagondo. Watu walikuwa wakikabwa au kunigwa na watu wasiojulikana wala kuonekana kwa macho. Watu hao wasioonekana walihisiwa kuwa ni matunge au matunu, yaani vizuu. Vizuu ni watu ambao kwa macho ya kawaida walikufa na kuzikwa, lakini kwa macho ya kichawi hawakufa bali walichukuliwa na wachawi kwa lengo la kuwatumikisha kama watumwa. Inasemekana vizuu hao waliweza kurudi nyumbani kwao na kuita wakiomba chakula. Sauti zao zilisikika kwa waliowaita lakini wakitoka nje vizuu hawakuonekana.

Watu wa kawaida wasiofahamu uchawi hawakuwa na uwezo wa kuwaona wala kufahamu ni namna gani wangewasaidia vizuu hao. Mwaka 1989 vizuu walikasirika na kuanzisha vurugu. Vizuu hao kwa kusaidiwa na wachawi waliweza kuingia ndani ya nyumba usiku hata kama milango imefungwa. Waliwaniga watu waliowakuta wamelala ndani ya nyumba walizoingia. Watu walianza kulala nje kwa kuogopa kunigwa punde walalapo ndani ya nyumba zao. Ilikuwa kujulikana kuwa ukilala nje hawakunigi ila ukilala ndani ya nyumba au chini ya mti ndio unanigwa. La ajabu ni kuwa waliokuwa wakinigwa hata wakilia au kupiga yowe hakuna mtu mwingine aliyeweza kusikia kwa sababu hata sauti

ilikuwa haitoki²⁵. Kisa hiki kinafanana na visa vingine vilielezwa hapo juu vya kuvunja mpaka kati ya uhai na kifo katika riwaya teule za Euphrase Kezilahabi.

2.2.2.3 Kusafirishwa na Mamba: Uvunjivu wa Kaida ya Mahali au Mazingira

Tukio hili linamhusu John tajiri mbadhirifu aliyesafirishwa na mamba. John alikuwa ni tajiri aliyekuwa na wafanyakazi wengi mjini Mwanza. Miongoni mwa wafanyakazi wake alikuwa ni Mkerewe mmoja aliyeitwa Manyigo. John alikuwa msumbufu sana ikifika wakati wa malipo ya mishahara ya wafanyakazi wake. Mkerewe baada ya kazi alienda kwa John kudai mishahara wake. John alikataa kumlipa si mara mbili au mara tatu. Mwisho Mkerewe alisema “Mimi naenda kwetu lakini pesa zangu lazima utanilipa”.

Hazikupita siku tatu, John alienda kuoga ziwani. Akiwa ziwani na wenzake, tena ni ufuoni alikamatwa na mamba. Mamba alimzamisha John ndani ya maji na kuibuka eneo la darajani. Alimwinua John juu hapo kana kwamba anawaonesha watu wamwone John. Watu walipojaribu kwenda kumwokoa John, mamba aliwasubiri na walipomkaribia aliingia na windo lake tena majini na baada ya hapo mamba wala John hawakuonekana tena.

Ilipita kama mwezi mmoja baada ya tukio hilo, jirani mmoja wa John alisafiri kwenda Ukerewe kwa ajili ya biashara. Katika kukusanya bidhaa, akafika mji mmoja uliokuwa na wafanyakazi wengi wakikusanya maembe na kuyapakia kwenye maguni. Jirani wa John alipomwangalia mtu mmoja miongoni mwa

²⁵Mama Karaba, mke wa Magesa Karaba miaka 67 jirani ya Pantaleo Nagano, kaka yake Kezilahabi (Utafiti, Machi 2019).

wapakiaji hao alishtuka na kutobandua macho yake katika kumtazama. Alimtazama mpaka mwenyeji wao, yaani mwenye mji alipobaini na kumwuliza kwa nini anamtazama sana mfanyakazi wake. Jirani wa John alijibu kwa mshangao kuwa mtu huyo anafanana sana na jirani yake wa huko Mwanza ila jirani yake huyo alikufa kwa kuliwa na mamba mwezi umepita sasa. Mwenyeji akamwuliza, “Jirani yako huyo anaitwa nani?” Akasema John. Mwenyeji akamwambia ebu mwite aje uongee naye kwa sababu ni John mwenyewe. John alipoitwa alikuja na kuthibitisha kuwa yeye ni John kweli. Ndipo mwenyeji akasema kuwa mimi nilikuwa nafanya kazi kwa John. John alikataa kunilipa pesa zangu kwa hiyo nilimtuma mamba amlete ili naye aje kufanya kazi nyumbani kwangu. Mlipodhani ameuawa na mamba badala yake mamba alitumika kama chombo cha usafiri kumleta kwangu. Hata hivyo niko tayari kumwachia kama ndugu zake watakubali kurudisha pesa zangu na faini nitakayowatoza. Jirani wa John alilazimika kuhairisha biashara na kurudi Mwanza siku hiyo hiyo. Alipofika Mwanza aliwaeleza ndugu zake John alichokiona Ukerewe na kiasi cha pesa kinachohitajika ili John aweze kurudi nyumbani kwake. Pesa zilichangwa na John alikombolewa. Inafikiriwa kuwa John bado yu hai kwa sababu mpaka mwaka 2010 John bado alikuwa anaishi²⁶.

2.2.2.4 Mamba Kama Kijiti na Kujibadilisha na Kusafirishwa Kama Samaki

Inaelezwa na Pantaleo Nagano kuwa mwanamke mmoja kutoka kijiji cha Mahande kama kilomita tatu na nusu hivi kutoka Namagondo, alikuwa na ugomvi na jirani yake. Akafunga safari kwenda kwa mganga katika kisiwa cha

²⁶Magesa Karaba, miaka 82 Jirani wa Kezilahabi (Utafiti, Machi 2019)

Ukara ili atengenezewe uchawi wa kumuua huyo jirani yake ambaye alimhisi kuwaua watoto wake. Mganga baada ya uaguzi akamwonesha huyo mama mjusi na kumpa kijiti fulani. Akamwambia kuwa kijiti hicho ni mamba na akiweke kwenye mkoba wake. Akifika nyumbani kwake akiguse na kitakuwa mamba ambaye atamtumia kumwangamiza adui yake. Huyo mama hakuamini maneno ya mganga na kudhani mganga anataka kula pesa zake bure kwa ujanja. Akauliza kuwa kijiti kinawezaje kuwa mamba? Mganga akamwambia nimemfanya mamba kuwa kijiti ili upate urahisi wa kumsafirisha na pia ili watu wengine wasigundue kuwa una mamba. Mama huyo akazidi kukataa na kusema haijamwingia akilini kuwa kijiti kidogo hicho kinawezaje kuwa mamba? Zaidi ya yote mama alisisitiza kuwa anataka mamba na si kijiti. Mganga alipoona mteja wake hamwamini alikipiga kijiti kile na kikageuka mamba mkubwa. Mama alikimbia na kupiga kelele kwa woga na biashara ikaishia hapo kwa sababu mama huyo alivunja masharti ya uganga²⁷.

Tukio lingine linalotaka kufafana na la mamba kama kijiti ni la kujibadilisha na kusafirishwa kama samaki. Inasimuliwa na Kakulu kuwa mzee mmoja alitaka kusafiri kuvuka ziwa kutoka Bugorora kwenda Qwisha. Mwenye mtumbwi alikataa kumchukua na hivyo akabaki Bugorora. Mtumbwi ulipofika katikati ya ziwa, mwenye mtumbwi aliona samaki mkubwa anaelea juu ya maji na kumwokota. Mtumbwi ulipofika Qwisha mwenye mtumbwi alishangaa kumwona yule mzee aliyemwacha Bugorora ndiye amekuwa mtu wa kwanza kushuka kutoka mtumbwini na alipoangalia samaki hakumwona. Yule mzee akamtambia

²⁷ Pantaleo Nagano, Miaka 95, ni kaka mkubwa wa Kezilahabi

kuwa, ulikataa kunipakia kwenye mtumbwi wako ukapenda samaki kuliko binadamu mwenzako: sasa samaki wako yuko wapi?²⁸

Kezilahabi ametumia kujibadilisha kichawi na kimazingaombwe kwa namna inayotaka kufanana na kisa cha mamba kama kijiti na cha kusafirishwa kama samaki kwa kumtumia paa katika riwaya ya *Nagona*. Paa anaweza kujibadilisha kuwa paa mnyama, kuwa binti mzuri au kiumbe wa ajabu (*Nagona*, uk. 34).

2.2.2.5 Kutumia Sura ya Mtu Mwingine Kufanyia Uchawi

Inaelezwa na mzee Biswaro Saja Nyahonge²⁹ kuwa katika kata ya Namagondo alikwepo mtu mmoja aliyeitwa Malezo. Malezo alikuwa na mke aliyeishiwa kuwa mchawi. Kila alipoambiwa Malezo kuwa mke wake ni mchawi Malezo hakukubali kwa sababu muda wote wa usiku alikuwa na mke wake na walikuwa wanalala kitanda kimoja. Siku moja huyo mwanamke alikamatwa kwa jirani wa Malezo usiku akiwanga. Waliomkamata wakasema wanampeleka kwa Malezo ili wamthibitishie kuwa mkewe ni mchawi. Wakati wamemkamata huyo mwanamke na kupiga kelele za mchawi kuelekea kwa Malezo, Malezo naye akawa amemshika mke wake mkono nyumbani mwake akiwasubiri ili wamlete mke wake huyu ambaye yeye tayari yuko naye nyumbani kwake. Walipokuwa nje mlangoni walimpigia Malezo kelele ya kufungua mlango haraka la sivyo akichelewa watamuua mke wake ambaye walikuwa wamemshika na tayari waliisha anza kumpiga. Malezo naye alijibu kuwa hamjui huyo mwanamke waliyemshika kwa sababu mke wake yuko naye chumbani. Wakamataji walianza

²⁸ Kakulu Makorokoro, miaka 59- mchezeshaji na kiongozi wa jiwe la Nyabulabeka (Mahojiano, Machi 2019).

²⁹ Mzee Saja anaishi jirani na Pantaleo Nagano, Saja alizaliwa mwaka 1912 Mahojiano yalifanyika Machi, 2019

kumpiga huyo mwanamke, wakati huo Malezo naye alitokea mlangoni akiwa amemshika mkono mkewe.

Wapigaji walipomwona Malezo na mkewe na kuwa mkewe yuko salama kabisa tena hajadhurika hata kidogo walishangaa. Macho ya mwanamke aliyekamatwa akiwanga yalipokutana na macho ya mke wa Malezo sura ya mke wa Malezo ilimtoka na akavaa sura yake halisi. Wapigaji walipomtazama vizuri wakamtambua kuwa ni mwanamke mwingine kabisa hapo kijijini. Walipoendelea kumtazama zaidi, mwanamke mchawi alivaa sura nyingine tofauti wasioifahamu na kutoweka ghafla na hawakumwona tena. Ndipo wakatambua kuwa kumbe mke wa Malezo si mchawi bali mwanamke huyo ndiye anayevaa sura ya mke wa Malezo na kuitumia kwa uchawi.

Saja anaeleza kuwa wakati mwanamke huyo alipokamatwa akiwanga nyumbani na kupelekwa kwa Malezo, sura yake nyingine ilikuwa nyumbani kwake na alikuwa anaonekana kabisa kuwa amelala kitandani jirani na mume wake. Swali la kujiuliza ni kuwa inawezekana vipi mtu kuvaa sura ya mtu mwingine au kuwa pahali pawili kwa wakati mmoja.

Mzee Saja anasema kuwa uchawi wa kutumia sura ya mtu mwingine au wa kuwa sehemu mbili kwa wakati mmoja unatumiwa sana katika Kisiwa cha Ukerewe. Kezilahabi naye ametumia uchawi huo kama mbinu mojawapo ya utunzi katika riwaya zake teule. Kwa mfano, amemtumia Kizee kinachobadilika sura na kuchukua sura za watu wengine katika riwaya ya *Mzingile* (uk. 107, 110) na mhusika jumui katika riwaya ya *Nagona* (uk. 49-52).

2.2.3 Visasili

Kuna visasili mbalimbali katika mazingira asilia ya Euphrase Kezilahabi. Baadhi ya visa hivyo ni pamoja na kisa cha Wakerewe kutomwua chatu kama ilivyokwishaelezwa (taz, uk. 87) pamoja na kisa cha jiwe la Nyabulebeka lililoko katika kisiwa cha Ukara wilayani Ukerewe.

2.2.3.1 Nyabulebeka Jiwe Linalocheza

Maelezo yalitolewa na Kakulu Makorokoro wakati mtafiti akishuhudia maajabu ya nyabulebeka. Katika kisiwa cha Ukara wilayani Ukerewe kuna jiwe la maajabu. Jiwe hilo linaitwa Nyabulebeka, yaani jiwe linalocheza. Jiwe hili linacheza likiimbiwa au kukanyagwa na wahusika tu. Historia ya kucheza kwa jiwe hilo inaanzia katika ugomvi wa ndugu wawili. Ndugu hao katika kupigana mmoja aliamfukuza mwenzake na yule aliyekuwa anafukuzwa alipofika katika miamba fulani iliyoko karibu na ziwa alipotelea hapo kimiujiza na hakuonekana tena. Kilichobaki pale ni alama za nyayo za mikono na miguu inayoonekana dhahiri hata sasa juu ya miamba hiyo. Mojawapo ya miamba hiyo ndiyo huitwa nyabulebeka. Baada ya miaka mingi kupita ukoo wa ndugu hawa waliokuwa wakifukuzana ulianza kupatwa na matatizo na majanga mbalimbali.

Matatizo hayo ni pamoja na magonjwa ya ajabu, kuzaa watoto wasio wa kawaida, kwa mfano: vilema, wadumavu, wenye mtindio wa ubongo, na wanawake kutoona siku zao, kutopata watoto katika ndoa na wengine kutooa au kuolewa. Walipoenda kwa waganga, uganga ulisema matatizo hayo yanasababishwa na ndugu yao mmoja aliyegeuka jiwe kutokana na ugomvi kati yake na ndugu yake. Ndugu huyo anataka atambikiwe na kutolewa makafara kila mwaka. Ndugu huyo anaitwa Nyabulebeka. Nyabulebeka kwa sababu katika

uhalisia wake kabla ya kugeuka jiwe alipenda kucheza, hivyo anataka acheze kama furaha ya uwepo wake. Ili acheze inatakiwa aimbiwe na kutingishwa. Mtingishaji anaimba wimbo wenye maneno ya kilugha yenye malengo ya kumsifu na kumhimiza acheze na kucheze huku akitaja majina ya mababu waliokufa zamani ambao walikuwa ni ndugu zake Nyabulebeka.

Mganga aliwaagiza ukoo huo wa Nyabulebeka kuwa ili wawe salama wanatakiwa wamtambikie Nyabulebeka angalau mara moja kila mwaka. La ajabu ni kuwa wasipofanya matambiko hayo katika tarehe zilizoamuriwa matatizo yanawaandama na hayatulii mpaka matambiko yafanywe. Zaidi ya yote, tarehe hizo zikifika wanatembelwa na chatu, nyoka mkubwa anayeweza kummeza hata binadamu, katika miji yao; hasa miji ya wale wanaosimamia hutoaji wa kafara za ukoo ikiwa ni pamoja na jiwe la nyabulebeka. Dhumuni la kutembelwa na chatu ni kuwakumbusha kuwa wakati wa kutoa kafara umekaribia. Masharti ya kuingia kwenye eneo lilipo jiwe la nyabulebeka ni kuvua viatu kabla ya kuingia na kutoa sadaka kabla ya kuchezesha jiwe la nyabulebeka³⁰.

2.3 Kiishilio

Sura hii imechunguza hali ya uchawi na mazingaombwe katika mazingira asilia ya Shaaban Robert na ya Euphrase Kezilahabi. Lengo lilikuwa ni kuthibitisha kama kuna matumizi ya uchawi na mazingaombwe katika mazingira asilia ya watunzi hao. Imebainika wazi kuwa kuna matumizi mengi sana ya uchawi na mazingaombwe katika mazingira asilia ya watunzi tajwa. Matumizi ya uchawi na mazingaombwe yaliyojitokeza zaidi ni watu na viumbe wanaofanya mambo ya ajabu, matukio ya ajabuajabu pamoja na uvunjivu wa kaida za uhalisia.

³⁰ Kakulu Makorokoro, miaka 59. Mchezeshaji wa jiwe la Nyabulebeka (Utafiti, Machi 2019).

Katika mazingira asilia ya Shaaban Robert na hasa ukoo wake, kwa mfano, kuna mwingiliano mkubwa sana kati ya wanadamu na majini kiasi cha mpaka kati ya binadamu na majini kuwa mdogo sana. Katika mazingira asilia ya Kezilahabi hakuna kabisa neno jini kwa sababu uchawi na mazingaombwe wa kutumia majini haupo katika kisiwa cha Ukerewe. Kinyume chake katika mazingira asilia ya Kezilahabi kuna uchawi wa kuchukuliwa matunu (yaani kuuawa kimazingaombwe na hivyo kuvunjwa kaida kati ya uhai na kifo). Pia katika mazingira hayo ya Kezilahabi kuna uchawi wa kufanyiwa vituko na watu wasioonekana. Matumizi ya uchawi na mazingaombwe yaliyobainishwa katika sura hii yamechunguzwa jinsi yalivyotumiwa katika riwaya teule katika sura zinazofuata. Sura ya tatu imechunguza athari ya mazingira asilia katika usawiri wa wahusika wa ajabu katika riwaya teule za Shaaban Robert na za Euphrase Kezilahabi.

SURA YA TATU

ATHARI YA MAZINGIRA ASILIA YA WATUNZI KATIKA USAWIRI WA WAHUSIKA WA AJABU KATIKA RIWAYA TEULE ZA SHAABAN ROBERT NA ZA EUPHRASE KEZILAHABI

3.0 Utangulizi

Sura hii imechunguza jinsi mazingira asilia ya watunzi yalivyoathiri usawiri wa wahusika wa ajabu katika riwaya teule za Shaaban Robert na za Euphrase Kezilahabi. Lengo lilikuwa ni kuchunguza athari ya mazingira asilia ya watunzi husika katika matumizi ya wahusika wa ajabu katika riwaya teule na kulinganisha matumizi ya wahusika wa ajabu kati ya Shaaban Robert na Euphrase Kezilahabi. Ili kufaulisha malengo hayo, nadharia ya Uhalisiamazingaombwe ilitumiwa kubainisha wahusika wa ajabu. Ilhali, Kiwewe cha Kuathiriwa ilitumiwa kulinganisha matumizi ya mbinu ya uchawi na mazingaombwe kati ya Shaaban Robert na Euphrase Kezilahabi.

Sura hii imegawanyika katika sehemu kuu mbili. Sehemu ya kwanza imefafanua maana ya wahusika wa ajabu. Sehemu ya pili imebainisha wahusika wa ajabu katika riwaya teule na kuchunguza uhalisia wao katika mazingira asilia ya watunzi wa riwaya husika. Pia matumizi ya wahusika wa ajabu kati ya Shaaban Robert na Euphrase Kezilahabi imelinganishwa katika sehemu hiyo. Wahusika wa ajabu waliobainishwa katika riwaya teule na kuchunguzwa katika mazingira asilia ya watunzi ni: wahusika wenye uwezo wa kujibadilisha kimazingaombwe, wahusika wanaoishi kati ya uhai na kifo na kuonekana na kutoweka ghafla

kimiujiza, wahusika wenye uwezo wa kuona na kufahamu jambo linalotendeka mbali na wenye uwezo wa kusoma na kufahamu mawazo ya mtu hata bila mtu kusema. Wengine ni wahusika wenye matendo na nguvu za ajabu, wahusika wenye uwezo wa kufuata kitu kilicho mbali sana kwa kukunjua mguu, wahusika wanaoweza kunusa harufu kama mbwa, wahusika jumui na wenye nafsi mbili pamoja na wahusika wenye hali ya kiungu isiyo bayana.

3.1 Wahusika wa Ajabu

Wataalamu mbalimbali wa fasihi wameeleza maana ya mhusika kwa namna mbalimbali. Njogu na Chimera (1999) wamemweleza mhusika kuwa ni kiumbe anayepatikana katika kazi ya kifasihi na ambaye anafanana na binadamu kwa kiasi fulani. Wasifu wa mhusika unategemea mkabala uliopo. Wahusika ni viumbe ambao hutumiwa na mwandishi katika mtiririko wa matukio kuelezea kisa chake. Wahusika hawa wanaweza kuwa ni watu, miti, wadudu, mizimu, misitu, wanyama, mawe na mashetani. Senkoro (2011) anasema wahusika ni watu, au viumbe waliokusudiwa wawakilishe dhana, mawazo au tabia za watu katika kazi ya fasihi.

Wahusika wameelezwa pia kuwa ni viumbe ambao hutenda na kutendewa. Wanatumiwa na msanii kusimamia hali mbalimbali za binadamu katika jamii wanamoishi. Wahusika wanazungumza na kuzungumziwa... Wahusika ni viumbe maalum wa mtunzi kwa vile ndio wanaotumiwa kutoa picha au kuwakilisha mawazo na fikra au maudhui yake kwa jamii inayowakilishwa na wahusika hao (Masebo, J. na Nyangwine, N. 2000: 142; Mlacha na Madumulla, 1991). Hivyo basi, wahusika katika kazi za fasihi huumbwa ili kujenga mori ya

aina fulani katika hisia za hadhira. Ni wawakilishi wa tabia, matendo, hulka na silka kulingana na muktadha au mazingira fulani maalum yanayoafikiana na mila na desturi za jamii husika. Kwa mfano, wahusika kama sungura hutumiwa kuhadaa hadhira, simba kutishia, mazimwi kuogofya wakati fisi hutumiwa kuchekecha hadhira kwa tabia zao za uroho, ulafi, uzembe na ujinga.

Wahusika ndio nguzo kuu ya dhamira na maudhui katika kazi ya fasihi. Wahusika hutumiwa na mwandishi wa kazi ya fasihi ili kuwakilisha hali halisi ya maisha ya binadamu katika jamii husika. Ili kufahamu sifa za wahusika katika kazi ya fasihi ni muhimu kuangalia: Majina waliyopewa, maneno yao, mwandishi anasema nini kuwahusu, wanatenda nini, wahusika wengine wanawasemaje, wana kazi gani au jukumu gani katika kazi husika; wana mtazamo gani, wana umuhimu gani, kukubalika kwao kama wahusika wa kifasihi na ushahidi na uchangamano wao (Wamitila, 2004).

Kazi zinazoegemezwa katika mitazamo ya kihalisia zinamsawiri mhusika kwa namna inayokaribiana sana na binadamu katika ulimwengu wa kawaida (Wamitila, 2003). Kinyume na kazi zenye kufuata mkondo wa uhalisia, kazi zinazoegemea mkondo wa uhalisiamazingaombwe zinamsawiri mhusika kwa namna isiyokaribiana na binadamu katika ulimwengu wa kawaida. Mhusika katika mkondo huu anaweza kufanya mambo ambayo hayawezi kufanywa na binadamu katika ukawaida wake. Wahusika hawa wanaweza kujitokeza katika sura tofauti tofauti zinazotofautiana na binadamu katika ulimwengu wa kawaida katika kazi moja ya kifasihi. Kwa mfano, ujenzi wa wahusika wenye nafsi mbili (nafsi tulivu na nafsi inayotembea ndotoni kichawi na kimazingaombwe). Pia

viumbe wa ajabuajabu kama mazimwi, mashetani, mizuka, mizimu, majitu, majini pamoja na wanyama hurejelewa. Hivyo, mhusika anaweza kujitokeza kama jini, malaika, mfu, mnyama au ndege na pia kuingia pasipoingilika na kula au kumeza yasiyomezeka katika uhalisia. Kwa sababu ya uhalisishaji wa kisaikolojia viumbe hawa wa kufikirika hupewa urazini na kuishi na kutenda kama binadamu wa kawaida kana kwamba ni watu halisi. Wahusika hawa hutumiwa na msanii kusimamia hali mbalimbali za binadamu katika jamii wanamoishi (Njogu na Chimera, 1999; Wamitila, 2003; Hegerfeldt, 2005).

Mturo (2018: 146) anatumia neno wahusika wa kinjonzi anapowaeleza wahusika wa kichawi na wa kimazingaombwe. Anasema:

Wahusika hawa wa kinjozi hutumiwa kueleza na kuwasilisha fikra na uwazaji wa kiwango cha juu na matukio yasiyokuwa ya kawaida. ... usawiri wa wahusika wa kinjozi ni pana mno na huweza kujumuisha bunilizi za kisayansi na kazi za kihalisiajabu (ambazo zinahusishwa na matukio yasiyokuwa ya kawaida na bila kutoa sababu ya kutokea kwake).

Maelezo ya wataalamu hao wa fasihi yanakubaliana na mhimili mojawapo wa nadharia ya uhalisiamazingaombwe unaotumiwa katika utafiti huu unaosema kuwa wasanii wanatumia wahusika wenye nafsi mbili na viumbe wa ajabuajabu kama mazimwi, mashetani, mizuka, majini na kurejelea misitu mikubwa, mito mikubwa, bahari na wanyama. Hivyo basi, wahusika wa ajabu wanakuwa wahusika wa kichawi na wa kimazingaombwe pale wanapotenda au kujitokeza katika hali inayokiuka uhalisia au uasilia wa maumbile au uwezo wa binadamu wa kawaida katika maisha halisi (Onchwati, 2016). Mhimili huo ulisaidia katika ubainishaji wa wahusika wa kichawi na wa kimazingaombwe katika riwaya teule.

Hivyo, kuwezesha mijadala na mahojiano nyanjani juu ya uhalisia wa kuwapo kwa watu na viumbe wenye matendo na sifa tajwa katika mazingira asilia ya watunzi wa riwaya teule.

3.2 Wahusika wa Ajabu katika Riwaya Teule

Shaaban Robert na Euphrase Kezilahabi katika riwaya zao teule wametumia wahusika mbalimbali wa ajabu wanaofanya matendo ya ajabu na miujiza ambayo si rahisi kufanywa na watu au viumbe husika katika uhalisia. Kwa hiyo, katika riwaya teule wahusika walibainishwa kwa kuegemea matendo na sifa zao na kuchunguzwa uhalisia wao katika mazingira asilia ya watunzi wa riwaya husika.

3.2.1 Wahusika Wenye Uwezo wa Kujibadilisha Kimazingaombwe na Wanaoishi Kati ya Uhai na Kifo na Kutoweka Kimiujiza na Wenye Kufahamu Mawazo ya Mtu

Katika sehemu hii kumesawiriwa wahusika wenye uwezo wa kujibadilisha kimazingingaombwe, kuishi kati ya uhai na kifo na kuonekana na kutoweka ghafla kimiujiza. Wenye uwezo wa kuona na kufahamu jambo linalotendeka mbali, na wenye uwezo wa kusoma na kufahamu mawazo ya mtu hata bila mtu kusema.

Kujibadilisha kimazingaombwe ni aina fulani ya uchawi na mazingaombwe unaomwezesha mtumiaji wa mbinu hiyo kujibadilisha na kuwa mtu mwingine au kitu kingine. Mtumiaji anaweza kujigeuza kiumri, umbo, na hata jinsi na pia kubadili vitu mbalimbali katika maumbo tofauti au kuwa vitu vingine tofauti kabisa (Manga na Anime, 1989). Mpalanzi (2018) anashadidia mawazo hayo ya

Manga na Anime kuwa kuna watu wenye uwezo wa kutumia miujiza au mbinu mbalimbali za kifantasia ikiwa ni pamoja na uwezo wa kutembea juu ya maji, kujibadilisha kuwa ng'ombe, nyoka, mizimu, mti wa mrumba au mpingo.

Maelezo ya wataalamu hao yanaonesha kuwa kuna watu wenye uwezo mkubwa wa kufanya miujiza kiasi cha kumbadilisha mtu au kitu au kujibadilisha mwenyewe na kuwa mtu mwingine au kitu kingine tofauti kabisa na umbo lake au sura yake asilia. Kitendo kama hicho cha kujibadilisha hakiwezi kuelezwa wala kufumbuliwa kwa kutumia nadharia za kihalisia wala kuthibitishwa kwa kutumia mbinu za kisayansi bali kwa kutumia nadharia ya uhalisiamazingaombwe pekee (Hegerfeldt, 2005).

Katika wilaya ya Rorya mkoni Mara nchini Tanzania, kwa mfano, kulikuwa na mtu kwa jina la Sango Ochwera (Sango alifariki mwaka 2011). Huyo alikuwa na uwezo wa kujibadilisha sura kuwa mwanamke, mnyama au kitu chochote kile apendavyo. Siku moja alijibadilisha fisi na watu (pamoja na mtafiti mwenyewe) wakawa wanamfukuza. Katika kumfukuza huko, alijibadili tena na kurudia sura yake ya kibinadamu na kuwacheka waliokuwa wanamfukuza kwa kuwaambia “Kwa nini mnamfukuza Sango Ochwera, nimewakosea nini mimi!” Inasemekana kuwa sio mara moja wala mara mbili Sango kufanya matukio hayo ya kubadilika na kuwa kiumbe kingine bali ilikuwa ni mazoea yake ya mara kwa mara. Matendo kama hayo yanapofanywa na mtu au kufanyiwa mtu inakuwa ni ukiamambile. Hii ni kwa sababu si jambo la kawaida katika uhalisia mtu kubadilika au kubadilishwa sura na kuwa fisi, nyani au mbwa.

Mpalanzi (2018), akizidi kuisitiza uwezo wa wachawi kufanya mazingaombwe na hata kubadilisha watu kuwa viumbe wengine anasema:

Mazingaombwe ni ufundi wa kutumia dawa ili kugeuza hali fulani na kuyaona masuala fulani kinyume cha uhalisia. Dhima ya mazingaombwe ni kuwahadaa watu. Kwa kutumia nguvu za miujiza, kundi hili hutumia ulaghai, hila na mbinu nyingine kama kutembea juu ya maji, moto na hata juu ya miiba. Wakati mwingine hugeuza watu kuwa paka, nyoka, mijusi, mbwa, simba na kadhalika.

Osore (2008) anaelezea kujibadilisha kimazingaombwe kama mabadiliko ya matukio na wahusika yanayohusishwa na ukiamambile kutoka hali fulani ya maisha au uwapo kwenda hali nyingine. Kujibadilisha kimazingaombwe ni fumbo au muujiza wa kushtukisha unaoshangaza na wa kutatanisha. Ukweli wake kukubalika katika maisha halisi na ya kila siku kwa akili ya kawaida kunabaki kuwa ni swali ambalo kiini cha jibu lake kinabakia kuwa kisasili. Ni jambo lisiloweza kuelezeka wala kufumbuliwa kisayansi au kwa kutumia mantiki au akili ya kawaida ya binadamu bali kwa kutumia uhalisiamazingaombwe. Lengo mojawapo la kutumia mbinu hii ni kuelezea mambo ya kawaida kwa njia isiyo ya kawaida. Zamora (2005) anasema kuwa uhalisiamazingaombwe utambulishwa kwa sifa yake ya kuunda maana ya kimazingaombwe kwa kuangalia vitu vya kawaida kwa namna isiyo ya kawaida.

Shaaban Robert katika riwaya ya *Adili na Nduguze* amemtumia mhusika jini, Huria binti Kisasi, kujibadilisha kimazingaombwe kwa namna na kwa sababu mbalimbali: Huria anajibadilisha kuwa viumbe mbalimbali ili kujiokoa au kumkwepa jini, Hunde mfalme wa Ngazi, aliyetaka kumuua kwa sababu Huria alikataa posa yake. Hunde anakusudia kumwonyesha Huria uwezo wake. Kwa

kuogopa kushambuliwa na Hunde, Huria alijibadilisha sura kila alipotoka kutembea. Hata hivyo kila Huria alipojibadilisha Hunde naye alijibadilisha na kunusa harufu ya Huria kama mbwa. Huria alipojigeuza panya, Hunde alijigeuza paka, akiwa paka yeye anakuwa chui, akiwa chui Hunde anajigeuza simba. Siku aliyojigeuza tandu yeye alikuwa nyoka akamfuata. Alipochoka kukimbia alimkamata. Kabla hajamhasiri, Adili alimpiga jiwe akafa (*Adili na Nduguze*, uk. 36).

Huria pia anajibadilisha msichana mzuri ili kumvutia Adili. Anajibadilisha ndege wa kutisha ili kumwokoia Adili baharini alipotupwa na ndugu zake ili kulipa fadhila ya wokovu aliyofanyiwa na Adili alipotaka kuuawa na jini, Hunde mfalme wa Ngazi (*Adili na Nduguze*, kur. 18, 34). Huria anajibadilisha sura za ajabu kila dakika moja ili kuonyesha uwezo wake walipotua kwa ghafla jahazini na Adili kwa lengo la kuwaadhibu Hasidi na Mwivu, ndugu zake Adili. Watu wote jahazini walishikwa na mshangao mkubwa kwa mabadiliko yake ya mfululizo, wakatoshika kuwa aliweza kubadili kitu chochote katika umbo alilotaka. Pia aliwabadilisha Hasidi na Mwivu manyani kama adhabu kwa matendo yao maovu (*Adili na Nduguze*, uk. 40). Namna Huria anavyoweza kujibadili sura na kuwabadili Hasidi na Mwivu manyani hakuwezi kufumbuliwa kwa kutumia sayansi wala kwa nadharia za kihalisia bali kwa kutumia nadharia ya Uhalisiamazingaombwe. Hii inajidhihirisha katika kipengele cha mhimili wa uhalisiamazingaombwe kinachosisitiza kuwa katika uhalisiamazingaombwe kaida za uasilia na uhalisia huvunjwa. Hivyo, binadamu anaweza kujibadilisha au kumbadilisha mtu mwingine sura na kuwa kitu kingine .

Huria ana uwezo wa kufahamu jambo linalotendaka mbali katika mazingira mengine tofauti. Alifahamu kuwa Adili ametoswa baharini na ndugu zake na pia alifahamu kuwa Adili hakuwaadhibi manyani, yaani Hasidi na Mwivu, lakini hakuwepo katika mazingira hayo (*Adili na Nduguze*, uk. 34, 42). Kitendo cha ajabu kisicho cha kawaida cha Huria kufahamu yanayotendeka katika mazingira mengine mbali na pale alipo kinathibitishwa na mhimili wa uhalisiamazingaombwe unaodai kuwa katika uchawi na mazingaombwe mipaka yote huvunjwa. Hivyo, hakuna mpaka kati ya jamii na jamii, nchi na nchi au mbali na karibu, kaida za uasilia na za uhalisia huvunjwa, hivyo, binadamu anaweza kujibadilisha sura na kuwa kitu kingine, kuingia popote bila kizuizi, kuzungumza na viumbe wengine na kufa na kuishi kwa wakati mmoja (Roh, 1925).

Shaaban Robert amewatumia wahusika wanaojibadilisha kimazingaombwe, wanaoweza kufahamu jambo linalotendeka katika mazingira mengine mbali na pale walipo na hata kufahamu jambo litakalotokea kabla halijatokea kwa kuathiriwa na mazingira yake asilia. Katika mazingira asilia ya Shaaban Robert matukio ya majini kujigeuza kuwa binadamu na hasa kuwa wasichana wazuri ni ya kawaida sana kiasi cha mpaka kati ya ulimwengu wa majini na wa wanadamu kuwa nyembamba sana. Kwa mfano, kisa cha jini kumwacha mtu uchi juu ya mbuyu mwaka 1967 barabara ya 18 Tanga Mjini (taz, uk. 83). Mtu huyo alimtongoza jini akifahamu kuwa ni msichana, lakini alipoachwa juu ya mbuyu uchi ndipo ilipojulikana kuwa alihadaishwa na jini aliyejibadilisha kuwa msichana.

Mara nyingi majini yamejigeuza wanawake wazuri ili kuwaadhibu wanaume wenye tabia ya kumtongoza kila mwanamke mzuri hata bila kumfahamu mwanamke huyo ni nani. Mfano mwingine wa majini kujibadilisha wanadamu na hata kuchukua sura halisi ya mtu anayefahamika ni wa dereva na jini (taz, uk. 70).

Katika jamii ya Shaaban Robert, licha ya majini wanaoweza kujigeuza watu au viumbe wengine (taz, kur. 70, 83), lakini kuna watu waliokuwa na uwezo wa kujigeuza kuwa viumbe wengine. Kwa mfano, Kibwana Jafari aliweza kujigeuza kiumbe kingine kulingana na muktadha. Akitaka kupita pori lenye wanyama wakali alijibadilisha simba. Akitaka kuvuka mto wenye maji mengi alijigeuza mamba ili avuke na akitaka kusafiri au kupita sehemu bila kutaka kuonekana alivaa hali ya utupu ili asionekane (taz, uk. 62). Kibwana Jafari alikuwa na uwezo wa kusoma na kufahamu mawazo ya watu na hata kufahamu matukio yatakayotokea katika jamii yao kabla ya kutokea kwa matukio hayo.

Shaaban Robert ametumia kujibadilisha kwa Huria kuwa viumbe mbalimbali katika azma ya kumkwepa Hunde kuelezea uchafu, uchoyo na ukandamizaji unaofanywa na wanaume wasioadilika. Wanaotumia nguvu, vyeo na uwezo wao kifedha kutaka kuwaoa wanawake. Amewatumia Huria binti Kisasi na jini, Hunde waziri wa Ngazi, aliyetaka kumwoa Huria kwa nguvu kama mfano kuelezea uovu, uchafu na ubinafsi wa wanaume ufisadi unapowapofusha. Hivyo, wanatakiwa wazazi kama Kisasi wenye mtazamo na maamuzi ya dhati katika kuwatetea binti zao na kuwaokoa katika makucha ya wanaume mafisadi ambao ni vigumu kwa wasichana kujinasua kutoka kwao kwa nguvu zao wenyewe. Hii ni

kwa sababu Kisasi alipigana na Hunde na kumshinda akakimbia (*Adili na Nduguze*, uk. 36). Zaidi ya yote wanatakiwa wanaume wenye huruma kama Adili ili kuwaokoa wasichana kwenye makucha ya ufisadi na inda ya wanaume wanaolazimisha kuwaoa wanawake bila ridhaa yao.

Shaaban Robert kwa kumtumia Huria kukataa posa ya Hunde aliyetaka kumwoa kwa nguvu bila ridhaa yake, anakusudia pia kueleza kuwa wasichana wanatakiwa kuwa huru kukubali kuolewa bila wanaume kuwalazimisha kwa kutumia vyeo vyao, pesa zao au kwa sababu tu ya mfumo dume ambao mara nyingi unampa mwaname nguvu ya kumchagua mwanamke amtakaye wakati mwanamke akinyimwa haki hiyo. Wanaume wenye mawazo hasi kama hao hawafai na Shaaban Robert anasema wanastahili kuuawa. Hii ndiyo maana Shaaban Robert amempa mhusika wa jinsi ya kike jina ‘Huria’. Jina la Huria limetokana na neno ‘Huru’ likimaanisha uhuru wa kutobanwa katika kutoa maamuzi au kufanya jambo lolote (Wafula, 1989).

Huria yu huru kufanya jambo lolote bila kuwajibika kwa yeyote katika matendo yake. Anakataa posa ya Hunde (jini) bila kushawishiwa na cheo na nafasi ya Hunde kama waziri wa Ngazi. Hii ni sawa na tamko la sheria ya ulinzi wa wanawake dhidi ya ukatili wa kijinsia Tanzania kifungu cha 16 kinachompa mwanamke haki ya kuingia katika ndoa pasipo kulazimishwa na mtu yeyote pamoja na uhuru wa kutoa mawazo bila kuzingatia tofauti za kijinsia (WiLDAF Tanzania, 2011).

Huria anatoa na kutekeleza maamuzi ya kumsaidia Adili katika tatizo lolote. Anawabadilisha Hasidi na Mwivi manyani na kumwamuru Adili kuwahadhibu kila siku. Yote haya anayafanya bila kuwashirikisha wazazi wake. Hii inaonesha kuwa majini yanatoa nafasi kubwa ya uamuzi kwa watoto wao wa kike kwa masuala yanayohusu maisha yao bila ya kuwaingilia tofauti na ilivyo kwa wanadamu. Hata hivyo kwa masuala mazito yanayohusu kubadilisha maamuzi waliyopitisha, wanalazimika kuomba ushauri kwa wazazi wao. Kwa mfano, Huria alipoombwa kuondoa adhabu ya kupigwa mijeledi na kuondolewa uhayawani Hasidi na Mwivu, alilazimika kuomba ushauri kwa baba yake, Kisasi mfalme wa majini (*Adili na Nduguze*, uk. 47). Kwa hiyo, Shaaban Robert anasisitiza zaidi kuwa watoto nao wanatakiwa kufahamu mipaka ya uhuru wao katika kutoa maamuzi. Hii ina maana kuwa uhuru usio na mipaka ni mbaya kuliko utumwa. Kwa kuzingatia hili Huria alipopewa barua ya Rai, mfalme wa Ughaibu, ya kuomba Hasidi na Mwivu kuondolewa uhayawani, hakutoa maamuzi peke yake bali aliipeleka kwa baba yake, Kisasi mfalme wa majini ili washauriane. Baada ya kushauriana, ombi la Rai lilikubaliwa na hivyo Hasidi na Mwivu waliondolewa uhayawani (*Adili na Nduguze*, uk. 47).

Shaaban Robert amemtumia pia Huria kujibadilisha ndege wa kutisha ili kumwokoza Adili katika hatari ya kufa maji, na hivyo kufanikisha azma yake ya kulipa fadhila na ahadi aliyotoa kwa Adili kueleza kuwa wema hauozi. Adili alimwokoza Huria mikononi mwa Hunde na sasa Huria naye amemwokoza Adili asizame baharini. Mwandishi anasisitiza kuwa wema asilia ni njema zaidi na ina thamani kubwa. Haiwezekani kulipika lote milele hata kama itatumika gharama kubwa kiasi gani. Kwa kusisitiza hili anasema:

Adili...alijibu. Deni langu limekwisha lipwa lote. Niliokoa maisha ya binti yako naye ameokoa yangu. Hapana deni tena kati yetu...Malkia wa majini alitabasamu akasema,...Wema wako ulikuwa asilia, nawe ulitangulia kuutenda; wa binti yangu ulikuwa wa kuigiza, naye ameutenda nyuma. Asili ya uigaji ni vitu mbalimbali. Havilinganiki wala havitalinganika milele (*Adili na Nduguze*, uk. 36).

Shaaban Robert kwa kumtumia Huria kujibadili ndege na kumwokoia Adili baharini, licha ya kuonekana kuwa Huria ametumia gharama kubwa kuliko Adili aliyetupa tu jiwe na kumwokoia Tandu, yaani Huria mwenyewe, mikononi mwa nyoka, yaani jini Hunde waziri wa Ngazi, lakini kwa kuwa Adili aliwahi kutoa msaada wake mwanzo bila kutarajia malipo yoyote, msaada wa Adili ni wa thamani zaidi na chochote atakachofanya Huria kwa Adili hakitatosha kulipa fadhila ya kile alichokifanya Adili. Hii ni sawa na msaada wa wazazi kwa watoto wao. Mzazi anashughulika na mtoto tangia akiwa tumboni, anapozaliwa, maisha ya utotoni mpaka mtoto atakapofikia umri wa kujitegemea. Mtoto huyo hata akiwa na uwezo kiasi gani, hawezi kusema kuwa anaweza kulipa gharama ya malezi aliyopatiwa na wazazi wake, na kudai kuwa amemaliza kulipa deni la wazazi na adaiwi kitu chochote tena na wazazi wake. Kwa maana hiyo, kutoa shukrani na heshima ya kudumu kwa wale waliokufanya kuwa hivyo ulivyo leo, ni jambo la muhimu na linalotakiwa kuzingatiwa na kila mtu.

Kubadilika kwa Huria kimazingaombwe pia kumetumiwa na Shaaban Robert katika riwaya ya *Adili na Nduguze* ili kuisitiza kuwa ni vyema kutenda mema hata bila kumfahamu ni nani unayemtendea. Adili kwa kumwokoia Huria mdomoni mwa Hunde, Huria alibadilika ndege na kumwokoia baharini alipotoswa na ndugu zake. Shaaban Robert anatumia kujibadilisha huku kwa Huria na kuuawa kwa Hunde kueleza falsafa yake ya kuwa uovu hushindwa na

wema siku zote. Na kuwa mshahara wa matendo mema na mabaya huanza kulipwa hapa hapa duniani.

Shaaban Robert anamtumia Huria kujibadilisha sura za ajabu na za kutisha wakati alipokuwa akitoa adhabu ya kuwabadilisha Hasidi na Mwivu manyani kueleza kuwa hakutakiwi kuwa na mzaha katika kukemea au kuawaadhibu waovu. Hivyo yeyote mwenye tabia chafu kama ya Hasidi na Mwivu anastahili kuadhibiwa bila huruma. Pia anamtumia Huria, kuwabadilisha Hasidi na Mwivu manyani, kueleza kuwa kila tendo baya linastahili kuadhibiwa bila kujali kuwa mkosaji ni nani. Sheria zisibadilishwe wala kutungwa kwa kulenga kundi fulani la watu katika jamii bali ziwe kwa ajili ya wote na kwa maslahi ya jamii nzima. Adili alipoomba sana ndugu zake wasiuawe kwa sababu hataeleweka vizuri katika jamii yake kwa sababu hao ni ndugu zake; Huria (jini) alibisha na kusema kuwa sheria za binadamu zinatatiza na hivyo hawataendelea milele (*Adili na Nduguze*, uk. 40).

Suala la haki katika sheria ni miongoni mwa mambo yaliyomshughulisha sana Shaaban Robert karibu katika riwaya zake zote teule. Kwa mfano, Katika riwaya ya *Kusadikika* anasema:

Karibu mashtaka yote yaliyoletwa mbele ya baraza na wafalme, watoto wao, matajiri au watu wengine maarufu yalikutubaliwa bila ya swali wala kiapo (*Kusadikika*, uk.7).

Ingawa hapa Shaaban Robert alikuwa anaizungumzia serikali ya kikoloni ya Mwingereza ya wakati huo, lakini suala hili linagusa serikali nyingi katika nchi

za Afrika ambapo viongozi wengi wanatumia vyeo vyao kufanya watakavyo na kupindisha sheria ili kutosheleza maslahi binafsi (Njoroge, 2014).

Kitendo cha Huria kujibadilisha kimazingaombwe na pia kuwabadilisha wanadamu Hasidi na Mwivu kuwa manyani ni mambo ambayo hayawezi kuthibitishwa kisayansi na wala kufumbuliwa kwa akili ya kawaida bali kwa kutumia nadharia ya uhalisiamazingaombwe. Kwa kuthibitisha hili Roh (1925) anasema kuwa katika uhalisiamazingaombwe kaida za uhalisia na uasilia huvunjwa, hivyo, binadamu anaweza kujibadilisha sura na kuwa kiumbe kingine, kuingia popote bila kizuizi na kuongea na viumbe wengine bila kizuizi cha namna za mawasiliano miongoni mwao.

Hali hizi za kujibadilisha sura na kuwabadilisha binadamu kuwa manyani, licha ya kuwa Shaaban Robert amezitumia kwa kuathiriwa na mazingira yake asilia kama ilivyothibitika, pia ni mbinu aliyochotwa kutoka nduni za fasihi simulizi. Kwa kiwango kikubwa ameiga kutoka masimulizi ya Alfu Lela Ulela (*Alfu Lela Ulela* Kitabu cha Kwanza, uk.10).

Kezilahabi naye amewatumia wahusika wanaojibadilisha kichawi na kimazingaombwe katika riwaya zake teule. Katika riwaya ya *Nagona* kujibadilisha kunaonekana kwa mhusika Paa. Paa anajitokeza kama mnyama ambaye anafuatiliwa nyayo zake. Anajitokeza kama kiumbe kilichofunikwa gubigubi na chenye uwezo wa kucheza bao na wanadamu, anajitokeza kama msichana mrembo na Msimuliaji Msaka Paa anamwita binti (*Nagona*, uk. 34). Mwindaji msaka paa hapa anamlinganisha paa na msichana.

Katika ngoma kuu, kizee kinamtia nguvu Msimuliaji kucheza. Anapomwambia kupiga magoti na kutazama chini, ghafla kitu kizito kinakaa juu ya mabega yake (*Nagona*, uk. 60). Kitu hicho kilichomkalia mabegani ni paa. Hashikiki mwili wake unateleza, si rahisi kumjua na kukuingiza katikati ya duara. Ni msichana mzuri ambaye hajapata kuonekana (*Nagona*, uk. 34). Paa akiwa katika umbo la msichana mzuri, akiwa kibandani na Mwindaji msaka paa, mwili wake unatoa mwanga na kumulika kibanda chote. Mwandishi anasema:

Niliona mwili wake unanza kutoa mwanga. Mwanga uliongezeka ukamlika kibanda kizima...Paa anakimbia huku mwili wake ukitoa mwanga, anaruka milima na kupotea (*Nagona*, uk. 37, 38).

Paa ana uwezo wa kujitokeza kama mnyama, kama msichana mzuri, kama kiumbe chenye kutoa mwanga, mwenye uwezo wa kuruka milima na kama kitu kisichojulikana. Kiumbe kama hicho kinachobadilikabadilika ni muujiza kupatikana katika maisha halisi. Hii ni kwa sababu ni muujiza kumpata katika uhalisia binadamu anayeweza kubadilika na kuwa mnyama kama paa, mwili wake kutoa mwanga kiasi cha kumulika chumba kizima, mwenye uwezo wa kuruka milima na pia kuwa kitu kizito cha ajabu kinachoweza kumkalia mtu mabegani na kumbana kwa mapaja yake.

Hali hii ya kubadilikabadilika haiwezi kuelezeka wala kufumbuliwa kwa kutumia nadharia za kisayansi au kaida za kijadi zenye mwono moja tu wa uhalisia. Kinyume chake katika kujibadilisha kimazingaombwe maajabu hayo yanafumbuliwa na kuonekana kama matukio ya kawaida na ya kila siku katika maisha ya mwanadamu. Hii ni sawa na mawazo ya Faustine (2019) anayesema:

Kujibadilisha kimazingaombwe ni mtindo wa kifasihi wenye sifa ya kuyaelezea matukio ya ajabu kama vile uchawi, mazingaombwe na fantasia kwa namna ya moja kwa moja isiyokinzana na ukweli au uhalisi wa maisha, na kuyafanya yaonekane kama ya kawaida (msisitizo ni wetu).

Paa anapojibadilisha msichana anakuwa na uwezo wa kumsoma mtu na kufahamu anayoyawaza. Mwandishi anasema:

Sasa tulikuwa wawili tu. Mimi mwindaji na paa... Nilianza kujiuliza moyoni, “Huyu msichana ni nani kwangu, na mimi ni nani kwake.” Alisimama. Alinitazama, akatabasamu. “Najua” alisema,... Unafikiri msichana ni nani kwa mvulana ambaye ameingia katika duara yake?... Nilianza kujiona mtu mzima tayari kushika madaraka na majukumu, “Je nimekua?” nilijiuliza kimoyomoyo. Aligeuka tena. “Najua umekua. Lakini haitakuwa! Labda siku ya ngoma kuu, nitakapokukalia mabegani na kubana shingo lako kwa mapaja yangu...” (*Nagona*, uk. 36).

Paa kuwa na uwezo wa kumsoma mtu na kufahamu anayoyawaza kunazidi kudhihirisha kuwa Paa ni mhusika wa ajabu. Uwezo wa paa kusoma mawazo ya mtu na kueleza matamania yaliyofichwa moyoni mwa mtu ni sawa na Raguna, mhusika mwanamke, katika riwaya ya *The Tin Drum* ya Grass Gunter. Raguna ana uwezo mkubwa wa kuona mpaka ndani ya nyoyo za watu. Anaweza sio tu kufichua yaliyomo moyoni mwa watu kwa usahihi bali pia kufichua siri za maisha yao vile vile (Waliaula, 2010).

Kujibadilisha kimazingaombwe kunajitokeza pia kwa mhusika Nagona. Babu anapoulizwa na mjukuu wake kuwa Nagona ni nini, anasema kuwa mtu yeyote mwenye uwezo wa kufikiri amepata kumjua. Anasema kwa muda wote wa uhai wake Nagona alimpiga chenga, mara nyingi alimwona kwa mbali na mara chache sana alikaribiana naye. Hakuweza kumweka mikononi mwake alipokaribiana naye. Daima alirudi kinyumenyume. Alipokuwa mvivu wa

kufikiri Nagona alimpotea kabisa na alipofikiri kwa makini alimtokea tena. La ajabu hata wale waliofanikiwa kumtia mikononi daima aliwaponyoka. Nagona yu karibu na kila mtu yuko popote tena pa wazi. Nagona anaonekana kama mtu atajituliza na kufikiri zaidi na kuona zaidi ya fikra. Nagona ni mwanga, ni kama jua lililopatwa na mwezi. Ukimwona hamu ya kumwona haliishi, akitoweka utamtafuta kila mahali. Kwenye mwanga Nagona hakosekani. Alipo uwongo umejitenga. Nagona hawezi kukuruhusu awe wako peke yako, ni wa kila mtu. Kila mtu anamtambua ndiyo maana anavuta na anaambaa (*Nagona*, uk. 44, 45).

Katika ngoma kuu Nagona anajitokeza tena. Mwandishi anasema:

Nilipotazama juu niliona mwanga ukipanda juu na kuacha giza kwetu. Kizee kilipiga kelele “Nagona”! Sauti yake haikuwa ya kizee tena...Sote sasa tulipiga kelele tukitazama juu, “Nagona! Nagona”! Polepole mwanga ulipanda juu ukatoweka kabisa, tukabaki gizani (*Nagona*, uk. 60).

Nagona pia anajitokeza kama mtoto mdogo wa kike anayezaliwa siku si zake kwa sababu ya kelele za vurumai za siku ya ngoma kuu. Nagona anajulikana kama mkombozi wa pili. Nagona kama alivyo Paa hujibadilisha na kuonekana kwa namna mbalimbali. Hali ya kubadilikabadilika kwa Paa na Nagona si ya kawaida katika maisha ya kawaida. Uwezo wa kufahamu awazoyo mtu, kuwa mwanga, kuonekana kama jua lililopatwa na mwezi na kama mtoto anayezaliwa kabla ya siku zake, ingawa mimba yake ni ya mamilioni ya miaka ni hali ambayo haiwezi kuelezwa kwa kutumia nadharia za kihalisia wala kuthibitishwa kisayansi bali kwa kutumia nadharia ya Uhalisiamazingaombwe. Hii inathibitishwa na mhimili wa Uhalisiamazingaombwe unaosema kuwa katika uhalisiamazingaombwe kaida za uasilia na za uhalisia huvunjwa. Hivyo, binadamu anaweza kujibadilisha sura

na kuwa kitu kingine, kuingia popote bila kizuizi, kuzungumza na viumbe wengine na kufa na kuishi kwa wakati mmoja (Roh, 1925).

Wafuasi wa uhalisiamazingaombwe wanaamini kuwa kuna wahusika wenye uwezo wa kufahamu mawazo yaliyojificha moyoni mwa mtu, wenye nafsi mbili (nafsi tulivu na nafsi inayotembea ndotoni kichawi na kimazingaombwe) na wanaoweza kujibadilisha kimazingaombwe (Mbiti, 2011; Macha, 2017; Faustine, 2019).

Wataalamu hao wanasisitiza kuwa, kwa imani za Kiafrika mchawi ni mtu mwenye nguvu za kimiujiza zinazomwezesha kutenda mambo mbalimbali yasiyo ya kawaida kama vile, kusababisha vifo, kujibadili au kumbadili mtu au kitu kingine katika sura au maumbo mbalimbali pamoja na kuwatumia viumbe wengine kutenda mambo mbalimbali tofauti na uhalisi wao.

Kezilahabi kwa kutumia kujibadilisha kwa paa (kufikiri) na nagona (kweli) anasisitiza umuhimu wa kufikiri ili kuupata kweli. Ili kuupata kweli na kuumiliki kunatakiwa kufikiri kwa makini na kwa dhati ya moyo ili kuyafahamu hata yale yaliyofichika katika nyoyo za watu. Kufikiri kunapopungua kweli uambaa na kutoweka, lakini kunapokuwa na kufikiri kwa makini kweli hujitokeza tena. Kezilahabi kwa kutumia kujibadilisha kwa paa na nagona anasisitiza kuwa kweli inatakiwa iwepo popote. Kila mmoja anatakiwa kuwa mkweli, kwa sababu kweli ni mali ya kila mtu na palipo na kweli uwongo umejitenga (*Nagona*, uk. 44).

Ingawa Shaaban Robert amemtumia Huria kama mhusika anayeweza kuonekana na kutoweka kimiujiza lakini wahusika wa namna hao wametumiwa sana na

Kezilahabi Katika riwaya ya *Mzingile*. Mfano ni mwanamke anyefuatana na Msimuliaji kimiujiza. Matendo na jinsi Mwanamke huyo anavyojitokeza na kutoweka ghafla peupe yanaonesha kuwa ni mhusika wa ajabu. Mwili wa mwanamke huyo unatoa mwanga wa kutosha kumulika njia, anaweza kuingia ndani ya nyumba hata milango ikiwa imefungwa. Ni mke wa Msimuliaji ingawa alikufa zamani. Hivyo, anaishi kati ya uhai na kifo. Zaidi ya yote ndiye mwanamke ambaye anaolewa tena na Msimuliaji na wanashirikiana kuanzisha dunia mpya (*Mzingile*, kur. 11, 12, 15, 112, 113).

Msimuliaji alipoamka usingizini jangwani alikuta khanga na kibuyu cha maji kilichoachwa na mwanamke huyo. Alipotazama kwa mbele kidogo alimwona mwanamke huyo amelala chali uchi. Alitembea kumwelekea akimeza mate mara mbilimbili kwa hamu ya kufanya naye ngono. Mwandishi anasema:

Nilipomkaribia nilimrukia juu kumkumbatia na kumpapasa hali nikisema kwa sauti “Nakupenda! Karne na karne nikikutafuta wewe!” Pale nilipoangukia hapakuwa na mtu. Palikuwa na mchanga uliokuwa kama tuta. Hakuna nilichoshika, isipokuwa mchanga. Nilichobusu ni mchanga. Niliutupa chini nikawa najipangusa mchanga uliokuwa umeenea mdomoni. Nilirudi kwenye kibuyu cha maji nikitema tema mchanga uliodhihaki upweke wangu na matamano yangu (*Mzingile*, uk. 15).

Hili ni tukio la ajabu, la kuchekesha na la kushangaza, na kama angelikuwepo mtu mwingine karibu na kumwona mtu akirukia hewani na kusema ninakupenda akidhania kumbusu mwanamke na kuishia kubusu mchanga angecheka na kuvunjika mbavu. Swali la kujiuliza ni kuwa mwanamke aliyekuwa anataka kubusiwa na Msimuliaji alipotelea wapi? Mwanamke huyu ni mhusika wa ajabu, ni kama mzuka. Hii ni kwa sababu binadamu wa kawaida anaweza kufanya maajabu lakini hawezi kuwa na uwezo wa kuvaa sura ya utupu na kupotea peupe

na asionekane kabisa. Hata hivyo, katika uchawi na mazingaombwe hii ni hali ya kawaida. Uhalali wa maoni hayo unathibitishwa na mhimili wa uhalisiamazingaombwe unaosema kuwa, wasanii hutumia mtindo wa ukumbushaji, mbinu rejeshi na ujenzi wa wahusika wenye nafsi mbili (nafsi tulivu na nafsi inayotembea ndotoni kichawi na kimazingaombwe). Pia mazingira hupewa kipaumbele na viumbe wa ajabuajabu kama mazimwi, mashetani, mizuka, mizimu, majini pamoja na misitu mikubwa, wanyama, mito na bahari hurejelewa.

Mturo (2018) anashadidia kuwa katika uchawi na mazingaombwe msanii anaweza kutumia wahusika wenye nafsi mbili na kurejelea wahusika wa ajabu kama mazimwi, mashetani, mizuka, majini pamoja na misitu mikubwa.

Katika mazingira asilia ya Kezilahabi wachawi wana uwezo wa kujibadilisha sura na kuchukua sura ya mtu mwingine au sura ya kiumbe kingine chochote na kutumia sura hiyo katika shughuli za uchawi. Kwa mfano, Kisa cha mchawi kumbadili mamba kuwa kijiti na kisa cha mchawi kutumia sura ya mke wa Malezo kufanyia uchawi usiku. Pia mchawi anaweza akajitokeza mbele yako na kutoweka ghafla peupe hasa wakati wa usiku akiwa uchi kabisa. Zaidi ya yote wafu kuwaita au kuwatokea ndugu zao na kuomba, kwa mfano, maji na kutoweka wanapoleteka kile walichoomba ni hali ya kawaida kabisa katika kisiwa cha Ukerewe (taz, kur. 99, 100). Hii inadhihirisha kuwa Kezilahabi ameathiriwa na mazingira yake asilia katika kutumia wahusika wa ajabu katika riwaya teule.

Mambo mawili yanajitokeza katika kumtumia huyu mwanamke wa kimiujiza. Jambo la kwanza ni utata wa Kezilahabi kutokuwa na uhakika wa hali ya maisha baada ya kufa. Msimuliaji anasumbuliwa na mawazo kuwa je, mtu anaweza kuishi baada ya kufa? Na je, kama kuna kuishi baada ya kifo maisha hayo ni ya namna gani na yana uhalisia kiasi gani? Swali hili linakosa majibu katika riwaya ya *Mzingile*.

Jambo la pili linalozungumzwa na Kezilahabi kutokana na mwanamke huyu wa kimiujiza ni tamaa ya ngono. Hii inasababishwa na mwanamke wa kimiujiza kujitokeza kwa Msimuliaji akiwa uchi. Hata hivyo, Msimuliaji hachukii kumwona mwanamke huyo akiwa uchi bali anavutiwa na hali hiyo na hivyo kumrukia ili kutosheleza tamaa yake ya tendo la ngono. Swali la kujiuliza ni kuwa kuongezeka kwa vitendo vya ubakaji na ngono nje ya ndoa kunasababishwa na wanawake kuvaa nusu uchi au tabia ya wanaume kufurahia kuwatazama wanawake wakiwa wamevaa hivyo ?

Kezilahabi kama mwandishi fuatishi, kutumia wahusika wa ajabu wanaojibadilisha kimazingaombwe, wanaoishi kati ya uhai na kifo na kutoweka kimiujiza na wenye kufahamu mawazo ya mtu, ameathiriwa na kutoathiriwa kwa viwango tofauti na Shaaban Robert. Kwa kuwatumia paa na nagona kujibadilisha kimazingaombwe katika riwaya ya *Nagona*, Kezilahabi ameiga kujibadilisha kimazingaombwe kwa Huria katika riwaya ya *Adili na Nduguze* ya Shaaban Robert. Jinsi Huria anavyojibadilisha kwa namna mbalimbali, ndivyo wanavyojibadilisha paa na nagona. Hata hivyo uigaji wa Kezilahabi si wa moja kwa moja kwa sababu namna paa na nagona wavyojibadilisha ni tofauti na

anavyojibadilisha Huria. Bloom (1925) anaelezea namna hiyo ya athari kwa kusema kuwa kwa kumwiga, msanii fuatishi huendeleza mada na mawazo ya msanii tangulizi lakini siyo kwa mwigo sisisi bali anayakamilisha kwa namna nyingine inayoonesha kuwa msanii tangulizi inawezekana alishindwa kuyakamilisha. Hapa msanii fuatishi mara nyingi anatumia “tabaini” kuendeleza mawazo hayo ya msanii tangulizi.

Aidha, kuna mbinu ya upotoshaji inayojitokeza katika tofauti kati ya Huria na Paa. Huria licha ya kujibadilisha mwenyewe ana uwezo wa kubadilisha watu kuwa viumbe wengine. Kwa mfano, aliwabadilisha Hasidi na Mwivu kuwa manyani. Hili halifanywi na Paa wala wahusika wengine wa ajabu wa Kezilahabi. Kinyume chake, Paa amepewa uwezo wa kusoma mawazo ya watu wengine na kufahamu wanayoyawaza hata bila ya wao kusema, uwezo ambao hauonekani kwa Huria wala kwa wahusika wengine wa Shaaban Robert. Kwa hiyo, hapa Kezilahabi amejaribu kutumia ugeuzaji kama mbinu mojawapo kati ya mbinu tano za upotoshaji ili kujiengua kutoka kwa athari za Shaaban Robert. Bloom (1973) anathibitisha hili kwa kusema kuwa msanii fuatishi hujaribu kujiengua kutoka kwa athari za msanii tangulizi kwa kutumia mbinu za kiisimu ili kuleta athari au fikra mpya katika kazi za fasihi kwa kujitenga na athari za msanii tangulizi. Msanii fuatishi hufanya hivyo kwa kutumia mbinu tano za upotoshaji za kiisimu ambazo ni: udondoshaji, uhamishaji, udunishaji, ujalizaji, na ugeuzaji.

Tofauti nyingine kati ya Kezilahabi na Shaaban Robert katika usawiri wa wahusika wa ajabu, ni matumizi ya mwanamke anayejitokeza na kutoweka kimiujiza na ambaye anaishi kati ya uhai na kifo katika riwaya ya *Mzingile*. Ingawa uwezo wa kutoweka ghafla kwa mwanamke huyu unaweza

kufananishwa na Huria katika *Adili na Nduguze* ya Shaaban Robert, lakini hali yake ya kuishi kati ya uhai na kifo haionekani kwa wahusika wa ajabu wa Shaaban Robert. Hivyo, kwa kumtumia huyu mwanamke wa kimiujiza Kezilahabi amebadili mada kwa kuachana na mada ya msingi ya Shaaban Robert ya kujibadilisha kimazingaombwe. Bloom (1973) anasisitiza hili kwa kusema kuwa hapa msanii fuatishi anajitahidi kubuni kwa ufundi wa hali ya juu mada nyingine tofauti kabisa na mada ya msanii tangulizi. Msanii fuatishi anafanya hivyo kwa kujitahidi kujitenga au kuachana na mada ya msingi ya msanii tangulizi ili kuonesha dhahiri kuwa kazi yake ina nguvu kuliko ya mtangulizi wake. Lengo la msanii fuatishi likiwa ni kujijengea utukufu au jina binafsi mbali na msanii tangulizi.

3.2.2 Wahusika kama Majitu na Wenye Matendo na Nguvu za Ajabu

Katika sehemu hii kumesawiriwa wahusika wenye nguvu za ajabu wanaoweza kubeba viumbe wakubwa kama nyangumi, wanaoweza kunusa harufu kama mbwa, wanaoweza kubeba na kuhamisha milima, kunywa maji yote ya mto, kufuata kitu kilicho mbali sana kwa kukunjua mguu na wanaoweza kukaa na mimba kwa maelfu ya miaka.

Shaaban Robert katika riwaya ya *Adili na Nduguze* anamtumia Mrefu kama jitu refu la ajabu na lenye nguvu kupindukia. Mwandishi akimweleza Mrefu anasema:

Mrefu alikuwa mwujiza katika viumbe. Alikuwa na miguu mikubwa na mapaja manene, kiuno cha utambo na kifua kipana; na shingo yake ndefu ilichukua kichwa kikubwa. Mabega yake ya mraba yalining'iniza chini mikono iliyokuwa na nguvu kama manjanika. Kwa kimo cha kukithiri alitembea baharini bila ya kuguswa na maji magotini, akafikia vilele vya milima kwa mikono yake. Aliweza kukamata ndovu chini au nyangumi baharini akamwoka kwa jua mbinguni. Sauti yake ilikuwa kama radi. Kwa wepesi wake wa ajabu wa kuzunguka dunia nzima kwa sekunde moja, alionekana kama kiumbe kilichoumbwa maalum kuokoa kitu motoni, baharini au katika hatari nyingine (*Adili na Nduguze*, uk. 27, 29).

Maelezo hayo yanadhihirisha kuwa Mrefu si mhusika wa kawaida. Hii ni kwa sababu ni muujiza kumpata binadamu wa kawaida anayeweza kufanana na Mrefu na kufanya anayoyafanya. Mrefu anaweza kutembea baharini bila maji kumfika magotini, mikono yake ni mirefu kiasi cha kufikia vilele vya milima, ana uwezo wa kumkamata nyangumi au ndovu na kumwoka kwa jua mbinguni. Si hivyo tu, bali pia Mrefu ana sauti kama radi na ni mwepesi kiasi cha kuzunguka dunia nzima kwa sekunde moja (*Adili na Nduguze*, uk. 27-28). Uajabu huo wa Mrefu unakubaliana na mhimili wa Uhalisiamazingaombwe unasema kuwa katika uchawi na mazingaombwe wasanii hutumia mtindo wa ukumbushaji, mbinu rejeshi na ujenzi wa wahusika wenye nafsi mbili (nafsi tulivu na nafsi inayotembea ndotoni kichawi na kimazingaombwe). Pia mazingira hupewa kipaumbele na viumbe wa ajabuajabu kama mazimwi, mashetani, mizuka, mizimu, majini pamoja na misitu mikubwa, wanyama, mito na bahari hurejelewa. Mhimili huu ni faafu kwa sababu umeuwezesha utafiti huu kuchungunguza viumbe wa ajabu na wa kufikirika kama Mrefu kama watu wa kawaida wanaopatika katika mazingira halisi katika jamii.

Kinachoshangaza ni kuwa mrefu mbali na uajabu wake, kutisha kwake, uwezo wake, nguvu zake, uchawi na mazingaombwe yake na kuwa mwujiza katika

viumbe; lakini Tukufu mfalme wa mji uliogeuzwa mawe hakuonekana kutishwa wala kutilia maanani maneno ya Mrefu. Mrefu anamtahadharisha Tukufu kuwa mfalme ni naibu wa Mungu duniani na kwa sababu ya amana kubwa aliyopewa anatakiwa kuwa mwadilifu katika matendo yake na kuachana na ibada ya mizimu. Mrefu anasisitiza kuwa kwa sababu ya uzima wa milele ibada ya mizimu ni maangamizi na ni ujinga mtupu (*Adili na Nduguze*, uk. 29).

Tukufu kwa kukita imani yake kwa mizimu anakataa maneno ya Mrefu na kwa hasira na kejeli anasema maneno ya Mrefu ni upuuzi mtupu. Kuwa inawezekana kwa sababu ya urefu wa Mrefu ubongo wake umeyeyushwa na jua. Kama amerogwa mizimu itawakomesha warogaji hivyo akae chini ya kivuli cha mizimu afurahi (*Adili na Nduguze*, uk. 29).

Mbali na Tukufu mfalme wa Fahari mji uliogeuzwa mawe, kukataa maonyo ya bure kutoka kwa Mrefu, hata hivyo naye anashadidia kuwa Mrefu kwa sababu ya urefu wake unaomfanya akaribie jua inawezekana jua limeunguza ubongo wake na hivyo kuharibu akili yake. Pia kwa uwezo wa Mrefu kuokoa kitu hatarini na kwa wepesi wake wa ajabu, na kuonekana kama kiumbe kilichoumbwa maalum kuokoa kitu motoni, baharini au katika hatari nyingine, Mrefu alimwoko Mwelekevu alipojitosa baharini (*Adili na Nduguze*, uk. 49).

Katika mazingira asilia ya Shaaban Robert kuna visa vya kweli vinavyohusiana na matukio ya kukutana na watu (majini) warefu kupitiliza. Kwa mfano, kisa cha Salehe Zongo na Mrefu (taz, uk. 61). Kwa sababu ya urefu wa Mrefu ambaye kwa maneno ya Salehe inaonekana walikuwa wanasimuliwa kuwepo kwa kiumbe

mrefu aliyeitwa Mrefu, alipitia chini ya magoti katikati ya mapaja ya mrefu akikimbia bila kuona upeo wa kimo cha Mrefu. Alichondelea kusema ni kuwa nimemwona mrefu, nimemwona mrefu. Hii inadhihirisha kuwa Shaaban Robert ametumia viumbe wa ajabu wanaopatikana katika mazingira yake asilia katika utunzi wake katika riwaya ya *Adili na Nduguze*. Shaaban Robert kwa kutumia jina na kisa cha Mrefu ametumia mwigo sisisi kwa kutumia jina lile lile la mrefu kama lilivyotumiwa katika mazingira yake asilia, yaani Machui mkoani Tanga alikozaliwa.

Urefu wa Mrefu unaakisi asili ya ujumbe alioubeba na kuutoa. Urefu wake unaashiria mawanda na mapana ya ujumbe mtakatifu aliokuwa nao. Mrefu anafananishwa na nabii aliyetumwa na Mungu akiwa na ujumbe mtakatifu kwa ajili ya kuokoa wenye dhambi. Shaaban Robert anasema kuwa Mrefu anaonekana kama kiumbe kilichoumbwa maalum kuokoa kitu motoni, baharini au katika hatari nyingine. Kinachomsikitisha Shaaban Robert ni kuwa, kwa sababu ya ibada ya kimizimu, ujumbe wa wokovu ulioletwa na Mrefu ulikataliwa.

Wafula (1989) anasema kuwa ujumbe wa Mrefu kama unavyoelezwa na Shaaban Robert ulikuwa ni ujumbe mzito ambao ni zaidi ya ujumbe unaoweza kutolewa na binadamu wa kawaida kwa wanadamu wenzake. Anaendelea kusema kuwa kukataa ujumbe wa Mrefu ambao Shaaban Robert aliamini kuwa ni kwa ajili ya uzima wa milele kulimfanya awalinganishe watu wa mji wa Fahari (mji uliogeuzwa mawe) na wenye mioyo migumu kama mawe. Watu kama hao kwa sababu ya ugumu wa mioyo yao iliyo kama mawe, ni bubu na ni viziwi na hivyo kuhlalisha hali ya kutokuwa na uhai ndani mwao.

Mrefu katika ujumbe wake anasema kuwa mfalme ni mwakilishi wa Mungu duniani. Kwa hiyo ufalme ni amana kubwa inayotaka uangalifu mkubwa kwa sababu ni dhima bora iliyowekwa mikononi mwa wanadamu. Kwa hiyo, anasisitiza kuwa wajibu wa kwanza wa mfalme ni kuwa mwadilifu katika matendo na maneno yake. Kila tendo, jema au baya ni mfano kwa raia wake. Na atambue kuwa kwa sababu ya maisha ya milele ibada ya mizimu ni ujinga mtupu. Mrefu anamwonya Tukufu kuwa uwezo usio hadhari ni kileo kibaya sana na ni vyema kufikiri kwa makini kabla ya kutoa jibu katika jambo lolote (*Adili na Nduguze*, uk. 29).

Mwandishi Shaaban Robert kwa kumtumia mhusika Mrefu na kisa cha mji uliogeuzwa mawe, inawezekana alikuwa anazungumzia tawala mbalimbali za kijadi katika bara la Afrika za wakati wake, jamii za Tanganyika zikiwemo. Tawala hizi zilikuwa bado zimekita imani zao katika ibada za kimizimu kiasi kwamba ilikuwa vigumu kuacha imani hizo. Hata hivyo, anasisitiza nguvu na uwezo wa imani ya Kikristo na Kiislamu kama suluhisho la kuwaondoa watu katika imani za kimizimu ambayo inaonekana kama upuuzi mtupu. Anasema kuwa ingawa wengi wanaweza kutaka kushikilia umizimu lakini kutokana na uwezo na athari za Ukristo na Uislamu umizimu utashindwa milele. Hii ndiyo maana Tukufu aliyewakilisha ibada ya kimizimu kwa kutojali onyo la Mrefu alisababisha miji mingine yote ya dola yake kugharikishwa, na kila kiumbe kilichokuwa na maisha katika fahari kugeuka jiwe.

Kezilahabi kwa namna inayokaribiana na Shaaban Robert katika riwaya ya *Nagona* anamtumia kizee kinachojitokeza katikati katika ngoma kuu, mwenye sauti kubwa inayoweza kusikika duniani kote. Mwandishi anasema:

Tulijikuta tunasukumwa na nguvu fulani kutoka kwenye kitovu cha duara. Sehemu ya katikati ya duara ikabaki tupu. Mwanga mkali ulijaa ile sehemu ya katikati. Mwanga ulipofifia na kutoweka, tuliona kizee chenye matege na mkongojo kimesimama katikati. Kizee kiliinua mkongojo wake juu kikasema kwa sauti, “Chezeni!”... Niliona kizee kikinijia pale nilipokuwa. Kilinitazama machoni, halafu kikainua fimbo yake na kugusa ushanga wangu wa shingoni. Kilishika nywele zangu za kichwani kikaniburuza hadi kwenye kitovu cha duara. Kiliugusa mwili wangu kwa fimbo kikasema, “Cheza!” Ghafla nilipata nguvu za ajabu... Nilipotazama juu niliona mwanga ukipanda juu na kuacha giza kwetu. Kizee kilipiga kelele “Nagona?” Sauti yake haikuwa ya kizee tena. Ilitoa mwangwi mkubwa ulioweza kusikika ulimwenguni kote (*Nagona*, uk. 59- 60).

Kila Kizee kilipokuwa kikimgusa Msimuliaji kwa fimbo, Msimuliaji alikuwa anapata nguvu zaidi za kucheza. Msimuliaji alipotazama juu na kuona mwanga ukipaa juu na kuwaachia giza, Kizee kilipiga kelele ‘Nagona!’ Na sauti yake haikuwa ya kizee tena. Ilitoa mwangwi mkubwa ulioweza kusikika duniani kote (*Nagona*, uk. 60). Kizee kilipiga kwa fimbo yake sehemu ya katikati ya duara na sehemu hiyo na kitovu cha duara vikazunguka. Matokeo yake palitokeza shimo kubwa na kizee kilitumbukia na kupotea. Hata hivyo shimo lilibaki wazi na wacheza ngoma waliogopa kupasogelea (*Nagona*, uk. 60). Huyu ni mhusika wa ajabu kwa sababu ni muujiza katika uhalisia kumpata mtu ambaye akikugusa tu unapata nguvu, ambaye sauti yake inaweza kusikika kote ulimwenguni na anayeweza kupaa na kuingia katika shimo lililoko angani na kutoweka.

Matendo, maneno, sauti, maumbile, miaka na uwezo wa wahusika wengi waliotumiwa na Kezilahabi katika riwaya ya *Nagona* si ya kawaida na ni muujiza kupatikana kwa wahusika kama hao katika maisha halisi. Hii ina maana kuwa,

“Kezilahabi kwa kutumia miujiza ya wahusika wa ajabu anajaribu kujumuisha na kuchanganya uhalisia na fantasia. Anakusudia kuunganisha na kuvunja mpaka kati ya kweli na uongo, ndoto na urazini, uhai na kifo, sasa na zamani (usasa na ukale), utoto na utu uzima na mbali na karibu. Kwa maana hiyo lengo la kutumia wahusika wa ajabu katika fasihi ni msisitizo wa umoja kati ya mazingaombwe na uhalisia (Flores, 1988).

Katika riwaya ya *Nagona* Kezilahabi anawatumia Nabii, Mtume, Mfuasi na Mtenzi kama wahusika wa ajabu wenye matendo yanayotaka kufafana.

Nabii anajieleza hivi:

Mwanamke hana hatia. Simlaumu. Walinifikiria kichaa, wale ambao hawakuniamini. Vichaa, wazinzi na maskini ndio waliokuwa wa kwanza kunizunguka na kunifuata. Walioteuliwa walijitahidi walivyoweza kuweka katika kumbukumbu niliyoyasema. Tatizo ni fasili na ufafanuzi...Waliniua mimi badala ya kuu Sphinx (*Nagona*, uk.26-27).

Maelezo ya Nabii kujihusu yanaonesha kuwa ni mhusika wa ajabu. Hii ni kwa sababu anasema kuwa aliuawa badala ya Sphinx. Yaani alikufa lakini bado anaongea na walio hai. Kwa hiyo ni mhusika mfu na wakati huo huo anaishi. Kufa au kuuawa ni jambo la kawaida linatokea kila siku katika maisha ya wanadamu. La ajabu na umazingaombwe katika maelezo ya Nabii ni maneno yake. Nabii anasema aliuawa badala ya Sphinx. Hakuna binadamu anayeweza kufa na kuishi kwa wakati huo huo. Yaani Nabii aliuawa lakini bado anaweza kuzungumza tena na walio hai na kueleza yeye mwenyewe kuwa aliuawa badala ya Sphinx. Hata hivyo, katika uchawi na mazingaombwe kuna uwezekano mkubwa wa mtu kufa na kuishi kwa wakati huo. Uwezekano huo unathibitishwa na mhimili wa Uhalisiamazingaombwe unaosema kuwa katika uhalisiamazingaombwe hakuna mpaka kati ya uhalisi na utohalisi. Hii ni kwa

sababu uhalisiamazingaombwe haukubaliani na uhusiano wa kadhia zinazotendeka katika maisha ya mtu kiutengano. Hali kama za uhalisi na ndoto, usasa na ukale, uhai na kifo, mbali na karibu, ugeni na uwenyeji na tamaduni zinaingiliana. Mhimili huu umetumika katika riwaya teule kwa sababu waandishi wametoa mawazo yao kwa namna mbalimbali kama vile kwa njia ya ndoto, kama majini, malaika, mashetani, kama vichaa na hata kama wafu. Hivyo, kwa kutumia mhimili huu mawazo na maoni ya wahusika yamepewa uzito stahiki bila kujali kuwa yametoka kwa njia ya ndoto, au yametolewa na mfu-hai, jini, malaika au mnyama.

Flores (1988) kama alivyonukuliwa hapo juu, anafafanua mhimili huo wa uvunjivu wa kaida kati ya uhai na kifo kwa kusema kwamba, “Uhalisiamazingaombwe unajumuisha uchanganyaji wa uhalisia na fantasia. Unakusudia kuunganisha na kuvunja mpaka kati ya kweli na uongo, ndoto na urazini, uhai na kifo, sasa na zamani (usasa na ukale), utoto na utu uzima na mbali na karibu. Kwa maana hiyo lengo la uhalisiamazingaombwe katika fasihi ni msisitizo wa umoja kati ya mazingaombwe na uhalisia”.

Maelezo ya Nabii bado yanasisitiza tu utata wa Kezilahabi juu ya maisha baada ya kifo. Hii inatokana na imani mbalimbali miongoni mwa jamii za Kiafrika juu ya maisha baada ya kifo, jamii asilia ya Kezilahabi ikiwemo. Kuna wanaoamini kuwa wafu wanarudi kuishi miongoni mwao kupitia: jina lake kutajwa mara kwa mara, kuzaliwa upya katika ukoo wake au kwa jina lake kuendelezwa kwa watoto wanaozaliwa kuitwa kwa jina lake (Mbiti, 1969). Mbiti anasisitiza kuwa Waafrika wanaamini kuwa marehemu/maiti bado ni mtu. Wengine wanaamini kuwa baada ya kufa wafu hurudi kuishi na kushirikiana na jamii zao katika shughuli

mbalimbali ingawa hawaonekani kwa macho (Temples, 1959; Schott, 2010; Mbiti, 2011). Imani hizi za kuendelea kuishi kwa wafu zinajitokeza sana katika jamii ya Kezilahabi.

Katika jamii ya Kezilahabi kuna imani ya baadhi ya watu waliokufa na kuzikwa makaburini kufikiriwa kuwa wako hai. Watu hao inaaminika kuwa wamechukuliwa na wachawi kimazingaombwe, na hivyo, wanaishi kwa kutumikishwa na wachawi hao. Kwa macho ya kawaida watu hao hawawezi kuonekana ila wanaweza kufanya matendo fulani yanayoashiria kuwa wanaishi. Wanaweza kujitokeza na kupotea ghafla au kumwita mtu kwa sauti yake halisi lakini mtu huyo asimwone. Kwa mfano, kisa cha kunigwa na Matunu kata ya Namagondo Ukerewe mwaka 1987 (taz, uk. 96).

Mtume naye anajieleza hivi:

Yote yaliyosemwa yalikuwa wazi na wafuasi wangu waliyasikia. ... Baadhi yao walinisikia nikiyakariri mbele ya Gabrieli na waliyajua vyema wakayaweka katika maandishi. ... Nilikimbia nikarudi na neno likavuka mipaka. Tatizo bado ni fasili. Palitokea ashab, tabilinna tafsir. ... Vita vya Badr vilisaidia, lakini kweli bado imefichama (*Nagona*, uk. 27).

Mtume ni mhusika wa ajabu, anaweza kuongea na malaika (Gabrieli), ana nguvu za ajabu na kwa nguvu hizo anabeba mlima uliokuwa unawazuia kuziona nyayo za paa na kuutupa pembeni (*Nagona*, uk. 27). Pia miujiza ya mhusika huyu inadhihirika zaidi alipousukuma kando mlima uliokuwa unamzuia mfalme kupata mwanga wa jua la asubuhi. Mwandishi anasema:

Tulipoufikia mlima mtume alifumba macho. Kwa nguvu kabisa aliusukuma mlima kwa bega. Mlima ulianza kusukumika polepole hadi ulipotoa nafasi ya kutosha (*Nagona*, uk. 32).

Kitendo cha binadamu kusukuma mlima si cha kawaida na kinamshangaza hata mfalme aliyetoa agizo la kusukuma mlima kama mtihani mojawapo wa kumpata paa. Hii inajidhihirisha kwa namna alivyowatazama wasaka paa kwa mshangao alipowaita kuwapa mtihani wa tatu (*Nagona*, uk. 32).

Mhusika mwingine wa ajabu ni Mfuasi. Mfuasi ni jina linalotokana na kitenzi fuata. Kufuata ni kitendo cha kutoka sehemu moja kwenda sehemu nyingine kwa makusudi maalum. Mfuasi ni mhusika wa ajabu kwa sababu, mfuasi, kama jina lake ananyoosha mguu wake mrefu na kufuata kiko cha mfalme alichokisahau Sibara umbali wa safari ya miaka saba (*Nagona*, uk. 33). Mguu wake ni mrefu kiasi cha kutoonekana ulikoishia na anapoukunja unatengeneza njia ya kufuatwa na wasaka paa. Mfuasi anasema paa anayetafutwa alipita juu ya mguu wake. Kwa hiyo mguu wake ni njia inayofuatwa na watu wenye azma maalum ya kutafuta kitu fulani. Mwandishi anamweleza hivi:

Miguu yake haikuwa inalingana. Mguu mmoja ulikuwa mfupi na mwingine mrefu sana. Hatukuweza kuona ulikoishia...Huo mguu ndio utakaokuelekeza uendako. Huu ndio mguu uendao mbali kwenye fikra na uzamapo haurudi bila wazo. Paa mmtafutaye alipita juu ya mguu huu. ...Mfuasi alianza kuukunja ule mguu mrefu hadi ulipokuwa sawa na mwingine (*Nagona*, uk. 28).

Mtu mwenye mguu mrefu ambao hauwezi kuuona ulikoishia kwa sababu ya urefu wake na unaoweza kukunjwa na kuwa sawa tena na mguu mwingine ni muujiza kuonekana duniani. Uajabu wa mhusika huyu unajidhihirisha zaidi pale wanapotumwa kufuata kiko cha mfalme alichokisahau Sibara umbali wa mwendo wa miaka saba. Mfuasi anaukunjua mguu wake na mguu huo kukunjuka kwa kasi na kwa muda mfupi mguu ukawa umesafiri umbali wa mwendo wa miaka saba na anapoukunja mguu unarudi na kiko cha mfalme (*Nagona*, uk. 33). Huyu

ni mhusika wa ajabu. Si rahisi katika uhalisia mguu wa binadamu kukunjuka, kuwa mrefu na kusafiri kilomita nyingi kwa kasi kiasi hicho kwa kukunjuliwa tu. Zaidi ya yote mguu wa Mfuasi ni wa ajabu zaidi kwa sababu ni mguu unaowaelekeza watu njia na una uwezo wa kwenda mbali kwenye fikra na uzamapo haurudi bila wazo (*Nagona*, uk. 28).

Mguu wa Mfuasi unaimiza kufikiri, kuwa ukizama katika kuwaza hautoki bure bali lazima utoke na wazo. Maoni hayo ni sawa na mawazo ya Plato aliyewahi kusema kuwa ili binadamu aweze kuishi maisha yenye maana ni lazima ajifunze kufikiri na katika kufikiri ndipo atakapofahamu ukweli kama ulivyo na lengo la kuwapo kwa kila kitu duniani (Karugendo, 2010). Kwa maana hiyo inawezekana Kezilahabi ametumia jina la Mfuasi kuisisitiza umuhimu wa kufikiri. Kuwa ili kuupata kweli ni lazima kufikiri. Amelinganisha fikra na safari ndefu isiyo na mwisho (urefu wa mguu wa mfuasi). Hata hivyo mtu yeyote atakayezama katika kuwaza na kufikiri kwa makini, hatatoka bure. Ni lazima atoke na wazo au jambo fulani la maana na lenye faida kwa jamii. Hilo atakalolipata ndilo kweli.

Mipaka ya umbali kutoka sehemu moja hadi sehemu nyingine si pingamizi kwa wahusika wa ajabu. Si ajabu kwa mhusika kusafiri kutoka bara moja hadi nyingine au kuzunguka dunia kwa dakika moja tu na pia kutumia muda huo huo kwenda mbinguni na kurudi. Mhusika wa ajabu anaweza kuwa pahali pengi kwa wakati moja, na kutenda mambo tofauti tofauti yasiyo ya kawaida na yasiyofumbulika kihalisia (Mbiti, 2011).

Mtenzi kama mhusika wa ajabu anajieleza hivi:

Mimi naitwa Mtenzi. Mimi ndiye mkausha maji. Mfuasi wa mwisho. ...Mtenzi aliinama akanywa maji yote yaliyokuwa mtoni (*Nagona*, uk. 28).

Ni muujiza binadamu wa kawaida kunywa maji yote ya mto tena mara moja. Hii inadhihirisha kuwa Mtenzi ni mhusika wa ajabu. Uajabu na mazingaombwe ya Mtenzi unajidhihirisha zaidi pale wanapopewa kulima robo heka ya shamba kavu katika ardhi ngumu ambayo jembe haliwezi kuingia ardhini hata robo inchi. Mtenzi alitapika maji aliyokunywa mtoni na kulowesha shamba lote na ardhi kuweza kulimika (*Nagona*, uk. 32). Utokawaida wa Mtenzi unazidi kuonekana walipokuwa wakitoka katika safari ya kumsaka paa. Alipofika pale wenzake walipomkuta alitapika maji yakajaa mto na kubaki akiyatazama maji hayo ya mto (*Nagona*, uk. 35). Hii inazidi kubainisha kuwa Kezilahabi ametumia wahusika wa ajabu katika riwaya ya *Nagona*. Khamis (2007) anakubaliana na wazo hili kwa kusema kuwa:

Kezilahabi amewapa wahusika wake nguvu za kichawi na miujiza. Wanaweza kuhamisha milima na kumeza maji yote ya mto na kuyatema tena na kunyoosha miguu kwa maelfu ya maili kuchukua kitu.

Wahusika hawa ni muujiza kuwakuta katika mazingira halisi. Hii ni kwa sababu ni muujiza kwa binadamu wa kawaida kunywa maji yote ya mto, kutapika maji yanayoweza kuloanisha shamba au kutapika maji yakajaa mto, kubeba na kuamisha mlima au kukujua mguu ukaenda umbali wa maili nyingi. Hata hivyo matendo na maelezo ya wahusika hao yakichunguzwa bado yanasadifu tu mawazo ya Kezilahabi kuwa katika kufikiri kunapatikana ufumbuzi wa matatizo yote. Kwa sababu ya fikra makini binadamu ametengeneza mashine ninazopasua milima ili kutengeneza barabara. Kwa fikra makini binadamu ametengeneza mabomu ya kuvuna mvua angani bila kusubiri mvua za misimu. Kwa kufikiri binadamu amefanikiwa kufanya ulimwengu kuwa kama kiganja cha mkono, na

hivyo, kuweza kuzunguka au kuona yote yanayotendeka duniani kwa dakika sifuri.

Katika riwaya ya *Kufikirika* Shaaban Robert anatumia wahusika wa ajabu pale anapowaelezea waganga wa mizizi wa Kufikirika kuwa wana uwezo wa kunusa kama mbwa miti iliyotakiwa kutibu ugonjwa fulani hata usiku wa manane maporini. Katika uhalisia ni muujiza kumpata mtu mwenye uwezo wa kunusa harufu ya miti porini kama mbwa na kuipata tena usiku wa manane.

Ingawa inaelezwa kuwa, katika mazingira asilia ya Shaaban Robert, Kibwana Jafari, mume wa kwanza wa mama yake Shaaban Robert, alikuwa na uwezo wa kutafuta mti wa dawa porini hata usiku wa manane kwa kunusa tu harufu ya mti huo (taz, uk. 62); lakini mbwa ndiye mnyama anayeaminika kwa kunusa harufu hata ya kitu kilicho mbali kuliko wanyama wote (Ngure, 2011). Kwa hiyo mwandishi amewalinganisha waganga wa mizizi na kuboea kwao katika kazi yao na uwezo wa mbwa katika kunusa ili kuthibitisha uwezo wa waganga hao katika kufahamu mahali miti hiyo ilipo porini hata wakiwa gizani. Mwandishi anasema:

Kundi la waganga wa mizizi lilikuwa ni kundi la watu ambao waliidilika sana katika utabibu wa maradhi mbalimbali kwa dawa za miti shamba...walikuwa na sifa kubwa kwa kazi hizi, na kuwa dawa zao zilikuwa mujarabu sana. Bila ya kitabu waliweza kunusa kama mbwa miti iliyotakiwa kwa kutibu ugonjwa fulani hata katika usiku wa manane maporini (*Kufikirika*, uk. 8).

Uwezo huo wa kunusa dawa porini tena usiku wa manane kwa waganga wa mizizi ni jambo ambalo si rahisi katika uhalisia. Hii ni kwa sababu licha ya kuwa binadamu hana uwezo wa kunusa kama mbwa pia binadamu hawezi kuona gizani

tena usiku wa manane porini. Kwa hiyo inapotokea binadamu kunusa, kuona na kuchuma dawa porini tena usiku wa manane huyo atakuwa ni mhusika wa ajabu.

Kibwana Jafari, katika mazingira asilia ya Shaaban Robert, licha ya kunusa harufu ya mti wa dawa porini hata usiku wa maneno lakini pia aliweza kunusa harufu ya aina ya ugonjwa kwa mgonjwa na kuihusisha na harufu ya mti au dawa inayoweza kutibu ugonjwa huo. Kwa hiyo, kabla ya kwenda porini kutafuta dawa akijiwa na mgonjwa, alikuwa ananusa kwanza harufu ya ugonjwa kwa mgonjwa na ndipo anakwenda porini kutafuta dawa. Akifika porini alikuwa anatambua harufu ya miti mbalimbali kulingana na harufu ya magonjwa yanayotibiwa na miti hiyo (taz, uk. 63).

Nchini Australia kuna mwanamke mmoja (Ari Kala, mwenye umri wa miaka 24) amegundulika kuwa ana uwezo wa kunusa harufu ya kifo. Ari anasema kuwa aligundua kipaji chake hicho akiwa na miaka 12 alipokwenda kumtembelea mjomba wake aliyekuwa amekaribia kufa na ndipo aliponusa harufu ya kifo ambayo haikutambuliwa na mtu yeyote. “Nilidhani ni harufu ya mabaki ya mwili wa mjomba kwa sababu ilikuwa harufu mbaya sana ambayo sijawahi kuinusa. Lakini hakuna mwingine aliyeweza kuinusa harufu hiyo” amesema Ari. Ari anasema kuwa baadaye alikuja kugundua kuwa mara kwa mara ameweza kunusa kifo na wakati mwingine anaona ni mzigo kuwa na talanta hiyo na huwa anatamani kuwaambia watu wanaotaka kufa lakini baadaye huacha kwa sababu hilo si jukumu lake. Kwa sasa Ari anawafundisha wanawake wenye umri kati ya

miaka 25-45 wanaotoka kwenye jamii zinazoamini uchawi kutumia vizuri talanta na vipaji vyao katika kuisaidia jamii³¹.

Kwa kutumia kisa hiki cha watu wenye uwezo wa kunusa harufu ya ugonjwa na harufu ya dawa ya kutibu ugonjwa husika katika mazingira asilia ya Shaaban Robert na kisa cha Ari kutoka Australia, jamii inaweza kuwabainisha watu wenye vipaji hivi vya ajabu vinavyovuka mpaka wa uhalisia kwa maendeleo ya jamii. Kwa mfano, utaalamu wa kunusa harufu ya ugonjwa na dawa ya kutibu ugonjwa husika inaweza kutumiwa kama mbadala wa vipimo vya magonjwa katika maabara. Mbinu hii inaweza kupunguza gharama na kuokoa muda.

Kezilahabi katika riwaya ya *Nagona* anamtumia mwanamke mjamzito anayeoga peke yake katika chemichemi kama mhusika wa ajabu. Mimba hiyo ni ya Mkombozi wa pili. Amekwisha kukaa hapo kwa miaka maelfu akisubiri kuzaliwa Mkombozi wa pili huku akijaribu katika uhai wake wote kuubeba ulimwengu lakini ameshindwa licha ya kujaribu tena na tena kwa uchovu na kukoga na kujaribu tena (*Nagona*, uk. 24). Mwanamke huyu alijifungua kitoto cha kike kabla ya siku zake siku ya ngoma kuu kwa sababu ya kelele na vurumai za siku hiyo. Wakati ule ule alipojifungua jua lilipatwa na akamwita mtoto huyo *Nagona* (*Nagona*, uk. 62).

Mwanamke huyo ni mhusika wa ajabu kwa sababu hakuna binadamu wa kawaida anayeweza kukaa na mimba maelfu ya miaka na pia kujaribu kuubeba ulimwengu ambao kwa hakika haubebeki. La ajabu zaidi ni kuwa licha ya kuwa na mimba

³¹ Imepakuliwa kutoka mtandaoni tarehe 02/06/2018.

kwa maelfu ya miaka, jambo ambalo haliwezekani kwa wastani wa miaka ya kuishi kwa binadamu, lakini mtoto anazaliwa kabla ya siku zake. Licha ya mwanamke huyu kuwa wa ajabu lakini mtoto aliye tumboni naye ni wa kimazingaombwe. Hii ni kwa sababu katika uhalisia haijawahi na pia haitatokea mtoto kukaa tumboni kwa maelfu ya miaka. Hii ni kwa sababu hakuna hata mtu aliyewahi kuishi miaka hata elfu moja.

Biblia (Mwanzo, 5: 27) inamtaja Methusela kama mtu aliyeishi miaka mingi kuliko watu wote duniani (miaka 969). Kwa hiyo, huyu mwanamke kuwa mjamzito kwa miaka maelfu halafu azae mtoto kabla ya siku zake ni kinyume kabisa cha uhalisia wa kawaida unaofahamika. Hata hivyo, katika uchawi na mazingaombwe hilo linawezeka kwa kutumia mhimili wa uhalisiamazingaombwe ulioishatajwa hapo juu (taz, uk. 134). Mhimili huo unasisitiza kuwa uhalisiamazingaombwe unakusudia kuunganisha na kuvunja mpaka kati ya kweli na uongo,... sasa na zamani (usasa na ukale), utoto na utu uzima na mbali na karibu. Kwa maana hiyo lengo la uhalisiamazingaombwe katika fasihi ni msisitizo wa umoja kati ya mazingaombwe na uhalisia". Hii ina maana kuwa katika uchawi na mazingaombwe hakuna kisichowezekana. Hivyo, kuna uwezekano wa mtoto kuishi kabla ya kutungwa mimba yake, kuwa na miaka elfu na kuwa na miaka sifuri kwa wakati huo huo au kuongea kabla ya kuzaliwa pia kukaa tumboni maelfu ya miaka.

Katika mazingira ya Kezilahabi kuna uchawi wa kufunga tumbo la mwanamke mjamzito. Hivyo, mtoto anakuwa tumboni lakini hakui. Kwa hiyo, mwanamke anaweza kukaa na mimba hata miaka kumi bila kujifungua na mtoto akaendelea kuwa salama na mzima kabisa tumboni. Hii inaweza ikatumiwa kuwasaidia

wanawake wazizae wakiwa wamepata mimba lakini wana majukumu fulani maalum ambayo wakiwa na mtoto mdogo itakuwa vigumu kuyakamilisha. Kwa mfano, mwanafunzi anaeendelea na kiwango fulani cha elimu itamwia vigumu kumlea mtoto mchanga na wakati huo huo akasoma kwa utulivu. Hivyo, kufunga mimba mpaka atakapomaliza masomo yake ni faida kwake.

Kezilahabi hata hivyo, anamtumia huyu mwanamke mwenye mimba ya mkombozi wa pili kuelezea juhudi za binadamu katika kujiletea maendeleo, amani na furaha ya kudumu katika maisha yake. Juhudi hizo hazizai matunda yoyote na kinyume chake ni shida, mashaka na mahangaiko yasiyo na mwisho (Mbatiah, 1998). Mwanamke mwenye mimba ya mkombozi wa pili anathibitisha hili anaposema:

Ulimwengu tambara bovu ... ni vigumu kuubeba. Katika uhai wangu wote nimekuwa hapa nikijaribu kuubeba. Nachoka, nakoga, najaribu tena na bado sijafanikiwa (*Nagona*, uk. 24).

Kwa kuwatumia wahusika kama majitu na wenye nguvu za ajabu Kezilahabi kama mwandishi fuatishi ameathiriwa na kutoathiriwa na Shaaban Robert kwa viwango tofauti. Kwa mfano, Kezilahabi ameandika kwa namna inayokaribiana sana na Shaaban Robert pale anapomwelezea mzee mwenye mkongojo pamoja na Mtume katika riwaya ya *Nagona*. Anasema kuwa mzee alipoita 'Nagona' Sauti yake haikuwa ya kizee tena, kwa sababu mwangwi wa sauti yake ilisikika duniani kote. Pia anasema mtume ana nguvu za ajabu, na kwa nguvu hizo aliusukuma mlima uliokuwa unamzuia mfalme kuota jua. Sauti ya kizee na nguvu za Mtume ni sawa na nguvu na sauti ya Mrefu katika riwaya ya *Adili na Nduguze* ya Shaaban Robert. Jinsi Mrefu anavyoweza kumkamata nyangumi

bahari au tembo porini na kumwoka kwa jua mbinguni ni sawa na Mtume anavyoweza kusukuma mlima. Pia jinsi sauti ya Mrefu ilivyo kali kama radi na kusikika duniani kote ndivyo ilivyo mwangwi ya sauti ya Kizee mwenye mkongojo inavyosikika duniani kote. Hii ina maana kuwa kabla ya Kezilahabi kuandika riwaya ya *Nagona* alisoma na kuvutiwa na jinsi Shaaban Robert alivyowasawiri wahusika wa ajabu katika riwaya ya *Adili na Nduguze*. Bloom (1973) anathibitisha hili pale anapo sema:

Kabla ya kuandika kazi yenye kuathiri ni lazima msanii asome na kuvutiwa na kazi au mwandishi wa kazi tangulizi. Kuathiriwa au ushawishi huo unakuwa mkubwa kiasi kwamba msanii fuatishi huandika kwa namna inayokaribia kuwa sawa na msanii tangulizi, ila kufikia hatua fulani anachepuka na kuonekana kuwa msanii tangulizi alikuwa na ushawishi mpaka kiwango fulani au katika vipengele fulani. Kutoka hapo mwandishi fuatishi huandika kwa namna na mtindo wake ingawa bado kwa juu juu au kidogo kidogo bado anaonekana kuathiriwa na msanii tangulizi.

Kezilahabi kwa kumtumia Mfuasi katika riwaya ya *Nagona* ameathiriwa na mhusika Mrefu katika riwaya ya *Adili na Nduguze* kwa kumwiga Shaaban Robert lakini si kwa mwigo sisisi. Hii ni kwa sababu Mrefu ni mrefu kiasi kwamba anaweza kupita baharini bila kuguswa na maji magotini. Ni mrefu kiasi cha kugusa juu ya vilele vya milima kwa mikono yake na kufikilia jua mbinguni na ni mwepesi kiasi cha kuzunguka dunia kwa sekunde moja. Sifa hizo za Mrefu ni sawa na za Mfuasi ingawa Kezilahabi anamwelezea Mfuasi kwa namna tofauti. Wakati Mrefu ni mrefu kwa mwili wake wote, Mfuasi mguu wake mmoja ndio mrefu, na unaoweza kukunjwa na kukunjuliwa. Wakati Mrefu anapoweza kuzunguka dunia nzima kwa sekunde moja. Mguu wa Mfuasi ndio unaokunjuliwa kufuata kwa muda mfupi kiko kilicho umbali wa safari ya miaka saba.

Ikichunguzwa kwa makini ni kuwa kinachoelezwa kwa kuwatumia Mrefu na Mfuasi ni kitu kimoja (wepesi wa kufanya jambo kwa muda mfupi), lakini tofauti ni katika namna ya uelezwaji. Bloom (1973) anathibitisha hili kwa kusema kwamba kwa kuiga, msanii fuatishi huendeleza mada na mawazo ya msanii tangulizi lakini siyo kwa mwigo sisisi bali anayakamilisha kwa namna nyingine inayoonesha kuwa msanii tangulizi inawezekana alishindwa kuyakamilisha. Hapa msanii fuatishi mara nyingi anatumia “tabaini” kuendeleza mawazo hayo ya msanii tangulizi.

Kezihabi kwa kumtumia mhusika wa ajabu Nabii kusema kuwa aliuawa badala ya sphinx (yaani ni mfu na wakati huo huo anaongea na walio hai), amejitenga kabisa na athari za Shaaban Robert. Hii ni kwa sababu Shaaban Robert hakuwatumia wafu wala walio hai kuwasiliana na wafu katika riwaya zake teule. Kezilahabi kwa kuwatumia wafu-hai ametumia namna nyingine tofauti kabisa ya kuwasawiri wahusika wa ajabu tofauti na Shaaban Robert. Bloom (1973) anasema kwamba kwa kubadili mada msanii fuatishi anajitahidi kubuni kwa ufundi wa hali ya juu mada nyingine tofauti kabisa na mada ya msanii tangulizi. Msanii fuatishi anafanya hivyo kwa kujitahidi kujitenga au kuachana na mada ya msingi ya msanii tangulizi ili kuonesha dhahiri kuwa kazi yake ina nguvu kuliko ya mtangulizi wake. Lengo la msanii fuatishi likiwa ni kujijengea utukufu au jina binafsi mbali na msanii tangulizi.

3.2.3 Wahusika Jumui na Wenye Nafsi Mbili na Wahusika Wenye Hali ya Kiungu Isiyo Bayana.

Shaaban Robert hakutumia wahusika jumui wala wenye nafsi mbili katika riwaya zake teule. Kinyume chake Kezilahabi amewatumia wahusika hao katika riwaya

za *Nagona* na *Mzingile*. Hii inadhihirisha kuwa Kezilahabi kama msanii fuatishi amejitahidi hapa kubuni namna tofauti ya usawiri wa wahusika wa ajabu tofauti kabisa na Shaaban Robert kama msanii tangulizi. Kuhusu ubunifu tofauti na msanii tangulizi au kubadili mada, Bloom (1973) anasema kwamba, msanii fuatishi anajitahidi kubuni kwa ufundi wa hali ya juu mada nyingine tofauti kabisa na mada ya msanii tangulizi. Msanii fuatishi anafanya hivyo kwa kujitahidi kujitenga au kuachana na mada ya msingi ya msanii tangulizi ili kuonesha dhahiri kuwa kazi yake ina nguvu kuliko ya mtangulizi wake. Lengo la msanii fuatishi likiwa ni kujijengea utukufu au jina binafsi mbali na msanii tangulizi.

Katika riwaya ya *Nagona*, kwa mfano, mhusika anaeungama kwa padri ni mhusika jumui. Mhusika jumui au mhusika wengi katika mmoja anaeungama dhambi za karne mbili kwa padri ni mhusika wa ajabu. Huyu ni mhusika wa ajabu kwa sababu miaka yake haeleweki kama ni zaidi ya karne mbili au ni sifuri. Ni mtu mmoja katika wengi, matendo, maneno na tabia za wahusika mbalimbali huwakilishwa na mtu mmoja. Ni mzinifu, mwuaji wa watu mbalimbali wakiwepo: Marais, Papa, Wayahudi na watumwa weusi. Pia ni fisadi mkubwa na muujumu uchumi. Anapoulizwa alitenda dhambi hizi kama nani kwa sababu hakuwa pote duniani. Anasema alizitenda dhambi hizo kama Padri, Rais, Daktari, Sheikh, Mhandisi, Profesa...Na anamalizia kwa kusema kuwa wako wengi katika mmoja wenye dhambi, yaani mtu mmoja mwenye nafsi nyingi (*Nagona*, uk. 49-52).

Kiuhalisia mhusika mmoja kuwakilisha nafsi nyingi ni kinyume cha kanuni za kiisimu katika urejelezi wa nafsi. Matinde (2012) anasisitiza kwa kusema kuwa katika sarufi hakuna nafsi nyingi zinazoweza kurejelewa katika umoja au nafsi moja inayoweza kurejelewa katika wingi. Na pia katika uhalisia ni muujiza kumpata mtu mwenye miaka zaidi ya karne mbili na wakati huo huo akawa mtoto wa miaka sifuri. Maelezo hayo yanamthibitisha mhusika anayeungama kwa Padri kama mhusika wa ajabu kwa sababu ni muujiza kumpata mtu kama huyo katika ulimwengu wa kawaida. Hata hivyo, kwa mtazamo wa kiuhalisiamazingaombwe wahusika jumui na wenye nafsi mbili ni wa kawaida na hujitokeza katika mazingira halisi. Hivyo basi, wasanii wanaotumia mbinu ya uchawi na mazingaombwe uwasawiri wahusika wao kwa kutumia mtindo wa ukumbushaji, mbinu rejeshi na ujenzi wa wahusika jumui na wenye nafsi mbili (nafsi tulivu na nafsi inayotembea ndotoni kichawi na kimazingaombwe) (Roh, 1925).

Katika mazingira asilia ya Kezilahabi kuna watu (wachawi) wenye uwezo wa kuwa na nafsi mbili (nafsi tulivu na nafsi inayotembea kichawi) (taz, uk. 100). Kwa kutumia nafsi hizo, mchawi anaweza kuonekana kama amelala kitandani nyumbani kwake (nafsi tulivu) lakini wakati huo huo akawa yuko mbali sana na kwake akifanya uchawi (nafsi inayotembea kichawi). Ikitokea nafsi inayotembea kichawi ikadhuriwa huko kwenye uchawi nafsi tulivu inadhurika pia.

Kezilahabi amemtumia mhusika wengi katika mmoja kuelezea msururu wa fujo na kukosekana kwa amani na utulivu katika historia ya maisha ya mwanadamu. Historia ya maisha ya mwanadamu imejawa na ukengeufu na ukame wa haki, ukame wa ukweli, ukame wa upendo, ukame wa amani, ukame wa utulivu,

ukame wa maelewano na matokeo yake ni kukosekana kwa maendeleo ya kweli yanayohitajika katika jamii husika (Haji, 2018). Kwa sababu ya fujo hizo kila analowaza binadamu ni kutenda dhambi tu siku zote (Biblia Takatibu, Mwanzo 6: 5).

Miongoni mwa matendo machafu yanayoelezwa na mhusika jumui ambayo yanaongeza fujo na ambayo yanatakiwa kuungamwa au kuachwa ni pamoja na uzinzi, uongo, kukosekana kwa maelewano na kuaminiana ndani ya ndoa, mauaji, kukosekana kwa haki katika vyombo vya sheria, wizi wa mali ya umma, vita kati ya mataifa, ubaguzi wa rangi, na kutoamini uwepo wa Mungu (*Nagona*, uk. 48-52).

Mhusika mwingine wa ajabu ni Kizee kinachoishi peke yake katika nyumba mbovu juu ya kilima. Kizee ndiye mhusika anayechukua sehemu kubwa ya masimulizi katika riwaya ya *Mzingile*. Uajabu wake unaomfanya afananishwe na Mungu unajidhihirisha katika matendo yake, maneno yake, sifa zake na jinsi wahusika wengine wanavyompambanua. Ana sifa kama vile Omnipotentia (Mwenyezi Mungu), Omniscientia (mwenye maarifa yote au mwenye kujua yote). Kizee kinasema jina lake limezungukwa na uajabuajabu. Kipofu anasema kuwa Kizee kinadai kufahamu mawazo yote ya kila mtu (*Mzingile*, uk. 60). Msimuliaji anaambiwa na mfanya majaribio katika maabara ya pangoni kuwa yeye anafikiri kila mtu anamfahamu Kizee na kuwa Kizee hakina makao maalumu. Kila mahali ni kwake. Ni kama mzururaji na yeyote aliyepata kuongea na undani wa dhamiri ya nafsi yake amefika nyumbani kwa Kizee (*Mzingile*, uk. 84-85).

Kizee yuko katika kitovu cha duara. Kinazuru mashamba ya fikra za wanadamu na kina uwezo wa kurutubisha. Kuwako kwake kulianza kama mzaha. Walimwita Kakulu (kazee), sasa anaitwa Kakulu na wajao watamwita Kakulu. Hakuna aliyewajua wazazi wake (*Mzingile*, uk. 93). Kizee kinabadilikabadilika na kufanana na baba yake Msimuliaji, kufanana na Msimuliaji mwenyewe na kinakuwa Kizee tena (*Mzingile*, uk. 107, 110).

Maelezo na sifa hizo zote zilizoelezwa hapo juu zinadhihirisha kuwa Kizee ni Mungu. Kwa kuthibitisha kuwa Kezilahabi amemtumia Kizee kama kiwakilishi cha Mungu, maelezo juu ya Kizee katika riwaya ya *Mzingile* yamelinganishwa na mafungu yanayozungumzia sifa na matendo ya Mungu katika Biblia.

Kizee kinasema kuwa wakati wa ujana wake kilikuwa na sifa za kila aina. Alipewa sifa kama vile Omnipotentia (Mwenyezi Mungu), Omniscientia (mwenye maarifa yote au mwenye kujua yote) (*Mzingile*, uk. 23). Si rahisi kumpata mtu mwenye sifa hizo kote duniani. Biblia Takatifu inasema kuwa Mungu ni wa milele, mwanzo na mwisho, ni Bwana, Mungu Mwenyezi, Muumba wa mbingu na dunia, hazimii wala hachoki, akili zake hazichunguziki (Isaya, 45:11-12; Ufunuo, 1: 8).

Kizee kinasema wasichana walimpenda ila udhaifu wake ulikuwa mmoja, alikuwa na uchu wa mabikira (*Mzingile*, uk. 23). Biblia inaeleza kuwa Yesu Kristo au Imanueli, yaani Mungu pamoja nasi, alizaliwa na bikira Mariamu kwa uwezo wa Roho Mtakatifu. Maandiko Matakatifu yanasema:

Mwezi wa sita malaika Gabrieli alitumwa na Mungu...kwa mwanamwali bikira...jina lake Mariamu... malaika akamwambia tazama, utachukua mimba na kuzaa mtoto mwanamume; na jina lake utamwita Yesu. Huyo atakuwa mkuu, ataitwa mwana wa aliye juu... Mariamu akamwambia malaika, litakuwaje neno hili nami sijui mume? Malaika akajibu akamwambia, Roho Mtakatifu atakujilia juu yako, na nguvu zake aliye juu zitakufunika kama kivuli; kwa sababu hiyo hicho kitakachozaliwa kitaitwa kitakatifu, Mwana wa Mungu (Luka, 1: 26-35).

Kwa maelezo hayo Kizee kinaposema kuwa uchu wake ulikuwa kwa mabikira anazungumzia tukio la kuzaliwa kwa Yesu kwa kumaanisha kuwa Yesu alizaliwa na Mungu kupitia kwa bikira Mariamu.

Kizee kinazidi kujithibitisha kuwa ni Mungu kinaposema kuwa kwa mara ya mwisho aliitumia fimbo yake kuchapa alipowafukuza wahuni fulani kutoka shambani mwake. Ili kutetea uhuni wao walitunga hadithi ya nyoka. Walipata ijara yao wao na vizazi vyao. Wahuni hao walipata shida sana baadaye. Pia Msimuliaji na mke wake wanamwelezea Kizee kuwa maisha ya kwanza ya wanadamu yalianzia katika ndoto zake, yakawa mabaya zaidi alipoamka na kuwafukuza kutoka bustanini (*Mzingile*, kur. 110, 121). Hapa pia Biblia Takatifu inadhihirisha kuwa wahuni wanaozungumzwa ni Adamu na Hawa, wazazi wa wanadamu wote. Shamba walilofukuzwa ni bustani ya Edeni na nyoka ni shetani.

Biblia Takatifu inasema:

Bwana Mungu akamtwa huyo mtu, akamweka katika bustani ya Edeni ailime na kuitunza... Basi nyoka akamwambia mwanamke, Ati! Hivi ndivyo alivyosema Mungu, Msile matunda yote ya miti ya bustani...Mwanamke alipoona ya kuwa ule mti wafaa kwa chakula... alitwaa katika matunda yake akala, akampa na mumewe, naye akala... Kwa hiyo Bwana Mungu akamtoa katika bustani ya Edeni, ailime ardhi ambayo katika hiyo alitwaliwa (Mwanzo, 2: 15- 3:23).

Maelezo hayo yanaonesha kuwa Kezilahabi amemtumia Kizee kumaanisha Mungu. Kwa maana hiyo, Kezilahabi basi amemkejeli, amemdhihaki na kumdunisha Mungu mno katika riwaya ya *Mzingile*. Kwa mfano, Msimuliaji anapoelekezwa kwenda kwa mfadhili na Kipofu anakutana tena na Kizee aliyemwacha kwenye nyumba mbovu kule kilimani tena akiwa uchi wa mnyama. Mwandishi anasema: Sikuamini macho yangu. Alikuwa yule yule Kizee niliyekutana naye kilimani, ila sasa kilikuwa kizee zaidi (*Mzingile*, uk. 57). Msimuliaji anapoongozwa na Kipofu kutoka pangoni wanasikia kilio cha mwanamke ajifunguaye. Mwanamke anazaa mapacha na kipofu anadai mimba hiyo ni ya Kizee ambaye kipofu anakiita bazazi (*Mzingile*, uk. 62-63). Pia Msimuliaji anapozungumza na kijana anayefuga mijusi jangwani wanamzungumza Kizee hivi:

“Ulimwona?” “Nani?” “Mzee” “Unamjua?” Alipita hapa na blanketi lake akiwa amejiharishia. Amezeeka sana sasa. Alitembea kwa kuyumbayumba kama aliye ndotoni. Alikuwa akiweweseka....Aliinua fimbo yake juu kutaka kunipiga...Alipoona sistuki alijaribu kukimbia kwa hasira kuelekea pale nilipokuwa nimesimama. Lakini alijikwaa katika shina la jani akaangukia kidevu hali blanketi lote likaishia kichwani. Hakuweza kusimama kwa nguvu zake mwenyewe. Nilipomwinua alijipangusa blanketi lake bichi, akachukua fimbo yake halafu akageuka kuendelea na safari yake... Alifuatwa na jeshi la nzi. Huruma tu ndiyo iliyoniwezesha kumkaribia...”Unajua mahali anapokaa?” “Nijuavyo mimi hana makao maalumu. Kila mahali ni kwake yeye ni kama mzururaji”. Mimi nimefika kwake mara mbili. Ni mzee mmoja maskini sana. Hana chochote cha maana pale nyumbani” (*Mzingile*, kur. 84, 85).

Mzee amedhihakiwa na kukejeliwa hapa kwa namna nyingi. Anafananishwa na bazazi ambaye kazi yake ni kutia wanawake mimba. Anajiharishia ovyo hovyoy. Hana nguvu kiasi cha kuangushwa na shina la nyasi. Hawezi kusimama peke yake na kwa harufu ya kinyesi cha muharo wake anafuatwa na jeshi la nzi. Hivyo, mtu kama huyo hakuna anayeweza kutaka kumkaribia isipokuwa wale

wenye huruma tu; kwani licha ya kuwa ni mzururaji lakini ni maskini asiye na kitu nyumbani kwake.

Kezilahabi hatumii dhihaka na kejeli kwa Mungu katika riwaya ya *Mzingile* pekee, bali hata katika riwaya ya *Nagona*. Kwa mfano, Mimi au Msimuliaji katika riwaya ya *Nagona* anaposhindwa kuchuma matunda katika bustani yenye matunda na maua yanayotoa mwanga, yasiyochumika na yanayoteleza kiajabuajabu anamlinganisha Mungu na mzee aliyezeeka anayeweka mitego isiyo na maana. Mwandishi anasema:

Nilisema kimoyomoyo, naye atakuwa amezeeka kutuwekea mtego huu mara ya pili. Nilipiga kelele; “Hakuna shetani wa kunichumia matunda haya nikala? Hakuna dhambi ya asili! (*Nagona*, uk.13).

Kezilahabi hapa ametumia maandiko ya Biblia Takatifu, hasa tukio la shetani kuwashawishi Adamu na Hawa kula tunda walilokatazwa wasile katika bustani la Edeni. Mungu ndiye anayekejeliwa kuwa amezeeka na ambaye kwa sababu ya kuzeeka kwake mtego wake hauwezi tena kumnasa mtu (Biblia Takatifu, Mwanzo: 3:1-6).

Mawazo hayo ya kuwa Kezilahabi anamkejeli Mungu na dini kwa ujumla yanaungwa mkono na Malugu (2016 : 66) anayesema kuwa:

Tumechagua kazi moja ya Euphrase Kezilahabi kushadidia kile kilichokuwa kikisemwa kuwa Kezilahabi ni mwandishi aliyelisawiri suala la dini kwa namna ya kukejeli asasi ya dini...

Kezilahabi katika kukejeli zaidi dini hasa za Ukristo na Uislamu anatumia tukio la ajabu la kiwiliwili cha mtu aliyekufa zamani, mtu huyo alipakatishwa Biblia Takatifu katika mkono mmoja na mwingine Korani Tukufu. Mdomo wa mtu

huyo ulikuwa umefungwa na kitambaa chenye maandishi,” Kimya ni Hekima”(Nagona, uk. 2-3). Mtu huyu alikuwa mjinga. Alikataa kutupa vitabu vyake. Walimuua...Wanamji (Nagona, uk. 5).

Tukio hili linaonesha kuwa mtu huyo aliuawa kwa sababu ya kutaka kuzungumzia habari za Mungu ambazo wanamji waliona kuwa hazina maana, hivyo hawakuwa tayari kuzisikiliza, na hivyo kumwambia atupe vitabu vya dini yaani Biblia na Kurani. Kushikilia msimamo wake wa kutotaka kutupa vitabu hivyo kuliwafanya wanamji kumwona kuwa ni mjinga na hivyo kumuua.

Kizee ni mhusika wa ajabu kweli kwa sababu anajitokeza kama binadamu (yaani kizee kilichozeeka, maskini na aliyetelekeza familia yake). Anajitokeza kama mtu aliyezaliwa kiajabu yaani Kakulu, kama Mungu na pia anakuwa kama Msimuliaji au baba na babu wa Msimuliaji. Katika maisha ya kawaida ni muujiza kumpata mtu kama huyo ambaye habainiki vizuri kiuhalisia.

Ingawa katika mazingira asilia ya Kezilahabi kulikuwa na watu (wachawi) walioweza kujibadilisha kimazingaombwe na watu waliokuwa na uwezo wa kufahamu anayoyawaza mtu moyoni mwake kama ilivyokwisha elezwa, lakini watu hao hawakuwa na sifa za uungu kama Mungu mwenyenzi na muumba wa vyote kama alivyo Kizee katika riwaya ya *Mzingile*. Kwa hiyo, licha ya baadhi ya sifa chache za mhusika Kizee kupatikana katika mazingira asilia ya Kezilahabi lakini kwa kiasi kikubwa Kezilahabi ameathiriwa na Biblia Takatifu katika kumsawiri mhusika Kizee.

Licha ya Kezilahabi kumtumia Kizee kumdhahki Mungu na kumkunisha kupita kiasi, lakini pia amemtumia kuzungumzia utamaduni wa baadhi ya jamii za Kiafrika katika taratibu za uendeshaji wa mazishi na nafasi ya Mungu katika maisha ya mwanadamu. Utamaduni umeelezwa na Ramadhani (2013) kuwa ni mfumo wa maisha au utaratibu wa maisha ambao jamii hufuata katika maisha yake ya kila siku ikijumuisha, mila, desturi, miiko, matambiko na jando na unyago. Utamaduni wa jamii ndio hutoa dira na mwelekeo wa namna mambo mbalimbali katika jamii yanapaswa kuwa na kuendeshwa na wanajamii wote ili kuleta mahusiano mazuri miongoni mwa watu, upendo, Amani, ushirikiano na kuheshimiana katika jamii.

Katika Anthropolojia ya Kimarekani utamaduni umeelezwa kama namna mbalimbali ambazo kwazo watu wanaoishi sehemu fulani duniani au jamii fulani, huanzisha na kuwasilisha tajriba zao za maisha na kutenda mambo kiubunifu. Utamaduni huambatanishwa na mambo kama vile uchawi na ushirikiano na imani za kimazingaombwe wakati mwingine hasa katika jamii za Kiafrika.

Kwa mawazo hayo ya kiantropolojia ya Kimarekani, utamaduni unaweza kuelezwa kuwa ni kanuni au utaratibu mzima wa mfumo wa maisha ambao jamii fulani imejikuta inafuata na kuikubali kama sehemu muhimu katika kuleta maelewano, umoja na amani katika jamii hiyo. Utamaduni hivyo ujumuisha lugha na matumizi yake, umri na jinsi, salamu, mavazi, namna ya kula, ibada, wakati, kilimo, biashara, sherehe, kuzaliwa, ndoa na hata kifo.

Kezilahabi anatumia kutumwa kwa Msimuliaji kumpelekea Kizee taarifa za msiba kuzungumzia utamaduni katika taratibu za uendeshaji wa msiba katika baadhi ya jamii za Kiafrika, jamii yake asilia ikiwemo. Katika jamii nyingi za Kiafrika msiba unapotokea mazishi mara nyingi hayawezi kufanyika kama jamaa wa karibu wa marehemu hawapo. Kwa mfano, ni vigumu kuzikwa kwa mtoto kama baba yake au mama yake hayupo. Hivyo utaratibu wa kumtuma mtu kumfuata mzazi huyo hufanyika. Hicho ndicho kilichomfanya Msimuliaji katika riwaya ya *Mzingile* kusafiri kwenda kumtafuta Kizee ili kumjulisha habari za msiba wa mwanaye na kumwomba ahudhurie mazishi hayo.

Umuhimu wa safari ya kumfuata Kizee ni kuwa hawawezi kuzika mpaka Kizee afike msibani. La ajabu ni kuwa Kizee anayeonekana kuwa ni Mungu anakataa kuhudhuria mazishi kwa madai kuwa hakumbuki kama amewahi kuwa na mtoto. Pia mtoto aliyeuawa naye haieleweki kuwa ni nani: Ni mwanamke yule aliyeuawa akitetea utamaduni wa Kiafrika na aliyekuwa akiwahutubia wanawake au ni Yesu. Zaidi ya yote hata Msimuliaji aliyetumwa kwa Kizee naye hasadiki kuwa huyo aliyeuawa alikuwa ni mtoto wa Kizee. Mwandishi akieleza mazungumzo kati ya Msimuliaji na Kizee, anasema:

“Nimetumwa kuja kukuona”. “Mimi!” Ndiyo. Wewe.” “Kuhusu?” “Kifo cha mwanao”. Nimekuja kukujulisha kuwa mwanao ameuawa...Sikumbuki kuwa na mtoto! Lakini haidhuru. Kwa nini walimuua?” “Alidai kuwa mwanao.”... Alidai kuwa na uwezo wa kila aina.” “Alidai kuwa wewe ndiye uliyemtuma kusema aliyoyasema.” “...Alisema kuna uwezekano wa kuishi milele.” Walimwamini! “Walimwita mwongo. Nafikiri alivuka mpaka alipodai kuwa ni mwanao, akapoteza uaminifu aliokuwa nao miongoni mwa watu. Kabla ya kusikia habari zake wazo la wewe kuwa na mtoto lilikuwa limesahaulika kabisa...Kama huwezi kuhudhuria mazishi wanaomba ruhusa ya kuzika... “Waambie ni wajibu wa kila anayekufa kuzikwa (*Mzingile*, uk. 21-22).

Umazingaombwe katika safari ya Msimuliaji ya kutimiza azma ya kitamaduni ni kuwa: Watu wanaomtuma Msimuliaji kwenda kumwita Kizee kuwa mtoto wake amekufa na kuwa hawawezi kuzika mpaka awepo ndio wauaji. Sababu kubwa ya kuuawa ni yeye kudai kuwa ni mtoto wa Kizee. Kama ni hivyo, kwa nini Kizee aitwe wakati wauaji wanafahamu kuwa huyo si mtoto wake? Msimuliaji mwenyewe anaposisitiza kuwa hawawezi kuzika mpaka Kizee awepo kwa sababu anayetarajiwa kuzikwa ni mtoto wake, anajichanganya tena anaposema kuwa marehemu alivuka mpaka alipodai kuwa ni mtoto wa Kizee. Kama anafahamu kuwa marehemu alikosea kujiita mtoto wa mzee kwa nini atumie muda huo wote na safari hiyo yote kumfuata mtu kwa ajili ya msiba anaofahamu fika kuwa haumhusu? Kizee mwenyewe naye inaonekana kama hajitambui. Anasema kwa sababu ya utamu wa ndoto hakumbuki kama amewahi kuwa na mtoto. Hata hivyo mpaka mwisho Kizee kinakataa kuhudhuria mazishi.

Kezilahabi kwa kutumia safari ya Msimuliaji kupeleka taarifa ya msiba anachanganya dini na utamaduni na hivyo kushindwa kuwa na hakika kuwa Kizee anayezungumzwa na mwanae aliyeuawa ni Mungu na Yesu au ni dhana fulani tu analotaka kuliibusha. Hata hivyo kukataa kwa Kizee kuhudhuria mazishi ya mwanae kunaweza kuwakilisha wazo la kuachana na baadhi ya miiko na taratibu fulani za mazishi zisizo na faida. Kwa mfano, kuna faida gani kukaa na maiti kwa muda mrefu bila kuzika kumsubiri mzazi ambaye katika uhai wa mtoto hakuwajibika kwa kitu chochote na wala hakutambua hata kuwa alikuwa na mtoto sehemu fulani.

Wazazi wanatakiwa kuwajibikia familia zao na hata watoto wanatakiwa kuwajibika kwa wazazi wao wakingali hai. Kama kuna haja ya kufuatwa kwa

baba, mama au mtoto, wafuatwe ili wawajibike mtu akiwa hai. Kwa mfano, wengi wanatoa michango mikubwa na kugharamia mazishi kwa pesa nyingi lakini mtoto au mzazi akiwa mgonjwa hawawajibiki kwa lolote katika matibabu yake. Wanasubiri afe ndipo waoneshe uwezo na ufahari wao. Biblia Takatifu inasema: Mwingine katika wanafunzi wake akamwambia, Bwana, nipe ruhusa kwanza, niende nikamzike baba yangu. Lakini Yesu akamwambia, Nifuate; waache wafu wakawazike wafu wao (Luka, 9: 60; Mathayo, 8: 21-22). Hii ina maana kuwa mtu akifa, amekufa, hivyo, kuweka masharti na vikwazo vingi vinavyoweza kurudisha nyuma maendeleo kwa ajili ya mwili wa marehemu ni hasara tupu. Kwa mfano, kuna faida gani na ni maandalizi gani ambayo watu wanaweza kufanya kwa muda wa mwezi mzima (wakiendelea kulipia gharama za kuhifadhi mwili) bila kumzika mtu aliyekufa?

Kezilahabi ametumia pia kujibadilisha kimazingaombwe kwa Kizee kuzungumzia nafasi ya Mungu katika maisha ya mwanadamu. Katika kubadilikabadilika kwa mhusika huyu kwa sababu ya kuzeeka kwake, Kezilahabi anatanika katika kumweleza Mungu kuwa ni nani. Anakosa uhakika kama Mungu anaweza kuwa Mungu muumba wa vitu vyote, baba yako, babu yako, wewe mwenyewe au hisia tu katika akili za mwanadamu. Hivyo, Mungu ni nani linabaki kuwa fumbo ambalo Kezilahabi ameshindwa kulifumbua katika riwaya ya *Mzingile*.

3.3 Kiishilio

Sura hii imechunguza wahusika wa ajabu katika riwaya teule za Shaaban Robert na za Euphrase Kezilahabi. Imebainika kuwa wote Shaaban Robert na Kezilahabi

wametumia wahusika wa ajabu kwa namna zinazofanana na kwa namna tofauti katika riwaya zao teule. Ingawa wote wametumia wahusika wa kisaikolojia kama majini, majitu, mashetani na malaika kwa namna fulani lakini matendo na tabia ya wahusika wa Shaaban Robert yanakaribiana na matendo ya watu wa kawaida wanaofanya mambo ya ajabu katika maisha halisi. Kinyume chake baadhi ya wahusika wa ajabu wa Kezilahabi uhalisia wao haupambanuliki vizuri. Zaidi ya yote, tofauti na Shaaban Robert, Kezilahabi ametumia wahusika jumui kama: mhusika wengi katika mmoja katika riwaya ya *Nagona* na mhusika Kizee mwenye taswira ya uungu katika riwaya ya *Mzingile*.

Kezilahabi anazidi kutofautiana na Shaaban Robert katika kuwapambanua wahusika. Wakati Shaaban Robert anapotumia mbinu za kijadi au nduni za fasihi simulizi kwa kiwango kikubwa katika kuwapambanua wahusika; Kezilahabi anatumia wahusika wengi batili ambao kwa kiwango kikubwa ni wahusika wa kiusasabaadaye.

Imedhihirika pia kuwa watunzi hao wameathiriwa na mazingira yao asilia kwa kiwango kikubwa katika kutumia kwao wahusika wa ajabu katika riwaya teule. Wakati Shaaban Robert akitumia zaidi wahusika majini Kezilahabi kwa upande wake ametumia zaidi wahusika wanaoishi kati ya uhai na kifo. Hii ni kwa sababu katika mazingira ya Shaaban Robert mwingiliano kati ya watu na majini ni mkubwa sana kiasi cha kufanya mpaka kati ya majini na watu wa kawaida kuwa mdogo sana. Ivyo hivyo, katika kisiwa cha Ukerewe, mazingira asilia ya Euphrase Kezilahabi, kutokewa na wafu ni jambo la kawaida na imekuwa ni sehemu ya maisha yao ya kila siku.

Shaaban Robert amewatumia wahusika wa ajabu kuelezea umuhimu wa kutenda mema na kusisitiza kuwa kila mmoja hulipwa kadri ya matendo yake. Anasisitiza mabadiliko kwa kuhimiza jamii kuwapa wanawake uhuru wa kuchagua mustakabali wa maisha yao na kuachana na ukale usio na faida kama vile ibada ya kimizimu. Kezilahabi kwa upande wake ametumia wahusika wa ajabu kujaribu kueleza umuhimu wa kufikiri. Amewatumia pia wahusika hao kutaka kumweleza Mungu kuwa ni nani, suala ambalo ameshindwa kupata uvumbuzi wake. Zaidi ya yote amewatumia wahusika hao kujaribu kufumbua fumbo la maisha baada ya kifo. Suala ambalo bado pia limekuwa ni kitendawili ambacho jibu lake bado halijapatikana. Hata hivyo, anahimiza kuwa ili kupata majibu hayo kinachotakiwa ni kufikiri. Sura inayofuata imechunguza matumizi ya matukio ya ajabuajabu katika riwaya teule za Shaaban Robert na za Euphrase Kezilahabi.

SURA YA NNE**ATHARI YA MAZINGIRA ASILIA YA WATUNZI KATIKA MSUKO
WA MATUKIO YA AJABUAJABU KATIKA RIWAYA TEULE ZA
SHAABAN ROBERT NA ZA EUPHRASE KEZILAHABI****4.0 Utangulizi**

Sura hii imengazia athari ya mazingira asilia katika matumizi ya matukio ya ajabuajabu katika riwaya teule za Shaaban Robert na za Euphrase Kezilahabi. Lengo lilikuwa chunguza athari ya mazingira asilia ya watunzi katika matumizi ya mbinu ya uchawi na mazingaombwe katika riwaya teule na kulinganisha matumizi ya mbinu ya uchawi na mazingaombwe kati ya watunzi Shaaban Robert na Euphrase Kezilahabi. Ili kufaulisha lengo hilo matukio ya ajabuajabu katika riwaya teule yamebainishwa na kuchunguzwa uwepo wake katika mazingira asilia ya watunzi kwa kutumia nadharia ya Uhalisiamazingaombwe. Aidha, matumizi ya matukio ya ajabuajabu kati ya Shaaban Robert na Euphrase Kezilahabi yamelinganishwa kuwa kutumia nadharia ya Kiwewe cha Kuathiriwa.

Sura hii imegawanyika katika sehemu kuu mbili. Sehemu ya kwanza imefafanua maana ya matukio ya ajabuajabu. Sehemu ya pili imebainisha matukio ya ajabuajabu katika riwaya teule na kulinganisha matumizi ya matukio hayo kati ya Shaaban Robert na Euphrase Kezilahabi. Matukio ya ajabuajabu yaliyochunguzwa ni: matukio ya ajabuajabu yanayotendwa na watu na viumbe wa kufikirika kama majini, mizimu, mizuka na majitu. Matukio ya ajabuajabu

yanayotendwa na wanyama na ndege. Pamoja na matukio ya ajabuajabu yanayotendeka yenyewe kutokana na ukiamambile.

4.1 Matukio ya Ajabuajabu

Tukio ni neno linalotumiwa kuelezea mabadiliko ya hali yanayotokea katika usemi na yanayoashiriwa na kutendeka au kufanyika. Tukio huweza kuwa tendo au mchakato unaosababishwa na mtu. Tukio huweza pia kutumiwa kuelezea tendo ambalo halikutendwa na mtu, kama mvua kuanza kunyesha (Wamitila, 2003).

Kuna matukio ya kawaida, na matukio ya ajabu. Matukio ya ajabu yako ya aina mbili: matukio ya ajabu katika hali ya kawaida na matukio ya ajabu katika hali ya uchawi na mazingaombwe. Tukio la ajabu katika hali ya kawaida ni tukio lisilo la kawaida lakini linaweza kufanywa na binadamu au kiumbe kingine chochote ambacho kwa uwezo au kwa mwonekano wake hakiwezi kufanya tukio kama hilo. Kwa mfano, tukio la Hasidi na Mwivu kumtumbukiza Adili baharini katika riwaya ya *Adili na Nduguze*, ni tukio la kawaida ingawa ni la kusikitisha. Hii ni kwa sababu ni jambo linaloweza kufanywa na binadamu yeyote mwenye tabia ya ufidhuli na mwenye matendo maovu.

Kitendo cha Adili kuokolewa na ndege baharini ni tukio la ajabu na la kushangaza. Hata hivyo ni tukio linaloweza kutokea na kuelezeka kwa kutumia akili ya kawaida ya binadamu. Tukio hili linakuwa la kimazingaombwe kwa sababu ndege aliyemwokoa Adili baharini hakuwa ndege wa kawaida, alikuwa ni jini aliyejigeuza ndege. Adili alipookolewa na ndege baharini na kwa kujua kuwa sasa atakuwa chakula cha ndege badala ya kufa maji, alizimia. Kitendo cha Adili

kutofahamu kuwa yule ndege hakuwa ndege, kwake ilikuwa ni mazingaombwe. Zaidi ya yote, kama wangekwepo watu ambao wangeshuhudia tukio la Adili kuopolewa na kubebwa na ndege, wangeeleza tu kuwa tumemwona ndege fulani mkubwa amemkamata mtu. Ni tukio la ajabu kwao, na kwa vile wasingejua kuwa yule ndege si ndege bali jini kwao pia ingekuwa ni mazingaombwe. Kwa Adili baada ya kujua kuwa yule ndege ni jini aliyejigeuza ndege, yaani baada ya kupata ukweli wenyewe, kwake mazingaombwe yalitoweka. Hii ina maana kuwa alifumbuliwa fumbo lenyewe na kubaini ukweli kutoka katika maluweluwe ya mazingaombwe. Kwa maana hiyo mazingaombwe yanaweza pia kuelezwa kama fumbo fulani ambalo limefumbwa kwa namna inayoshinda akili ya kawaida ya binadamu kung'amua maana ya ndani iliyofumbatwa katika fumbo hilo (Roh 1925). Kwa maana hiyo, kwa mfumbaji, kwa mfano, Huria, kwake fumbo si fumbo na mazingaombwe si mazingaombwe. Kwa hiyo basi, tukio la ajabu linakuwa la kimazingaombwe pale ambapo kutokea na kutendeka kwake ni zaidi ya utambuzi wa kawaida wa akili ya binadamu (Williams 1995).

Kakulu katika riwaya ya *Mzingile* kuzungumza lugha mbalimbali kama vile Kiingereza na Kifaransa ingawa hakupata nafasi ya kujifunza au kufika katika jamii ambazo zinazungumza lugha hizo ni tukio la ajabu katika hali ya kawaida. Watu wanamshangaa Kakulu na kujiuliza kuwa amepataje kufahamu na kuzungumza lugha hizo (*Mzingile*, uk. 62). Hata hivyo hawatahusisha tukio hilo na mazingaombwe. Kinyume chake tukio la mtoto kuzungumza akiwa tumboni kabla ya kuzaliwa ni tukio la ajabu na ni la kimazingaombwe. Kwa mfano, Kakulu katika riwaya ya *Mzingile* alianza kuzungumza hata kabla ya kuzaliwa.

Mwandishi anasema:

Wakati alipokuwa bado tumboni mwa mama yake alisikika mara nyingi akizungumza. Mara nyingi aliingilia kati mazungumzo yaliyokuwa yanaendelea kati ya mama yake na wanawake wengine. Mwanamke mmoja akisema, “Jana mume wangu amerudi hoi”, sauti itasikika toka tumboni mwa mwenzao, “Umbea huo!” Walimwita mtoto wa mchawi kabla hata hajazaliwa (*Mzingile*, uk. 1)

Matukio ya ajabuajabu kama hayo ambayo hayawezi kuelezeka kwa kutumia nadharia za kihalisia wala za kisayansi, ndiyo yaliyochunguzwa uhalisia wake katika mazingira asilia ya Shaaban Robert na ya Euphrase Kezilahabi. Matukio hayo ni mengi katika riwaya teule za Shaaban Robert na za Euphrase Kezilahabi. Nadharia faafu kwa ajili ya kukabiliana na matukio hayo yanayokwenda kinyume cha sayansi na uhalisia ni nadharia ya uhalisiamazingaombwe. Roh (1925) anashadidia kwa kusema:

Tunaifahamu dunia, si kama tumeamka tu kutoka ndotoni, lakini tunaitazama kwa macho mapya. Tumetunukiwa mtindo au mbinu mpya ambayo kwa hakika ni zaidi ya mwono halisi wa ulimwengu huu, mtindo ambao huelezea ulimwengu halisi na mazingira yake. Ulimwengu huu na mazingira yake bado ni ngeni na haujaeleweka vizuri kwa mawazo ya kiuhalisia. Umejaza mbinu au ufundi na hali mbalimbali ambazo zimefunika vitu vyote kwa maana ya ndani ambayo ufunua miujiza na maajabu ambayo kila mara yanatisha na kuchafua amani na usalama wa vitu vya asili na vya kawaida.

Matukio ya ajabuajabu yaliyobainishwa katika riwaya teule na kuchuchunguzwa uwepo wake katika mazingira asilia ya Shaaban Robert na ya Euphrase Kezilahabi ni: matukio ya ajabuajabu yanayotendwa na watu na viumbe wa kufikirika kama majini, mizimu na majitu. Matukio ya ajabuajabu yanayotendwa na wanyama na ndege. Pamoja na matukio ya ajabuajabu yanayotendeka yenyewe kutokana na ukiamambile. Ukiamambile ni uwezo usio wa kawaida,

unaozidi kiwango cha kawaida cha utendaji wa binadamu au kiumbe kingine chochote kinachohusika (Wamitila 2003).

4.2 Matukio ya Ajabuajabu Katika Riwaya Teule

Katika uandishi unaotumia uchawi na mazingaombwe matukio ya ajabuajabu hutokea sana. Wamitila (2003) anasema kuwa matukio ya ajabuajabu yanaweza kutendwa na binadamu au kiumbe kingine chochote au kutendeka zenyewe kutokana na ukiamambile. Matukio ya ajabuajabu hayatokei katika ombwe, bali kunakuwa na sababu ya kutokea kwake ikiwa ni pamoja na ujumbe muhimu uliokusudiwa na mtunzi unaobebwa na tukio husika.

4.2.1 Matukio ya Ajabuajabu Yanayotendwa na Watu na Viumbe wa Kufikirika kama Majini, Mizimu na Majitu

Katika riwaya za Shaaban Robert na za Euphrase Kezilahabi kuna matukio mbalimbali ya ajabuajabu yanayotendwa na watu na viumbe wa kufikirika. Katika riwaya ya *Adili na Nduguze* Shaaban Robert anamtumia Mrefu, kiumbe wa ajabu, kutamka laana na miji yote inagharikishwa na vitu vyote pamoja na wanadamu katika mji wa Fahari inageuka mawe kwa laana iliyotamkwa tu bila kuguswa na kitu chochote. Pia Mrefu anatamka tu maneno na mti wa mkomamanga unaota, unakua na kuzaa matunda siku hiyo hiyo (*Adili na Nduguze*, kur. 29, 30).

Zaidi ya yote Katika riwaya ya *Kusadikika* Shaaban Robert anamtumia Salihi kutamka tu maneno na mara hiyo wakawa vipofu wote wawili: Salihi na Sapa (*Kusadikika*, uk. 28). Salihi kabla ya upofu alionekana kufanikiwa kwa kila jambo au kitu chochote kile alichoomba kiasi kwamba Sapa akatunga hila ya

kugawana sawa na Salihi kitu chochote atakachoomba. Sapa alidai kuwa Salihi hana matumizi na mali hiyo aliyoipata kwa kuomba. Salihi alikubali na papo hapo akainua mikono juu akaomba upofu na wote wawili wakawa vipofu (*Kusadikika*, uk. 28). Sapa alidhani Salihi angeomba mambo mazuri kama mali au ufalme lakini ikawa kinyume kabisa. Hili ni tukio la ajabu kwa sababu katika uhalisia ni muujiza mtu kuinua mkono juu na kusema nataka kuwa kipofu halafu wakawa vipofu kwa kusema maneno tu tena saa hiyo hiyo.

Kezilahabi kwa upande wake katika riwaya ya *Nagona* anamtumia mfalme ambaye paa yuko katika milki yake kutazama jiwe lililokuwa ukutani. Mfalme kwa kutazama tu kunafanya mionzi kutoka machoni mwake na kuandika juu ya jiwe, na kwa kutazama tu tena kunafanya kipande cha jiwe chenye maandishi kukatika. Mwandishi anasema:

Tutahitaji kitambulisho, Nabii alisema. Mfalme alitutazama, kisha alielekeza macho yake kwenye jiwe lililokuwa ukutani. Mionzi ilitoka machoni mwake na kuandika juu ya jiwe. Mfalme aliendelea kulitazama, mionzi ilikata kipande kidogo chenye maandishi. Msichana alikichukua akatupa (*Nagona*, uk. 33).

Miji kugharikishwa na watu na vitu vyote katika mji wa Fahari kuwa mawe na mtu kuwa kipofu kwa maneno tu ya kusemwa pamoja na kipande cha jiwe kukatwa kwa mionzi inayotoka machoni kwa kutazamwa tu bila kuguswa na mtu ni matukio ya ajabu. Katika mazingira asilia ya Shaaban Robert kuna watu waliokuwa na uwezo wa kusema maneno tu na jambo baya likakupata. Kwa mfano, kisa cha vijana wawili kuvua baharini siku ya Idi cha Jafari Kibwana (taz, uk. 74). Jafari aliwakataza watu wasiende porini au kuvua samaki siku ya Idi na kuonya kuwa watakaokaidi na kwenda kuvua siku hiyo watatumbukia baharini na

kugeuka mawe. Vijana wawili walikaidi na kwenda kuvua siku hiyo. Vijana hao walitumbukia baharini na sehemu hiyo walipotumbukia palizuka mawe mawili, moja limesimama na lingine limeinama. Mawe hayo yanafanana kabisa na sura za binadamu. La ajabu zaidi ni kuwa mawe hayo hata yakipigwa picha hayapigiki (taz, uk. 75).

Licha ya Shaaban Robert kutumia tukio la miji kugarikishwa na mji wa fahari kugeuka mawe na upofu wa Sapa na Salihi kwa kuathiriwa na mazingira yake asilia; Tukio la kugarikishwa kwa miji na watu kubadilika mawe, Shaaban Robert inawezekana amelitumia kwa kuathiriwa pia na Kurani Tukufu na Biblia Takatifu. Kwa mfano, kisa cha gharika ya Nuhu na kisa cha mke wa Lutu kugeuka kuwa nguzo ya chumvi (Biblia Takatibu, Mwanzo 7: 19-22; 19: 17-26).

Katika tukio la upofu wa Sapa na Salihi, Shaaban Robert ameathiriwa na masimulizi ya *Alfu Lela Ulela* kitabu cha nne hasa kisa cha baba Abdalla kipofu na Walii. Kama ilivyo tamaa ya Sapa katika riwaya ya *Kusadikika* ya kutarajia kupata mafanikio kwa kutegemea bahati ya Salihi na kudai kuwa Salihi hana matumizi na mali hiyo ndivyo ilivyo kwa baba Abdalla kipofu katika *Alfu Lela Ulela* kutaka kujinufaisha kwa kuchukua mali yote ya Walii kwa madai kuwa Walii hana hitaji la kuwa na mali nyingi. Walii licha ya kumwachia Abdalla magunia themanini yote ya dhahabu kinyume cha makubaliano ya kila mmoja kuchukua magunia arobaini arobaini, Abdalla bado alilazimisha kupewa kichupa cha mafuta na kupakwa dawa jicho la kulia ili apate mali zaidi licha ya kutahadharishwa na Walii kuwa atakuwa kipofu akipakwa jicho hilo. Tofauti kati ya visa hivi ni kuwa Abdalla anamlazimisha Walii kumpaka mafuta machoni na

kuwa kipofu, kinyume chake salihi anasema maneno tu na wote wawili, Sapa na Salih, wanakuwa vipofu.

Katika mazingira asilia ya Kezilahabi matukio ya watu kusema au kutazama tu kitu na jambo fulani linatokea ni mengi. Kwa mfano, kuna watu wanaohisiwa kuwa ni wachawi wa macho, kwa kutazama tu chakula hata bila kukigusa sumu inaingia kwenye chakula na ukila chakula hicho unaweza kufa. Anaweza kukuangalia na ukimeza hata mate tu tumbo litauma na usipotibiwa utakufa. Kwa kuthibitisha hilo Mbiti (2011: 167) anasema :

It is believed too that a witch can cause harm by looking at a person or speaking to him words intended to inflict harm on him. ...in some cases it is even held that powerful magic can make a person change into an animal or bird which then goes to attack the victim.

Inasadikiwa kuwa mchawi ana uwezo wa kumdhuru mtu kwa kumtazama, kumnyoshea vidole au kwa kumnenea maneno yatakayomdhuru. ...katika mazingira mengine, pia inasadikiwa kwamba mchawi anaweza kumbadilisha mtu akawa mnyama au ndege ambaye huenda kumdhuru mtu aliyekusudiwa (tafsiri yetu).

Katika mazingira asilia ya Euphrase Kezilahabi wengine wanatumia uchawi na mazingaombwe ya kutazama kwa kuweka maji kwenye mtungi halafu anayatazama maji yale na kuita jina la mtu anayetakiwa kudhuriwa au kutibiwa. Kwa kuita tu jina na kwa tuzama maji kwenye mtungi sura ya mtu anayeitwa itajitokeza kwenye maji yale, na hivyo kuwa rahisi kumfanya jambo lolote. Kwa mfano, kama mtu alipotea kwa muda mrefu bila kujulikana alipo au yupo sehemu fulani na hataki kurudi nyumbani, anapoitwa kwenye maji hayo kwa kuambiwa rudi nyumbani, anazinduka kule alipo na kufunga safari ya kurudi nyumbani. Hii inasadifu mhimili wa uhalisiamazingaombwe unaosema kuwa katika uhalisiamazingaombwe kaida zote za uhalisia na za uasilia huvunjwa. Hivyo,

hakuna mpaka kati ya jamii na jamii, nchi na nchi au mbali na karibu. Kwa hiyo, katika uchawi na mazingaombwe, umbali kati ya sehemu mbili hakuwezi kuwa kikwazo cha kufanyika kwa jambo lililokusudiwa.

Wengine wameenda mbali zaidi kuwatibu wagonjwa hasa waliovunjika wakiwa mbali hata bila kuwagusa. Anachofanya ni kutazama shina la mgomba kama kiwakilishi cha mgonjwa anayetaka kumtibu, halafu anakanda shina la mgomba kwa muda ule aliokubaliana na mgonjwa na hata mgonjwa akiwa umbali wa maili elfu tano atasikia maumivu ya ukandaji huo na mwisho kupona sawa na yule aliyekwenda kwa mtaalamu huyo wa tiba ya kukanda mgomba. Kwa maana hiyo, Kezilahabi kumtumia mfalme kutazama tu jiwe kufanya jiwe kukatika kumetokana na kuwapo kwa matukio kama hayo katika mazingira yake asilia.

Katika sayansi ya tiba kumefanywa utaalumu wa kuchukua damu za watu na kuhifadhi kwenye mtandao ambapo ugonjwa wowote ukiingia mwilini unaonekana kwenye mtandao na hivyo unaweza kutibiwa ukiwa mbali na hata bila wewe kujua. Kinyume chake pia unaweza kuuawa kwa kutumia njia hiyo hiyo. Hii ni sawa kabisa na matumizi ya uchawi na mazingaombwe wa kusema au kutazama kwa lengo la kudhuru au kutibu. Kinachoweza kusionzwa hapa ni kuwa uchawi na mazingaombwe ikitumiwa kwa mtazamo chanya inaweza kuleta maendeleo katika jamii husika. Kwa mfano, tiba kwa njia ya kukanda shina la mgomba inaweza kutumika kupunguza msongamano wa wagonjwa hospitalini pamoja na gharama za usafiri.

Shaaban Robert alikusudia kutumia tukio la vitu vyote katika mji wa Fahari kubadilishwa mawe kukemea tamaduni na ukale usiofaa kama: ibada ya mizimu, kutoa kafara ya wanadamu na kuabudu viumbe kama miti na mawe (*Adili na Nduguze*, kur. 27, 29). Pia alikusudia kutumia tukio la upofu wa Sapa na Salihi ili kutoa funzo kwa jamii na hasa kwa wale wenye wivu wanapooona wenzao wamefanikiwa. Anaasa kuwa kila mmoja ana bahati yake. Hivyo, jaribu bahati yako na usitegemee kufanikiwa kwa namna na njia zile zile alizopitia mwingine, kwani bahati ya mwenzio usilalie nje (*Kusadikika*, uk. 31). Watu wengi katika jamii zetu si wabunifu ila wanaishi kwa kuigilizia na kufanya kama wengine wanavyofanya. Wakiona mmoja kafungua duka na kupata faida wote watafungua duka bila kufahamu kuwa duka inakwepo kwa sababu ya wateja. Hivyo, wote wakifungua maduka wateja watakosekana na matokeo yake wote watafilisika.

Licha ya mafunzo yalitajwa hapo juu, hata hivyo, kuna swali la kujiuliza juu ya nguvu na thamani ya maneno yetu. Inatokeaje maneno tu ya kutamkwa yakaleta Baraka au laana? Kuna nini ndani ya maneno? Kwa mfano, laana iliyotamkwa katika Biblia Takatifu juu ya mji wa Babeli kati ya mwaka 740 na 686 Kabla ya Kristo (White, 1955) bado inadumu mpaka leo. Biblia inasema kuwa Babeli (mji wa Iraq ya zamani) haitakaliwa na watu tena, bali watalala hayawani wakali wa nyikani, nyumba zao zitajaa bundi na majini watacheza huko (Isaya, 13:19-22). Neno hilo limekuwa hivyo mpaka leo. Mfalme Saddam Hussein wa Iraq alipojaribu kushindana na neno hilo kwa kukusudia kujenga upya pale palipokuwa na mji wa Babeli ya zamani alishambuliwa na kuuawa na umoja wa majeshi ya Uingereza na Marekani mwaka 2006.

Kinachotakiwa kujifunza ni kwa namna gani maneno yatumike. Maneno yanaweza kuleta laana au mibaraka kwetu na kwa jamii zetu (Clemence, 2020). Clemence anasema kuwa maneno yanaweza kuwa faraja kwa mtu yeyote yule. Maneno yanaweza kuamsha akili ya mtu na kubadilisha maisha kama yatatumika vizuri. Kinyume chake, maneno yanaweza kuleta maafa na maangamizi ya milele kama yatatumika vibaya. Maneno uumba, na mauti na uzima huwa katika uwezo wa ulimi; na waupendao watakula matunda yake (Biblia Takatifu: Mwanzo, 1:3-26; Mithali, 18: 21). Kwa mfano, Waafrika kwa kukaririshwa kuwa hawawezi kufanya kitu chochote bila msaada wa Wazungu wamekuwa tegemezi kwa mambo yote. Vile vile watoto wa kike wamekuwa duni wakilinganishwa na watoto wa kiume kwa sababu ya maneno yayo hayo.

Nguvu ya maneno inazidiki kujidhihirisha katika maombi ya Mrefu, baada tu ya kuomba, mkomamanga uliota, ukakua na kuanza kuzaa komamanga moja kila siku kuanzia siku hiyo ya kuota kwake. Kila chembe katika komamanga hilo ilikuwa chakula na kinywaji kwa ajili ya Mwelekevu, binti wa mfalme wa Fahari, mji uliogeuzwa mawe. Mwandishi anasema:

..., Mrefu aliomba mkomamanga uote. Mkomamanga huo ulizaa komamanga moja kila siku. Kila chembe katika komamanga hilo ilikuwa chakula na kinywaji mbalimbali. Kwa mti ule wa ajabu binti mfalme aliweza kuishi maisha ya faraja. Mwisho alionywa kuwa siku ya kuona mti ule umezaa matunda mawili ajue Adili, mwokozi wake amefika. Hilo ndilo lililomjulisha siku ile kuwa mgeni wake si mwingine ila Adili (*Adili na Nduguze*, uk. 30).

Katika maisha ya kawaida tukio la kuota na kukua na hata kufikia hatua ya kuzaa matunda kwa mti kama vile mkomamanga ni hali ya kawaida kabisa na wala hakuna swali katika tukio kama hilo. Hii ni kwa sababu katika uasilia miti huota,

hukua na mwisho kuzaa matunda. Hata Yesu ambaye kwa mujibu wa Biblia inaaminika kuwa ni muumba wa vitu vyote, anakubaliana na kanuni hii ya asili ya mbegu kupandwa, kuota na kumea kwa hatua mbalimbali na kwa siku kadhaa mpaka kufikia hatua ya kutoa matunda. Yesu anasema:

...ufalme wa Mungu, mfano wake ni kama mtu aliyemwaga mbegu juu ya nchi; akawa akilala na kuondoka, usiku na mchana, nayo mbegu ikamea na kukua, asivyojua yeye. Maana nchi huzaa yenyewe, kwanza jani, tena suke, kisha ngano pevu katika suke. Hata matunda yakiiva, mara atapeleka mundu, kwa kuwa mavuno yamefika (Biblia Maandiko Matakatifu, Marko 4: 26-29).

Katika mkomamanga wa Mrefu uasilia unabatilishwa katika mambo mengi. Jambo la kwanza ni namna mkomamanga ulivyoota. Mrefu hakupanda mbegu bali aliomba tu na mkomamanga ukaota. Jambo la pili ni mkomamanga kutoa tunda moja kila siku kuanzia siku hiyo hiyo ulipoota. Na la ajabu zaidi ni mkomamanga kuwa sehemu ya utabiri, kuwa siku utakapozaa matunda mawili itakuwa ni siku ya kufika kwa Adili kumwoko Mwelekevu. Mkomamanga kuzaa matunda mawili ni tukio la kawaida kabisa, lakini kuzaa kunapohusiana na kufika kwa mtu ni tukio la ajabu na ni kinyume cha uhalisia. Hata hivyo, katika uchawi na mazingaombwe yale yanayoonekana kutowezekana katika hali ya kawaida yanawezekana kwa urahisi na kwa wepesi wa ajabu. Roh (1925) anathibitisha hili kwa kusema kuwa tumegundua mtindo mpya unaopindua asili juu chini. Yaani kanuni au sheria za asili zinabadilishwa na mambo yanaonekana kuwa kinyume cha uhalisia unaofahamika.

Shaaban Robert ametumia utabiri mara nyingi katika kazi zake za fasihi kwa mfano, sehemu kubwa ya riwaya ya *Kufikirika* ni uganga na utabiri. Katika

mazingira asilia ya Shaaban Robert na hasa katika ukoo wake wengi walikuwa ni waganga na watabiri. Hata Shaaban Robert mwenyewe alikuwa mtabiri (Maggati na Wenziwe, 2021). Kwa mfano, Mwishehe Ulenge ndugu yake Shaaban Robert mama mmoja baba tofauti alimwendea Shaaban Robert na kumwomba amwagulie kama safari yake kwenda Unguja kutokea Tanga itakuwa shwari au itakuwa na mkosi. Shaaban Robert alimwambia atandaze mikono yake mezani. Aliangalia mistari katika mikono ya Mwishehe na kutoa utabiri. Utabiri ulisema kuwa safari itakuwa salama wakati wa kwenda lakini wakati wa kurudi atapata taabu sana baharini. Shaaban Robert pia alimwagulia kuwa katika maisha yake atachelewa sana kupata watoto (taz, uk. 60).

Leo katika sayansi imegundulika kuwa tofauti kati ya watu iko katika mistari midogo midogo iliyoko katika mikono hasa katika vidole. Hii ndio maana alama ya vidole hutumiwa kutofautisha watu. Ili kuthibitisha hilo, watu wanasainishwa kwa kutumia alama za vidole na hasa dole gumba. Hata hivyo, ili kuthibitisha tofauti za saina hizo za vidole ni lazima wataalamu husika waangalie tofauti hizo kwa kutumia mashine. Shaaban Robert hakuhitaji mashine bali kuangalia alama katika mistari tu iliyoko katika mikono ya mtu ilitosha kwake kumfahamu mtu na maisha yake yatakavyokuwa mpaka mwisho wake.

Uwezo huo wa Shaaban Robert wa kufahamu yatakayotokea katika maisha ya mtu kwa kutazama tu mikono, na yale yanayotokea kwa mkomamanga wa Mrefu bado ni fumbo na hayawezi kuelezwa wala kufumbuliwa kwa kutumia nadharia za uhalisia wala za kisayansi, bali zinatakiwa zitazamwe kwa namna nyingine

tofauti kwa sababu zinaonekana kuumba uasilia tusioufahamu (Merrel 1975).

Roh (1925) anathibitisha hili kwa kusema:

Inaonekana dhahiri kuwa nafasi ya miujiza ya kinjozi inasahaulika kabisa na badala yake ulimwengu wetu halisi unajitokeza kwa namna mpya na kwa uwazi zaidi kama siku mpya machoni petu. Tunaitambua dunia hii, ingawa kwa sasa, siyo kama waotao, bali tunautazama kwa macho mapya. Mbali na hayo tumepewa mtindo mpya ambao ni wa uhakika na wa kweli unaofaa kuelezea na kuchambulia dunia hii.

Roh hapa anaeleza kuwa matukio hayo ya ajabuajabu yanayojitokeza katika ulimwengu huu siyo ndoto wala si matukio ya kubuni tu bali ni halisi na ni namna mpya ambayo kwayo ulimwengu unatakiwa utazamwe, na nadharia pekee inayofaa kuchambulia matukio hayo ni nadharia yauhalisiamazingaombwe.

Shaaban Robert anaelezea zaidi matukio ya ajabuajabu yaliyofungamana na imani ya tiba za asili katika riwaya ya *Kufikirika* ambazo anatamani zibadilike. Tiba hizo ni kama vile tiba ya kutegemea makafara, mazinguo, hirizi na mashetani. Kwa mfano akizungumzia vitabu vya hirizi, majini na mashetani, anasema:

Ndani ya vitabu hivyo sanamu mbalimbali zilionyeshwa kama vile za nusu moja mtu na ya pili mnyama;... Madude makubwa kama tembo au nyangumi yaliyoweza kuingia na kutoka ndani ya chupa ndogo na sura nyingi za vioja kabisa (*Kufikirika*, uk.19-20).

Haya ni matukio ya ajabu kwa sababu kutokana na uzito na kimo cha nyangumi na ukubwa wa tembo si rahisi na ni vigumu katika uhalisia tembo au nyangumi kuingia na kutoka ndani ya chupa ndogo. Uzito wa nyangumi mkubwa ni kati ya tani mia mbili hadi mia tatu na ulimi tu wa nyangumi ni tani tatu ambao ni zaidi ya tembo mkubwa. Mdomo wa nyangumi unaweza kuhifadhi tani 90 za chakula

na maji akiufumbua mpaka mwisho. Ili nyangumi ashibe anakula kilo 3600. Baadhi ya mishipa ya nyangumi ni mipana kiasi kwamba binadamu anaweza kuogelea ndani ya mishipa hiyo bila kugusa pembeni. Ukubwa wa nyangumi unakadiriwa kuwa kati ya mita thelathini hadi hamsini³². Tembo ndiye mnyama mwenye umbo kubwa kuliko wanyama wote wa porini. Tembo mzima huwa na wastani wa uzito wa tani 6. 6 na kimo cha hadi mita 4³³. Hivyo wanyama hao kuingia katika chupa ndogo na kutoka ni muujiza kutokea katika uhalisia wala kisayansi haikubaliki lakini katika uchawi na mazingaombwe ni hali ya kawaida, tena ni matukio ya kweli na yanayoaminika katika jamii husika. Hii inashadidiwa na mhimili wa Uhalisiamazingaombwe unaosema kuwa katika uchawi na mazingaombwe kaida zote za uhalisia na za uasilia huvunjwa. Hivyo, binadamu anaweza kujibadilisha sura na kuwa kitu kingine, kuingia popote bila kizuizi, kuzungumza na viumbe wengine na kufa na kuishi kwa wakati mmoja. Kwa hiyo, kitendo cha nyangumi au tembo kuingia na kutoka ndani ya chumba ndogo ni hali ya kawaida katika uchawi na mazingaombwe.

Ingawa kuna matukio mengi ya majini kuingia mahali popote hata kwa kupitia sehemu nyembamba sana katika mazingira asilia ya Shaaban Robert, lakini matukio ya kimazingaombwe kama ya wanyama wakubwa kama tembo na nyangumi kuingia na kutoka ndani ya chupa dogo hayapatikani sana katika mazingira asilia ya Shaaban Robert. Shaaban Robert ameyatumia matukio hayo kutokana na athari za masimulizi ya Alfu Lela Ulela ambayo yanaonekana kuathiri kwa kiwango kikubwa uandishi wake. Kwa mfano, katika kisa cha mvuvi

³² Kutoka internet tarehe 24 May 2017 saa 2: 36 alasiri.

³³ Kutoka internet tarehe 28 Oktoba, 2019

na jini, jini linaingia ndani ya gudulia ndogo ambalo katika uhalisia hata mguu wake hauwezi kutosha. Mwandishi anasema:

...mvuvi...akanena,...nakushihi kwa hisani yako, uniambie kama kweli wewe ulikuwamo ndani ya gudulia hili' Jini likamjibu, 'ndiyo nilikuwamo'. Mvuvi akasema 'kwa hakika siwezi kusadiki. Gudulia hili haliwezi kuingia hata guu lako moja, iliwezekanaje mwili wako mzima kuingia humu? Basi siwezi kusadiki kabisa mpaka nikuone ukiingia'. Basi jini likaanza kujigeuza moshi, ukatandazika pwani na baharini kama kwanza, kisha ukajikusanya pamoja ukaanza kurudi pole pole ndani ya gudulia usibakie nje hata kidogo. Halafu sauti ikatoka guduliani ikimwambia mvuvi, 'Ewe mvuvi usiyesadiki, angalia nimo ndani ya gudulia, je, Sasa wasadiki?' (*Alfu Lela Ulela* Kitabu cha Kwanza, uk. 15).

Tukio hili la kimazingaombwe linadhirihisha athari za wazi za masimulizi ya Alfu Lela Ulela kwa Shaaban Robert. Mwandishi ametumia tukio la ajabu hapa ili kuonyesha jinsi jamii ya Kufikirika ilivyokita imani yake katika kutegemea makafara, mazinguo, hirizi, mashetani, majini na utabiri. Mwandishi anathibitisha hili kwa kusema:

Utabiri ulioshinda katika shindano la waganga ulitiwa katika vitabu maelfu yasiyo idadi. Vitabu hivo vilieleza namna mbalimbali za ramli. Ilitazamiwa kuwa vitabu hivi vyote vitakuwa mwanga wa kumulikia katika mafunzo ya watoto wa nchi ya Kufikirika (*Kufikirika*, uk. 20).

Ingawa jamii asilia alikozaliwa na kukulia Shaaban Robert ilikita imani yake, na hata sasa, katika kutegemea uganga wa mizizi, makafara, mazinguo, hirizi, mashetani na utabiri sawa na jamii ya Kufikirika (*Kufikirika*, uk. 8); hata hivyo, Shaaban Robert anasisitiza kuwa wakati wa kutegemea vitu hivyo tu bila kutafuta tiba za hospitalini na elimu mpya umepita. Hili linadhihirika kwa mtoto wa Mfalme kuponjwa hospitalini na si kwa kafara ya damu ya mjinga na mwerevu ilivyotarajiwa. Shaaban Robert anaonekana kupinga kwa sauti kali sana imani hizi za kushikilia ukale uliopitwa na wakati ikiwa kumeisha patikana mbadala

wake wenye manufaa zaidi. Hii inajidhihirisha katika riwaya zake karibu zote. Kwa mfano, katika riwaya ya *Adili na Nduguze* anapinga kwa sauti kali ibada ya mizimu na kuabudu vitu kama miti na viumbe vinginevyo. Kwa kemeo hilo miji yote inagharikishwa na kila kiumbe chenye uhai katika mji wa Fahari kikageuka jiwe (*Adili na Nduguze*, uk. 29).

Tofauti na Shaaban Robert ambaye ametumia matukio mengi ya kichawi na ya kimazingaombwe yanayotendwa na watu wanaoonekana dhahiri, matukio mengi katika riwaya za Kezilahabi yanatendwa na watu wasioonekana au wanaoonekana na kutoweka. Katika riwaya ya *Nagona*, kwa mfano, katika ukurasa wa kwanza pekee kuna: kikohozi cha mtu asiyeonekana, nyayo za mtu anayetembea asiyeonekana, sauti za watu wasomao vitabu wasioonekana, vicheko vya watu wasioonekana na kuchapwa na watu wasioonekana (*Nagona*, uk. 1). Kuna kupondwa na mayai viza na mtu asiyeonekana, mji wenye watu wengi lakini hawaonekani ingawa unapishana nao njiani, kupigwa kofi ndani ya nyumba na mtu asiyeonekana (*Nagona*, uk.2, 3).

Kezilahabi ametumia matukio ya ajabuajabu yanayotendwa na watu wasioonekana pia katika riwaya ya *Mzingile*. Kwa mfano, Msimuliaji baada ya kurudi kijijini kwao, akitoka makaburini karibu na mbuyu alihisi kama mtu anamfuata. Alitazama nyuma hakuna kitu. Akasikia mtu akipiga makofi kama ishara ya kumwambia arudi. Licha ya kutazama nyuma kwa haraka safari hii, lakini hakuona mtu (*Mzingile*, uk. 100). Zaidi ya yote ametumia matukio yanatendwa na watu wanaoonekana na kupotea ghafla kimiujiza. Mfano wa matukio ya ajabu yanayotendwa na watu wanaoonekana na kupotea au kutoweka

ghafila peupe ni tukio la mwanamke anayefuatana na msimuliaji kimiujiza katika riwaya ya *Mzingile*, ambaye ameelezwa katika sura iliyotangulia kama mhusika wa ajabu. Hapa Kezilahabi kama mwandishi fuatishi kutumia matukio yanayotendwa na watu au viumbe wasioonekana, tofauti na Shaaban Robert anayetumia matukio yanatendwa na watu au viumbwe wanaoonekana dhahiri, amejitenga na athari za Shaaban Robert kwa kuonesha upekee na uasilia kwa kujitenga kabisa na namna ya uandishi wa Shaaban Robert na hata namna yake mwenyewe. Lengo lake likiwa ni kujitenga na aina yoyote ya mabaki au masalio (masazo) ya athari kwa nia ya kuwa na uhuru kamili au mafanikio binafsi (Bloom, 1973).

Zaidi ya yote, kusikia sauti ya mtu anayekohoa, nyayo za mtu atembeaye, sauti za watu wasomao vitabu na kuchapwa ni matukio ya kawaida yanayotokea kila siku katika maisha ya mwanadamu. Matukio hayo yanakuwa ya ajabu na ya kichawi pale yanapotendwa na watu wasioonekana kwa macho ya kawaida ya mwanadamu. Hii ni kwa sababu katika uhalisia ni muujiza watu kufanya matendo kama kukohoa, kucheka, kuchapa na kusoma bila kuonekana au kupotea ghafla peupe.

Matukio kama hayo hutokea sana katika kisiwa cha Ukerewe, mazingira asilia ya Euphrase Kezilahabi. Kwa mfano, kuchapwa viboko na watu wasioonekana katika nyumba ya kulala wageni ya 'Peace land' mjini Nansio mwaka 2001. Pia maaskari kupondwa na limao na watu wasioonekana katika operesheni ya kuhamisha watu kwenda katika vijiji vya ujamaa katika kijiji cha Maregea mwaka 1975 (taz, uk. 92). Hii inadhihirisha kuwa Kezilahabi ametumia matukio haya ya ajabuajabu kwa kuchota kutoka mazingira yake asilia ya Ukerewe.

Matukio ya nyangumi na tembo kuingia na kutoka ndani ya chupa ndogo (kujidogoisha) na matukio ya kujibadilisha kimazingaombwe pamoja na matukio ya kutenda bila kuonekana yanaweza kutumika kwa dunia ya leo kwa mtazamo chanya katika kubana matumizi na kurahisisha usafirishaji katika biashara. Kwa mfano, kama mtu atataka kusafirisha ng'ombe kutoka Shinyanga Tanzania kwenda Dubai, anaweza kuwadogoisha ng'ombe hao au kuwageuza kuwa hata vijiti vidogo vidogo au hata kuwa mchanga na kupakia hata ng'ombe elfu kumi kwenye kichupa kidogo na hivyo kuwasafirisha kwa urahisi na kwa gharama nafuu hadi Dubai. Akifika Dubai atawatoa ndani ya chupa na kuwageuza tena kuwa ng'ombe. Hii inathibitishwa na kisa cha kusafirisha mamba kama kijiti katika mazingira asilia ya Euphrase Kezilahabi (taz, uk. 98).

Shaaban Robert anaeleza matukio mengine ya ajabu yanayotendwa na watu katika riwaya ya *Kufikirika* ikiwa ni pamoja na miti yote ya Kufikirika kukauka kwa kuchimbwa mizizi chini. Ndege wa mfugo na wa hewa wote walikwisha. Nafaka, ngozi zote na wanyama wote wa mifugo na wa misitu waliisha. Sababu ya kuisha kwa vitu hivyo vyote ni kuwa vilitumiwa kutibu ugumba wa Mfalme na utasa wa Malkia (*Kufikirika*, uk. 9-11).

Si rahisi na ni vigumu katika hali ya kawaida vitu hivi vyote kutumika kama dawa ya kunywa, kuvalishwa au kupaka na kuisha kwa matumizi ya watu wawili tu katika nchi nzima. Hii ni kwa sababu watu, yaani mfalme na malkia hata kama watakunywa au kula kwa namna gani hawawezi kufanya vitu hivyo vyote kuisha kwa namna hiyo peke yao.

Mwandishi anakusudia kueleza kuwa kwa sababu ya ufisadi na matakwa binafsi ya watawala wachache mali yote ya nchi inaweza kutumika na nchi kubaki jangwa, kuwa maskini, kuwa na njaa na kuwa na maradhi yasiyotarajiwa. Kwa mfano, Rais Mobutu Seseko wa Zaire aliiba mali ya Zaire kwa kiwango cha kufisha na kuwaacha wananchi wakiwa na umaskini wa kutisha. Mobutu alikuwa na meli yake binafsi iliyoitwa Kamanyola iliyomzungusha katika mto Kongo akila na kunywa vinywaji kutoka Ulaya.

Mobutu alikuwa na Kasri kijijini kwao Gbadolite lenye vyumba mia moja na hoteli za kitalii za nyota tano, 'Motel Zekele'. Katika harusi ya binti yake iliyofungwa mwaka 1992 shela tu iligharimu dola elfu sabini sawa na shilingi za Kitanzania milioni mia moja sitini, cheni na heleni zikigharimu dola milioni tatu. Alikuwa akinyoa ubelgiji na watoto wake walikuwa wakisoma Ufaransa na kurudi Zaire kila mwisho wa wiki. Alikuwa amewaajiri waganga wa kienyeji mia moja ikulu. Mwaka 1975 aliwachukua karibu waganga na wachawi wote wa Zaire kwenda Ujerumani ili kufanyia uchawi timu ya mpira ya Zaire. Wakati akifanya haya yote, huduma za muhimu kama za hospitali, elimu na barabara zikiwa zimekosekana kabisa kwa watu wake anaowaongoza.³⁴

Matendo hayo ya Mobutu ni taswira halisi ya viongozi wengi katika nchi nyingi za kiasia. Nchi nyingi zinabaki jangwa kwa sababu ya ukataji ovyo wa miti na uchomaji mkaa. Uwindaji haramu unaofadhiliwa na baadhi ya viongozi unawamaliza wanyama mbugani. Madini yanachimbwa bila usimamizi mzuri na

³⁴ Imepakuliwa kutoka internet lite m.facebook tarehe 30/05/2019 saa 2.29 Asubuhi

kubakiza mashimo na ardhi isiyo na rutuba. Haya yote yanafanyika ili kushibisha matumbo ya viongozi wachache walafi na wabinafsi wasiotosheka. Hii ndiyo maana Oka (2002) akimnukuu Okri katika riwaya ya Okri ya *The Famished Road* (1991) anasema kuwa Okri anasema aliandika kutokana na hasira, umaskini uliomzunguka na mwelekeo hasi wa serikali na mateso kwa wananchi. Ulikuwa wakati wa ufisadi mwingi nchini Nigeria. Kuwa madarakani na kuwa na nguvu kisiasa kulimaanisha kujinyakulia mali kwako na kabila lako (Okri, 1990).

Shaaban Robert katika kuelezea tukio la wanyama, miti, na rasilimali zingine zote za nchi ya Kufikirika kwisha kwa sababu ya kutibu ugumba wa mfalme na utasa wa malkia anatumia lugha ya kifantasia. Hii ni tofauti na Kezilahabi anayetumia lugha yenye maneno yanayopunguza kuaminika kwa matukio anayoyaeleza na kuchanganya au kuhamisha ndimi. Khamis (2007) akiunga mawazo ya Godek (2005), anasema lugha ya kifantasia ni ile inayotumika kuelezea matukio ya kiajabu yasiyoweza kuaminika kihalisia. Lugha hiyo imetiwa chumvi kiasi cha kuvuka mipaka ya kimantiki kwa lengo la kutaka kuaminisha hali isiyokuwa ya kawaida. Kwa mfano, Shaaban Robert akielezea wingi wa wanyama waliochinjwa ili kutibu ugumba wa Mfalme wa Kufikirika anasema:

Damu ya wanyama hao wakati wa kuchinjwa ilishuka katika mito ikatiririka pamoja na maji hata katika bahari ya Kufaulu. Wekundu wa damu husemwa kuwa uliweza kuonekana katika bahari na mabaharia wa nchi nyingine waliokuwa wakisafiri baharini wakati ule (*Kufikirika*, uk. 11).

Si rahisi katika uhalisia damu ya wanyama waliochinjwa kwa ajili ya watu wawili tu kuwa mto na kutiririka na kuenea baharini. Hata hivyo matumizi ya lugha ya

kifantasia yanadhihirisha kuwa Shaaban Robert amechota kwa kiwango kikubwa kutoka nduni za fasihi simulizi.

Swali la kujiuliza ni kwa nini Shaaban Robert atumie lugha ya kifantasia kuelezea ugumba wa mfalme na utasa wa malkia wa nchi ya Kufikirika kiasi cha kufanya maelezo yake kupungua kiwango cha kuaminiwa. Ili kujibu swali hili ni vizuri ikaeleweka kuwa Shaaban Robert aliajiriwa kama mtumishi katika serikali ya kikoloni ya Mwingereza. Hivyo, kama mtumishi alikuwa anataka kudumisha heshima kwa mwajiri wake na wakati huo huo kama Mwafrika alitaka kupigania haki ya Waafrika wenzake.

King'ei (1999) anasema kuwa Shaaban Robert alijikuta katika mtafaruku mkubwa wa mvutano. Upande mmoja alitaka kuwastahi wakuu wake wa kikoloni na huku pia akitaka kuendeleza harakati za ukombozi wa ndugu zake Waafrika. Kwa hiyo ukichunguza maelezo yake juu ya matumizi ya rasilimali zilizotumika kutibu ugumba wa mfalme na utasa wa malkia, Shaaban Robert alikuwa akiisema serikali ya kikoloni kuwa ilikuwa inachota mali na rasilimali za Tanganyika na kuacha umaskini mkubwa kwa Waafrika walio wengi kwa lengo la kutosheleza mahitaji ya wakoloni wachache ambayo pia hayatoshelezeki hata kama rasilimali zote za nchi zikimalizika.

Kezilahabi kwa upande wake ametumia kuchanganya ndimi na kuhamisha ndimi katika kuelezea baadhi ya matukio ya ajabu katika riwaya zake teule. Kwa mfano, ametumia maneno ya Kilatini: *metaphysica* na *sphinx*. Neno *metaphysica* kwa mfano, ni neno lenye asili ya lugha ya Kilatini lenye maana ya tawi la falsafa

linaloshughulika na kanuni ya asili ya vitu ikiwa ni pamoja na kanuni ya kufikirika kuhusu uwepo. Kwa ujumla inahusu sayansi ya uwepo wa vitu vinavyovuka mipaka ya uhalisia au akili na ung'amuzi wa binadamu (Ponera na Mkomwa, 2019: 475). Kezilahabi kama mwandishi fuatishi kueleza matukio ya ajabu yanayotendwa na watu na viumbe wa kufikirika, kwa kuchanganya na kuhamisha ndimi tofauti na Shaaban Robert anayetumia lugha ya kifantasia, anakusudia kama ilivyokwisha elezwa awali, kuonyesha upekee na uasilia kwa kujitenga kabisa na namna ya uandishi wa Shaaban Robert na hata namna yake mwenyewe. Lengo lake likiwa ni kujitenga na aina yoyote ya mabaki au masalio (masazo) ya athari kwa nia ya kuwa na uhuru kamili au mafanikio binafsi (Bloom, 1973).

Kuhusu neno sphinx, kwa mfano, katika riwaya ya *Nagona*, Mwandishi anasema: “Wangeliua Sphinx” Nabii alianza mazungumzo. “Kama wasingegundua mafuta,” Mtume aliongezea, “hali isingekuwa hivi” (*Nagona*, uk. 35). Kezilahabi amechanganya ndimi hapa kwa kutumia neno la Kilatini sphinx badala ya shetani katika Kiswahili.

Sphinx ni kiumbe cha kimiujiza katika visasili vya Kiyunani. Inaaminika kuwa ana kichwa cha binadamu, mwili wa simba na mara nyingine na mabawa ya tai. Inasimuliwa kuwa ni mdanganyifu, msaliti na muuaji (Ponera na Mkomwa, 2019: 459). Maelezo hayo yakilinganishwa na wasifu wa shetani kama anavyoelezwa katika Biblia yanadhihirisha kuwa matendo na tabia za sphinx ni sawa kabisa na ya shetani.

Biblia inasema:

Ninyi ni wa baba yenu, Ibilisi (shetani) na tamaa za baba yenu ndizo mpendazo kuzitenda. Yeye alikuwa mwuaji tangu mwanzo; wala hakusimama katika kweli, kwa kuwa hamna hiyo kweli ndani yake. Asemapo uongo, husema yaliyo yake mwenyewe; kwa sababu yeye ni mwongo na baba wa uongo (Yohana, 8: 44).

Tofauti hapa kati ya Kezilahabi na Shaaban Robert katika matumizi ya lugha ya kuelezea matukio ya ajabuajabu, inaonesha kuwa Kezilahabi kwa sababu amehandika riwaya zake teule katika kipindi cha usasabaadaye ambapo kuna mchanganyiko wa tamaduni mbalimbali na athari za utandawazi anachanganya lugha na kuiandikia ulimwengu mpana. Kinyume chake Shaaban Robert katika riwaya teule licha ya kutumia lugha ya kifantasia, maandiko yake yamebanwa katika utamaduni finyu wa jamii za Afrika Mashariki.

4.2.2 Matukio ya Ajabuajabu Yanayotendwa na Ndege na Wanyama

Katika riwaya ya *Adili na Nduguze* Shaaban Robert anatumia matukio mawili yanayotendwa na Wanyama. Tukio la kwanza linatendwa na wanyama pale manyani yanapopanda na kuendesha farasi kama binadamu wa kawaida wafanyavyo. Tukio la pili ni pale manyani yanapokula na kulala chumba kimoja na binadamu tena katika vitanda vilivyotandikwa barabara (*Adili na Nduguze*, uk. 9, 46). Ingawa si ajabu kwa binadamu kupanda na kuongoza farasi, lakini hata nyani kupanda na kuendesha farasi ingawa ni tukio la ajabu na la kushangaza lakini wakifundishwa wanaweza kuendesha na kuongoza farasi. Pia nyani kula na binadamu ni jambo linalowezekana. Hata hivyo, matukio haya ni ya ajabu na ya kimazingaombwe kwa sababu kuna hali ya kuhadaa macho ya watazamaji ndani yake. Hii ni kwa sababu hawa nyani wanaozungumzwa wanaonekana kuwa ni

manyani lakini kihalisia ni binadamu. Kwa kudhibitisha umazingaombwe wa tukio la manyani kuendesha farasi mwandishi anasema:

Farasi wa Adili na yule wa Ikibali walikwenda sambamba njiani. Nyuma yao yaliandama manyani juu ya farasi. Kila mtu aliyeona manyani yamepanda farasi alistaajabu. Mnyama kupandwa na mnyama ilikuwa upeo wa miujiza kwa watu. Vinywa vya umati wa watu vilikuwa wazi kwa mvumo wa Lo salala! Wakati umefika wa mawe kusema, miti kujibu na wanyama kuwa watu (*Adili na Nduguze*, uk. 9).

Mwandishi akisisitiza utokawaida wa tukio hilo anasema, “Ikibali aligeuza uso wake kwa Adili akasema kwa ucheshi, “mbwa wanatubwekea kama walionusa mtara wa windo.” Adili alikubali kwa kuinamisha kichwa akatabasamu” (*Adili na Nduguze*, uk. 9). Kwa Ikibali, watazamaji na hata kwa mbwa tukio hili ni la kimazingaombwe, lakini kwa Adili na nduguze, yaani manyani, wanaofahamu ukweli wenyewe ni tukio la kawaida kwa sababu wanafahamu kuwa hao wanaoonekana kwa macho ya kawaida kama manyani si manyani bali binadamu.

Mwandishi anapozungumzia tukio la manyani hao kula na Adili anasema:

Adili alipochukua kijiko, uma au kisu kulia chakula, manyani yake yalifanya vile vile. Kuona vile watumishi walidukuana wakanong’onezana kuwa labda bwana wao alipata wazimu... Haikutazamiwa kuwa aliweza kukubali dhila ya kula na manyani mkono kwa mkono. Watumishi wote walikirihika, lakini Adili hakuwatazama kamwe... Walipomaliza kula Adili alichukua kitambaa akajifuta midomo. Manyani yalipewa vitambaa vyao yakajifuta pia. Watumishi wake walijizuia wasicheke lakini haikuwezekana waliangua kicheko mbele ya bwana wao, “kwa- kwa- kwa!” Adili hakusema neno. Alijua kuwa kama mtu yeyote angalionga jambo kama lile asingeweza kujizuia kucheka... Watumishi walitaka kutazama kama vile vitanda viwili vitalaliwa na manyani! Lahaula, walimwona Adili amelala chumba kimoja na manyani. Walipotosheka kuwa bwana wao amekuwa mwehu walienda zao na mioyo iliyoghadhabika (uk. 46).

Hawa manyani wanaozungumzwa walikuwa ni ndugu wawili wa Adili: Hasidi na Mwivu. Hasidi na Mwivu hawakufurahia Adili alivyogawa mali aliyoipata

toka katika mji uliogeuka mawe ingawa aligawana nao mali hiyo sawa. Pia hawakuridhika na uamuzi wa Adili kukataa kuwapa mchumba wake kuwa mke wao au kushirikiana nao mke mmoja yaani Mwelekevu. Kwa sababu hizo walimtosa Adili baharini na kuokolewa na Huria. Kwa hiyo Huria aliwabadilisha Mwivu na Hasidi kuwa manyani kama adhabu kwa tendo lao hilo oву la kumtosa Adili baharini.

Tukio la Hasidi na Mwivu kuwa manyani si la kawaida katika maisha halisi bali ni tukio la ajabu lisilotarajiwa kutokea katika uhalisia. Hata hivyo katika uchawi na mazingaombwe kwa kutumia nadharia ya Uhalisiamazingaombwe hilo linawezekana. Hii inathibitishwa na mhimili wa uhalisiamazingaombwe unaosema kuwa katika uhalisiamazingaombwe hakuna mpaka kati ya jamii na jamii, nchi na nchi au mbali na karibu, kaida za uasilia na za uhalisia huvunjwa. Hivyo, binadamu anaweza kujibadilisha au kubadilishwa sura na kuwa kitu kingine, kuingia popote bila kizuizi, kuzungumza na viumbe wengine na kufa na kuishi kwa wakati mmoja.

Katika mahojiano kati ya mtafiti na wenyeji wa Tanga, mazingira asilia ya Shaaban Robert, kuhusu uwezo wa jini kumbadili binadamu katika sura nyingine au kumfanya kuwa kiumbe kingine; kati ya watu 20 waliohojiwa, watu 17 walisema jini hana uwezo wa kumgeuza binadamu kuwa kiumbe kingine ila jini anaweza kujibadilisha na kuvaa sura ya binadamu. Watu 2 walisema hawana uhakika na mtu 1 alisema hajui. Wenyeji hao wanasema kuwa binadamu anaweza kufanyiwa uchawi na binadamu mwenzake kwa kumtumia jini lakini hawajasikia katika historia ya jamii zao kitendo cha jini kumbadili binadamu kuwa kiumbe kingine.

Swali la kujiuliza ni kuwa, kwa nini Shaaban Robert atumie tukio ambalo haliko katika uhalisia wa mazingira yake asilia? Katika kulijibu swali hili ni lazima ifahamike kuwa mwandishi wa kazi ya fasihi haathiriwi na mazingira asilia alikozaliwa, kulelewa na kukulia tu, bali kuna mazingira mengine yanayoweza kumuathiri. Mojawapo ni kusoma vitabu, kusikiliza pamoja na kuona picha mbalimbali kama za tamthilia na kadhalika (Ayiera, Ontieri na Ayodi, 2017).

Shaaban Robert kwa kiwango fulani imedhihirika kuwa ameathiriwa na usomaji wake wa vitabu vya *Alfu Lela Ulela* (Wafula 1989). Hii ni kwa sababu matukio ya watu kubadilishwa kuwa viumbe wengine yako mengi sana katika vitabu hivyo. Shaaban Robert ameathiriwa moja kwa moja na baadhi ya matukio hayo kiasi cha kuyaamisha na kuyatumia katika riwaya zake kama yalivyo katika vitabu vya *Alfu Lela Ulela*. Kwa mfano, kisa cha Sidi-Nouman kubadilishwa kuwa mbwa na Amina mkewe aliyekuwa mchawi. Kinaelezwa hivi:

...Amina akafahamu kuwa nilimfuata makaburini, akashikwa na hamaki kupita kiasi na uso wake ukabadilika kwa hasira...nikamtazama kwa hofu na kuwaza itakuwaje baadaye. Ndipo akashika gudulia la maji, akatumbukiza mkono wake ndani yake huku akinuia maneno ambayo sikuyafahamu. Kisha akaninyunyizia usoni mwangu, na kupiga ukelele kama mwenye wazimu akinena, ewe baa pokea tuzo la upelelezi wako, ugeuke mbwa. Basi baada ya maneno kumtoka tu kinywani mwake na bila kujijua kuwa kuna mabadiliko yanayopitia mwilini mwangu, kwa ghafla nilijiona si mtu tena (*Alfu Lela Ulela*, kitabu cha nne, uk. 14).

Ingawa kisa hiki kinahusu kubadilishwa kwa binadamu kuwa mbwa lakini kitendo hiki hakikufanywa na jini kama ilivyo katika *Adili na Nduguze*, bali kilifanywa na binadamu aliyekuwa mchawi kwa binadamu mwenzake. Kisa kilichofanywa na jini kuwabadilisha binadamu kuwa mbwa na kinachoonekana dhahiri kuwa kimetumiwa na Shaaban Robert katika *Adili na Nduguze* ni kisa

kinachopatikana katika *Alfu Lela Ulela* Kitabu cha Kwanza cha mzee wa kwanza na mbwa wawili weusi. Mbwa hao wawili ni nduguze huyo mzee wa kwanza. Kuwa kwao mbwa kulitokana na tabia zao za wivu na kutofurahia mafanikio ya ndugu yao pia kutokuwa na shukrani kwa ndugu yao licha ya ndugu huyo kuwagawia mali yake baada ya wenyewe kupoteza mali katika biashara.

Mwandishi anasema:

Hata nilipofika bandarini nikasimamishwa na mwanamke mmoja mzuri, ijapokuwa alivaa nguo za kimaskini, akanijia na kunishika mkono wangu kunibusu, na kunisihi nimwoe, tena aliahidi kuwa atakuwa mke mwema kwangu, basi mwisho nikakubali...Humo safarini nikazigundua tabia zake nzuri alizokuwa nazo hata nikaanza kumpenda mno, lakini ndugu zangu walinionea kijicho kwa kule kufanikiwa kwangu, wakanifanyia shauri waniue. Usiku mmoja tulipokuwa tumelala walituchukua na kututumbukiza baharini. Walakini, kwa kuwa mke wangu alikuwa ni jini hakuniacha nizame ila alinichukua kisiwani...Nikamshukuru mke wangu sana kwa yote aliyonifanyia, na kumsihi sana asiwaue ndugu zangu. Nilipokwisha kuituliza hasira yake, mara akanichukua..., mpaka juu ya paa la nyumba yangu naye mara akatoweka...Hata nilipokwenda nyumbani kwangu nikawaona mbwa wawili weusi wenye nyuso za huzuni sana wamekuja kuonana na mimi. Nikastaajabu mno, lakini yule jini ambaye alikuja tena aliniambia, 'Usistaajabu kuona mbwa hawa, kwani ni ndugu zako wawili. Nimewaadhibu wakae katika umbo hili muda wa miaka kumi'. Halafu baada yaa kunieleza mahali niwezapo kusikia habari zake, akatoweka (*Alfu Lela Ulela* Kitabu cha Kwanza, uk. 11-12).

Muktadha na mfululizo wote wa tukio ili la mzee na mbwa wawili weusi unafanana kabisa na tukio la Hasidi na Mwivu kubadilishwa na jini, Huria binti Kisasi, kuwa manyani. Tofauti ni kuwa Hasidi na Mwivu walibadilishwa kuwa manyani wakati ndugu hawa wawili walibadilishwa kuwa mbwa. Shaaban Robert hapa ameiga kwa mwigo sisisi yaani wa moja kwa moja kutoka *Alfu Lela Ulela*. Shaaban Robert ametumia matukio ya ajabu hapa ili kuonesha kuwa watu wenye tabia za uchoyo, ubinafsi na wivu wa kupitiliza ni sawa na wanyama. Watu wenye tabia hizo, kwa mfano, za watu wengi kutaka kushiriki au kugombania mke mmoja, kutofurahia mafanikio ya wenzao ingawa mafanikio hayo

yanawafaidia wote, wanafaa kuwa wanyama na si binadamu. Si hivyo tu, bali pia Shaaban Robert anakusudia kutumia tukio la kubadilishwa Hasidi na Mwivu kuwa manyani na tukio la kula na manyani chumba kimoja kuzungumzia suala la utamaduni.

Katika utamaduni wa jamii asilia ya Shaaban Robert haikubaliki kwa binadamu kula na wanyama tena wa porini. Pia kuwalaza katika vitanda vilivyotandikwa vizuri tena vya dhahabu ni kufuru kwa jamii asilia ya Shaaban Robert. Watumishi wa Adili walipoona hili walishindwa kujizuia na kucheka hadharani mbele za bwana wao.

Licha ya tabia njema na adabu iliyotakiwa kwa watumishi kuwa nao kwa bwana zao kwa kufuata utamaduni wa Kiafrika, yaani kwa Waafrika si heshima kwa mdogo kumcheka mkubwa au watumishi kumcheka bwana wao hadharani mbele yake. Kitendo kama hicho ni utovu wa nidhamu na ilikuwa ni sababu tosha ya kufukuzwa kazi kwa watumishi hao. Lakini mwandishi anasema kuwa Adili hakuwajali. Hii ina maana kuwa Adili alifahamu kuwa kitendo chake cha kula na manyani mkono kwa mkono tena kuwapa vitambaa kufuta midomo yao ni kinyume kabisa na utamaduni ambao watumishi wake nao waliufahamu. Kwa hiyo mwenye makosa zaidi kiutamaduni na anayestahili kudharauliwa ni Adili na si watumishi wake. Hii inathibitishwa pale watumishi wake walipohakikisha kuwa Adili tena liwali nadhifu wa Janibu amelala chumba kimoja na manyani tena manyani yakiwa yamepanda katika vitanda; mwandishi anasema kuwa walipotosheka kuwa bwana wao amekuwa mwehu walienda zao na mioyo iliyoghadhabika (*Adili na Nduguze*, uk. 46).

Swali la kujiuliza ni kwa nini Shaaban Robert atumie mazingaombwe hapa na kukubali kwenda kinyume na utamaduni wa jamii yake? Shaaban Robert amemtumia Adili hapa kama kielelezo cha msamaha na upendo kwa wakosaji. Adili anakubali kupata madhila haya yote kwa sababu ya tabia yake ya upendo uliochanganyika na huruma na msamaha kwa watu wasiostahili kusamehewa. Adili anaamua kuingia gharama yote hii ikiwa ni pamoja na kujiandaa kuchapwa badala ya manyani kama Huria hatokubali ombi la Rai la kuwasamehe manyani; kula na manyani, kuchekwa, kudharauliwa na kulala nao chumba kimoja. Yote haya yanafanywa na Adili bila kujali mabaya yote aliyotendewa na manyani yaani Hasidi na Mwivu ndugu zake.

Mwandishi amemtumia Adili kama kielelezo cha mfano bora wa kuigwa katika jamii. Anasema kuwa wanatakiwa watu kama hao, ambao wako tayari kujikalifu takalifu ilipolazimu, kujidhabihu dhabihu ilipotakiwa na kusamehe msamaha ulipobidi. Watu wenye mioyo miema isiyokata tamaa, wavumilivu, wenye huruma na akili ya upembuzi. Kama hata nusu ya watu duniani wangukuwa na mawazo na matendo kama hayo, mambo makubwa na bora zaidi yangefanywa, na nusu ya matatizo ingetoweka na kuishi maisha ya peponi hapa duniani (*Adili na Nduguze*, uk. 45).

Manyani, yaani Hasidi na Mwivu waligeuzwa manyani kwa sababu ya tabia na matendo yao ambayo pia ni kinyume na utamaduni wa Kiafrika. Waligeuzwa manyani kwa sababu ya wivu, uchoyo, ubinafsi na kutaka washiriki mke mmoja wanaume watatu. Katika utamaduni wa Kiafrika hakuna utamaduni wa mke mmoja kuolewa na wanaume watatu kwa wakati mmoja. Kitendo cha Adili kuwazuia kushiriki mke mmoja, Mwelekevu, ndicho kilichowaghadhabisha na

kuwasababisha kumtosa Adili baharini. Matokeo yake, jini, Huria binti Kisasi, aliwageuza kuwa manyani kama adhabu kwa matendo yao maovu. Shaaban Robert anatetea utamaduni wa Kiafrika kwa kutaka utaratibu wa ndoa ufuatwe kama inavyotakiwa katika utamaduni wa Kiafrika. Kwa kusisitiza hili mwandishi anasema:

...kuna mambo yanayofaa na yasiyofaa kushiriki. Ndoa ni jambo moja kati ya yale yanayokataa ushirika. Ushirika katika ndoa unapasa wanyama na ndege. Mtu anatukuzwa mno kuliko mnyama. Huchukiza akiishi katika maisha duni. Inapasa watu wa wakati ujao katika Afrika, Asia na Janibu kuishi katika maisha bora ya utu, na kufanya dunia mahali pa kiasi, siyo mahali pa ulafi na uchafu. Mwanamume hakukusudiwa kuwa fahali wa kila mtamba, wala mwanamke kuwa tembe la kila jogoo (*Adili na Nduguze*, uk. 32).

Shaaban Robert anakusudia kuzungumzia mambo mengi katika tukio hili. Moja, heshima ya ndoa na kujali utu wa mwanamke. Ndoa inatakiwa iwe ni makubaliano ya watu wawili: mwanaume na mwanamke, waliokubaliana wenyewe kwa matashi yao binafsi, kuwa wataishi pamoja kama mume na mke (WiLDAF Tanzania, 2011). Katika kisa hiki ni Adili pekee ndiye aliyekubaliana na Mwelekevu na si ndugu zake. Kwa hiyo ndugu zake kutaka kuingilia ndoa hiyo na kutaka nao kumwoa Mwelekevu si heshima ya ndoa. Na kwa hili Shaaban Robert anasema haifahi wala haikubaliki. Utu wa mwanamke kama binadamu mwenye matashi na hiari ya uchaguzi pia lazima uzingatiwe. Mwanamke asichukuliwe kama nguo au bidhaa ambayo mtu anaweza kununua halafu akamgawia mwingine au wanaume wakashirikiana kumtumia kama watakavyo wao. Mwanamke anatakiwa awe huru kuchagua nani awe mume wake kwa hiari yake mwenyewe na si vinginevyo. Hili limesisitizwa pia na Shaaban Robert wakati Hunde alipotaka kulazimisha kumwoa Huria bila utashi wa Huria mwenyewe. Huria hakukubali kulazimishwa hata kama ilielekea kugharimu

maisha yake. Kitendo cha Adili kumwua nyoka, yaani Hunde na Hasidi na Mwivu kuwa manyani, inathibitisha kuwa Shaaban Robert anachukizwa sana na ndoa za kulazimishwa. Hivyo, wanaolazimisha kuoja kwa nguvu, iwe ni kwa sababu ya utajiri wao, vyeo vyao au kwa sababu ya nafasi zao katika jamii wanastahili kuwa wanyama, kama Hasidi na Mwivu walivyobadilishwa kuwa manyani.

Jambo la pili analozungumzia Shaaban Robert hapa ni desturi au utamaduni wa kurithi wanawake mara wanapofiwa na waume zao. Mara baada ya Hasidi na Mwivu kumtosa Adili baharini waligawana mali zake na kugombana wakishindana nani amwoe Mwelekevu. Katika tamaduni nyingi za Kiafrika kuna mila ya kurithi wanawake mara wafiwapo na waume zao. Mara nyingi mwanamke hana uamuzi katika suala hili na akikataa kurithiwa anayang'anywa mali zote za mumewe, kama walivyofanya Hasidi na Mwivu, bila kujali amechangia kiasi gani katika kupatikana kwa mali hizo. Kwa mfano, sehemu kubwa ya mali ya Adili ilitoka katika mji uliogeuzwa mawe ambayo ilikuwa ni milki ya Tukufu, baba yake Mwelekevu. Kitendo cha Mwelekevu kuamua kujitosa baharini ili asirithiwe na Hasidi au Mwivu ni kielelezo tosha kuwa Shaaban Robert hakubaliani na mila ya kurithi wanawake kwa nguvu bila utashi wao binafsi.

Jambo la tatu analozungumzia Shaaban Robert katika tukio hili la Hasidi na Mwivu kuwa manyani, ni tofauti kati ya tamaduni mbalimbali katika kutoa maamuzi. Hasidi na Mwivu walidai kuwa kama mume mmoja katika Afrika aliweza kuoja wake wengi, na mke mmoja katika Asia aliweza kuolewa na wanaume kadhaa, isingelikuwa vyema kama nao ndugu watatu wa Janibu

wangalishiriki uzuri wa mke mmoja? (*Adili na Nduguze*, uk. 32). Shaaban Robert ametumia swali hili ili kusisitiza kuwa kila jamii ina utamaduni wake. Hivyo, jambo linaweza kuwa jema na la kufaa kabisa na lisilo na dhara lolote kwa jamii za Kiafrika kulingana na utamaduni wao lakini jambo hilo hilo linaweza kutofaa kabisa kwa nchi za Ulaya au Asia. Kwa hiyo, mtu yeyote au nchi yoyote isilazimishe utamaduni wake kutumika kutolea maamuzi katika utamaduni wa jamii nyingine. Kama ndugu zake Adili walikuwa wanaona kuwa inafaa na inakubalika kwa jamii za Asia mke mmoja kuolewa na wanaume wengi basi ingefaa wawe Waasia, na kwa vile haiwezekani ni lazima wakubaliane na utamaduni wa Kiafrika. Haifai hata kidogo kutumia sheria au utaratibu wa maisha katika jamii mmoja kutolea maamuzi katika jamii nyingine tofauti. Kwa mfano, baadhi ya nchi za Ulaya zimehalalisha ndoa ya jinsia moja katika nchi zao ingawa madhara yake yanaeleweka bayana kibaiolojia. Matokeo yake wanalazimisha utekelezaji wa maamuzi yao hayo katika nchi za Afrika. Hii ni kinyume cha haki na utu.

Shaaban Robert anatumia tukio la Hasidi na Mwivu kuwa manyani kuasa na kutoa utabiri wa aina ya maisha yafaayo kwa Afrika ya wakati ujao, kwa mfano, wakati wetu huu. Maisha hayo ni pamoja na kuheshimiana, kuwa na kiasi, kuachana na tabia za kinyama kama ulafi, uchafu na uzinzi. Mwandishi anasema:

Mtu anatumizwa mno kuliko mnyama. Huchukiza akiishi katika Maisha duni. Inapasa watu wa wakati ujao katika Afrika, Asia na Janibu kuishi katika maisha bora ya utu, na kufanya dunia mahali pa kiasi, siyo mahali pa ulafi na uchafu (*Adili na Nduguze*, uk. 32).

Mbali na nasaha hizo za Shaaban Robert, maisha ya kinyama kama vile uchafu, ulevi na ngono nje ya ndoa katika Afrika na dunia kwa ujumla yamezidi kiasi cha

kufanyika hadharani mbele za watu na bila aibu. Picha za uchi, filamu za ngono, ndoa ya jinsia moja na kila aina ya uchafu ushabikiwa na kushangiliwa na kufurahiwa na watu wengi huku ngono nje ya ndoa imekuwa ni mtindo wa kisasa na kupewa majina mengi sana ya kuihalalisha (Amisah, 2005; Waruguru, 2013). Tukio la nyani kupanda na kuendesha farasi katika riwaya ya *Adili na Nduguze* ni sawa na tukio la simba na pundamilia kumbeba msimuliaji na mke wake kuwapeleka juu ya mlima katika riwaya ya *Mzingile* ya Euphrase Kezilahabi. Msimuliaji pamoja na mwenzake (mkewe) walipowaona watoto wawili wanaong'ara kama wao juu ya mlima waliamua kwenda kuwaona, ndipo pundamilia na simba walipojitolea kuwapeleka. Mwandishi anasema:

“Nitakupeleka,” pundamilia alisema. “Na mimi nitakupeleka,” Simba alimwambia mwenzangu. “Na tufanye mashindano, tuone nani atafika kwanza pale kileleni,” pundamilia alitoa wazo. Tulipanda juu ya migongo yao, na mara walianza kukimbia kuelekea kileleni (*Mzingile*, uk. 126).

Si suala la kawaida na halitarajiwi katika uhalisia wanyama kama pundamilia na simba kujitokeza wenyewe na kuhiari kuwabeba wanadamu. Inapotokea wanyama kama hao kuhiari kuwabeba wanadamu inakubalika kuwa tukio hilo si la kawaida, ni la ajabu na la kushangaza.

Tofauti kati ya tukio la manyani kuendesha farasi katika riwaya ya *Adili na Nduguze* na tukio la simba na pundamilia kuwabeba msimuliaji na mkewe katika riwaya ya *Mzingile* ni kuwa, manyani wa *Adili na Nduguze* si manyani au wanyama wa kawaida kama walivyo simba na pundamilia wa *Mzingile*, bali ni wanadamu waliobadilishwa kuwa manyani. Kwa hiyo tukio, la simba na pundamilia kuhiari kuwabeba wanadamu ni la ajabu katika hali ya kawaida lakini tukio la manyani kupanda na kuendesha farasi ni la ajabu na ni la

kimazingaombwe. Hii ni kwa sababu manyani hao wanaoonekana kwa macho ya kawaida kuwa ni manyani ni wanadamu waliobadilishwa kuwa manyani.

Hata hivyo Kezilahabi inawezekana ametumia mafungu ya Biblia katika kuzungumzia tukio la simba na pundamilia kuwabeba wanadamu kwa hiari yao kama ishara ya amani, mahusiano mema na umoja kati ya viumbe wote katika ulimwengu mpya wa kinjozi anaoufikiria (Biblia Takatifu, Isaya 11: 6-9).

Kezilahabi anatumia sherehe za matumaini ya mwezi ujao zinazofanyika katika mji wa watu wasioonekana kwa macho kama tukio la ajabu linalofanywa na wanyama na ndege katika riwaya ya *Nagona*. Sherehe hizo usherehekewa kwa vicheko vya binadamu na wanyama. Mwandishi anasema:

Wakati huo tulisikia vicheko vingi sana nje, vya wanyama na vya binadamu. Hii hutokea mara moja kwa mwezi. Twende nje ukatazame mwenyewe. Nje tuliwasikia fisi wakicheka na nyani wakilialia. Mjini vilisikika vicheko vya kila aina. Upande wa Mashariki palionekana mwezi mpevu mwekundu. “Siku kama ya leo wanaiita siku ya matumaini ya mwezi ujao (*Nagona*, uk. 6).

Katika riwaya ya *Mzingile* Kezilahabi anatumia ndege anayemwongoza njia Msimuliaji na mke wake walipopotea. Ndege huyo alifanana na yule ambaye Msimuliaji alimwona njia panda. Ndege huyo alifahamu kuwa msimuliaji hajui njia sahihi ya kufuata kati ya njia tatu zilizokuwa mbele yake na kumwonyesha njia sahihi na kumwongoza njia hadi mtoni. Alipofahamu kuwa msimuliaji yuko mahali sahihi alitoweka (*Mzingile*, uk. 11-12, 119). Mwandishi akieleza jinsi ndege alivyomwongoza msimuliaji na mke wake, anasema:

Tulimfuata, akawa ametangulia mbele akirukaruka toka mti hadi mti. Akitua kwenye mti aliimba wimbo huo huo. Tukawa tunafuata wimbo gizani. Mwishowe tulifika kwenye chemichemi. Ndege akatoweka (*Mzingile*, uk. 119).

Viumbe kama wanyama kufahamu na kupanga sherehe siku moja na binadamu ni tukio la ajabu, na hata ndege kufahamu kuwa mtu amepotea njia na kuwaongoza ni tukio la ajabu ambalo si rahisi kutokea katika maisha halisi. Hata hivyo, katika uchawi na mazingaombwe ni hali ya kawaida. Hili linathibitishwa na mhimili wa uhalisiamazingaombwe ulioelezwa awali kuwa katika uchawi na mazingaombwe hakuna mpaka kati ya jamii na jamii, nchi na nchi au mbali na karibu, kaida za uasilia na za uhalisia huvunjwa, hivyo, binadamu anaweza kujibadilisha sura na kuwa kitu kingine, kuingia popote bila kizuizi, kuzungumza na viumbe wengine na kufa na kuishi kwa wakati mmoja. Kwa hiyo, katika uchawi na mazingaombwe binadamu na wanyama kama nyani, mbwa na simba kuwa na mipango ya pamoja ni suala la kawaida.

Kinachoonekana dhahiri ni kuwa inawezekana hatujafahamu vizuri mazingira yetu na mahusiano yaliyoko kati ya binadamu na viumbe wengine. Kwa mfano, Mamajusi kutoka Mashariki ya mbali, inawezekana Urusi, kwa kusoma na kufahamu elimu ya anga, walipoona nyota isiyo ya kawaida angani walifahamu kuwa nyota hiyo inaonyesha kuwa mtu mashuhuri, yaani Masihi amezaliwa mahali fulani. La ajabu nyota hiyo iliwaongoza njia mpaka Bethlemu katika nchi ya Israeli na ilipofika mahali alipolazwa Yesu katika holi la ng'ombe, nyota ikasimama pale pale. Ajabu zaidi tena ni 'nyota' baada ya kutambulika njama za Herode za kutaka kumwua mtoto Yesu, nyota hiyo hiyo ikawaongoza kurudi kwao kwa njia tofauti (Biblia Takatifu, Mathayo 2:1-12).

Swali ni kuwa ndege wanafahamuje kuwa mtu huyu amepotea au kuna mawasiliano gani kati ya nyota na wanadamu na nyota kufahamu matukio katika maisha ya binadamu, ni maswali ambayo hayawezi kujibiwa kwa kutumia akili na ufahamu wa kawaida wa binadamu. Kwa mfano, katika mazingira asilia ya Shaaban Robert kuna sherehe za kila mwaka za kutoa kafara kwa majini au kwa mizimu yao katika kisiwa cha Chumbagama (taz, uk. 74). Ikifika tarehe za sherehe hizo na watu wakasahau kuhudhuria, majini hupiga ngoma kisiwani hapo kuwaalika au kuwakumbusha kuwa tarehe za sherehe zimefika na hivyo wajiandae kwa sherehe hizo. La ajabu pia katika sherehe hizo ni kuhudhuria kwa aina fulani ya ndege weupe ambao wanafika sambamba na wenyeji katika sherehe hizo na muda sherehe zinapoisha ndege hao huruka kwa vilio vinavyoashiria kufurahia sherehe na kutoweka pale wenyeji wanapotoka hapo kisiwani.

Katika mazingira asilia ya Kezilahabi kuna mahusiano ya aina yake kati ya watu wanaoitwa wachawi na wanyama kama mamba. La ajabu katika mahusiano hayo ni uwezo wa mamba kutumwa na mchawi na kusafiri kwenda umbali wowote kwenda kumkamata mtu, na humkamata yule tu aliyetumwa kumkamata bila kukosea au kumkamata mwingine asiyekusudiwa. Mamba huyo atasafirisha windo lake ndani ya maji salama bila kudhurika mpaka kwa mchawi aliyemtuma. Mfano ni kisa cha John mbadhirifu aliyesafirishwa na mamba (taz, uk. 97). La ajabu ni kwa namna gani mamba anaweza kumsafirisha mtu akiwa amemzamisha ndani ya maji bila huyo mtu kufa kwa kukosa hewa? Hata hivyo katika uchawi na mazingaombwe hakuna linaloshindikana.

Katika Biblia Takatifu, kwa mfano, Yona anamezwa na samaki na kuwa ndani ya tumbo la samaki kwa siku tatu na mwisho samaki kumtapika akiwa salama kabisa tena pale alipotakiwa kwenda (Yona 1: 17; 2: 10). La ajabu zaidi ni kwa yule aliyekusudiwa kukamatwa na mamba, hata kama hakuwa na mazoea ya kwenda ziwani lakini siku hiyo lazima dhamiri itamlazimisha na kwenda ziwani ili akamatwe na mamba. Matukio kama haya hayawezi kuelezeka kisayansi, lakini ni matukio halisi yanayotokea katika jamii husika na jamii haitilii shaka hutokeaji wake kwa sababu ingawa ni matukio ya ajabu hata hivyo ni mwono wa uhalisia wa maisha yao ya kila siku (Bowes, 2004).

Kezilahabi katika kutumia matukio yanayotendwa na ndege na wanyama ameathiriwa na Shaaban Robert kwa kumwiga lakini si kwa mwigo sisisi. Hii ni kwa sababu Kezilahabi (mwandishi fuatishi), sawa na Shaaban Robert (mwandishi tangulizi) ametumia ndege na wanyama wanaotenda maajabu. Tofauti kati ya ndege na wanyama wa Kezilahabi na wale wa Shaaban Robert ni kuwa ndege na wanyama waliotumiwa na Kezilahabi ni halisi. Kinyume chake ndege na wanyama wa Shaaban Robert si ndege na wanyama halisi. Kwa mfano, ndege wa Shaaban Robert aliyemwoko Adili baharini katika riwaya ya *Adili na Nduguze* hakuwa ndege bali alikuwa ni jini, Huria binti Kisasi, aliyejibadilisha ndege. Manyani yanayokula na Adili kwa kutumia uma na vijiko na baadaye kupanda na kuongoza farasi, hayakuwa manyani bali ni binadamu, Hasidi na Mwivu, waliobadilishwa manyani na Huria binti Kisasi. Ilhali, simba na pundamilia wa Kezilahabi waliowabeba Msimuliaji na mkewe na ndege aliyewaongoza njia ni wanyama na ndege halisi.

Kwa mantiki hiyo hapo juu, Shaaban Robert anakusudia kueleza kuwa ndege na wanyama kwa wenyewe hawana uwezo wa kuyatenda hayo waliyoyatenda. Kinyume chake Kezilahabi anakusudia kujibu kuwa ndege na wanyama wana uwezo wa kutenda mambo fulani ambayo yanaaminika kuwa yanaweza kutendwa na binadamu tu. Hivyo, ni kana kwamba Kezilahabi amekusudia kuongeza maarifa fulani ambayo anadhani Shaaban Robert hakuwa nao juu ya uwezo wa viumbe wengine kama ndege na wanyama. Bloom (1973) akielezea mwigo katika nadharia ya Kiwewe cha Kuathiriwa anasema kuwa kwa kuiga, msanii fuatishi huendeleza mada na mawazo ya msanii tangulizi lakini siyo kwa mwigo sisisi bali anayakamilisha kwa namna nyingine inayoonesha kuwa msanii tangulizi inawezekana alishindwa kuyakamilisha. Hapa msanii fuatishi mara nyingi anatomia “tabaini” kuendeleza mawazo hayo ya msanii tangulizi.

4.2.3 Matukio ya Ajabuajabu Yanayotendeka Yenyewe Kutokana na Ukiamabile

Mojawapo ya matukio ya ajabu yanayotendeka yenyewe aliyotumia Shaaban Robert ni pamoja na kuwaka moto kwa nyoka (jini Hunde mfalme wa Ngazi) aliyeuawa na Adili ambaye alitaka kumwua tandu (jini Huria binti Kisasi) katika riwaya ya *Adili na Nduguze*. Mwandishi anasema:

Kitambo kidogo aliona nyoka aliyemwua anawaka moto. Mara moja alikuwa majivu matupu. Kufumba kope na kufumbua mahali palipokuwa na majivu palitokea chemichemi ya maji safi. Mambo haya yalikuwa mwujiza mkubwa sana kwa Adili (*Adili na Nduguze*, uk.18).

Hunde alitaka kumwua tandu, yaani Huria binti Kisasi, kwa sababu Huria alikataa kuolewa naye. Kuwaka moto, kuwa majivu na kutokea kwa chemichemi ya maji safi katika majivu ya nyoka aliyewaka moto baada ya kuuawa ni muujiza kutokea

katika maisha ya kawaida. Uajabu wa tukio hili unazidi kuweka wazi kuwa Shaaban Robert ametumia matukio ya ajabuajabu katika riwaya ya *Adili na Nduguze*. Mwandishi ametumia tukio hili la ajabu ili kudhihirisha kuwa mwisho wa waovu ni kuangamizwa na kutoweka milele. Zaidi ya yote waovu wanapotoweka mazuri yanashamiri, yaani palipokuwa na majivu ya nyoka pakatokea chemichemi ya maji safi.

Katika utangulizi wa *Kusadikika* Shaaban Robert anasema kuwa nchi ya Kusadikika ni nchi isiyoandikika, ramani yake ni adimu kupatikana na njia ya kufikia nchi hiyo haikanyagwi kwa nyayo bali fikra. Maelezo hayo tu, yanathibitisha kuwa nchi hiyo siyo nchi ya kawaida kama zilivyo nchi zingine. Mwandishi anaeleza kuwa nchi hiyo imepakana na nchi ya Anasa, nchi ya Majaribu, Bahari ya Kufaulu na Safu ya Milima ya Jitihadi. Hayo maelezo yanathibitisha kuwa Kusadikika ni nchi ya ajabu mno. Hii ni kwa sababu hakuna nchi duniani isiyokanyagwa kwa nyayo, isiyoandikika wala kuchorwa ramani yake.

Mwandishi amekusudia kutumia uajabu wa nchi ya Kusadikika ili kuwatahadharisha wasomaji wake kuwa yale watakayoyasoma katika riwaya hii wasiyaangalie kwa mtazamo wa nchi fulani maaalum. Bali kila jambo litakalomgusa katika dhamiri yake ajue kuwa linamhusu na jamii yake. Massawe (2014: 75) akizungumzia hili anasema:

Hii si nchi ya kawaida tunayoifahamu, ni nchi ya ajabu mno. Kwa kutumia mandhari ya aina hii Shaaban Robert amefaulu kusawiri madhila mengi yaliyofanywa na serikali ya Kikoloni kwa wananchi wa nchi nyingi za Afrika na kwingineko kulikotawaliwa na wakoloni hao. Aliyoyasawiri ni uporaji wa mali za wananchi, utawala wa mabavu, dhuluma ya haki, elimu

duni kwa wananchi, huduma duni za afya, na kuwalazimisha wananchi kufanya kazi katika mashamba ya wakoloni kwa malipo kidogo. Kwa kutumia mandhari halisia hasingeweza kusawiri mambo yote haya na kazi zake zikaruhusiwa kuchapwa na kusomwa na wananchi mbele ya serikali ya Kikoloni.

Wakati Shaaban Robert anapotumia tukio la ajabu la nchi ya Kusadikika kama nchi isiyoandikika, ramani yake ni adimu kupatikana na njia ya kufikia nchi hiyo kutokanyagwa kwa nyayo bali fikra; Kezilahabi anatumia tukio la kupotea kwa jengo alilokuwa akikaa mfalme aliyemtunza Paa baada ya Wasaka paa kukabidhiwa Paa na kutoka nje ya jengo hilo kama tukio la ajabu linalotendeka lenyewe. Mwandishi anasema:

Tulipotazama nyuma hatukuona tena jengo! Tulishangaa. “Jengo limekwenda wapi?” Niliuliza. Sasa mmo kwenye duara,” Paa alisema “Hamtaliona jengo tena kutoka nje. Iliyobaki ni kuelekea kati. Nitawaongoza njia (*Nagona*, uk. 34).”

Si jambo la kawaida kutokea katika maisha ya kawaida jengo kubwa linalokaliwa na watu wengi kutoweka na kutoonekana tena mara tu watu wanapotoka ndani yake. Kutoweka kwa jengo hili ni tukio la ajabu linalotendeka lenyewe. Matukio kama hayo ya kutokea na kupotea ghafla tena peupe kwa vitu kama majengo, miji, meli au mitumbwi ziwani ni mengi katika mazingira asilia ya Kezilahabi. Kwa mfano, katika kisa cha Ebiaro Nyabateso (taz, uk. 91) wavuvi waliona meli inawajia kama inataka kugonga mtumbwi wao lakini meli hiyo ikapotea ghafla karibu yao peupe. Kwa hiyo Kezilahabi kutumia matukio kama hayo ni kwa sababu ya athari ya matukio yaliyoko katika jamii yake.

Tofauti na Shaaban Robert, Kezilahabi ametumia miti na misitu inayocheke, bustani yenye matunda na maua yanayotoa mwanga, yasiyochumika na yanayoteleza kiajabuajabu kama tukio la ajabu linalotendeka lenyewe (*Nagona*,

kur.1, 13). Katika uhalisia binadamu kucheka ni jambo la kawaida lakini kicheko kinapotolewa na miti au misitu ni tukio la ajabu na la kuogofya. Mwandishi anasema: Nilisikia vicheko karibu kutoka katika kila mti. Msitu mzima ulianza kunicheka. Ghafla miti yote iliacha kucheza na vicheko vikaisha (*Nagona*, uk. 1).

Hili ni tukio la ajabu na la kuogofya, yaani kuchekwa na miti na misitu si suala la kawaida na haliwezi kufumbuliwa au kueleweka kwa kutumia mantiki wala kwa kutumia nadharia za kihalisia bali kwa kutumia nadharia ya Uhalisiamazingaombwe. Wana uhalisiamazingaombwe wanasema kwamba, matukio ya uchawi na mazingaombwe yanayoonekana yenye hali za kuogofya na kuduwaza yachukuliwe kama matukio ya kawaida. Wanasisitiza kuwa matukio hayo yachunguzwe kama matukio ya kawaida yanayotokea katika jamii na kuhusisha matukio hayo na kile yanachokisawiri katika maisha ya kawaida katika jamii husika (Wamitila, 2003).

Katika mazingira asilia ya Kezilahabi kuna mti ambao umeota ukingoni kabisa mwa ziwa na matawi yake yamening'ining'ia kabisa majini. La ajabu ni kuwa majani ya mti huo hayadondoki majini hata iweje. Hata hivyo visa vya miti na viumbe wengine kuzungumza au kutenda kama binadamu ni kisa cha 'Ebiaro Nyabateso' au kichaka kinachotembea na kisa cha 'Nyabulebeka' au jiwe linalocheza (taz, uk. 91, 102).

Ebiaro hutokea ziwani hasa kwa wavuvi wanapovua katikati mwa ziwa. Kichaka hicho kinajitokeza na kujongea kikiwaelekea wavuvi hao kukiwa na sauti kama za watu wasioonekana ikitoka katika kichaka hicho. Kwa sababu ya tukio hilo wavuvi wamefundishwa kuwa wakiwa ziwani wakiona tukio kama hilo

wasiseme, kwa mfano, unaona kichaka hicho! Wakibaki kimya watapata samaki wengi sana siku hiyo lakini wakisemezana wanaweza kutumbukia ziwani na kupoteza maisha yao.

Kinyime chake, Nyabulebeka ni jiwe la maajabu lililoko katika mazingira asilia ya Kezilahabi. Jiwe hilo linaitwa nyabulebeka kwa sababu likiimbiwa linacheza. La ajabu zaidi ni kuwa jiwe hilo lenye uzito wa tani takriban hamsini, huwa linacheza linapoimbiwa na mtu fulani tu maalum ambaye amerithishwa kusimamia jiwe hilo. Mtu huyo anaimba akitaja mizimu yao au majina ya babu zao waliokufa zamani na anapoimba na kukanyaga jiwe hilo kidogo tu, jiwe linaanza kucheza.

Suala la uasilia kuongea, kucheza au kuimba halikutumiwa na Kezilahabi tu lakini limetumika hata katika maandiko matakatifu. Biblia Takatifu inasema: Mchana husemezana na mchana, usiku hutolea usiku maarifa. Hakuna lugha wala maneno sauti yao haisikilikani. Sauti yao imeenea duniani mwote, na maneno yao hata miisho ya ulimwengu (Zaburi, 19: 2-4). Nyota, mwezi na jua vinamsifu Mungu. Pia Biblia inasisitiza kuwa nyota za asubuhi kwa pamoja humwambia Mungu (Zaburi, 148:3; Ayubu 38: 7).

Mchunguzi wa sayansi ya Biblia katika maswala ya anga, Geoffrey Cornelius (1996) anasema kuwa nyota zina usiri mkubwa wa uumbaji na kuna uwezekano mkubwa kuwa nyota zinazungumza. Wanasayansi wa Kimarekani kwa kutumia chombo chao cha NASA (chombo cha ugunduzi wa Mars) wamegundua kuwa nyota zinazungumza ; na pia zinakufa ingawa hazina uhai. Wameenda mbali zaidi kwa kusema kuwa sauti na maneno yaliyozungumzwa miaka zaidi ya mia tano

iliyopita hayajapotea yako tu angani. Wanachoshindwa bado ni kuhusisha maneno hayo na mtu aliyeyasema.

Katika kutumia matukio yanayotendeka yenyewe kutokana na ukiamambile, Kezilahabi kama mwandishi fuatishi amejitahidi kujitenga kwa kiasi fulani na athari za Shaaban Robert. Wakati Shaaban Robert anapotumia nyoka aliyeuawa na Adili kuwaka moto na majivu yake kuwa maji safi, Kezilahabi anatumia miti inayochekeka na jengo linalotoweka ghafla na kutoonekana tena. Hivyo, hapa Kezilahabi ameonesha upekee na uasilia kutoka katika athari za Shaaban Robert na hata katika riwaya zake tangulizi. Bloom (1973) anasema kwamba, kwa kutumia upekee na uasilia mwandishi fuatishi hujitenga kabisa na namna ya uandishi wa msanii tangulizi na hata namna yake mwenyewe. Lengo la msanii fuatishi hapa ni kujitenga na aina yoyote ya mabaki au masalio (masazo) ya athari kwa nia ya kuwa na uhuru kamili au mafanikio binafsi.

4.3 Kiishilio

Sura hii imechunguza athari ya mazingira asilia ya watunzi katika matumizi ya matukio ya ajabuajabu katika riwaya teule za Shaaban Robert na za Euphrase Kezilahabi. Lengo lilikuwa chunguza athari ya mazingira asilia ya watunzi katika matumizi ya mbinu ya uchawi na mazingaombwe katika riwaya teule na kulinganisha matumizi ya mbinu ya uchawi na mazingaombwe kati ya watunzi Shaaban Robert na Euphrase Kezilahabi. Uchunguzi wa athari ya mazingira asilia katika matumizi ya mbinu ya uchawi na mazingaombwe katika riwaya teule ulifanywa kwa kutumia nadharia ya Uhalisiamazingaombwe. Ihali, nadharia ya

Kiwewe cha Kuathiriwa ilitumiwa kulinganisha matumizi ya mbinu ya uchawi na mazingaombwe kati ya watunzi Shaaban Robert na Euphrase Kezilahabi.

Imebainika kuwa watunzi wote wawili wametumia kwa kiwango kikubwa matukio ya ajabuajabu katika riwaya zao teule kwa kuathiriwa na mazingira yao asilia na hivyo kufanikiwa kufikisha ujumbe waliokusudia kwa jamii husika. Zaidi ya kuathiriwa na mazingira asilia Shaaban Robert ameathiriwa na masimulizi ya Alfu Lela Ulela. Kezilahabi kwa upande wake ameathiriwa pia na Biblia pamoja na lugha ya Kilatini aliyojifunza katika seminari ya Kikatoliki.

Imebainika kuwa kuna viwango mbalimbali vya kufanana na kutofautiana kati ya waandishi hao katika kutumia kwao matukio ya ajabuajabu katika riwaya zao. Kwa mfano, tukio la manyani kupanda na kuendesha farasi katika riwaya ya *Adili na Nduguze*; linafafana kwa namna fulani na tukio la simba na pundamilia kumbeba Msimuliaji na mke wake kwa mashindano kuelekea juu ya mlima katika riwaya ya *Mzingile*. Matukio mengi ya ajabu katika riwaya za Shaaban Robert kwa kiwango kikubwa yameelezwa kama visa, na kwa kutumia nduni za fasihi simulizi. Sababu za kutokea kwake zimeelezwa wazi na watendaji, watendewa na watendwa wote wanaonekana kwa macho na mara nyingine wamehusishwa hata na washuhudiaji au watazamaji. Kinyume chake katika riwaya za Kezilahabi matukio mengi ya ajabuajabu yameelezwa kwa muhtasari na kwa mfululizo wa taswira au jazanda. Watendaji wengi wa matukio haowaonekani ingawa matokeo ya matendo yao ni bayana.

Tofauti nyingine katika matumizi ya mbinu ya uchawi na mazingaombwe kati ya Shaaban Robert na Euphrase Kezilahabi ni kuwa Shaaban Robert ametumia matukio ya uchawi na mazingaombwe kwa mtazamo chanya zaidi wakati Kezilahabi ametumia matukio hayo kwa mtazamo hasi zaidi. Hii ina maana kuwa matumizi ya uchawi na mazingaombwe katika riwaya za Shaaban Robert yamekusudiwa kama namna ya kujilinda, kuleta wokovu na kuadhibu waovu, wakati katika riwaya za Kezilahabi sehemu kubwa ya matumizi ya matukio ya uchawi na mazingaombwe ni kudhuru bila kuchagua wema na waovu. Pia hali iko hivyo hivyo katika mazingira asilia ya watunzi hao. Katika mazingira asilia ya Shaaban Robert wanaohusika na matukio ya ajabuajabu yanayohusiana na majini wanaonekana watu wa maana na wenye heshima katika jamii hiyo na jamii inawaita wataalamu. Kwa upande wa Kezilahabi wanaohusika na matukio ya ajabuajabu kwa sababu kwa kiasi kikubwa kazi yao ni kudhuru wanaitwa wachawi na hawatazamwi vizuri katika jamii hiyo.

Tofauti hizo zinafanya dhamira katika riwaya za Shaaban Robert kufasirika kwa urahisi na kile akizungumziacho kuonekana moja kwa moja katika mazingira halisi. Kinyume chake kumekuwa na utata mkubwa katika kufasiri kile anachokilenga au anachokimaanisha Kezilahabi kwa sababu ya kutumia kwake mfululizo wa taswira na jazanda.

Zaidi ya yote, wote Shaaban Robert na Kezilahabi wametumia matukio ya ajabuajabu kuiasa jamii juu ya madhara na faida ya matumizi ya maneno yetu. Maneno yanaumba na yanaua. Hivyo, maneno yakitumiwa katika kuwatia watu moyo, kuwahamasisha, kuwafariji na kuwaambia kuwa wanaweza, wanaopokea maneno hayo wanaweza kubadilika na kuwa watu bora, wema, wenye uwezo na

ambao wanaweza kuwa na mchango mkubwa sana kwa maendeleo ya jamii husika. Mwisho, wote Shaaban Robert na Kezilahabi wametumia matukio ya ajabuajabu kueleza kuwa uchawi na mazingaombwe ikitumiwa kwa mtazamo chanya inaweza ikaiitea jamii husika maendeleo makubwa ikiwa ni pamoja na kurahisisha mawasiliano, kupunguza gharama za usafiri pamoja na kuokoa muda. Sura inayofuata imechunguza matumizi ya uvunjivu wa kaida katika riwaya teule za Shaaban Robert na za Euphrase Kezilahabi.

SURA YA TANO

ATHARI YA MAZINGIRA ASILIA YA WATUNZI KATIKA UVUNJIVU WA KAIDA ZA UHALISIA KATIKA RIWAYA TEULE ZA SHAABAN ROBERT NA ZA EUPHRASE KEZILAHABI

5.0 Utangulizi

Sura hii imechunguza athari ya mazingira asilia ya watunzi katika matumizi ya uvunjivu wa kaida za uhalisia katika riwaya teule za Shaaban Robert na za Euphrase Kezilahabi. Lengo lilikuwa kuthibitisha kama uvunjivu wa kaida uliomo katika riwaya teule umetokana na athari ya mazingira asilia ya watunzi wa riwaya hizo au la. Hili kufaulisha lengo hilo, uvunjivu wa kaida uliomo katika riwaya teule umebainishwa na kuchunguzwa uwepo wake katika mazingira asilia ya watunzi hao. Zaidi ya yote matumizi ya uvunjivu wa kaida katika riwaya teule umelinganishwa kati ya Shaaban Robert na Euphrase Kezilahabi. Katika kutekeleza lengo hilo maana ya uvunjivu wa kaida imeelezwa na aina zake zimebainishwa.

Aina za uvunjivu wa kaida iliyochunguzwa na kuchanganuliwa kutoka katika riwaya teule ni: uvunjivu wa kaida za mahali au mazingira, za mbali na karibu, kaida za kimawasiliano kati ya binadamu na viumbe wengine, uvunjivu wa kaida kati ya uhai na kifo, uvunjivu wa kaida kati ya ndoto na uhalisia pamoja na uvunjivu wa kaida za kuhesabu wakati.

Sura hii imegawanyika katika sehemu mbili. Sehemu ya kwanza imeelezea maana ya uvunjivu wa kaida. Sehemu ya pili imebainisha matumizi ya uvunjivu wa kaida katika riwaya teule na kuchanganua kwa kulinganisha matumizi ya uvunjivu wa kaida kati ya Shaaban Robert na Euphrase Kezilahabi katika riwaya teule.

5.1 Uvunjivu wa kaida

Uvunjivu wa kaida ni kitendo cha kufuta au kuondoa vikwazo au vizuizi vyote vinavyoweza kufanya jambo lililokusudiwa kufanyika kutofanyika (Vutagwa, 2013). Kuna vizuizi vya umbali kwa mfano kati ya dunia na mbinguni. Kuna vizuizi vya mahali au mazingira, kwa mfano si rahisi kuingia ndani ya nyumba milango ikifungwa bila ya kutumia funguo. Kuna vizuizi vya kimawasiliano kati ya binadamu na viumbe wengine, kwa mfano haiwezekani kuelewana kati ya binadamu na wanyama kwa kutumia lugha ya kutamkwa. Pia kuwasiliana na viumbe wengine wa kufikirika kama malaika, mashetani, majini na mazimwi si rahisi. Pia si rahisi kufa na kuishi kwa wakati huo huo au kuwa macho na kuwa usingizini kwa wakati mmoja (Masamba na Wenzake, 1999: 1; Matinde, 2012; J.S.Mdee, Njogu, Shafi. A, 2011; Biblia Takatifu: Zaburi, 88: 10; 115: 17, Mhubiri, 9: 5, 10).

Uvunjivu wa kaida pia hujitokeza katika ndoto na uhalisia na katika kuhesabu wakati. Katika ndoto matukio mengi yanatokea kwa wakati mmoja na kwa muda mfupi sana. Mtu anaweza kulima, kupanda mahindi, mahindi kuota, kupaliliwa, kukomaa na kuvunwa katika ndoto ya dakika tatu tu. Katika ndoto mhusika anakuwa na nafsi mbili: nafsi tulivu na nafsi inayotembea kimiujiza ndotoni

(Freud, 1965; Farady, 1972: 38). Kupanda mazao ya aina yoyote na kuota, kukua, kukomaa na kuvunwa kwa muda wa dakika tatu na pia mtu kuwa na nafsi mbili ni kinyume cha uhalisia. Mtunzi wa kazi ya fasihi anapoeleza matukio kwa njia ya ndoto kwa namna ya matukio ambayo katika uhalisia yangehitaji muda mrefu kukamili na kwa kutumia wahusika wenye nafsi mbili inasemwa kuwa ni uvunjivu wa kaida. Kwa upande mwingine uvunjivu wa kaida hujitokeza katika wakati tuamavu na uduara wa wakati ambapo matukio yanaweza kutokea kwa wakati mmoja na kujirudia tena. Hapa mhusika anaweza kutenda jambo kwa miaka mingi zaidi ya miaka ya kawaida ya kuishi kwa binadamu. Pia mwandishi ana uhuru mkubwa wa kuamua kisa chake kianzie wapo na anaweza kuhitimisha masimulizi hayo popote pale (Onoda, 2017).

Katika uvunjivu wa kaida, mipaka kati ya jamii na jamii, mbali na karibu, wanadamu na viumbe wengine, uhai na kifo na hata utoto na utu uzima huvunjwa. Katika mitindo mingine ya uandishi kama vile uhalisia ni vigumu kwa mhusika kuvunja mpaka kwa mfano kati ya uhai na kifo. Yaani haiwezekani wafu wakaonekana kurudi na kufanya kama walio hai au mtu kuishi kati ya ufu na uhai. Pia si rahisi kwa mtu kusafiri na kufika sehemu fulani kwa namna za ajabu bila kutumia mbinu halisia za usafiri unaofahamika au kuingia mahali pasipoingilika kwa namna ya kawaida au kubadili umbo lake na kuwa kiumbe kingine (Biblia Takatifu: Mhubiri 9:5, Danieli 3: 24-27; Masamba, 1999; Mpalanzi, 2016). Hata hivyo katika uvunjivu wa kaida hayo yote yanawezekana. Hii ndiyo maana Roh (1925) anasema kwamba tumegundua mtindo mpya unaopindua asili juu chini. Yaani kanuni au sheria za asili zinabadilishwa na

mambo yanaonekana kuwa kinyume cha uhalisia unaofahamika. Kwa mfano, mwanaumme kupata ujauzito, miti kucheka, milima kujongea na wafu kuishi.

Wamitila (2003) anasisitiza mawazo hayo ya Roh kwa kusema kuwa wahusika katika riwaya zinazotumia mbinu ya uvunjivu wa kaida wana tabia ya kuvunja kanuni za hali ya kuwako au hali ya ki-ontolojia. Anaeleza hali ya ki-ontolojia kuwa ni utanzu wa metafizikia unaojijhusisha na masuala kama hali ya vitu, kuwako kwake, maana zake n.k. Tunaposema hali ya ki-ontolojia kwa hiyo hurejelea hali ya kuwako ya kitu fulani. Tunapoitumia dhana hii kuhusiana na fasihi hurejelea wahusika, matendo, mandhari n.k. Je, wahusika wana hali gani ya kuwako? Je, wahusika wanaopatikana katika kazi fulani wanaweza kutambulishwa na kiwango gani na kipi cha uhalisia (Wamitila, 2003: 57)?

5.2 Uvunjivu wa kaida katika riwaya teule

Shaaban Robert na Euphrase Kezilahabi wametumia uvunjivu wa kaida kwa namna zinazofanana na kwa namna tofauti katika riwaya zao teule.

5.2.1 Uvunjivu wa Kaida za Mahali au Mazingira na wa Mbali na Karibu

Uvunjivu wa kaida za mahali au mazingira ni aina au namna ya kufuta viziwi vya mahali na mazingira. Kwa mfano, si rahisi kutoka au kuingia ndani ya gereza lenye milango iliyofungwa imara na kuta zilizoimarishwa bila kupitia mlangoni. Lakini katika kuvunja kaida za mahali au mazingira mhusika anaweza kuingia ndani ya nyumba kupitia sakafu inayofunguka na kufunga yenyewe na kutokea ukutani kana kwamba hakuna kizuizi chochote (Mesaki, 1993).

Uvunjivu wa kaida kati ya mbali na karibu ni pale ambapo umbali kati ya sehemu mbili tofauti hauki kikwazo cha kushindikana kufanyika kwa jambo. Hii ina maana kuwa muda ambao mhusika anaweza kuchukua kufika umbali wa maili milioni moja ni sawa na ule atakaotumia kufika umbali wa maili sifuri. Kwa mfano, umbali kati ya dunia na mbinguni ni mrefu na haukadiriki. Hivyo, haiwezekani mtu kufunga safari ya kwenda mbinguni. Hata hivyo, katika uvunjivu wa kaida umbali huo hufutwa na mjumbe anaweza kwenda mbinguni na kuleta habari za huko kwa kutumia muda mfupi sana (Safari, 1993). Kwa hiyo mazingira yasiyoingilika kwa hali ya kawaida yanapoingilika bila kizuizi chochote na umbali usiofikika unapofikika kwa urahisi kabisa, hapo ndipo uvunjivu wa kaida za mahali au mazingira na mpaka kati ya mbali na karibu inasemwa kuwa imevunjwa.

Mwandishi wa riwaya ya *Adili na nduguze* anavunja mpaka pale Huria anapobadilika kuwa ndege wa kutisha na kumwopoa Adili baharini na kuruka naye juu zaidi angani. Kwa sababu ya ndege kuruka juu zaidi Adili anapoteza fahamu. Adili anapopata fahamu anajikuta katika himaya ya majini na yule ndege anajibadilisha na kuwa msichana mzuri (*Adili na Nduguze*, uk. 34). Hapa mpaka kati ya mbali na karibu unavunjwa. Haijulikani kuwa nchi ya majini iko umbali gani na pale baharini Adili alipotumbukizwa. Pia uwezo wa Huria kujua kuwa Adili ametumbukizwa baharini na kujibadilisha ndege mkubwa na kwenda kumwoko wakati Huria mwenyewe alikuwa mbali na eneo la tukio haelezwi. Hata hivyo, katika uandishi unaotumia uvunjivu wa kaida kati ya mbali na karibu ni jambo la kawaida. Hii inakubaliana na mhimili mojawapo wa nadharia ya uhalisiamazingaombwe unaodai kuwa kazi zinazoegemea mkondo wa uchawi na

mazingaombwe huvunja Kaida zote za uasilia na za uhalisia. Hivyo, kuondoa mpaka kati ya jamii na jamii, nchi na nchi au mbali na karibu. Kwa hiyo, binadamu anaweza kuona na kufahamu kinachotendeka mbali, kufika mbali kwa muda sifuri na kuingia popote bila kizuizi. Kwa hiyo, tukio hili la kumwokoza Adili baharini linadhihirisha kuwa katika uvunjivu wa kaida mipaka ya mbali na karibu huvunjwa. Hivyo, hakuna tofauti kati ya mbali na karibu.

Uvunjivu mwingine wa kaida ya mahali au mazingira ni pale Jini Huria binti Kisasi alipokwenda kumwadhibu Adili kwa sababu ya kusahau kuwaadhibu manyani. Yaani, Hasidi na Mwivu ndugu zake. Mwandishi anasema:

Hakuwahi kutafuta minyororo siku ile, na usiku alisahau kuyapiga akalala. Saa saba usiku Huria alitokea na hasira imemjaa tele. Alisema kuwa alikuwa jini...alimpiga Adili kiboko mpaka akazimia...Siku moja ikipita bila kuyapiga kiboko hiki kitaishia mwilini mwako. Macheche ya moto yalitoka kinywani mwake alipokuwa akiamuru hili, na mara neno la mwisho lilipotamkwa akatoweka (*Adili Na Nduguze*, uk. 41).

Kitendo cha Huria kuingia na kutoweka ghafla kwa Adili bila kuingilia na kutokea mlangoni si cha kawaida. Pia Huria kufahamu kuwa Adili hakuyachapa manyani wakati hawakai pamoja ni suali lisiloweza kuelezeka kiuhalisia. Hii ina maana kama ilivyoelezwa hapo juu kuwa, katika uvunjivu wa kaida za mahali au mazingira mhusika anaweza kuingia mahali popote bila kizuizi, anaweza kuona na kufahamu matukio yanayotokea sehemu fulani hata bila kuwepo mahali hapo. Mambo hayo hayawezekani katika uhalisia (Mesaki 1993).

Ili kuthibitisha zaidi suala la uvunjivu wa mipaka ya mahali na ya mbali na karibu, Shaaban Robert anamtumia tena jini Huria. Huria anarudi tena kwa Adili ili kumwadhibu kwa sababu hakuwachapa manyani. Hakuwachapa kwa sababu

alikuwa na barua ya mfalme Rai iliyoandikwa kwa Huria na kwa Kisasi mfalme wa majini ili kuwaomba wawasamehe manyani. Mwandishi anasema:

Adili alipolala mtingisho mkubwa ulitokea chumbani mwake sakafu ikapasuka. Kuzinduka uso wake ulikutana na uso wa Huria (*Adili na Nduguze*, uk. 47).

Huria anaingia kwa Adili kupitia sakafu inayopasuka kutokana na ujio wake. Kitendo cha Huria kuingia kwa Adili kutokea ardhini kupitia sakafu inayopasuka pia kufahamu kuwa Adili hakuwachapa manyani na hawakai pamoja nalo si suala la kawaida. Mpalanzi (2018) anasema:

Wachawi wanatumia mbinu nyingi za kifantasia. Uchawi ni amali inayoweza kumfanya mtu kusafiri umbali mrefu, kuingia pasipoingilika kwa hali ya kawaida kwa kutumia pembe na mgwisho mweusi (msisitizo ni wetu).

Hii inadhihirisha kuwa katika uandishi unaotumia uvunjivu wa kaida, viziuzi vyote vya mahali na vinavyosababishwa na umbali kati ya sehemu moja na nyingine vinavunjwa na mambo yasiyowezekana katika uhalisia yanafanyika kwa urahisi na kwa wepesi wa kushangaza. Katika uvunjivu wa kaida ya mahali na ya mbali na karibu mhusika anaweza kusafiri ndani ya ardhi au kwenda hata mbinguni na kuingia popote hata bila njia rasmi anayopitia kujulikana. Shaaban Robert anathibitisha hili katika riwaya ya *Kusadikika* kwa kumtumia Ridhaa, mjumbe wa mbinguni, kuwa:

Mjumbe huyu alisafiri kuelekea mbinguni ili kuyapeleleza mambo ya huko yalivyo kama alivyoamuriwa...kwa msaada wa malaika aliyesimamia mambo ya wanadamu aliweza kufika mpaka halmashauri kubwa za mbinguni (*Kusadikika*, uk. 34).

Mpaka sasa katika uhalisia hakuna ambaye amefanikiwa kufika mbinguni na kurudi na taarifa za huko (Biblia Takatifu: Mithali, 30: 4). Hata hivyo katika uvunjivu wa mpaka kati ya mbali na karibu safari kama hizo zinawezekana kwa sababu mhusika anaweza kusafiri kimawazo na kwenda popote bila kizuizi chochote.

Shaaban Robert inawezekana ametumia uvunjivu wa kaida kati ya mbali na karibu na ya mahali kutabiri juu ya maendeleo ya sayansi na teknolojia inayoambatana na utandawazi. Hii ni kwa sababu katika utandawazi dunia inakunjwa na kuwa ndogo kama kijiji (kiganja cha mkono) ambapo mtu anaweza kuona yote na kufika popote katika kijiji hicho kwa muda mfupi sana (Kevago, 2017; Croucher , 2004: 10). Hapa chini kumenukuliwa hotuba ya Rais wa awamu ya tatu wa Tanzania, Mheshimiwa Benjamin Mkapa aliyoitoa Desemba 5, 2003 iliyonukuliwa na Rose Haji yenye anuani: “TANZANIA: Utandawazi ni jambo la Uhakika Halikwepeki.” Mkapa anasema:

...utandawazi si jambo jipya, kilicho kipya ni kasi na msamiati na istilahi yake. “Maana kiini cha utandawazi ni mahusiano ya karibu ya watu wa asili na maeneo tofauti-yawe mahusiano ya kijamii, kitamaduni, kibiashara, kiteknolojia na kadhalika.” Anasema, “Wangoni walipotoka Afrika ya Kusini kuja Tanzania ilikuwa aina ya utandawazi wa enzi hizo. Tofauti ni kuwa pale ambapo walitumia miaka kufika hapa, leo unaweza kusafiri umbali huo kwa ndege kwa saa tatu tu. Wamisionari wa dini zote walipotuletea imani mpya, ulikuwa utandawazi. Tofauti mojawapo ni kuwa leo wanaweza kuhubiri kwa njia ya satelaiti na televisheni dunia nzima kwa wakati mmoja, na si lazima waje mpaka Afrika.” ...zamani watu walifanya biashara baina ya bara moja na jingine, wikalipana kwa kubadilishana bidhaa, na kutumia muda mwingi. Leo biashara hiyo inaendelea, lakini bidhaa zimekuwa nyingi zaidi, na zinabadilishwa kwa kasi kubwa. Sasa hivi kuna teknolojia ya biashara kwa njia ya mtandao wa intaneti. Fedha nayo peke yake ni biashara ambapo mamilioni ya fedha yaweza kutoka pembe moja ya dunia kwenda pembe nyingine kwa sekunde chache tu. Na kinachochochea kasi hiyo ni maingiliano ya teknolojia ya kisasa. Kama utandawazi ungekuwa gari, basi teknolojia ndiyo mafuta yake.”

Hii ndiyo maana Shaaban Robert anasema kuwa ‘Mrefu’ kwa sababu ya wepesi wake anaweza kuzunguka dunia nzima kwa sekunde moja (*Adili na Nduguze*, uk. 29). Pia Ridhaa kwa msaada wa malaika amefanikiwa kufika mbinguni na kuleta habari za huko nchini Kusadikika (*Kusadikika*, uk. 34).

Hapa mwandishi anavunja mpaka kati ya mbali na karibu yaani kati ya dunia na mbingu. Ridhaa anasafiri mpaka mbinguni kwa msaada wa malaika na kufanikiwa kuleta habari za huko licha ya umbali kati ya mbingu na dunia kutokukadirika. Flores (1988) anasema:

Uhalisiamazingaombwe unajumuisha uchanganyaji wa uhalisia na fantasia. Unakusudia kuunganisha na kuvunja mpaka kati ya kweli na uongo, sasa na zamani (usasa na ukale), na mbali na karibu. Kwa maana hiyo lengo la uhalisiamazingaombwe katika fasihi ni msisitizo wa umoja kati ya mazingaombwe na uhalisia. Hii inadhihirisha kuwa katika uvunjivu wa kaida mipaka yote huvunjwa na kuta zote za umbali na za mahali au za kimazingira huondolewa kabisa.

Uvunjivu wa mpaka wa umbali kati ya mbingu na dunia umetumika sana katika Biblia Takatifu. Kwa mfano, Henoko kwenda pamoja na Mungu na kutoweka, maana Mungu alimtwaa. Eliya kupanda mbinguni kwa upepo wa kisulisuli. Na Shadraka, Meshaki na Abednego kuokolewa na Yesu (mwana wa miungu) kwa muda sifuri katika tanuru la moto (Mwanzo, 5: 24; 2Wafalme 2: 11; Danieli, 3: 23-27).

Shaaban Robert kwa kumtumia Ridhaa katika riwaya ya *Kusadikika* amevunja mpaka kati ya mbali na karibu yaani mbingu na dunia ili kuzungumzia nafasi ya dini katika kujenga namna ya maisha yatakiwayo. Shaaban Robert kwa kusoma Kurani na Biblia anatumia maandiko matakatifu yanayosema kuwa kuna maisha

ya furaha mbinguni baada ya kufa. Maisha hayo ya raha ni kwa ajili ya watakaotenda mema hapa duniani na kwa watakaotenda mabaya yatakuwa ya huzuni (Biblia Takatifu, Luka 16).

Shaaban Robert anasema kuwa jukumu la kila mtu ni kutenda mema bila kusubiri kusifiwa na wanadamu hapa duniani. Kuwa baada ya maisha ya hapa duniani zawadi au adhabu inawangojea watu mbinguni kulingana na matendo yao. Hivyo, hata kama matendo mema yaliyotendwa hayakushangiliwa hapa duniani, inawezekana kwa sababu ya ujinga, wivu au dharau, watendaji wasikate tamaa. Hii ni kwa sababu watendaji hao hawatasahaulika mbinguni na mbingu itawafanyia makumbusho ya milele (*Kusadikika*, uk. 35).

Mwandishi anaendelea kusesitiza kuwa furaha ya kweli na ya milele iko mbinguni. Neno mbinguni hutumika kumaanisha eneo ambalo liko juu zaidi nje ya ulimwengu halisi wa kimwili, makao ya Mungu na malaika ambao ni viumbe wa kiroho walioumbwa na Mungu na mahali ambapo baadaye watakatifu wataishi (Biblia Takatifu: Mwanzo, 28:12; Zaburi, 11:4; Mathayo, 6:9; 1Wafalme, 8:27; Yohana, 6:38; Mathayo, 24:36). Shaaban Robert anasema kuwa ili kupata furaha ya mbinguni kila mtu anatakiwa kujiandaa vizuri na kwa bidii zote hapa duniani. Watakaopata upendeleo mkubwa mbinguni ni pamoja na mataifa yatendayo haki, koo zenye wema, na watu waadilifu katika maisha yao. Watu wa namna hao watastawi katika ulimwengu. Wakikishika kitu kidogo huwa kikubwa kwa bidii zao, haba huwa kingi kwa utunzaji wao mwema, kibaya huwa kizuri kwa kusahihisha kwao, na kwa saburi yao matumaini yao hutimizwa kama walivyotazamia ama zaidi (*Kusadikika*, uk. 38).

Shaaban Robert kwa kutumia uvunjivu wa kaida kwa kuvunja mpaka wa umbali kati ya mbingu na dunia ameelezea imani ya kidini yenye matendo. Kuwa ili kupata maisha mema hapa duniani na baadaye mbinguni, si kukaa na kusubiri kwa imani, bali ni kutenda kazi kwa juhudi na maarifa na kwa uadilifu wote.

Maelezo hayo ya Shaaban Robert ni kinyume kabisa na mawazo na mafundisho potofu yaliyojengwa miongoni mwa watu wengi na madhehebu ya kidini juu ya kuombewa ili kupata utajiri kimiujiza. Utajiri haupatikani kwa miujiza bali kwa kufanya kazi kwa bidii. Biblia inasema: Mawazo ya wenye bidii huuelekea utajiri tu; Bali kila mwenye pupa huuelekea uhitaji. Mwenye bidii katika kazi zake? Huyu atasimama mbele za wafalme; Hatasimama mbele za watu wasio na cheo (Mithali, 21: 5, 22: 29). Kwa hiyo kuombewa na wachungaji wa madhehebu ya kidini halafu mtu abweteke kwa kukaa kivivu bila kufanya kazi na kutegemea au kupata utajiri kimazingaombwe ni ujinga na ni kinyume na maagizo ya maandiko matakatifu (Mithali, 13: 4, 19: 15, 20: 4, 24:30).

Kezilahabi kwa upande wake anatumia uvunjivu wa mipaka kati ya mbali na karibu katika riwaya ya *Nagona* pale wasaka paa walipotakiwa kuleta kiko cha mfalme alichokisahau Sibara umbali wa mwendo wa miaka saba. Kiko hicho kilitakiwa kipatikane siku hiyo jioni. Kisipopatikana wasaka paa wote wanakatwa vichwa. Mfuasi anavunja kizuizi hicho cha umbali kwa kukunjua mguu wake na mguu huo kurudi na kiko hicho kwa muda mfupi sana. Mwandishi anasema:

Mwaka jana nilienda nchi ya Sibara...Ni mwendo wa miaka saba toka hapa. Huko nilisahau kiko changu. Nakitaka kiko hicho leo jioni...Mfuasi aliuachia mguu kuelekea Kaskazini. Mguu wake mrefu ulianza kukunjuka kwa kasi. Baada ya muda mfupi alianza kuukunja kwa kasi ile ile. Kati ya vidole vya mguu huo palikuwa pamepachikwa kiko (*Nagona*, uk. 33).

Umbali wa mwendo wa miaka saba unavunjwa kwa Mfuasi kukunjua mguu wake na mguu huo kurudi na kiko cha mfalme. Kitendo cha mguu kukunjuka kwa urefu huo ni kinyume cha kanuni za kimaumbile na hata utambuzi wa mguu kuweza kupachika kiko hauelezeki kiuhalisia. Hata hivyo kiko cha mfalme kinaletwa. Mfalme anashangaa kwa sababu hata yeye naye alifahamu kuwa haiwezekani kiko hicho kuletwa siku hiyo hiyo kulingana na umbali kati ya nchi yake na nchi ya Sibara. Ili kukabiliana na matukio kama hayo inahitajika nadharia inayovunja kaida kati ya mbali na karibu. Nadharia faafu ni nadharia ya Uhalisiamazingaombwe kwa kutumia mhimili wake ambao tumekwisha kuutaja hapo awali. Mhimili huo unasisitiza kuwa kazi zinazoegemea mkondo wa uchawi na mazingaombwe huvunja Kaida zote za uasilia na za uhalisia. Hivyo, kuondoa mpaka kati ya jamii na jamii, nchi na nchi au mbali na karibu. Kwa hiyo, binadamu anaweza kuona na kufahamu kinachotendeka mbali, kufika mbali kwa muda sifuri na kuingia popote bila kizuizi.

Kezilahabi ametumia uvunjivu huu wa mpaka kati ya mbali na karibu kutaka kueleza kuwa hakuna kinachoshindikana kama mwanadamu atatumia akili yake katika kufikiri. Katika fikra makini hutokea uvumbuzi na utatuzi wa vikwazo vingi. Anasema kuwa huu ndio mguu uendao mbali kwenye fikra na uzamapo haurudi bila wazo (*Nagona*, uk. 28).

Shaaban Robert anaelezea uvunjivu mwingine wa kaida za mahali au mazingira pale msichana mzuri, jini, yaani Huria binti Kisasi, anapoelekeza kidole chake cha shahada chini na ardhi kupasuka na msichana kuingia ndani yake. Mwandishi anasema:

Baada ya hayo msichana alielekeza kidole chake cha shahada chini. Mara moja ardhi ilipasuka akaingia ndani yake. Alipokwisha jitia ndani ardhi ilijifunga sawia (*Adili na Nduguze*, uk. 18).

Hii ina maana kuwa katika uvunjivu wa kaida za mahali au mazingira mhusika anaweza kuingia mahali popote bila kizuizi chochote. Hapa Huria anavunja kaida mbili za mahali: Ni muujiza ardhi kupasuka kwa mtu kuelekeza tu kidole chini bila kuguswa au kutumia kifaa chochote kuchimbia ardhi hiyo. Pia mtu akifukiwa ardhini si rahisi kuendelea kuishi. Mambo hayo ni miujiza kutokea katika uhalisia (Mesaki, 1993). Hii ndiyo maana Adili alipoona matendo hayo ya Huria alihitimisha kuwa hakuwa binadamu bali jini (*Adili na Nduguze*, uk. 18).

Hii inadhihirisha kuwa katika uandishi unaotumia uvunjivu wa kaida ya mahali au mazingira, vizuizi vyote vya mahali vinavunjwa na mambo yasiyowezekana katika uhalisia yanafanyika kwa urahisi na kwa wepesi wa kushangaza. Katika uvunjivu wa kaida ya mahali mhusika anaweza kusafiri ndani ya ardhi na kuingia popote hata bila njia rasmi anayopitia kujulikana. Hii inazidi kudhihirisha kuwa Shaaban Robert ametumia uvunjivu wa kaida za uhasilia katika riwaya ya *Adili na Nduguze*. Uvunjivu huu wa kaida ni sawa kwa namna fulani na tukio la watu wawili kutoka ardhini katika riwaya ya *Nagona* ya Euphrase Kezilahabi.

Kezilahabi kwa kueleza tukio la watu wawili kutoka vumbini, yaani ndani ya ardhi, anasema:

Mara, mahali fulani karibu nao, waliona kitu fulani kikijiviringisha ndani ya vumbi halafu mtu aliibuka akiwa ameenea vumbi jeupe....yule mtu kutoka vumbini alisema, ‘Mimi pia ni mcheza ngoma. Nilikuwa katika mazoezi ya mazingaombwe nitakayoyaonyesha siku hiyo ya ngoma kuu....Alipokuwa akisema maneno hayo aliibuka mtu mwingine kutoka vumbini. Alitokea pembeni kidogo na pale walipokuwa (*Nagona*, uk. 39).

Mtu wa kwanza kutoka vumbini anapomkanusha mtu wa pili kutoka vumbini kuwa haiwezekani kutenganisha roho na mwili, mtu wa pili anasema kuwa naye alikuwa anafikiri hivyo lakini baada ya kupoteza roho yake alipoambiwa kuisafisha katika mto wa uzima wa milele amegundua kuwa roho na mwili vinaweza kutenganishwa (*Nagona*, uk. 40). Tukio la watu kuibuka kutoka vumbini na pia kusafisha roho na roho kupotea na bado mtu akaishi ni uvunjivu wa kaida za uhalisia.

Katika maisha halisi si jambo la kawaida na haiyumkiniki mtu kukaa ndani ya ardhi akiwa amefunikwa na udongo akaishi. Vile vile si rahisi mtu akatoa roho yake, yaani uhai wake akautenga na kiwiliwili na kwenda nayo mtoni kuisafishana kuendelea kuishi. Biblia Takatifu inathibitisha kwa kutumia kisa cha Kora, Dathani na wenzao kufa kwa kufukiwa na ardhi walipoongoza uasi dhidi ya Musa (Hesabu, 16: 27-33) na mfalme Herode kutokwa na roho, yaani alikufa kwa sababu ya kusifiwa kuwa ni Mungu. Biblia inasema:

Basi siku moja...Herode...akatoa hotuba...Watu wakapiga kelele, wakisema, ni sauti ya Mungu, si sauti ya mwanadamu. Mara malaika wa Bwana akampiga, kwa sababu hakumpa Mungu utukufu; akaliwa na chango, akatokwa na roho (Matendo ya Mitume 12: 21-23).

Fungu hilo linathibitisha kuwa roho inapomtoka mtu ina maana mtu huyo anatokwa na uhai, yaani anakufa. Kitabu cha Mwanzo kinapigilia msumari kabisa pale Raheli mke wa Yakobo alipokuwa katika kufa wakati akijifungua, kwa kusema: Ikawa hapo katika kutoa roho yake, maana alikufa, akamwita jina lake Benoni,..(Biblia Takatifu: Mwanzo, 35: 18). Hivyo, si rahisi katika uhalisia mwili na roho kutenganishwa na mtu akaendelea kuishi. Kinyume chake katika uhalisiamazingaombwe ni hali ya kawaida. Hii inathibitishwa na mhimili wa uhalisiamazingaombwe unasisitiza kuwa katika uchawi na mazingaombwe kuna mwingiliano mkubwa kati ya uhalisi na ndoto, uhai na kifo, sasa na zamani na uhalisi na utohalisi. Inawezekana mtu anapoota ndipo yupo katika uhalisi na wakati yu uhalisini ndipo yu ndotoni au anapokufa ndipo yu hai na anapokuwa hai ndipo huwa ufuni. Hii ni kwa sababu katika uhalisiamazingaombwe hakuna mpaka kati ya uhalisi na utohalisi. Hii inadhihirisha kuwa uhalisiamazingaombwe haukubaliani na uhusiano wa kadhia zinazotendeka katika maisha ya mtu kiutengano. Hali kama za uhalisi na ndoto, usasa na ukale, uhai na kifo, mbali na karibu, ugeni na uwenyeji na tamaduni zinaingiliana.

Kezilahabi hata hivyo ametumia roho hapa kwa maana tofauti na roho ya uhai. Roho ambayo haiwezi kutenganishwa na mwili na mtu akaendelea kuishi ni pumzi ya uhai. Biblia inathibitisha kwa kusema: Bwana Mungu akamfanya mtu kwa mavumbi ya ardhi, akampulizia puani pumzi ya uhai; mtu akawa nafsi hai (Mwanzo, 2: 7). Biblia inasisitiza zaidi kwa kusema: Kila kitu cheye pumzi ya roho ya uhai puani mwake kikafa, kila kilichokuwako katika nchi kavu (Mwanzo, 7:22). Kezilahabi hapa anazungumzia akili badala pumzi ya uhai. Biblia pia inathibitisha kuwa akili, yaani uwezo wa kufikiri na kutoa maamuzi nayo huitwa

roho. Inasema: Bwana akasema, Roho yangu haitashindana na mwanadamu milele. ...Njia zote za mtu ni safi machoni pake mwenyewe; bali BWANA huzipima roho za watu (Mwanzo, 6:3; Mithali, 16: 2).

Kwa kutumia ushahidi wa mafungu hayo ya Biblia, inaweza kusemwa kuwa, Kezilahabi kwa kutumia uvunjivu wa kaida wa watu wawili kutoka mavumbini na kusafisha roho katika mto wa uzima wa milele alikusudia kusesitiza umuhimu wa kutumia akili zaidi katika kufikiri bila kudhohofishwa na matakwa, madhaifu au matendo ya mwili. Hii ni kwa sababu matendo ya mwili hupingana na akili siku zote na yeyote anayejishikamanisha na matendo ya mwili uwezo wake wa kufikiri unapungua kabisa. Hivyo, Kezilahabi anasisitiza kuwa ili kufikiri vizuri ni bora kujitenga na matendo ya mwili na kuambatana na matendo ya akili. Matendo ya mwili yameelezwa katika Biblia kuwa ni pamoja na uasherati, uchafu, ufisadi, ibada ya sanamu, uchawi, uadui, ugomvi, wivu, hasira, fitina, faraka, uzushi, husuda, ulevi, ulafi na mengine yanayofanana na hayo. Kinyume chake matendo ya roho (akili) ni upendo, furaha, amani, uvumilivu, utu wema, fadhili, uaminifu, upole, na kiasi (Wagalatia, 5: 19-23).

Tukio la uvunjivu wa kaida ya mahali ya jini, Huria binti Kisasi, aliyetumiwa na Shaaban Robert katika riwaya ya *Adili na Nduguze*, kuelekeza kidole chini na ardhi kupasuka na kujitia humo, ni sawa na kisa cha mtu wa bara aliyemwoa Mdigo katika mazingira asilia ya Shaaban Robert (taz, uk. 66). Katika kisa hicho mwanamke aliyemchukua mtu wa bara kichawi anaunyoosha mbuyu mkono na mbuyu unapasuka na wanaingia ndani kisha mbuyu unajifunga. Visa kama hivyo ni vingi katika mazingira asilia ya Shaaban Robert. Hivyo, inawezekana kabisa

kuwa Shaaban Robert ametumia kisa cha jini kunyoosha mkono chini na ardhi kupasuka kwa sababu ya uwepo wa matukio hayo katika mazingira yake asilia.

Tukio lingine la kuvunja mipaka ya mahali na ya mbali na karibu ni katika safari ya mjumbe wa ardhi, Amini, katika riwaya ya *Kusadikika*. Shaaban Robert anasema:

Amini alishuka katika ardhi kwa msaada uliopatikana kwa hila kwa mangera, ndege wakubwa kabisa walishao katika ardhi lakini walalao Kusadikika. Wakati wa kwenda chini Amini alijifunga bila ya kujulikana juu ya paja la mangera aliyekuwa amelala fofofu usiku. Kulipokucha ndege huyo aliamka akaruka mpaka chini (*Kusadikika*, uk. 40- 41).

Kitendo cha amini kusafiri kwa kumtumia ndege kwenda ardhini ni kitendo kisichowezekana katika uhalisia. Hii ni kwa sababu hata ndege mwenyewe kuruka na kuingia ardhini ni jambo lisilowezekana. Hata hivyo katika uvunjivu wa kaida hii ni hali ya kawaida kwa sababu katika uvunjivu wa kaida yale yanayoonekana kutowezekeka katika uhalisia ni ya kawaida na wala hadhira haitilii shaka hutokeaji wake (Flores, 1988).

Shaaban Robert ametumia sana viumbe ndege katika uandishi wake hasa kama njia ya usafiri unaoambatana na wokovu katika shida. Matumizi haya ya ndege wanaotumika kusafiria au kama njia ya wokovu katika shida na watu wanaobadilishwa wanyama mfano Ndugu zake Adili kugeuzwa manyani ni athari za vitabu vya *Alfu Lela Ulela* kwa Shaaban Robert. Katika *Alfu Lela Ulela* Kitabu cha Pili (uk. 8 &11) Sindbad anaokoka kwa kujifunga katika mguu wa Rok na wa tai na kuruka naye juu na kumwoko. Hii ni sawa na Amini katika riwaya ya *Kusadikika* kujifunga katika paja la Mangera ndege wakubwa walishao katika

ardhi, na Adili katika *Adili na Nduguze* kuokolewa na tai ndege mkubwa na wa kutisha.

Mwandishi alitumia ndege viumbe hapa kama kiwakilishi cha usafiri wa ndege Ulaya. Usafiri huo haukuwa dhahiri sana kwa nchi ya Tanganyika iliyokuwa inakaribia kujitawala lakini haikujiandaa kwa bandari wala viwanja vya ndege. Hivyo lengo lake lilikuwa kwamba maandalizi ya mambo mazuri yanayotarajiwa ni vyema kufanyika mbele kabla ya tukio lenyewe. Anasema:

Ukitaka biashara ya vitabu isitawi watu hawana budi kufunzwa kusoma kwanza. Kusoma kusipotangulia vitabu vizuri vitaonekana vibaya. Kabla ya kujenga msikiti watu lazima wafunzwe utukufu wa dini mbele. Bila ya hivyo msikiti mtakatifu utakuwa kama mkahawa mchafu tu. Kadhalika mfano, kama nchi haina bandari ya namna yoyote, haiwezi kutazamia kufikiwa na vyombo. Kila azimio katika maisha hutaka neno fulani kufanyizwa mbele ili kuyashawishi maendeleo yake (*Kusadikika*, uk. 43).

Uvunjivu mwingine wa mipaka kati ya mbali na karibu ni kule kutumbukia kwa Auni mjumbe wa Magharibi katika mkondo wa mto uliokuwa ukikimbia kwa nguvu na kwa kasi kama umeme. Kwa kasi ya maji ya mto huo Auni alitumia masaa kumi badala ya miaka kumi kama angekuwa anatembea kwa miguu kufika nchi ya Iktisadi. Mto huo uliitwa Maangamizi ya Matumizi, mto mmoja katika mito ya uharibifu mkubwa na yenye nguvu nyingi kabisa duniani (*Kusadikika*, uk. 31).

Katika maisha ya kawaida na kulingana na maumbile ya binadamu mtu kutumbukia katika mto wenye kasi kiasi hicho na kutoka salama ni muujiza wa pekee. Kwa sababu kasi ya mto huo ni kubwa kuliko mwendo wa kawaida wa ndege Ulaya. Hata hivyo katika uvunjivu wa kaida hali hiyo inawezekana. Hii

inashadidiwa na mhimili wa uhalisiamazingaombwe unaosema kuwa katika uhalisiamazingaombwe kaida za uasilia na za uhalisia huvunjwa, hivyo, binadamu anaweza kujibadilisha sura na kuwa kitu kingine, kuingia popote bila kizuizi, kuzungumza na viumbe wengine na kufa na kuishi kwa wakati mmoja.

Mwandishi ametumia uvunjivu huu wa mpaka kati ya mbali na karibu ili kuelezea uharibifu na maangamizi makubwa yaletwayo na matumizi mabaya ya rasilimali za nchi au za mtu binafsi. Anasema:

Watu watumiao mali zao kwa ubadhirifu husemwa kuwa wametumbukia katika maangamizi ya matumizi. Mwisho watu hao huvunjwavunjwa katika maanguko ya umaskini, yaani, njaa, kiu na uchi. Watu watumiao mali zao kwa uangalifu huyaepa maanguko ya umaskini...Hazina kubwa kufanywa kwa kukusanya senti moja moja kama safari ndefu ifanywavyo kwa mwendo wa hatua moja moja.... Ujinga wa matumizi yetu hututenga na hazina zetu, na uvivu wa kunyanyua hatua zetu hutucheleweshwa nyuma siku zote. Mtu yeyote asiyelitunza pato lake dogo hawezi kuwa tajiri, na yeyote asiyejali kwenda hatua moja mbele huwa mzigo mzito kwa wasafiri wenziwe (*Kusadikika*, uk. 32).

Shaaban Robert anaonekana kukerwa sana na tabia ya matumizi mabaya ya mali na uvivu uliokithiri katika jamii hasa katika jamii yake ya watu wa pwani. Anafananisha matumizi mabaya ya mali pamoja na uvivu na mto wa uharibifu na maangamizi ambao mtu akitumbukia huvunjwavunjwa na kuangamia katika maanguko ya umaskini, yaani, njaa, kiu na uchi. Anataja baadhi ya matumizi ya kijinga yanayomaliza mali ambayo ni pamoja na: Ngoma na tafrija za kufukarisha, kuo na kuoachana kila siku, kuo wake wengi, kuzaa watoto wengi na kutowasomesha ipasavyo. Katika jamii ya Shaaban Robert kuna sherehe ya kutoa kafara kwa majini zinazofanyika Chumbagama na Kijibweni kila mwaka

(taz, uk. 74). Katika sherehe hizo karibu nusu ya chakula chote kilichovunwa kwa mwaka husika hutumika katika sherehe hizo za siku moja.

Kwa mantiki ya Shaaban Robert jamii inaaswa kuwa, kila mmoja afanye kazi kwa bidii, watu wependane, watumie mali zao kwa hekima, na asiwepo mwenye kupenda kuwabughudhi wenzake kwa matatizo yake kama anayo njia ya kuyapunguza au kuyatatua (*Kusadikika*, uk. 32).

Kezilahabi kwa namna sawa na Shaaban Robert anavunja mpaka kati ya mbali na karibu katika riwaya ya *Mzingile*. Uvunjivu huu unajitokeza Msimuliaji akiwa katika safari ya kwenda kwa Mfadhili. Msimuliaji anachukuliwa na mkondo wa maji na kujikuta amelala karibu na nyumba ya Mfadhili. Mwandishi anasema:

Nilijihisi nateleza. Ghafla miguu yangu iliinuliwa na mkondo mkali wa maji nikaviringishwa kama pia. Muda wa kupiga kelele sikuupata. Nilijikuta nimelala karibu na nyumba ndogo iliyokuwa na mwanga ndani. ... “Je yawezekana nyumba ya Mfadhili ikawa hii.” ...Sikuwa mbali na mlango. Nilipojitokeza tu mlango, mwenye nyumba alisikia nyayo zangu (*Mzingile*, uk. 56).

Katika maisha ya kawaida mtu kuchukuliwa na mkondo mkali wa maji na badala ya mkondo mkali huo kumgharikisha unampeleka pale alipotarajia bila kuokolewa au kupata msaada wowote ni muujiza na ni jambo la kushangaza. Katika uvunjivu wa kaida safari kama hiyo ni ya kawaida na inawezekana hata bila kutegemea vyombo vya usafiri vinavyojulikana na vilivyozoeleka. Vikwazo vyote huvunjwa na mahali pasipojulikana au pasipoingilika ufikika kwa urahisi wa ajabu. Msimuliaji anapotoka kwa Mfadhili anateleza tena na kuanguka majini

kama ilivyokuwa katika safari yake ya kwenda kwa Mfadhili. Mwandishi anasema:

Upepo baridi uliniashiria nitembee kwa uangalifu. Lakini ghafla niliteleza nikaanguka majini. Nilijaribu kuogelea kuja juu lakini nguvu sikuwa nazo. Nilipopata fahamu nilijiona bado nimo gizani. Nilihisi naguswa na kitu fulani. Nilistuka. “Naona sasa uko tayari.” We nani?” Nilisikia mcheko ulioniondolea wasiwasi (*Mzingile*, kur. 59-60).

Kitendo cha Msimuliaji kusafiri ndani ya maji aliyotumbukia huku hajitambui akiwa amepoteza fahamu na kutoka salama bila msaada wowote ni uvunjivu wa kaida ya mahali na ya mbali na karibu. Katika kipengele hiki Kezilahabi anaonekana kumwiga Shaaban Robert kwa mwigo sisisi katika kuvunja mpaka kati ya mbali na karibu. Hii ni kwa sababu wote: Auni mjumbe wa Magharibi katika riwaya ya *Kusadikika* na Msimuliaji katika riwaya ya *Mzingile* wanachukuliwa na mkondo wa maji yaendayo kwa kasi na kupotelewa na fahamu na mwisho wanapozinduka wanabaini kuwa wamefika pale walipotarajia. Hii inakubaliana na mhimili wa nadharia ya Kiwewe cha Kuathiriwa inayosema kuwa kabla ya kuandika kazi yenye kuathiri ni lazima msanii asome na kuvutiwa na kazi au na mwandishi wa kazi tangulizi. Kuathiriwa au ushawishi huo unakuwa mkubwa kiasi kwamba msanii fuatishi huandika kwa namna inayokaribia kuwa sawa na msanii tangulizi (Bloom, 1973). Maoni hayo yanathibitisha kuwa uandishi wa Euphrase Kezilahabi umeathiriwa na Shaaban Robert kwa baadhi ya vipengele katika riwaya teule.

Hata hivyo, Kezilahabi kwa kutaka kupunguza athari za kumwiga Shaaban Robert kwa mwigo sisisi anatumia ujalizaji kama mbinu mojawapo ya upotoshaji kuvunja mpaka kati ya mbali na karibu kwa kumtumia mhusika Mfuasi katika riwaya ya *Nagona*. Licha ya Mfuasi kama alivyo Ridhaa katika riwaya ya

Kusadikika kuvunja mpaka kati ya mbali na karibu, mguu wa Mfuasi pekee ndiyo unaosafiri kwenda Sibara wakati viungo vingine vya mwili wake vikiwa pale pale alipokuwa na wasaka paa wenzake. Mfuasi anakunjua mguu wake ulio mrefu na mguu huo kukunjuka kwa kasi ya ajabu na kwa muda mfupi mguu huo unarudi na kiko kilichokuwa umbali wa mwendo wa miaka saba (*Nagona* uk. 33).

Shaaban Robert ametumia sana uvunjivu wa mipaka ya mahali au mazingira na wa mbali na karibu hasa kwa kuwatumia majini na wanadamu kutokana na athari za mazingira yake asilia. Katika mazingira ya pwani alikozaliwa majini yana uwezo wa kuingia na kutoka ndani ya nyumba hata bila kupitia mlangoni. Yanaweza kujitokeza au kuingia na kusafiri ndani ya mti unaopasuka wenyewe pia yanaweza kuingia na kukaa mahali fulani bila kuonekana (taz, uk. 67, 74). Kibwana Jafari aliweza kusafiri kwenda Kongo kwa muda mfupi, aliweza kushuka ndani ya mtumbwi wakiwa katikati mwa bahari na kutembea juu ya maji bila kuzama na pia aliweza kukurukisha mstari na ukafika mbali sana kwa dakika sifuri (taz, uk. 63-65). Pia Osale Otango kuingia na kutoka ndani ya gereza hata kama milango ikiwa imefungwa (taz, uk. 77). Hiyo ni baadhi ya mifano inayoonesha kuwa uvunjivu wa kaida ya mahali au mazingira na kati ya mbali na karibu umetumika sana katika mazingira asilia ya Shaaban Robert.

Kinyume chake Kezilahabi kama msanii fuatishi inawezekana ametumia upotoshaji kama mbinu ya kutaka kujiengua kutoka kwa athari za Shaaban Robert kwa kutumia mbinu za kiisimu ili kuleta athari au fikra mpya katika kazi za fasihi. Amefanya hivyo kwa kutumia udunishaji na ugeuzaji ambazo ni mbinu mbili kati ya tano za upotoshaji (Bloom, 1975). Kezilahabi amefanya hivyo kwa kuathiriwa na maendeleo ya sayansi na teknolojia ya kisasa katika kuvunja kaida

za mahali au mazingira. Kwa mfano, ametumia milango inayofunguka na kujifunga yenyewe wakati wasaka paa walipokuwa wakiingia na kutoka katika ngome ya mfalme aliyemtunza paa katika himaya yake (*Nagona*, uk. 29).

Matumizi haya ya milango ambayo kwa uhalisia wa maisha ya sayansi na teknolojia ya kisasa ambapo milango kwa kutumia umeme imetengenezwa kwa namna ya kufunguka na kufunga yenyewe kwa kukaribiwa tu na mtu; kama yangetokea kipindi cha uandishi wa Shaaban Robert na katika jamii za Afrika Mashariki ya wakati huo ingehesabika kuwa ni uvunjivu wa kaida. Hii ndiyo maana Hegerfeldt (2005) anasema:

Maana ya uchawi na mazingaombwe iangaliwe si kwa mwono uliotuama yaani wa Roh pekee bali kwa kutegemea utamaduni wa jamii na maendeleo yaliyofikiwa na jamii husika kwa wakati huo (msisitizo ni wetu).

Hii ni kwa sababu jambo au tukio fulani linaweza kuonekana kama ni la uvunjivu wa kaida au la kawaida tu kulingana na tofauti za kitamaduni, kiwakati, za kimazingira au za maendeleo ya sayansi na teknolojia za jamii zinazohusika.

5.2.2 Uvunjivu wa Kaida za Kimawasiliano Kati ya Binadamu na Viumbe Wengine

Mawasiliano ni kupashana habari au kubadilishana ujumbe baina ya wawasilianaji, mfano, mtu na mtu au mtu na kikundi cha watu. Viumbe wengine kama wanyama nao huwasiliana ingawa mawasiliano yao yanahusisha ishara na sauti tofauti na binadamu ambaye hutumia lugha katika mawasiliano (Mdee, J.S, K. Njogu na Shafi, A 2011). Mawazo hayo ni sawa na maoni ya Sapir (1921: 2) anayesema kuwa:

Lugha ni njia ya mawasiliano ambayo ni maalumu kwa wanadamu tu na isiyo silika ambayo hutumiwa kuwasilisha mawazo, hisia na matakwa kwa kutumia ishara ambazo hutolewa kwa hiyari (tafsiri yetu).

Lugha ya binadamu tofauti na mawasiliano ya wanyama inajitokeza katika viwango viwili: Sauti na maana. Viwango hivyo huunganishwa ili kupata neno lenye maana tofauti, kwa mfano, fonimu, maneno na sentensi. Kinyume chake mawasiliano ya wanyama hayawezi kuchanganuliwa kwa kuanzia kipashio kidogo hadi kikubwa. Hii ni kwa sababu namna ya mawasiliano yanayotumia lugha ya kutamkwa hutumiwa na binadamu pekee. Massamba (1999: 1) anasema kuwa ni wanadamu pekee ndio watumiao lugha na ni jamii zao ndizo zinazoteua na kuyapa maneno maana wayatakayo na jinsi gani miundo ya lugha zao iwe. Kwa hiyo, inapotokea wanyama na viumbe wengine kama majini, malaika na ndege kutumia lugha ya kutamkwa na kuwasiliana na wanadamu kwa kutumia lugha bila utata wowote hapo ndipo inaposemwa kuwa kaida au kizuizi cha mawasiliano kati ya binadamu na viumbe hao kimevunjwa. Kwa sababu si jambo la kawaida kwa viumbe kama wanyama kuwasiliana na binadamu kwa kutumia lugha. Hivyo, inapotokea mnyama kama simba kuongea na binadamu tukio kama hilo ni la ajabu na si jambo la kawaida; ni uvunjivu wa kaida ya mawasiliano kati ya wanadamu na wanyama.

Katika uchawi na mazingaombwe kaida za kimawasiliano kati ya binadamu na majini, lugha moja na nyingine huvunjwa, hivyo binadamu na majini wanawasiliana kwa kutumia lugha bila kizuizi chochote. Kwa mfano, katika riwaya ya *Adili na Nduguze* Kitendo cha mwandishi Shaaban Robert kumtumia jini Huria na wazazi wake, yaani Kisasi mfalme wa majini na malkia Mjeledi, kuwasiliana na Adili bila kizuizi cha lugha ni uvunjivu wa kaida za mawasiliano

kati ya binadamu na viumbe wengine wasiotumia lugha ya kutamkwa kama ilivyo kwa binadamu. Mwandishi anasema:

Adili...alijibu. Deni langu limekwisha lipwa lote. Niliokoa maisha ya binti yako naye ameokoa yangu. Hapana deni tena kati yetu....Malkia wa majini alitabasamu akasema,...Wema wako ulikuwa asilia, nawe ulitangulia kuutenda; wa binti yangu ulikuwa wa kuigiza, naye ameutenda nyuma. Asili ya uigaji ni vitu mbalimbali. Havilinganiki wala havitalinganika milele (*Adili na Nduguze*, uk. 36).

Hapa Adili anazungumza na majini kama binadamu wenzake bila kizuizi chochote cha tofauti ya lugha kati ya binadamu na majini. Mwandishi amevunja kaida za kimawasiliano kati ya binadamu na majini ili kuelezea faida ya matendo mema. Anasisitiza kuwa huruma na matendo mema yanayotendwa bila kutarajia faida yoyote kwa mtendewa ni bora zaidi na faida yake itapatikana siku isiyotarajiwa lakini kwa wakati sahihi. Pia tendo jema linalotendwa kwanza ni la thamani kubwa na halilipiki lote kwa sababu gharama yake haikadiriki.

Uvunjuvu mwingine wa kaida za mawasiliano kati ya binadamu na majini ni pale mfalme Rai alipoandika barua ya kumwomba Adili msamaha kwa jini Huria na kwa Kisasi mfalme wa majini. Tofauti ya lugha kati ya binadamu na majini hakuzingatiwi katika uandishi wa barua hii. Zaidi ya yote kama majini wanafahamu kusoma maandishi na herufu za kibinadamu si suala la kujishughulisha nalo. Kinachoangaliwa ni kuwa barua imefika na kusomwa na Huria na Kisasi mfalme wa majini na majibu yametolewa kuwa Adili amesamehewa. Hii ina maana kuwa katika uandishi unaotumia uvunjivu wa kaida, tofauti za kimawasiliano kati ya binadamu na wanyama na hata kati ya binadamu na majini pia zinaondolewa kabisa.

Faida kubwa ya kutumia njia hii katika kazi za fasihi ni kuwa mwandishi anaweza kumtumia mhusika kufanya lolote atakalo na kuwasiliana na mtu au kiumbe kingine chochote bila pingamizi lolote. Shaaban Robert katika riwaya ya *Kusadikika* anavunja kaida za kimawasiliano kati ya binadamu na viumbe wa kufikirika kama malaika na shetani. Ridhaa mjumbe wa mbinguni baada ya kufika mbinguni kwa msaada wa malaika anafanikiwa kuleta ujumbe wa mambo ya mbinguni nchini Kusadikika. Pia shetani anafanikiwa kunyemelea halmashauri mbili za mbinguni na kufanikiwa kueneza umbea wa siri za mbinguni nchini Kusadikika.

Shetani kuzungumza na wanadamu na kuwaletea umbea au uongo wa siri za mbinguni ni suala la kuwazika ambalo haliaminiki katika uhalisia wa maisha ya kawaida na ya kila siku. Hata hivyo, katika uvunjivu wa kaida za kimawasiliano, kuwasiliana na kuingiliana kati ya binadamu na malaika, mashetani, majini na hata wafu ni suala la kawaida. Mwandishi anasema kuwa Ridhaa mjumbe wa mbinguni anafanikiwa kusikiliza na kuzungumza na malaika na kuleta habari za mbinguni Kusadikika (*Kusadikika*, uk. 35).

Licha ya kuwa lugha ya malaika na ya mbinguni kutojulikana kwa wanadamu katika hali halisi lakini Ridhaa anafanikiwa kuvunja mpaka wa mawasiliano kati ya malaika na wanadamu na kufaulu kuleta habari za mbinguni nchini Kusadikika. Hii inadhihirisha kuwa katika uvunjivu wa kaida mipaka yote huvunjwa na kuta zote za mawasiliano uondolewa kabisa.

Shaaban Robert katika kutumia uvunjivu wa kaida za kimawasiliano kati ya binadamu na malaika inawezekana ameathiriwa na Maandiko Matakatifu. Kwa

mfano, katika Biblia: Ibrahimu na Lutu wanaongea na kuwakaribisha malaika waliokuja kuunguza Sodomu kama na wanadamu wa kawaida. Malaika wa Mungu anaongea na Manoa na mke wake kuhusu kuzaliwa kwa Samsoni kama mtu aongevyo na rafiki zake (Mwanzo, 18: 1-15; 19:1-3, 12-13; Waamuzi, 13: 1-20).

Kuvunjwa kwa kaida za kimawasiliano kati ya wanadamu, malaika na mashetani kumeonekana tena wakati Ridhaa anapoelezea ulinzi mkali unaofanywa na malaika kwa halmashauri mbili za mbinguni: Hifadhi na Dhahiri. Halmashauri hizi zililindwa ili zisisogelewe na upelelezi wa kiumbe mwingine yeyote ila malaika. Mwandishi anasema:

Walakini mjumbe wetu alisikia kuwa pengine zilinyemelewa kwa siri sana na mashetani kwa kusudi la kusikiliza mambo yaliyokuwa yakisemwa huko. Kisha mashetani hao walishuka chini na umbea. Umbea huo ulienezwa Kusadikika na nchi nyingine nyingi na mashetani hao ili kuuthibitisha uwezo wao kwa watu waliowaamuru kuwa walikuwa na nguvu na elimu juu ya mambo yote. Haikudhaniwa kuwa mashetani hao waliweza kupata habari zote, lakini walipata kuokota hapa neno moja na pale maneno mawili au zaidi. Ukufi huo wa Habari ulitosha kumwezesha shetani kufanyiza uvumi mkubwa sana kwa wanadamu (*Kusadikika*, uk. 36-37).

Kitendo cha mashetani kuzungumza na wanadamu na kuwaletea umbea wa mambo ya mbinguni ni muujiza kutokea katika maisha ya kawaida. Hii ni kwa sababu katika uhalisia si rahisi kwa binadamu kuwaona na hata kuzungumza na viumbe wa kufikirika kama mashetani, mazimwi na malaika. Lakini katika uandishi unaotumia uvunjivu wa kaida za kimawasiliano ni jambo la kawaida. Hii inakubaliana na mhimili mojawapo wa nadharia ya Uhalisiamazingaombwe unaodai kuwa kazi za fasihi zinazoegemea mkondo wa uchawi namazingaombwe hutoa kipaumbele kwa mazingira na viumbe wa ajabuajabu kama mazimwi,

mashetani, mizuka, majini pamoja na misitu mikubwa, wanyama, mito na bahari hurejelewa. Uchawi na mazingaombwe kwa ujumla kama anavyodai Zamora (2005), utambulishwa kwa sifa yake ya kuunda maana ya kimazingaombwe kwa kuangalia vitu vya kawaida kwa namna isiyo ya kawaida. Mwandishi amemtumia shetani badala ya watu waovu na malaika kusimamia watu wenye matendo mema.

Imani ya shetani kuwakilisha matendo maovu kama uongo, wivu na wizi si ya dini ya Kiislamu tu lakini ni imani ya dini nyingi duniani ikiwepo na Ukristo pia. Kwa mfano, katika Biblia Takatifu shetani anatajwa kama baba wa uongo. Biblia inasema:

Ninyi ni wa baba yenu, Ibilisi (shetani), na tamaa za baba yenu ndizo mpendazo kuzitenda. Yeye alikuwa mwuaji tangu mwanzo; wala hakusimama katika kweli, kwa maana hamna hiyo kweli ndani yake. Asemapo uongo, husema yaliyo yake mwenyewe; kwa sababu yeye ni mwongo, na baba wa uongo (Yohana, 8: 44).

Kutokana kisa cha shetani kuwakilisha waongo, wambea na wauaji; Shaaban Robert anaionya jamii kujihadhari na watu waongo wanaotumia ujanja kutengeneza umbea na kueneza uongo huo au kuvujisha siri za serikali kwa maslahi yao binafsi.

Uvunjivu wa kaida za kimawasiliano kati ya binadamu na viumbe wengine umejitokeza sana katika mazingira asilia ya Shaaban Robert. Kwa mfano, Jafari Kibwana kaka yake Shaaban Robert inaelezwa na Jafari Mhunzi kuwa alikuwa anaongea na kuwasiliana na majini kama mtu anavyoweza kuzungumza na rafiki au watumishi wake bila kizuizi chochote cha lugha ya mawasiliano (taz, uk. 74).

Kuvunjwa kwa kaida za kimawasiliano kati ya binadamu na viumbe wengine ni uigizaji wa nduni za fasihi simulizi katika fasihi andishi. Mbinu hii haijatumiwa na Shaaban Robert peke yake katika uandishi. Mbinu hii imetumika hata katika maandiko matakatifu kama Biblia na Kurani Tukufu. Kwa mfano, katika Biblia mipaka ya mahali na ya kimawasiliano huvunjwa pale nyoka anapozungumza na Hawa, punda anapooonea na Balaamu, Yona kumezwa na kusafirishwa akiwa hai ndani ya tumbo la samaki na Mungu kuongea na samaki aliyemmeza Yona (Mwanzo, 3:1-5, Hesabu, 22: 27-30; Yona, 1: 17; 2:1, 10).

Kezilahabi naye ametumia uvunjivu wa kaida za kimawasiliano kati ya wanyama na wanadamu katika riwaya zake teule. Katika riwaya ya *Nagona* uvunjivu wa kaida za kimawasiliano kati ya binadamu na wanyama umejitokeza pale wanyama na binadamu wanaposhirikiana kucheka kwa pamoja siku ya matumaini ya mwezi ujao. Mwandishi anasema:

Wakati huu tulisikia vicheko vingi sana nje, vya wanyama na vya binadamu. Hii hutokea mara moja kwa mwezi... Nje tuliwasikia fisi wakicheka na nyani wakilialia. Mjini vilisikika vicheko vya kila aina. Upande wa mashariki palionekana mwezi mpevu mwekundu. Siku kama ya leo wanaiita siku ya matumaini ya mwezi ujao (*Nagona*, uk. 6).

Katika maisha ya kawaida binadamu huweza kucheka. Lakini inapotokea wanyama kama fisi na nyani kucheka pamoja na wanadamu tena kwa siku maalum inayojulikana na inayopangwa, basi tukio kama hilo si la kawaida, ni uvunjivu wa kaida. Hii ni kwa sababu wanyama kama fisi na nyani hawawezi kufahamu na kushirikiana na binadamu katika kupanga siku na wakati maalum wa matukio katika maisha ya jamii ya wanadamu. Tukio hili linakuwa la kimazingaombwe kwa sababu linakiuka uhalisia na kuonesha kuwa wanadamu

wanaweza kukubaliana na wanyama wengine kama fisi au nyani na kuagana kuwa tarehe fulani ikifika tutafanya jambo fulani. Kuwezekana kwa mawasiliano kati ya binadamu na wanyama kunashadidiwa na mhimili mojawapo wa uhalisiamazingaombwe unaosema kuwa katika uchawi na mazingaombwe kaida za uasilia na za uhalisia huvunjwa. Hivyo, binadamu anaweza kujibadilisha sura na kuwa kitu kingine, kuingia popote bila kizuizi, kuzungumza na viumbe wengine na kufa na kuishi kwa wakati mmoja.

Katika riwaya ya *Mzingile* uvunjivu wa kaida za kimawasiliano kati ya wanadamu na wanyama nao unajitokeza. Msimuliaji pamoja na mwenzake (mkewe) walipowaona watoto wawili wanaong'ara kama wao juu ya mlima waliamua kwenda kuwaona, ndipo pundamilia na simba walipojitolea kuwapeleka. Mwandishi anasema:

“Nitakupeleka,”pundamilia alisema. “Na mimi nitakupeleka,” Simba alimwambia mwenzangu. “Na tufanye mashindano, tuone nani atafika kwanza pale kileleni,” pundamilia alitoa wazo. Tulipanda juu ya migongo yao, na mara walianza kukimbia kuelekea kileleni (uk. 126).

Si rahisi na ni ajabu kutokea katika uhalisia wanyama kama simba na pundamilia kuzungumza na binadamu na hata kuwasiliana wenyewe kwa wenyewe kwa kutumia lugha ya kutamkwa kama inavyotumiwa na binadamu. Suala kama hilo linapotokea linakuwa la uvunjivu wa kaida za kimawasiliano. Hii ni kwa sababu kuna tofauti baina ya lugha ya wanadamu na mawasiliano ya wanyama. Massamba (1999) anasema kuwa ni wanadamu pekee ndio watumiao lugha na ni jamii zao ndizo zinazoteua na kuyapa maneno maana wayatakayo na jinsi gani miundo ya lugha zao iwe. Lugha za wanadamu zina tofauti za msingi dhidi ya njia zingine za mawasiliano za viumbe wengine. Inapotokea wanyama

kuzungumza na kuelewana na wanadamu ni muujiza na ni jambo la kushangaza ambalo ni kinyume na uhalisia.

Pinker (1994: 334) anashadidia ili anapozungumzia utabaka wa lugha kwa kusema:

Mfumo wa mawasiliano ya viumbe wasio wanadamu yana muundo wa aina tatu: Milio yenye ukomo...ishara za kianolojia zenye kuendelea ambazo zinaonesha namna ya hali ilivyo...au seti isiyo na utaratibu ya mabadiliko ya mada...Wakati lugha ya mwanadamu zina muundo tofauti kabisa ambapo tabia ya mfumo wa muungano uitwao sarufi huifanya lugha ya mwanadamu kuwa iso ukomo... enye kuherufika... na kutungika.

Lugha ya binadamu ina uwili kutokana na kujitokeza katika viwango vya sauti na maana. Katika sauti: mofu, fonimu na leksimu huunganishwa ili kupata neno lenye maana tofauti. Kinyume chake mawasiliano ya wanyama hayawezi kuchanganuliwa kwa kuanzia kipashio kidogo hadi kikubwa. Lugha ya wanadamu hufungamana na utamaduni wa jamii husika na hurithishwa kizazi hadi kizazi kutegemea utamaduni na mazingira yaliyomlea na kumkuza mtu husika. Mtoto yeyote ana uwezo wa kuzungumza lugha yoyote kutegemea mazingira alimokulia tofauti na wanyama ambao huzaliwa na mlio ambao hauwezi kuathiriwa na utamaduni na mazingira. Kwa mfano, ng'ombe na mbuzi hata wakikaa pamoja kwa muda mrefu kiasi gani hakuna atakayeathiriwa na sauti ya mwenzake (Mdee, 2001; Matinde, 2012; Chully, 2017). Hii ndiyo maana inapotokea simba na pundamilia kuzungumza lugha ya binadamu na kujadiliana wenyewe na pia kuzungumza na wanadamu katika riwaya ya *Mzingile* inakuwa ni kinyume cha uhalisia na hivyo kukubalika kuwa Kezilahabi ametumia uvunjivu wa kaida katika utunzi wake.

Shaaban Robert na Euphrase Kezilahabi wamefanana na kutofautiana katika kutumia uvunjivu wa kaida za kimawasiliano katika riwaya zao teule. Shaaban Robert amevunja kaida za kimawasiliano kati ya wanadamu na viumbe wengine kwa kutumia viumbe dhahania kama majini, mashetani na malaika wanaoonekana wazi kwa binadamu, kuongea nao na hata kuwapatia msaada. Viumbe hivyo vimewasiliana na binadamu bila kuwa na kizuizi cha lugha na wengine kutoa msaada mkubwa kwa binadamu; jambo ambalo si la kawaida katika uhalisia wa maisha ya binadamu. Kwa mfano, Adili kupelekwa na Huria binti Kisasi katika himaya ya majini na kuongea nao (*Adili na Nduguze* uk. 34-35), Ridhaa mjumbe wa mbinguni kuwasiliana na kusafirishwa na malaika anayeshughulikia mambo ya wanadamu na mashetani kuzungumza na wanadamu na kuwaletea umbea wa mambo ya mbinguni (*Kusadikika*, uk. 34, 36-37).

Kezilahabi kwa upande wake ametumia wanyama na ndege wanaowasiliana na wanadamu au wenyewe kwa wenyewe kwa kutumia lugha. Kwa mfano, katika riwaya ya *Nagona* amemtumia paka anayeonekana kumfahamu na kumngojea Msimuliaji, wanyama wanaocheka na kushiriki mipango ya sherehe za mwandamo wa mwezi pamoja na wanadamu (*Nagona*, kur. 2-3, 6) na simba na pundamilia wanaongea na Msimuliaji na mke wake na kuwabeba kwa mashindano ya mbio kuelekea juu ya mlima katika riwaya ya *Mzingile* (kur,125-126).

Shaaban Robert kutumia majini kuwasiliana na wanadamu ameathiriwa kwa kiwango kikubwa na mazingira asilia ya pwani yaani mkoani Tanga alikozaliwa pamoja na vitabu vya *Alfu Lela Ulela*. Katika jamii ya Shaaban Robert kuishi, kuoja, na hata kuwafuga majini ni suala la kawaida (taz, uk. 74). Pia vitabu vya

Alfu Lela Ulela ambavyo inaonekana Shaaban Robert amevisoma sana vimejaza hadithi zinazohusiana na matukio ya majini kuzungumza na wanadamu ambayo baadhi yake Shaaban Robert ameyaigilizia kwa mwigo sisisi (*Alfu Lela Ulela: Kitabu cha 1,2,3*).

Kwa upande wa Kezilahabi ingawa hapa inawezekana ameathiriwa na Shaaban Robert kwa kiasi fulani lakini ameathiriwa zaidi na maandiko ya Biblia pamoja na mazingira asilia ya kwao Ukerewe. Katika kitabu cha Hesabu 22: 28-30 Biblia inasema:

Bwana akakifunua kinywa cha yule punda, naye akamwambia Balaamu, “Nimekutenda nini, hata ukanipiga mara tatu hizi? Balaamu akamwambia punda; “Kwa sababu umenidhihaki; laiti ningekuwa na upanga mkononi ningekuua sasa hivi”. Yule punda akamwambia Balaamu, Je! Mimi si punda wako, nawe umenipanda maisha yako yote hata leo? Nimezoea kukutenda hayo? Akasema, La!

Balaamu hapa anaongea na punda kama mtu anayehojiana na binadamu mwenzake. Pia katika kitabu cha Mwanzo sura ya 3: 1-4 Biblia inasema:

Nyoka alikuwa mwerevu kuliko wanyama wote aliowaumba Bwana Mungu. Nyoka akamwambia mwanamke, “Ni kweli kuwa Mungu amewazuia kula matunda yote ya miti iliyoko bustanini?” Mwanamke akamjibu nyoka: “Miti yote ya bustanini twaweza kula; isipokuwa matunda ya mti ulio katikati ya bustani ndiyo Mungu amesema, ‘Tusiyale wala kuyagusa, tusije tukafa.’” Lakini nyoka akamwambia mwanamke: “Hamtakufa hakika, kwa maana Mungu anajua ya kwamba siku mtakayokula matunda ya mti huo, mtafumbuliwa macho, nanyi mtakuwa kama Mungu, mkijua mema na mabaya.”

Aya hizo zinadhihirisha kuwa nyoka na wanyama wengine inawezekana kabla ya dhambi walikuwa wanaongea na kuwasiliana na binadamu bila kizuizi chochote. Pia kwa Wakerewe, jamii asilia ya Kezilahabi, zaidi ya kumtukuza na kumheshimu chatu, nyoka asiyeuawa na anayehesabika miongoni mwa mizimu ya Wakerewe, wanaamini kuwa wachawi wana uwezo wa kuwazoeshwa wanyama

kama ng'ombe, mamba, paka pia na ndege kama bundi na kuwatumia kwa shughuli za kichawi. Kwa mfano, ng'ombe anatumiwa na wachawi wa Kikerewe kama chombo cha usafiri usiku wanapokwenda katika shughuli zao za kichawi. Pia mamba anaweza kutumwa na kumkamata mtu na kumsafirisha salama ndani ya maji mpaka kwa mchawi aliyemtuma. Mfano ni kisa cha John mbadhirifu aliyesafirishwa na mamba (taz, uk. 97). Biblia inazidi kuisitiza kuwa katika nchi mpya baada ya kuharibiwa kwa dunia hii uhusiano na mawasiliano kati ya wanadamu na viumbe wengine kama anavyodai Kezilahabi yatarudishwa tena. Isaya na Hosea katika Biblia Takatifu wakizungumzia nchi mpya ambayo Mungu atawapa washindi wa dhambi wanasema:

Mbwa-mwitu atakaa pamoja na mwana-kondoo, na chui atalala pamoja na mwana-mbuzi, simba atakula majani kama ng'ombe na wataongozwa na mtoto mdogo. Mtoto anyonyaye atacheza na kutia mkono wake katika tundu la nyoka lakini hawatamdhuru maana katika mlima mtakatifu wa Mungu dunia yote itajawa na kumjua Mungu. Mungu atafanya maagano na wanyama, ndege na wadudu naye atavunja upinde na upanga na silaha vitoke katika nchi na kuwalalisha salama salimini (Isaya, 65:25,11. 6-9; Hosea, 2: 18).

Kezilahabi inawezekana ameathiriwa na mafungu hayo ya Biblia yanayozungumzia mbwa mwitu na chui kukaa pamoja na kondoo na mwana mbuzi. Wanyama hao katika uhalisia hawawezi kukaa pamoja hata dakika moja, kwa sababu mbwa mwitu na chui ni wanyama wala nyama wanaowatumia kondoo na mbuzi kama chakula chao. Kezilahabi yeye amewatumia simba, chui na fisi wanyama wala nyama wakila majani huku wakicheza kwa amani na kuongea na kifaru, pundamilia na wanyama wengine ambao kwa hali halisi ni maadui zao. Biblia inaposema mtoto anyonyaye atatia mkono wake katika tundu la nyoka bila nyoka kumdhuru na mtoto mdogo kuwaongoza wanyama wakali na

hatari kama simba na chui inasisitiza amani na mapatano kati ya viumbe katika nchi mpya.

Kezilahabi ameathiriwa na maneno haya anaposema kuwa Msimuliaji na mkewe walitembea katikati ya wanyama wakiwapapasa manyoya. Mkewe akiwa mbele ya simba akichezeachezea manyoya ya shingoni. Baadaye simba na pundamilia kuhiari kuwabeba kwa mashindano kuelekea juu ya mlima walipo watoto wawili mapacha wanaong'aa. Maelezo hayo yanadhihirisha kuwa licha ya kuathiriwa na mazingira asilia ya Ukerewe, Kezilahabi ameaathiriwa na Biblia katika kuvunja kaida za kimawasiliano kati ya wanadamu na viumbe wengine.

5.2.3 Uvunjivu wa Kaida Kati ya Uhai na Kifo.

Ili kuelewa vizuri juu ya uvunjivu wa kaida kati ya uhai na kifo ni vyema maana ya uhai na kifo ikawekwa bayana. Katika kueleza maana ya uhai na kifo maelezo ya uumbaji wa mwanadamu kutoka katika Biblia Takatifu yamerejelewa. Mwanadamu ameumbwa kwa muunganiko kati ya mavumbi ya ardhi na pumzi ya uhai. Biblia inasema, “Bwana Mungu akamfanya mtu kwa mavumbi ya ardhi, akampulizia puani pumzi ya uhai, mtu akawa nafsi hai (Mwanzo, 2:7).

Kwa hiyo nafsi hai au uhai wa mwanadamu ni muunganiko wa mavumbi ya ardhi na pumzi ya uhai (mavumbi ya ardhi+ pumzi ya uhai= nafsi hai). Kwa mantiki hiyo uhai unaweza kuelezwa kuwa ni muunganiko wa mavumbi ya ardhi yaani mwili au kiwiliwili na pumzi ya uhai (Mwanzo 6: 17; 7:15, Ayubu 33: 4). Kinyume chake kifo kinaweza kuelezwa kuwa ni mavumbi ya ardhi au mwili kutoa pumzi ya uhai. Kifo kwa maana hiyo ni kitendo cha kutenganishwa kwa mavumbi na pumzi ya uhai. Mwanadamu anapokufa pumzi ya uhai humtoka na

huacha kuishi na kuwa mfu, hivyo hawezi kufanya jambo lolote wala kuwasiliana na walio hai (Zaburi, 104: 29; Mhubiri, 3: 19; Zaburi, 146: 4; Mhubiri, 9: 5,10).

Peter (1974) anaeleza kifo kuwa ni hali ya mifumo yote ya mwili kwa muda zaidi ya masaa ishirini na nne kuacha kufanya kazi kama kupumua, kuhisi, kujongea, mapigo ya moyo kutoendelea hata kwa kusaidiwa kwa mashine au madawa ya kuhamasisha. Tofauti na maoni hayo juu ya uhai na kifo, Mbiti (1969) alifanya uchunguzi jinsi suala la uhai na kifo linavyoelezwa au linavyofahamika katika jamii mbalimbali za Kiafrika.

Mbiti aligundua katika utafiti huo kuwa katika jamii nyingi za Kiafrika, watu waliokufa karibuni kama vizazi vitano hivi wanahesabika kama watu walio katikati ya uhai na kifo hivyo amewaita wafu-hai. Hii ni kwa sababu ufu wao haujakamilika. Watu hao anasema bado wanamudu lugha mbili: lugha asilia waliyotumia wakiwa hai na lugha ya mizimu ambapo wanaelekea kuwa sehemu yake kwa sasa. Wafu-hai bado wanahesabika kama watu, hawajawa mizimu kamili. Wanaweza kurudi katika familia zao mara kwa mara na kushirikiana nao katika shughuli mbalimbali kimiujiza. Kwa sababu bado ni wanadamu wanakuwa walinzi wa familia zao na kama daraja kati ya familia zao na Mungu. Anasema kuwa wafu-hai wanatakiwa na wakati huo huo wanaogopwa. Kama familia zao ziliwajali na kuwatunza vyema wakati wa uhai wao na pia kuwafanyia mazishi ya heshima wataleta mibaraka. Kama hawakufanyiwa vizuri wataleta laana ikiwa ni pamoja na mikosi na magonjwa ya ajabuajabu. Walio hai wanapotakuna nao wanaogopa kwa sababu wanaamini kuwa watu hao wamekufa tayari na hivyo kukutana nao ni uvunjivu wa kaida kati ya uhai na kifo (Mbiti, 1969).

Shaaban Robert hakutumia uvunjivu wa kaida kati ya uhai na kifo katika riwaya zake zote teule. Kinyume chake Kezilahabi ametumia uvunjivu wa kaida kati ya uhai na kifo katika riwaya za *Nagona* na *Mzingile*. Hii ina maana kuwa Kezilahabi kama mwandishi fuatishi ameamua hapa kujitenga kabisa na athiri za Shaaban Robert kwa kubadili mada na kuja na mada tofauti kabisa na Shaaban Robert. Bloom (1973) kwa kutumia nadharia ya Kiwewe cha Kuathiriwa anasema kuwa kwa kubadili mada, msanii fuatishi anajitahidi kubuni kwa ufundi wa hali ya juu mada nyingine tofauti kabisa na mada ya msanii tangulizi. Msanii fuatishi anafanya hivyo kwa kujitahidi kujitenga au kuachana na mada ya msingi ya msanii tangulizi ili kuonesha dhahiri kuwa kazi yake ina nguvu kuliko ya mtangulizi wake. Lengo la msanii fuatishi likiwa ni kujijengea utukufu au jina binafsi mbali na msanii tangulizi.

Katika riwaya ya *Nagona* kuvunjwa kwa mpaka kati ya uhai na kifo kunajidhihirisha katika maneno ya Nabii. Nabii anasema:

Waliooteuliwa walijitahidi walivyoweza kuweka katika kumbukumbu niliyoyasema. Tatizo ni fasili na ufafanuzi...Waliniua mimi badala ya kuua Sphinx (*Nagona*, uk. 26-27).

Hapa Nabii anasema aliuawa na wakati huo huo anazungumza na waliohai kana kwamba hajafa na hivyo kuvunja kaida kati ya uhai na kifo. Hii ni kwa sababu ni vigumu kubaini kuwa Nabii yuko katika kundi gani, kundi la wafu au kundi la walio hai.

Katika riwaya ya *Nagona* uvunjivu wa kaida kati ya uhai na kifo unajitokeza zaidi Kizee kilichokuwa kikiwaongoza Ego, ID na SUPEREGO kutembelea viwanda vilivyokufa kilipowauliza kama wako hai au wamekufa. Wenyewe

baadaye walishindwa kuwa na hakika kama wa hai au wamekufa. Na kizee kinasisitiza kuwa mahali hapo walipokuwa hapajapata kukanyagwa na aliye hai. Kizee kinasema kuwa kilianza kufa tangu siku kilipozaliwa na wote humo wanamwogopa, wanamwita kifo (*Nagona*, uk. 20-21).

Visa hivyo vinaonesha uhalisia katika jamii nyingi za Kiafrika, jamii asilia ya Kezilahabi (Wakerewe) ikiwemo. Kwa Wakerewe mawasiliano kati ya walio hai na wafu au watu wanaohisiwa kuwa wamekufa kurudi na kufanya matukio fulani kwa familia au katika jamii zao ni jambo la kawaida. Mfano, kisa cha kunigwa na matunu mwaka 1989 katika Kijiji cha Namagondo (taz, uk. 96). Hivyo, Kezilahabi kutumia uvunjivu wa kaida kati ya uhai na kifo ni kutaka kuelezea uhalisia wa maisha katika jamii yake.

Katika maisha ya kawaida mawasiliano kati ya watu ni suala la kawaida na la kila siku. Ingawa ni suala la ajabu lakini pia kumetokea mawasiliano kati ya walio hai na wafu hata katika maandiko matakatifu. Kwa mfano, mfalme Sauli katika Biblia Takatifu (I Samweli, 28: 12-15) alimwomba mchawi wa Endori kumpandishia Samweli ambaye alifariki zamani naye akaongea naye. Mtu aliye hai kuwasiliana na wafu au na kifo linakuwa suala la kimazingaombwe kwa sababu kuna hali ya kuhadaisha uoni au uelewa wa yule aliyehai aingiaye katika mawasiliano hayo. Katika mawasiliano kati ya Sauli na Samweli, mchawi wa Endori anasema, ‘Namwona mungu anatoka katika nchi’..., Sauli anamwuliza, ni mfano wa nini? ..mchawi anajibu, ‘Ni mzee anazuka; naye amefunikwa vazi’ (I Samweli, 28: 13-14). Hapa inaonekana kuwa anayejitokeza kuongea na Sauli ni mungu na si Samweli. Hii inamaana kuwa katika mawasiliano na wafu kuna

uongo au viini macho, yaani yule anayeonekana kwa sura ya aliyefariki ni mungu (shetani) au mfano tu wa sura ya mtu fulani lakini si mtu huyo kihalisia.

Biblia Takatifu inathibitisha kabisa kuwa wafu hawajui neno lolote wala hawawezi kufikiri wala kufanya mawasiliano yoyote na walio hai. Kwa maana walio hai wanajua kwamba watakufa; lakini wafu hawajui neno lolote, wala hawana ijara tena; maana kumbukumbu lao limesahaulika (Zaburi, 88:10, 115:17; Mhubiri, 9:5).

Katika uvunjivu wa kaida kati ya uhai na kifo mpaka kati ya uhai na kifo huvunjwa, hivyo mtu anaweza kufa na kuishi kwa wakati huo huo. Msimuliaji anasema kuwa walifikiri juu ya kizee na kujiuliza kama walikuwa hai au walikuwa wamekufa (*Nagona*, uk. 23). Zaidi ya msimuliaji kuishi kati ya ufu na urazini wanatembelea viwanda vinavyosimamiwa na walio hai na kutoa taarifa kwa serikali bila pingamizi lolote. Katika uvunjivu wa kaida mipaka ya kimawasiliano kati ya walio hai na wafu huvujwa na mhusika anaweza kuingia na kutoka ufuni bila pingamizi lolote, yaani mtu anaweza kufa na kuwa hai wakati huo huo. Flores (1988) anathibitisha hili kwa kusema kwamba uchawi na mazingaombwe unajumuisha uchanganyaji wa uhalisia na fantasia. Unakusudia kuunganisha na kuvunja mipaka kati ya ukweli na uongo, ndoto na urazini na uhai na kifo.

Kezilahabi anasimulia katika riwaya ya *Mzingile* kisa cha kipofu anayeongea na msimuliaji akiwa safarini kutoka kwa Kizee. Kipofu anaeleza historia ya maisha yake kutoka kuzaliwa, asili ya upofu wake, kupiga marimba hadi kukanyagwa na

lori lililomvusha mstari kati ya uhai na kifo. Hapo ndipo msimuliaji anapohisi kuwa anaongea na mtu mfu. Mwandishi anasema:

Unajua binadamu tu waoga sana. Tunajenga majengo marefu na kuruka angani lakini tunasubiri kichaa fulani, vijidudu vidogo vya malaria, au ajali vituvushe mstari huo. Tunasindikizwa kaburini na wadudu wadogo ili kutuondolea aibu ya woga (uk. 51-52).

Kudhihirisha wasiwasi wake kuwa anaongea na mfu, Msimuliaji anashtuka na kumuuliza kipofu kuwa anataka kumwambia kuwa anazungumza na mtu aliyekufa! Kipofu anamhakikishia kwa kumwambia kuwa amekuja kumshukuru, kwa sababu siku ya mazishi yake alikuwa akiwatazama wote kutoka upande mwingine. Ijapokuwa Msimuliaji bado alikuwa mtoto, lakini anaelezwa na kipofu kuwa kwa ujasiri wake yeye ndiye aliyekuwa wa kwanza kutupia mchanga kaburini mwake (*Mzingile*, uk. 52).

Mazingaombwe katika uvunjivu huu wa kaida kati ya uhai na kifo hapa yanajitokeza katika mambo mawili. Jambo la kwanza ni kwa waliohudhuria katika mazishi ya kipofu walimzika wakidhani kuwa wamemzika mtu wakati kipofu mwenyewe (aliyekuwa anazikwa) alikuwa akiwatazama kutoka upande wa pili na kumfahamu hata mtu wa kwanza kutupia mchanga kaburini mwake. Kwa sababu ya uoni wa wazikaji kuhadaika na kuzika kitu tofauti na binadamu, kwao ni mazingaombwe. Jambo la pili ni kwa Msimuliaji mwenyewe. Msimuliaji alikuwa anaongea na kipofu akidhani kuwa anaongea na mtu wa kawaida anayeishi katika uhalisia wa maisha, lakini anashtushwa na kipofu anapomwambia kwamba alikufa kwa ajali ya kukanyagwa na lori lililokuwa likiendeshwa na dereva mlevi. Maelezo haya yanaonesha kuwa Msimuliaji hakufahamu kuwa kipofu aliyekuwa akiongea naye alikuwa ni mfu. Kwa maana

hiyo, Msimuliaji kwa sababu ya kuhadaika na kutofahamu ukweli wa mambo mpaka anafumbuliwa macho na kipofu kwake mawasiliano hayo yalikuwa ni mazingaombwe. Kinyume chake, kwa kipofu haikuwa ni mazingaombwe kwa sababu alikuwa anafahamu ukweli wote.

Kitendo cha walio hai na wafu kuwasiliana ni hali isiyo ya kawaida katika ulimwengu halisi. Lakini katika uvunjivu wa kaida hakuna mpaka kati ya uhai na kifo. Mtu anaweza kufa na kuwa hai na kufa tena na kuwa hai wakati huo huo. Kipofu aliuawa kwa sababu ya kuimba juu ya wakati ujao. Viongozi wakakasirishwa na jinsi alivyodai kuona zaidi ya wenye macho. Makusudi, akagongwa na lori ili akawaimbie sisimizi kwenye giza la milele (*Mzingile*, uk. 80).

Kisa cha kipofu kurudi kutoa shukrani kwa Msimuliaji kwa sababu ya Msimuliaji kuwa wa kwanza kutupia mchanga kaburini mwake siku ya mazishi yake yanasadifisha mawazo ya Mbiti (1969) kuwa Waafrika wanaamini kuwa wafu-hai wanaweza kurudi kutoa mibaraka au laana kulingana na walivyotendewa wakiwa hai ikiwa ni pamoja na jinsi mazishi yao yalivyoshughulikiwa kwa heshima. Hii ndiyo maana kifopu (mfu-hai) anarudi kutoa shukrani kwa Msimuliaji.

Katika mazingira asilia ya Kezilahabi kuna matukio mengi ya watu waliokufa na kuzikwa kurudi na kuishi tena. Kwa mfano, kisa cha kuzika shina la mgomba (taz, uk. 94). Katika kisa hiki, Jeftha Masota alikufa na kuzikwa lakini yeye alikuwa anawaona watu walivyokuwa wakilia na kuzika shina la mgomba wakidhani wanamzika mtu.

Uvunjivu mwingine wa kaida kati ya uhai na kifo katika riwaya ya *Mzingile* unajitokeza pale mwanamke anapomwambia Msimuliaji kuwa mwanamke aliyekuwa akifuatana naye muda wote alikuwa ni mke wake. Kinachomchanganya msimuliaji ni kuwa mke wake alikuwa amekufa zamani. Iweje mke aliyekufa kujitokeza kwake na kuongea naye? Anapoulizwa na huyo mwanamke kuwa kama akimwona mke wake atamtambua? Anajibu kuwa atamwonaje? Mwanamke anamjibu kuwa, kwa kutumia vizuri upya wa mboni zake (*Mzingile*, uk. 114-115). Maneno hayo ya mwanamke wa kimiujiza yanathibitisha kuwa katika uchawi na mazingaombwe kuna uwezekano wa kuishi kati ya uhai na kifo. Mawazo hayo yanashadidiwa na mhimili wa uhalisiamazingaombwe unaosema kuwa watunzi wa kazi za fasihi zinazoegemea mkondo wa uhalisiamazingaombwe huvunja kaida zote za uasililia na za uhalisia. Hivyo, kuondoa mpaka kati ya mbali na karibu, ndoto na uhalisi na kati ya uhai na kifo. Kwa hiyo, mhusika anaweza kufa na kuishi kwa wakati mmoja. Hili linazidi kuthibitishwa na Oka (2002) akielezea riwaya ya Okri ya *The Famished Road* (1991) anatumia kisa cha kufa na kuzaliwa na kufa na kuzaliwa tena mpaka safari tano kwa Azaro kusesitiza kuwa katika uchawi na mazingaombwe hakuna kinachoshindikana. Katika uchawi na mazingaombwe mtu anaweza kuishi kati ya uhai na kifo, kuwa macho na kuwa usingizini, kuwa mtoto na kuwa mzee na hata kuwa pahala pengi kwa wakati mmoja.

Kezilahabi licha ya kutatanishwa na kuwepo uwezekano wa maisha baada ya kifo, hata hivyo anamtumia mwanamke anayefuatana na msimuliaji kimiujiza kueleza kuwa haiwezekani kutambua mambo bila kutumia vizuri mboni au macho yetu, yaani akili zetu. Inawezekana Kezilahabi anakusudia kueleza kuwa

tuna macho lakini hatuoni, tuna masikio lakini hatusikii na tuna akili lakini hatufikiri. Hivyo, ili kufikia kiwango cha juu cha utambuzi ni lazima milango yote ya fahamu itumike upya na kwa umakini wa hali ya juu. Kezilahabi anasisitiza sana matumizi ya akili au fikra safi karibu katika riwaya zake zote teule. Kwa mfano, katika riwaya ya *Mzingile* anasema kuwa baada ya mto hakuna kingine isipokuwa kina cha fikra safi katika upweke (uk. 14). Pia katika riwaya ya *Nagona* anasema kuwa, huu ndio mguu uendao mbali kwenye fikra na uzamapo haurudi bila wazo (uk. 28). Kwa hiyo hapa Kezilahabi anatumia uvunjivu wa mpaka kati ya uhai na kifo kufundisha namna mpya ya kutazama mambo. Kuwa katika fikra makini hutokea uvumbuzi na utatuzi wa vikwazo vingi (*Nagona*, uk. 28).

Tofauti na Shaaban Robert ambaye hakutumia uvunjivu wa mpaka kati ya uhai na kifo Kezilahabi anaingia na kutoka katika ufu bila wasiwasi na kuvunja kaida kati ya uhai na kifo. Hii inamfanya msomaji kushindwa kufahamu mara nyingine kuwa hapa Msimuliaji anazungumza kama mtu aliye hai au kama mfu. Ingawa katika sehemu hii, licha ya Kezilahabi kuathiriwa na mazingira asilia ya Ukerewe lakini ametumia upotoshaji kwa kujaribu kujitenga kutoka kwa athari za Shaaban Robert, kwa kutumia mbinu ya ujalizaji ambayo ni mbinu mojawapo ya upotoshaji ya kiisimu ili kuleta athari au fikra mpya katika kazi za fasihi (Bloom 1973).

Katika kisiwa cha Ukerewe kuna visa na imani kuwa watu wao waliokufa waliweza kurudi nyumbani kwao na kuongea na walio hai wakiomba maji au chakula. Wafu hao walionekana dhahiri kwa sura zao lakini walitoweka ghafla walipotaka kupewa kile walichoomba. Wengine ingawa sauti zao zilisikika lakini

sura zao hazikuonekana. Wengine walienda mbali zaidi kwa kutangaza na kubandika orodha ya majina ya wafu watakaoshiriki katika mchezo wa mpira wa miguu. Kwa mfano kati ya mwaka 1987 na 1989 katika kijiji cha Bugorora mechi ya mpira ilitangazwa na wafu na majina ya watu fulani waliokufa kijijini hapo na vijiji vya jirani yalibandikwa kuwa watakuwepo katika mchezo huo.

Siku ya mchezo huo watu wengi walihudhuria kushuhudia mechi hiyo ya wafu. Ingawa hawakuwaona wachezaji kwa macho lakini sauti zao, kelele za kushangilia na mdundo wa mpira uliokuwa ukichezwa zilisikika (taz, uk. 94). Hii inadhihirisha kuwa Kezilahabi amekusudia kutumia uchawi na mazingaombwe kuelezea uhalisia ambao upo katika jamii yake na kwa namna inayoeleweka kwa jamii husika.

5.2.4 Uvunjivu wa Kaida Kati ya Ndoto na Uhalisia

Mtaalamu wa masuala ya ndoto kutoka Marekani Calvin Hall (1966), anaelezea ndoto kama mfululizo wa picha halisi zinazoonekana, zimtokeazo mtu aliyeko usingizini. Ndoto mara nyingi huwa na tukio moja au zaidi, wahusika wengi akiwemo mwotaji mwenyewe na mfululizo wa matendo na mazungumzo ambayo yanamhusisha mwotaji. Ndoto hushabihiana na sinema ya tamthilia ambapo mwotaji ni mhusika na mtazamaji...Tangu wakati huo wa matukio ya ndoto yanapotokea mwotaji anahisi kuwa anaona vitu halisi kabisa (Farady, 1972: 38).

Jung (1974: 4) naye anaelezea ndoto kuwa ni matokeo ya mawazo au utendaji wa akili katika kuyarudisha yale yaliyotokea katika maisha ya mtu katika mazingira yake muda kabla ya uotaji huo. Hivyo anasema kuwa kile kinachootwa sicho cha kwanza bali ni kile kinachotokana na mawazo na matendo yaliyotangulia. Kwa

hiyo ndoto inaweza kuelezwa kuwa ni mfululizo wa picha, mawazo, mihemko na hisia ambazo kwa kawaida hutokea akilini mwa mtu katika hatua fulani fulani za usingizi. Hii hutokea kwa kuyarudisha yale yaliyotokea katika maisha yake au katika mazingira yake muda kabla ya uotaji huo.

Mambo yafuatayo ni muhimu kuhusu ndoto: Lazima mtu awe usingizini. Mara nyingi ni matokeo ya matukio aliyopitia mwotaji muda kabla ya usingizi. Ni njia ya kutimiza matamania au matarajio ya mwotaji ambayo hayajitimizwa katika uhalisia. Ndoto nyingi zinakuwa na maana na si lazima mwotaji kubaini maana hiyo. Na pia ndoto yaweza kudhihirisha vipaji vilivyojificha.

Ndoto imejumuishwa katika utafiti huu kama sehemu ya uvunjivu wa kaida kwa sababu katika ndoto mwotaji anakuwa na nafsi mbili: nafsi tulivu na nafsi inayotembea ndotoni kichawi na kimazingaombwe. Kwa mujibu wa Sigmund Freud (1965) nafsi tulivu ni mwili halisi wa mtu inayokuwa mahali halisi pale mtu alipolala na inayoweza kuguswa na inayoweza kuonekana na mtu yeyote wa kawaida. Wakati nafsi inayotembea ndotoni ni ile akili au mawazo ya mtu yanayoweza kutengana na kiwiliwili na kusafiri kwenda sehemu mbalimbali na kufanya mambo mbalimbali mtu awapo usingizini.

Katika ndoto mtu anaweza kwenda sehemu yoyote, kuingia popote bila kizuizi na kufanya au kuona mambo mengi sana kwa muda mfupi. Katika ndoto mtu anaweza kusafiri kutoka bara moja hadi nyingine, kuanza darasa la kwanza hadi kupata digrii, kuzaliwa hadi kuoza na kulima hadi kuvuna. Haya yote yanawezekana katika ndoto ya dakika tano tu.

Uchanganuzi wa data katika sehemu hii umeongozwa na mhimili wa nadharia ya uhalisiamazingaombwe unaosema kuwa katika uhalisiamazingaombwe uhalisi na ndoto huingiliana. inawezekana mtu anapoota ndipo yupo katika uhalisi na wakati yu uhalisini ndipo yu ndotoni. Hii ni kwa sababu katika uhalisiamazingaombwe hakuna mpaka kati ya uhalisi na utohalisi au kuwa macho na kuwa usingizini. Hii ina maana kuwa uhalisiamazingaombwe haukubaliani na uhusiano wa kadhia zinazotendeka katika maisha ya mtu kiutengano. Hali kama za uhalisi na ndoto, usasa na ukale, uhai na kifo, mbali na karibu, ugeni na uwenyeji na tamaduni zinaingiliana.

Katika riwaya ya *Kusadikika* Shaaban Robert anasimulia ndoto ya kipofu, Sapa. Ndoto yenyewe si ndoto kwa maana ya ndoto kama ilivyoelezwa, bali ni maneno ya hila yaliyotungwa na Sapa mwenyewe ili afaidi bahati ya Salihi. Salihi alikuwa na bahati ya kupewa kila kitu alichoomba kwa mtu yeyote. Kwa mtazamo wa Sapa, Salihi hakuwa na matumizi na vitu alivyovipata kwa maombi hayo. Hivyo alitunga hila kuwa aliota ndoto kuwa Salihi akiomba kitu chochote tena bila kugawana naye sawa, dua yake haitapokelewa. Hata hivyo kwa kuzingatia mhimili wa uhalisiamazingaombwe unaotumika katika uchanganuzi huu maneno hayo ya Sapa yanahesabika kuwa ni ndoto kwa sababu katika uhalisiamazingaombwe hakuna mpaka kati ya kuwa macho na kuwa ndotoni.

Mwandishi anasema:

Kipofu wa pili alijibu, ‘Bwana wangu mwema, mimi naitwa Sapa na mwenzangu ni Salihi. Salihi haombi neno akalikosa. Ameishi maisha haya tangu ujana wake, lakini vitu alivyovipata kwa maombi aliyofanya alikuwa hana matumizi navyo. Nilipoona hivyo nilimwambia kuwa niliota ndoto kuwa akiomba kitu chochote tena bila kugawana na mimi sawasawa, dua lake halitapokelewa hata kidogo..., lakini pale pale mwenzangu aliinua mikono juu akaomba upofu, na kabla sijatanabahi, sisi sote wawili tulikuwa vipofu (*Kusadikika*, uk. 29-30).

Uvunjivu wa kaida katika matokeo ya ndoto hii ya kutunga ni kitendo cha Salihi kuinua mkono na kuomba upofu na wote wawili kuwa vipofu dakika hiyo hiyo. Katika maisha ya kawaida si rahisi na ni ajabu kwa mtu kuinua mkono na kuomba wawe vipofu na mara hiyo wote wawili kuwa vipofu bila macho yao kuguswa na kitu chochote. Kisayansi wala kimantiki ya kawaida haiwezekani kuthibitishwa jinsi maneno ya kutamka tu yanavyoweza kumfanya mtu kuwa kipofu. Hii ina maana kuwa nadharia za kihalisia na zile za kisayansi haziwezi kuchunguza na kuthibitisha jinsi maneno ya kutamka tu yanavyoweza kumtia mtu upofu. Hili kukabiliana na matukio kama hayo inahitajika nadharia inayochanganya uhalisia na mazingaombwe kwa wakati moja katika uchanganuzi wake; nadharia faafu ni nadharia ya Uhalisiamazingaombwe.

Marwick (1970) na Bronowski (1978) wanasema kuwa, uhalisiamazingaombwe hutofautiana na sayansi inayoangalia uhalisia kwa namna moja tu ya mantiki. Uhalisiamazingaombwe hutazama uhalisia kwa namna mbili tofauti: Namna ya kawaida ya maisha ya kila siku katika ulimwengu halisi na mazingira asilia. Na namna nyingine ni ile ya kimiujiza, inayopita akili ya kawaida ya mwanadamu yaani ile inayopindua kanuni za asili juu chini. Kwa hiyo kitendo cha Salihi na Sapa kuwa vipofu kwa maneno tu ya kutamka inawezekana katika uvunjivu wa

kaida za uhalisia kwa kutumia miujiza inayopita ung'amuzi wa akili ya kawaida ya binadamu.

Kisa hiki cha upofu wa Sapa na Salihi katika riwaya ya *Kusadikika* ni sawa na kisa cha Baba Abdalla Kipofu katika masimulizi ya *Alfu Lela Ulela* Kitabu cha Nne. Baba Abdalla alikuwa kipofu kwa sababu ya tamaa ya kutaka kufaidi au kuchukua hazina yote ya Walii licha ya Walii kukubali wagawane nusu kwa nusu. Mwandishi anasema:

Walii alipokwisha kipokea kile kisanduku akaniambia nifumbue jicho langu la kushoto, naye akalipaka mafuta taratibu. Hata nilipolifumbua tena nikaona mali za kila namna zisizo hesabu zimetandazika, kama zilizo mbele yangu...choyo na tamaa ya mali ilinishika...Basi nikazidi kumshikilia walii anipake jicho langu la kulia, lakini yeye alikataa kata kata...Nikamjibu kwa hasira,...tafadhali...fanya hivi nikuambiavyo...Walii...akatwa mafuta na kunipaka kidogo katika jicho langu la kulia...na saa ile ile nikawa kipofu kama hivi unionavyo sasa (*Alufu Lela Ulela*, uk. 5, 7)!

Shaaban Robert inawezekana ameathiriwa kwa kiasi fulani na kisa hiki kutoka masimulizi ya *Alfu Lela Ulela* katika kuzungumzia kisa cha upofu wa Sapa na Salihi. Tofauti kati ya Shaaban Robert na masimulizi ya *Alfu Lela Ulela* ikichunguzwa kwa makini ni kuwa Shaaban Robert ametumia uvunjivu wa kaida kwa Salihi kusema tu maneno kwa kuinua mikono na wakawa vipofu yeye na Sapa lakini kitendo cha Walii kumpaka Baba Abdalla Kipofu mafuta jicho la kulia naye Abdalla kuwa kipofu ni cha kawaida na kinaweza kufanywa na kila mtu. Hata hivyo kitendo cha Walii kumpaka Abdalla mafuta jicho la kushoto na kumfanya kuona hazina zote za dunia ni cha uvunjivu wa kaida kwa sababu kupakwa mafuta tu machoni hakuwezi kukufanya uone mali zote za dunia tena karibu nawe, yaani mbele yako.

Kezilahabi kwa upande wake ametumia ndoto zaidi ya Shaaban Robert. Hii ni kwa sababu zikichunguzwa kwa makini karibu riwaya zote teule za Euphrese Kezilahabi ni kama maelezo yote ya mwandishi ni ndoto. Katika riwaya ya *Mzingile*, kwa mfano, Kezilahabi anaposimulia historia ya maisha ya Kakulu ambayo ndiyo yamechukua sehemu kubwa ya riwaya hiyo, kuanzia kuzaliwa kwake kimazingaombwe, kazi zake na umashuhuri wake, anamaliza kwa kusema: Ingawa nilikuwa nusu macho, nusu usingizi siku hiyo kisa chote sasa nakikumbuka (*Mzingile*, uk.7). Diegner (2002: 45) anakubaliana na madai hayo kwa kusema kuwa hata jina la kitabu ‘Nagona’ katika lugha ya Kikerewe, lugha mama ya mwandishi wake, Euphrase Kezilahabi, ni jina la mwanamke likiwa na maana ya kukoroma au mwanamke anayekoroma. Kukoroma ni tendo linalotokea mara nyingi mtu akiwa usingizini. Sigmund Freud (1965) pamoja na wanaisaikolojia mbalimbali wanakubaliana kuwa mtu akiwa usingizini ni mara chache sana ikatokea asiote hata ndoto moja.

Pamoja na mawazo hayo ya Diegner, lakini pia katika kuhojiana na wenyeji wa Ukerewe mtafiti ameelezwa kuwa Nagona ni jina la kike lenye maana ya mtu wa yote, anayejua mambo yote. Nagona ni kila kitu. Ni mali ya kila mtu, ni mtu ambaye kila kitu kinachokuja kinampata. Nagona ni jina la binti wa kaka yake Kezilahabi anayeitwa Tungaraza (baba moja mama tofauti). Kezilahabi kwa hiyo ameipa kitabu jina la binti wa kaka yake. Kile anachokiita Diegner kukoroma kwa mujiwa wa Wakerewe ni ‘kugona’ na si nagona³⁵.

³⁵ Jeremia Magafu, miaka 65, mume wa Nagona, pamoja na mzee Biswaro Nyaonge miaka 107 (Utafiti, Machi 2019).

Riwaya ya *Mzingile* licha ya kuwa ina ndoto nyingi sana lakini Kezilahabi ametumia namna mbili tofauti kuwasilisha ndoto katika riwaya hii. Namna ya kwanza ni ile ya kawaida ya kusimulia ndoto baada ya mtu kutoka usingizini kama ilivyo katika riwaya zake tangulizi kama vile *Rosa Mistika*. Namna ya pili ni ile ambayo baada ya kusimulia tukio ndipo anaposema “Nilikuwa nusu macho nusu usingizini sasa nakumbuka”. Namna hii ya pili inavunja zaidi mpaka kati ya ndoto na uhalisia kwa maana kuwa mwotaji anakuwa kati ya kuwa macho na kuwa usingizini.

Maelezo juu ya kisasili cha kuzaliwa Kakulu kuwa inawezekana kuwa ni ndoto tu inaweza kumfanya msomaji kutokuwa na uhakika wa uhalisia wa kisasili hicho. Hata hivyo ni muhimu kufahamu kuwa mwandishi anaweza kutumia ndoto ili kuelezea uhalisia anaoufahamu vilivyo. Pamoja na hayo ndoto ya muda mfupi au ya siku moja aliyoota Msimuliaji imejumuisha mambo mengi na karibu mtukio yote ya riwaya ya *Mzingile* yamejengwa juu ya ndoto ya kisasili cha kuzaliwa Kakulu. Hii ni kwa sababu, kama anavyodai mwandishi kuwa katika ndoto kama kipengele cha uvunjivu wa kaida hakuna lisilowezakana.

Ndoto nyingine Msimuliaji anaota akiwa safarini akimfuata mwanamke kwa nyuma jangwani baada ya kuvuka mto. Anasema:

Niliota mtu akinisemesha. ...alikuwa amefunikwa na hali ya mawingumawingu au labda ukungu. Sura yake sikuweza kuitambua. Alinitazama bila kusema neno kwa muda. Nilijaribu kuinua kichwa lakini kilikuwa kizito. Nilitaka kupiga kelele lakini kinywa kilikataa kufunguka na ulimi ulikuwa mkavu. Halafu alianza kuzungumza. “Karibu!” alisema akininyooshea mikono miwili. Nilijaribu kusimama, sikuweza. Aliendelea, “Baada ya mto hakuna kingine isipokuwa kina cha fikra safi katika upweke. Umekwisha kuingia katika duara. Karibu!” Aliendelea kuninyooshea mikono huku akitabasamu. Aliniangalia nikihangaika bila nguvu za kuinuka (*Mzingile*, uk. 14).

Ndoto hii ingawa haieleweki vizuri lakini ikichunguzwa inaonekana inaendeleza mawazo ya Kezilahabi ya kusisitiza umuhimu wa kufikiri ili kufikia ufumbuzi wa matatizo na vikwazo mbalimbali. Sehemu isiyoeleweka vizuri ni pale Msimuliaji anaposhindwa kumwona na hivyo kutomtambua aliyekuwa akimsemesha ndotoni. Anasema mtu aliyekuwa akimsemesha katika ndoto alikuwa amefunikwa na hali ya mawingumawingu au ukungu na sura yake hakuweza kuitambua.

Baada ya kushuka mlima msimuliaji alipokuwa akitoka kwa Mzee, alipumzika chini ya kivuli cha mti na kulala usingizi. Aliota kuwa wako kanisani na kanisa zima lilikuwa limejaa wanafunzi. Mwandishi anasema:

Tulikuwa tukiimba kwa masikitiko...Mimi nilikuwa nikilia. Tulipotoka kanisani rafiki zangu walinipa pole kwa kushindwa mtihani. Walinisaidia kufunga mizigo. Nilipokuwa naondoka Padri mmoja alikuwa nyuma yangu akinifukuza kama mbwa "Nenda nyumbani kwa mama yako! Wewe hukuteuliwa! Wewe ni mwizi tu wa ujuzi!" Nilijikuta nimo safarini peke yangu. Fisi walikuwa wakinifuata. Nguvu za kukimbia sikuwa nazo. Nilianguka chini. Fisi walinijia mbio na walipoanza kuingiza meno yao mwenye tumbo langu nilipiga kelele halafu ghafla nikaamka (*Mzingile*, uk. 40-41).

Ndoto hii ni taswira ya historia ya maisha ya elimu ya Kezilahabi katika seminari ya Kikatoliki ya Mtakatifu Maria iliyopo Nyegezi Mwanza kutoka mwaka 1957 hadi 1966 akiwa na azma ya kusomea upadri baadaye. Nia ya kusomea upadri ilisitishwa na familia yake kwa madai kuwa hawezi kuwa padri kwa sababu kaka yake ambaye aliitwa Vicent tayari aliisha kuwa padri kwa hiyo hawawezi kuwa mapadri watoto wawili wa mama mmoja. Kwa hiyo ndoto ya Msimuliaji kufukuzwa seminari ni matokeo ya mawazo yaliyokuwa akilini mwake kabla ya uotaji wa ndoto hiyo. Hii inasadifu mawazo ya Jung (1974) juu ya ndoto kama

alivyokwishaeleza kuwa ndoto ni matokeo ya mawazo au utendaji wa akili katika kuyarudisha yale yaliyotokea katika maisha ya mtu katika mazingira yake muda kabla ya uotaji huo.

Jambo la kuzingatia ni kuwa kile kinachotokea ndotoni si lazima kifanane moja kwa moja na mawazo au tukio lilitokea kabla ya ndoto hiyo. Hata hivyo ndoto haiwezi kuwa ndoto bila kuwa na uhusiano fulani na hali fulani katika maisha halisi. Kwa kuthibitisha hili Mturo (2018: 266) anasema:

Katika ndoto kunakuwa na mazingaombwe na uajabuajabu ambapo kwa jicho la uhalisia si rahisi kukubaliana na ujumbe wa ndoto hizo. Ndoto haiwezi kuwa ndoto bila kukitwa katika uhalisi wa aina fulani wa kiyakinifu au wa kidhahania. Vivyo hivyo, ndoto haiwezi kufasiriwa pasipo kujengewa muktadha, na muktadha haujengeki katika ombwe tupu ila katika uhalisia wa aina fulani wa kiyakinifu au wa kidhania. Hivyo ndoto inaweza kuangaliwa kuwili: kama ukweli wa maisha unaojikariri katika ndoto au kama ishara inayobashiria matukio ya baadaye katika mustakabali wa maisha ya mtu.

Ndoto nyingine ni juu ya mwanamke aliyekamatwa akiwahutubia wanawake. Mwanamke huyu alipelekwa katika jengo la Starehe la Olympus ili akawaburudishe wanawaume kwa kudhalilishwa utu wake kwa kucheza dansi uchi. Kwa kukataa kucheza ingawa malipo yake ya siku moja yalikuwa makubwa kuliko mshahara wa Profesa kwa mwezi, huyu mwanamke aliyekuwa akiwakilisha Afrika aliuawa akipambana. Mwandishi anasema:

Hivyo ndivyo walivyomuua akipigana, ili neno la padre mlevi lipate kutimizwa na Afrika mpya iliyokuwa macho ipate kuzaliwa. Nilikuwa nusu macho, nusu usingizini. Nakumbuka (uk. 75).

Ndoto hii inazungumzia gharama ya kutetea utu na maadili bora ya jamii za Kiafrika. Huyu mwanamke ambaye ni mwakilishi wa Afrika na utamaduni wake

hakukubali kudhalilishwa utu wake hata kwa kupewa pesa kiasi gani. Alisimama imara na kupambana hadi kifo bila kutoa nafasi kwa heshima na utu wake kuchezeza hadharani kwa kupewa kipande cha mkate.

Msimuliaji anaelezea mfululizo wa ndoto alizoota alipolala katika nyumba mojawapo usiku wa kwanza aliporudi kijijini kwao. Anasema:

Niliota nimemkaba mtu shingo. Nikajiona nina kisu halafu damu yake ikanirukia machoni. Mara kile kichwa kikabadilika kikawa cha mzee niliyemfahamu hapo zamani....Safari hii niliota nikifanya mapenzi na mwanamke ambaye pia ghafla alibadilika kuwa ni mwanamke niliyemfahamu zamani. Niliota tena. Nyati mkali alikuwa akinifukuza. Sikuwa na nguvu za kukimbia. Niliona mti. Nilijaribu kuupanda lakini nilikuwa siendi juu. Nyati alikuja mbio alipoinama kutaka kunipiga pembe, nilipiga kelele. Sauti haikutoka. Nikashtuka na kuanguka chini ya kitanda kwa kishindo (uk. 101).

Ndoto hizo za Msimuliaji zimetokana na matukio yaliyomtokea kabla ya uotaji wa ndoto hizo. Kwa mfano mtu ambaye Msimuliaji anaota amemkata shingo na anayebadilika kuwa mtu aliyemfahamu zamani ni yule mzee ambaye amekuwa akikutana naye mara kwa mara na aliisha fanya jaribio la kumwua. Pia mzee huyo anapobadilika sura, sura hiyo mpya ni ya baba yake Msimuliaji ambaye tayari alikuwa anamfahamu hata kabla ya kuota ndoto hiyo. Mwanamke anayemwota kufanya naye tendo la ngono ni mkewe na ndiye mwanamke aliyekuwa anajitokeza kwake mara kwa mara. Pia ndiye mwanamke aliyepotea katika mazingira ya kutatanisha alipomrukia ili kumkumbatia na kumbusu.

Hata hivyo kwa kulinganisha matumizi ya ndoto kati ya Shaaban Robert na Euphrase Kezilahabi katika riwaya teule imebainika kuwa Kezilahabi kama Mwandishi fuatishi amejitenga kabisa na athari za Shaaban Robert na kazi yake kuwa na upekee na uasilia. Hapa Kezilahabi amejitenga kabisa na namna ya

uandishi wa Shaaban Robert na hata namna yake mwenyewe. Lengo lake likiwa ni kujitenga na aina yoyote ya mabaki au masalio (masazo) ya athari kwa nia ya kuwa na uhuru kamili au mafanikio binafsi (Bloom, 1973).

5.2.5 Uvunjivu wa Kaida za Kuhesabu Wakati

Katika maarifa ya kila siku wakati ni utaratibu wa mfuatano au mfululizo wa matokeo. Hii ina maana kuwa wakati ni mpito wa matokeo ya mambo yanayotukia katika maisha. Rimon (2002) anaeleza wakati kuwa ni mpangilio wa matukio katika hadithi. Wamitila (2003) anaeleza wakati kama dhana katika fasihi inayotumiwa kuelezea vipindi ambapo hali na matukio yanayosimuliwa na huwasilishaji wake hutokea.

Mulokozi (2017) akieleza dhana ya wakati kwa kuzingatia falsafa ya kijadi ya Kiafrika, anasema dhana ya wakati ni pana na ni tata. Inachanganya mambo matatu: udawari, udakizi na ufungamano na matukio. Anasema dhana ya wakati inachukuliwa kuwa dawari (duara) kwa sababu ina mzunguko usio na mwisho, yaani zamani, sasa, kesho na zamani tena. Udakizi unajitokeza kwa sababu udawari wa wakati si duara iliyotuama, bali ni mzunguko unaodakiza ambao unasonga mbele kwenye hatua ya juu zaidi badala ya kubakia pale pale. Aidha, anaendelea kueleza kuwa wakati ni kituo cha makutano kati ya muda, mahali, watu na matukio, hivyo si dhahania.

Oxford English Dictionary (2021) imeeleza wakati kama neno la kutaja ama mfuatano wa matokeo au muda ama kipindi ambapo jambo linatokea. Kwa maelezo hayo wakati unaweza kutazamwa kwa vipindi vitatu: wakati uliopita (tukio liliwahi kutokea), wakati uliopo (tukio linaendelea sasa) na wakati ujao

(tukio litaendelea baada ya sasa). Kwa mantiki hiyo, wakati unapimwa kwa matokeo yanayojirudiarudia bila kubadilika. Kipimo cha kawaida cha wakati ni siku au muda wa mzunguko moja wa dunia yetu unaoonekana kutokana na mabadiliko ya mchana na usiku. Siku moja inagawanywa katika masaa 24 na saa 1 ina dakika 60 na dakika 1 ina sekunde 60. Muda wa dunia yetu kukamilisha mzunguko moja kuzunguka jua huitwa mwaka. Mfuatano huu wa vipimo vya wakati kwa mfululizo wa matokeo huitwa wakati wa kiufuatano.

Si rahisi na haiaminiki katika uhalisia kuwa wakati unaweza kusimama, kurudi nyuma au kwenda mbele haraka tofauti na mwendo wa saa wa kawaida na wa kila siku kama ilivyoolezwa hapo juu. Inapotokea, kwa mfano, baada ya kufika saa kumi jioni masaa yakarudi nyuma na kuonekana ni saa mbili asubuhi au masaa yakaenda haraka kutoka saa mbili asubuhi na kuwa saa mbili usiku au yakasimama bila kusonga mbele wala kurudi nyumba; inakuwa ni ajabu na ni jambo linaloogopesha si wanadamu tu lakini hata na viumbe vingine pia. Kwa hiyo uvunjivu wa kaida hujitokeza pale wakati unapohesabika tofauti na mwendo wa kawaida wa kuhesabu wakati uliozoeleka. Hii ina maana kuwa katika uvunjivu wa kaida wakati unaweza kurudi nyuma, unaweza kusimama au kukimbia haraka tofauti na mwendo wa kawaida wa wakati unaofahamika. Kwa hiyo katika uvunjivu wa kaida kunaweza kuzalishwa namna tatu za kuhesabu wakati katika fasihi: wakati wa kiufuatano, wakati uliotuama au wakati tuamavu na wakati wa kiduara au uduara wa wakati.

Uchanganuzi wa data katika sehemu hii uliongozwa na mhimili wa nadharia ya Uhalisiamazingaombwe unao sema kuwa wakati na mahali vina uhusiano wa

kiduara na si wa kiufuatano. Mhimili huu unasisitiza kuwa jambo linaweza kutokea wakati mmoja, ambalo linaweza lisiwe la kwanza, na kuweza kujirudia pahali pengine kwa namna nyingine (Roh 1925). Mhimili huu ni faafu kwa sababu wakati na muda wa matukio katika vipengele fulani katika baadhi ya riwaya teule hautabiriki, kuna mduara mkubwa na unaomchanganya msomaji wa riwaya hizo. Hii ni kwa sababu nyakati zote yaani wakati wa kiufuatano, wakati tuamavu na wakati wa kiduara zinaweza kujitokeza katika riwaya moja na kwa wakati moja. Hivyo kwa kutumia mhimili huo utafiti umezingatia zaidi ujumbe uliokusudiwa na mwandishi katika uduara, utuamavu na ufuatano huo wa wakati.

5.2.5.1 Wakati wa Kiufuatano

Kwa kuegemea nadharia ya Newton (1997) wakati wa kiufuatano ndio wakati unaoonyesha uhalisia wa mambo tofauti na mawazo na mtazamo wa mtu binafsi. Ni wakati unaofululiza moja kwa moja kwa mfuatano wa matukio kutoka mwanzo kuelekea mwisho. Matukio yanaanzia mwanzo na kukua kadri muda unavyosonga mbele kama vile: kuzaliwa, utoto, ujana, utu uzima, uzee na mwisho kifo. Kwa mfano katika riwaya ya *Kufikirika*, mwandishi anaanza na kisa cha ugumba wa mfalme na utasa wa Malkia. Jitihada za kutafuta na kuzaliwa kwa mtoto zinafuata. Kuzaliwa kunafuatiwa na mtoto kupelekwa shule, kunafuatia kuugua kwa mtoto na mwisho ni kesi ya Utubusara na Ujingahasara. Kwa maana hiyo hakuna uvunjivu wowote wa kaida katika wakati wa kiufuatano. Hii ni kwa sababu ni wakati unaofahamika na unaohesabiwa kwa namna sawa na watu wote. Uvunjivu wa kaida hujitokeza tu pale wakati wa kiufuatano unapogongana na wakati tuamavu au unapoingiliana na uduara wa wakati.

5.2.5.2 Wakati tuamavu

Wakati uliotuama au wakati tuamavu ni wakati ambao hausongi mbele, ni wakati uliosimama, mambo na maisha hayasongi wala hakuna mabadiliko yoyote ingawa siku na tarehe zinasonga mbele. Mara nyingi wakati tuamavu usababishwa na hali ambapo jamii husika hushikilia ukale usiofaa na kutotaka mabadiliko yoyote. Hali ya watu katika jamii hiyo inadumu kuwa duni, kwa mfano, hakuna tofauti ya kimaisha kati ya watu walioishi miaka mia iliyopita na wanaoisha sasa katika jamii hiyo.

Ingawa wote Shaaban Robert na Euphrase Kezilahabi wametumia wakati tuamavu kwa kiwango fulani katika riwaya zao teule lakini Shaaban Robert ndiye ametumia wakati huo kwa uwazi katika riwaya ya *Kusadikika* peke yake. Hii inajidhihirisha katika kesi ya wajumbe sita waliotumwa kuzuru nchi mbalimbali ili kujifunza na kuleta elimu hiyo Kusadikika. Wakati katika kesi hiyo umetuama au umesimama. Hii ni kwa sababu umbali au muda kati ya kutumwa kwa mjumbe mmoja na mwingine ni mrefu sana. Kwa mfano, Buruhani, mjumbe wa kwanza, alitoka Kusadikika akiwa kijana na kurudi akiwa mzee kabla ya kutumwa mjumbe mwingine (*Kusadikika*, uk. 13). La ajabu ni kuwa wajumbe wote sita, licha ya kuwepo tofauti ya miaka mingi sana kati ya kutumwa kwa mjumbe mmoja na mwingine, lakini wote walikuwa wazima gerezani hata bila mmojawapo wa wajumbe wa mwanzo kufa gerezani kwa uzee. Hapo ndipo wakati uliotuama unapojitokeza katika riwaya ya *Kusadikika*. Hii ni kwa sababu katika uhalisia masaa usonga mbele daima na haiwezekani kusimama au kurudi nyuma. Hii inaonesha kuwa, kwa habari ya kutumwa kwa wajumbe hawa wakati haukusonga mbele bali ulisimama au kutuama.

Katika uchawi na mazingaombwe kwa kutumia mhimili wa Uhalisiamazingaombwe ulielezwa hapo juu unaosisitiza kuwa jambo linaweza kutokea wakati mmoja, ambalo linaweza lisiwe la kwanza, na kuweza kujirudia pahali pengine kwa namna nyingine. Hii ni kwa sababu wakati na muda wa matukio katika vipengele fulani katika baadhi ya riwaya teule hautabiriki, kuna mduara mkubwa na unaomchanganya msomaji wa riwaya hizo. Nyakati zote yaani wakati wa kiufuatano, wakati tuamavu na wakati wa kiduara zinaweza kujitokeza katika riwaya moja na kwa wakati moja. Hivyo kwa kutumia mhimili huo utafiti umezingatia zaidi ujumbe uliokusudiwa na mwandishi katika utuamavu huo wa wakati katika riwaya ya *Kusadikika*.

Wakati uliotuama katika nchi ya Kusadikika kulimaanisha kuwa hakukuwa na mabadiliko yoyote yaliyotokea Kusadikika kutokana na taarifa au elimu iliyoletwa na wajumbe hao sita. Hii inaonesha kuwa katika nchi ya Kusadikika wakati ulikuwa umetuama kwa sababu elimu iliyoletwa na wajumbe wote sita haikupokelewa na kusadikika ikabakia pale pale ilipokuwa bila ya kupiga hatua yoyote kimaendeleo. Kwa mujibu wa Shaaban Robert wakati unatakiwa uhesabike kutokana na mabadiliko yanayotokea katika jamii. Kama jamii haitakuwa ikipiga hatua yoyote kimaendeleo: leo na jana, mwaka huu na mwaka jana, karne hii na karne iliyopita hazitakuwa na tofauti yoyote kwa sababu hali itakuwa ni ile ile. Kinachozingatiwa hapa na Shaaban Robert kwa kuwatumia wajumbe hawa sita ni kukamilika kwa tukio na si muda unaotumika katika kufanya tendo husika. Kwa hiyo basi, umuhimu wa wakati ni kama wakati utatumika kuzalisha kitu fulani au kutumika katika kumfanya binadamu kupiga hatua kimaendeleo kutoka sehemu A kwenda sehemu B.

Shaaban Robert ametumia wakati tuamavu katika riwaya ya *Kusadikika* ili kuzungumzia baadhi ya tamaduni zilizopitwa na wakati. Inaonekana Shaaban Robert alikuwa anasumbuliwa sana na wazo la Waafrika kushikilia baadhi ya mila ambazo kwake alizona kuwa hazifahia au zimepitwa na wakati. Hii ni kwa sababu, licha ya suala ili kujitokeza katika riwaya ya *Kusadikika* linajitokeza katika riwaya ya *Adili na Nduguze* na hata katika riwaya ya *Kufikirika*. Katika riwaya ya *Adili na Nduguze*, mfalme wa mji wa Fahari anakataa mawazo ya Mrefu juu ya kuachana na ibada ya mizimu. Pia katika riwaya ya *Kufikirika* mfalme anakataa mtoto wake asifundishwe elimu ngeni. Anahimiza afundishe juu ya historia ya Kufikirika, habari za watu wa kale, habari za uganga, sadaka na nadhiri, uwezo wa makafara, majini na mashetani (*Kufikirika*, uk. 22). Zaidi ya yote mtoto huyo anapougua inatakiwa kafara ya damu ya mwerevu na mjinga ili kumponya. Katika riwaya ya *Kusadikika* viongozi wanakataa mawazo yote mapya yaliyoletwa na wajumbe sita. Mawazo hayo yalikuwa mazuri sana na yangefuatwa yangeleta maendeleo makubwa kwa nchi ya Kusadikika. Mawazo hayo yanakataliwa kwa sababu ni kinyume cha utamaduni wao, yaani mazoea yao tangia mababu.

Kinachoonesha kuwa Shaaban Robert alitaka mabadiliko ni kuwa katika riwaya ya *Adili na Nduguze* ibada ya mizimu ilishindwa kwani mji wa Fahari uligeuka mawe na miji mingine kugharikishwa. Mwelekevu, kama lilivyo jina lake, ndiye pekee aliyepona na kupewa chuo mbili, yaani Biblia na Kurani. Hii ni ishara ya kushindwa kwa baadhi ya tamaduni zisizofaa za asili na nafasi yake kuchukuliwa na Ukristo na Uislamu. Pia katika riwaya ya *Kufikirika* elimu yote ya asili aliyopatiwa mtoto wa mfalme ilimfanya augue na hakuponywa na kafara ya damu

ya wanadamu, yaani mjinga na mwerevu, bali hospitalini. Hii ina maana kuwa kutoa damu au maisha ya watu kama kafara ni ujinga na ukale wa kikatili usiofaa. Kinyume chake kumpeleka mgonjwa hospitalini ni bora zaidi. Zaidi ya yote katika riwaya ya *Kusadikika* Kushinda kwa karama katika kesi iliyokuwa inamkabili kunaonesha ushindi wa kupokea mazuri mapya kwa maendeleo na kuachana na kushikilia ukale na tamaduni zilizopitwa na wakati.

Anachoeleza Shaaban Robert ni kuwa kila jamii ina utamaduni wake kulingana na mazingira ya jamii hiyo. Utamaduni hutofautiana baina ya jamii moja na nyingine. Hata hivyo tamaduni zinaweza kuathiriana na kufanya vipengele vya utamaduni wa jamii moja kuwa sehemu ya utamaduni wa jamii nyingine kulingana na mabadiliko kiwakati. Hii ina maana kuwa kama kuna mazuri yaliyoko katika jamii yaendelezwe na mabaya yaachwe. Wakati huo huo jamii moja isisite kuiga na kutumia mambo mazuri yaliyoko katika utamaduni wa jamii nyingine.

Coker (1990) akishadidia mawazo hayo anasema:

Safari kuelekea maisha ya kesho ni muhimu iongozwe na hekima na busara za jana ya jamii husika. Hata hivyo wazee wenye hekima wanasisitiza kuwa tamaduni huwa zinabadilika. Hatujui mambo yote katika maisha ya leo ingawa bado tunajifunza...Kwa hiyo tuko tayari kujifunza mambo mapya na kuachana na ya kale yasiyo na faida. Kama unavuka mto mkubwa ili kumuoa mke ni lazima huwe tayari kwa hatari ya kusafiri usiku kwa mtumbwi.

Coker anasema kuwa ingawa tunayafahamu yaliyopita katika jamii zetu lakini safari ya maisha ni kujifunza siku zote. Hii ni kwa sababu hata leo tunayoiishi hatuifahamu vizuri na hivyo tuwe tayari kubadilika. Tuyaache mabaya ya nyuma yanayofahamika tayari kwa kujifunza mazuri yenye faida kwa maisha ya kesho yawe yanatoka ndani ya jamii yetu au nje yake. Jamii inapokataa kupokea mazuri

yaliyoko katika utamaduni wa jamii nyingine kwa kushikilia ukale usio na faida jamii hiyo itabaki nyuma daima. Shaaban Robert analizungumzia hili na kulisisitiza sana kwa kutumia mbinu ya wakati kuelezea tamaduni tuamavu.

Mbinu ya wakati katika uvunjivu wa kaida ni jambo la kawaida kwani hudokeza mwendo mrefu wa mwanadamu katika kusaka mafanikio ambayo hatimaye hufikiwa baada ya mapambano dhidi ya vizuizi vingi ambavyo hutanzuliwa kwa namna ya kimazingaombwe. Hilo ndilo lilikuwa kusudi na matarajio ya Kusadikika katika kuwatuma wajumbe sita kwenda nchi mbalimbali ili kujifunza na kuleta elimu ambayo kama ingepokelewa na kutumiwa vizuri Kusadikika ingepiga hatua kwa kusahau jana na kuishi leo na kesho. Hata hivyo watawala wa Kusadikika hawakuwa tayari kuachana na jana yao na hivyo kubakia katika wakati usiosonga mbele, yaani wakati uliotuama na kufurahia hali kuwa hivyo hivyo ilivyokuwa juzi na jana na kutopenda kuona leo wala kufikiria kesho ya mambo mapya na maendeleo katika nchi yao.

Mkumbwa (2012) anapozungumzia dhana ya wakati kwa mawazo ya kihemenitiki anasema kuwa wakati waweza kupelekwa mbele au kurudishwa nyuma kwa lengo la kupeleka ujumbe na si kueleza hali fulani katika wakati huo. Mukstadha wa wakati hubeba maana ya maisha na mazingira ya kijiografia. Kwa mfano mwandishi anaweza kutumia wakati kubainisha mwachano wa kimaendeleo baina ya mtu na mtu, jamii na jamii, taifa na taifa na hata baina ya mataifa ya Afrika dhidi ya yale ya Wazungu. Hii ndiyo maana wajumbe sita waliotumwa na Kusadikika kwenda nchi nyingine walikuta nchi hizo zimepiga hatua za kimaendeleo kuliko nchi yao. Kilichofaa Kusadikika kufanya, sawa na nchi nyingine yoyote ile, ni kupokea mawazo hayo na kuyafanyia kazi kulingana

na mazingira yao na si kukataa kila wazo jipya kwa madai tu kuwa mawazo hayo ni kinyume na utamaduni au mazoea yao tangia enzi za mababu zao.

Shaaban Robert ametumia wakati tuamavu kwa lengo la kutaka kufikisha ujumbe maalumu kwa jamii za Kiafrika za wakati huo na kutabiri hali inayotakiwa iwe kwa jamii hizo baada ya kujipatia uhuru wake. Ikumbukwe kuwa Shaaban Robert aliandika Riwaya ya *Kusadikika* wakati nchi nyingi za Afrika zikiwa katika harakati za kudai uhuru wake. Wakati huo baadhi ya Waafrika walienda nchi mbalimbali za Ulaya kusomea taaluma mbalimbali kwa ajili ya kurudi kuongoza na kuendeleza nchi zao zilizokaribia kujitawala. Watu hao ni sawa na wajumbe sita waliotumwa na nchi ya Kusadikika kwenda nchi mbalimbali ili kujifunza mambo yaliyowezezana kuletwa kwa manufaa ya nchi na watu wake. La kushangaza ni kukataliwa kwa ujumbe wote ulioletwa na wajumbe hao.

Kuishi kwa wajumbe hao sita na wote kuwa kizuizini na kuja kutoka wakiwa hai bila hata mmoja kufa kwa uzee, ingawa muda kati ya kutumwa kwa mjumbe mmoja na mwingine ni mrefu mno, ndicho kidhihirisho cha wakati tuamavu katika riwaya ya *Kusadikika*. Hivyo, kufanya wakati huo kuwa wa kimazingaombwe. Hii inaonyesha kuwa hakukuwa na mabadiliko yoyote ya kimaendeleo katika nchi ya Kusadikika tangia enzi za kutumwa kwa mjumbe wa kwanza hadi mjumbe wa sita hata mpaka wakati wa kukamatwa kwa Karama. Hii inamaanisha kuwa hali ya taifa hilo la wakati uliopita haina tofauti na leo na wakati ujao hali itakuwa hivyo hivyo. Hii ilisababishwa na Kusadikika kuwa na viongozi wasiopenda mabadiliko pamoja na kushikilia tamaduni zao au ukale uliopitwa na wakati.

Miongoni mwa mambo makuu yaliyoelezwa na ujumbe wa wajumbe sita, ambayo yalikuwepo katika jamii ya Shaaban Robert na Tanganyika ya wakati huo, ambayo yalidumu kwa muda mrefu bila mabadiliko yoyote na kufanya ione kane kuwa wakati umetuama katika nchi ya Kusadikika ni kuwa watu walikuwa: wanashirikiana nyumba moja na mifugo, waliishi katika nyumba za makuti, barabara za vumbi, bila madaraja ya kuvuka mito, bila bandari wala viwanja vya ndege; kunywa maji yasiyo safi na salama, kilimo kisichostawishwa, kutokwepo kwa hospitali wala vituo vya afya, kuwa na vita vya mara kwa mara kati ya jamii moja na nyingine, serikali zenye kutumia nguvu na mamlaka yasiyo kiasi, wabadhirifu wa mali ya umma, kutumia mali katika ngoma na tafrija za kufukarisha, kuoja na kuachana kila siku, kuoja wake wengi, kuzaa watoto wengi wasioolelewa kingwana kwa kutofunzwa dhima zao katika dunia pamoja na uvivu na uharibifu wa mazingira. Kama hali hiyo iliyokuwa nyuma itakuwa haijabadilika hata leo na miaka ijayo hali itakuwa hivyo hivyo basi wakati katika jamii hiyo itakuwa imetuama.

Shaaban Robert anatumia kukataliwa kwa ujumbe wa wajumbe sita kuonesha uhalisia wa jamii nyingi za Kiafrika kwa mfano wa kutoendelea kwa muda mrefu na kubaki pale pale kwa kushikilia tamaduni zisizofaa na hivyo muda hausongi. Kwa mfano, jamii nyingi za kifugaji licha ya kuwa na ng'ombe wengi lakini bado zinaishi katika maisha duni ikiwa ni pamoja na nyumba mbovu huku wakioa wake wengi na kuzaa Watoto wengi wasioweza kuwasomesha. Shaaban Robert anataka ifahamike kuwa kusonga kwa miaka sio muhimu, muhimu ni kufanya kazi kwa bidii ili kupiga hatua mbele za maendeleo na kujifunza mapya mazuri kutoka kwa jamii zingine. Shaaban Robert anasisitiza hili kwa kusema kuwa,

‘Matendo makubwa huchukua wakati mwingi kukamilika. Kwa hivi haifai kuchelewa. Kila dakika moja, na kila nukta moja, ni hazina; isipite bila kutiwa alama kwa tendo jema’ (*Kusadikika*, uk. 39).

Shaaban Robert anasema kuwa kushikilia ukale usio na faida ni hasara. Mtu anaweza akakua kimwili na kuishi miaka mingi, lakini kama hapigi hatua ya kimaendeleo, anaweza, kwa mujibu wa Shaaban Robert, kuhesabika kuwa ana miaka sifuri ingawa ana miaka mia ya kuishi; wakati huo huo mtu anaweza kuwa na umri mdogo lakini akahesabiwa kuwa na miaka mingi kulingana na maendeleo aliyojiletea yeye binafsi na taifa lake kwa ujumla. Shaaban Robert anasisitiza hili kwa kumtumia Karama na Majivuno waziri Mkuu wa Kusadikika. Kwa mfano, Majivuno anaposhikilia ukale kwa kusema kuwa hekima ni kitu adimu kupatikana na mtu asiye mvi, yaani asiye na miaka mingi ya kuishi. Weusi wa nywele za mshtakiwa, yaani karama, waonyesha waziwazi ujinga alio nao (*Kusadikika*, uk. 10). Karama anajibu kwa hekima mawazo haya yaliyopitwa na wakati kwa kusema kuwa, ‘Elimu ilipokuwa haijulikani duniani, mvi zilihesabika kama alama ya hekima. Fikara hii ilikuwa njema sana, lakini wakati wake umepita wala haurudi tena. Sasa kama mtu hakuelimishwa, mvi zake hazihesabiwi kama dalili ya hekima. Jambo lisilobadilika ni kuwa mzee anastahili heshima ya kijana siku zote’ (*Kusadikika*, uk. 10).

Sengo (1975: 61) anakubaliana na mawazo hayo kwa kusema kuwa:

Baadhi ya watu wana wazo kuwa la zamani ndilo jema na lolole geni ni duni. Jambo la kumaizi ni ukweli kwamba dunia yetu inabadilika kwa haraka. Mabadiliko haya huenda na wakati. Ili jamii inayohusika na mabadiliko haya iweze kufuatana na wakati, jamii hiyo inapaswa kuwa na uwezo wa kuchuja bora ya jana na bora ya leo kuunganishwa pamoja kwa usalama zaidi. Kwa hivyo si vyema kushikilia kwamba yaliyopita ndiyo mema tu au yajayo tu ndiyo yenye manufaa.

Mawazo hayo ya Sengo yakiunganishwa na ya Shaaban Robert, jamii inaaswa kuwa, maendeleo si jana wala leo au umri wa kuishi, bali matendo mema na hekima na busara ya mtu ndiyo yazingatiwe katika kutoa maamuzi ya kipi bora cha kufaa kufuatwa kwa maendeleo ya jamii husika.

5.2.5.3 Uduara wa Wakati

Uduara wa wakati ni wakati usiofuliza moja kwa moja. Unaweza kwenda haraka, ukasimama au kurudi nyuma. Wakati na mahali vina uhusiano wa kiduara na si wa kistari, yaani jambo linaweza kutokea wakati mmoja, ambalo linaweza lisiwe la kwanza, na kuweza kujirudia pahali pengine kwa namna nyingine (Khamis, 2003: 82; Gromov, 2009:126). Hii ina maana kuwa katika uduara wa wakati matukio yanaweza kujirudia na tukio la mwisho likawa la kwanza na la kwanza kuwa la mwisho na kujirudia tena (www.drummerword.com/forums/index.php?).

Uduara wa wakati ni wakati unaoonekana kama ni wa kiduara wa kimzunguko ambao sio lazima uwe unaonesha kuelekea mwisho fulani au jambo fulani, lakini ujirudia na kujizungusha katika uduara wa matukio (Garnier, 2013: 81-83).

Uduara wa wakati umejumuishwa katika uvunjivu wa kaida za wakati kwa sababu katika uduara wa wakati mtu anaweza akaishi maelfu ya miaka, pia mtu anaweza kufanya matukio ya karne nyingi lakini akawa ameishi siku moja tu duniani; jambo ambalo ni kinyume na uhalisia wa kawaida katika kuhesabu wakati (Biblia Takatifu: Zaburi 90: 4, 2Petro 3: 8; Kurani Tukufu: Surat Haji, 47).

Matukio katika uduara wa wakati huingiliana na kubadilika karibu kila siku, yaani mambo mapya huzaliwa kila dakika. Pia si lazima mtu asafiri kuona

matukio katika upande mwingine mwa dunia, bali kwa kutumia teknolojia na maendeleo ya kisasa, kwa mfano simu, mtu anaweza kuona matukio yanayotokea kote duniani kwa muda mfupi sana.

Shaaban Robert hakutumia uduara wa wakati katika riwaya zake teule, kinyume chake Kezilahabi ametumia sana uduara wa wakati katika riwaya za *Nagona* na *Mzingile*. Hii ina maana kuwa Kezilahabi kama mwandishi fuatishi kwa kutumia uduara wa wakati katika riwaya za *Nagona* na *Mzingile* ameonsha upekee na uasilia kwa kutoathiriwa na Shaaban Robert. Bloom (1925) anasema mwandishi fuatishi huonesha upekee na uasilia kwa kujitenga kabisa na namna ya uandishi wa msanii tangulizi na hata namna yake mwenyewe. Lengo la msanii fuatishi kuonesha uasilia na pekee kati utunzi ni kujitenga na aina yoyote ya mabaki au masalio (masazo) ya athari kwa nia ya kuwa na uhuru kamili au mafanikio binafsi.

Msimuliaji katika riwaya ya *Nagona* alipofika katika nyumba ya Padri katika mji wenye watu wasioonekana kwa macho wala kuongea, anaomba maji kwanza kabla ya kunywa kileo alichomiminiwa na Padri. Padri anasema hakuna maji kwa sababu maasi yamegeuza maji kuwa damu; na kuwa ni karne ya nne yuko katika mji huo. Mwandishi anasema:

Akatabasamu akasema, “Hakuna maji hapa. Maasi ya karne nne yamegeuza maji ya mji huu kuwa damu tupu. ... Mimi ni Padiri wa mji huu. Hii karne ya nne niko hapa...Najua huelewi. Lakini utaelewa siku ikifika...Nashukuru umefika mapema. Lakini kama isingekuwa ajali usingefika mapema...Umetumia karne moja tu kufika hapa. Isingekuwa hiyo ajali ungetumia karne zote nne (*Nagona*, uk. 4).

Maelezo hayo ya Padri yanaonesha kuwa Kezilahabi ametumia uduara wa wakati katika riwaya ya *Nagona*. Hii ni kwa sababu si rahisi katika uhalisia mtu kuishi

kwa muda wa karne nne wala kusafiri kwa karne nzima. ‘Mimi’ anashangazwa sana na maelezo hayo ya Padri. Yeye kwa upande wake anaona ni muda mfupi sana ametumia kufika mahali hapo. Katika uduara wa wakati kuna uvunjivu mkubwa wa kaida za kuhesabu wakati. Muda unaweza kwenda mbele haraka sana, ukasimama au kurudi nyuma. Kwa mfano, Msimuliaji alipofika katika kundi la waliokuwa wanazungumza na roho zao anaambiwa na kiwiliwili asipoteze wakati hivyo aanze kuzungumza na roho yake. Mwandishi anasema:

Anza! Muda ambao tumekwisha tumia katika mazungumzo yetu ni karibu miaka kumi. Usiendeleo kupoteza muda. Miaka kumi! Lakini nimefika hapa dakika kumi tu zilizopita! Kosa ni lako. Umekuwa msahaulifu sana na unazungumza kama mtu asiye na akili. Inachukua miezi kutamka neno moja (*Nagona*, uk. 16).

Kiwiliwili kinamwambia msimulizi kuwa atakapojua kuzungumza na roho yake vizuri mambo yatakwenda kwa haraka kidogo. Kuwa mazungumzo yaliyokwisha yamechukua miaka kumi na mitano. Kuwa huo si mwanzo mbaya (*Nagona*, uk. 17). Wakati kiwiliwili kinapozungumzia miaka kumi na mitano, msimuliaji anaona kuwa ni tukio la dakika kumi na tano tu.

Maelezo hayo yanaonyesha kuwa watu wawili wanaweza kuwa mahali pamoja na kwa wakati mmoja lakini wakahesabu muda kwa namna tofauti. Hii ni athari ya utandawazi inayoonekana katika uandishi unaotumia uvunjivu wa kaida za kuhesabu wakati. Athari hizo zinazua migongano ya kuhesabu muda kati ya wahusika hasa wakati wengine wanapotaka kuhesabu wakati kiufuatano na wengine kiduara. Kwa mfano, Wakati ‘Mimi’ anafikiri kuwa ametumia dakika kumi Kiwiliwili kinazungumzia miaka kumi. Kwa kiwiliwili wakati unasonga mbele haraka zaidi wakati kwa ‘Mimi’ wakati unakwenda kwa namna ya kawaida

ya kuhesabu saa. Hii inazidi kudhihirisha kuwa Kezilahabi ametumia uvunjiu wa kaida za wakati katika riwaya ya *Nagona*.

Licha ya Kezilahabi kutumia wakati kimazingaombwe kwa lengo la kutaka kubainisha kuwa matumizi ya wakati yanaweza kutofautiana kati ya mtu na mtu au jamii moja na nyingine, lakini pia amekusudia kusesitiza umuhimu wa kutumia wakati kwa busara na kutokukubali kupoteza muda bila sababu ya maana. Suala la kujali na kuwa mwangalifu kutumia muda kwa faida ni miongoni mwa masuala yanayomshughulisha sana Kezilahabi katika uandishi wake. Kezilahabi amefananisha wakati na titi la nyati ambalo hukamuliwa kwa shaka (*Nagona*, uk. 44).

Kezilahabi anazungumzia tabia iliyojengeka sana katika jamii zetu ya kuzungumza sana au kusubiri tukio fulani litokee na kukaa kulijadili tu tukio hilo kwa muda mrefu bila kufikiri kufanya jambo lolote la kimaendeleo. Wanaozungumza tu bila kufikiri amewafananisha na wasahaulifu na watu wasio na akili. Hayo maelezo ni sawa na mawazo ya Spencer, akinukuliwa na Mihanjo (2004: 13) juu ya uwezo wa kufikiri wa mtu mweusi. Anasema:

Wanadamu wa rangi nyeusi wamejaliwa kuwa na akili isiyoweza kujizamisha katika uwazaji mtupu. Akili ya mwafrika imejifungia katika mitokezo tu. Yaani akili yake hutegemea hisia zaidi kuliko mawazo. Kwa hiyo akili ya mwafrika hushindwa kupokea fikra za kifalsafa, fikra ambazo ni za daraja la juu.

Hegel akinukuliwa na Mihanjo (2004: 13-14) anayashadidia mawazo hayo ya Spencer kuwa Afrika imezama katika dimbwi la giza ambapo akili yake haijafikia kwenye kiwango cha fikara pembuzi au fikara za jumla. Kezilahabi anasisitiza kuwa wanaozungumza bila kufikiri ni sawa na mtu anayechukua miezi kutamka

neni moja. Anasema kuwa ili kuipata kweli na kuimiliki ni lazima kufikiri, bila kufikiri kweli inaambaa na kupotea (*Nagona*, uk. 44).

Watu wasiofikiri juu ya matatizo yanayawakabili wao binafsi na yanayoikumba nchi yao, wasiofikiri juu ya namna ya kutatua migongano iliyopo na wasiofikiri juu ya hali ya maisha yao kwa ujumla wanabaki kuwa watu wa kubururwa tu na watu wengine (*Nagona*, uk. 20).

Zaidi ya yote Kezilahabi ametumia uvunjivu wa kaida ya wakati kueleza kuwa kuupata au kuijua kweli si jambo rahisi na inahitaji muda mwingi sana na uangalifu mkubwa sana hata baada ya kuipata. Anazungumzia hili pale Msaka paa na wenzake wanapoingia na wanapotoka kwa mfalme aliyemficha paa katika himaya yake. Mwandishi anasema:

“Hatuna tena cha kuficha!” mmoja alisema. “Asikujue!” mwingine alimpigia kelele paa...Sasa ghafla tulijiona wenye maarifa. Tulijihisi hivyo, lakini hatukujua kwa nini. “Najihisi nimezeeka sana,” Nabii alisema. “Mimi pia” wengine waliongezea mmoja mmoja. “Tumekaa hapa kwa muda gani?” niliuliza. “Karibu miaka mia nne na hamsini,” paa alijibu (*Nagona*, uk. 34).

Hawa wasaka paa, inaonekana kwa hesabu za siku za kawaida, walikaa wakifanya mtihani wa kumpata paa kwa mfalme aliyekuwa na paa katika himaya yake kwa muda wa siku tano. Lakini wanapotoka kwa mfalme huyo siku ya tano wakiwa wamepata maarifa yaani kweli wanajihisi wamezeeka jambo linalowafanya waulizane kuwa wamemaliza muda gani kwa mfalme huyo. Paa anawajibu kuwa ni miaka mia nne hamsini. Siku tano kuwa miaka mia nne na hamsini ni uvunjivu wa kaida za kuhesabu wakati.

Kezilahabi ametumia uvunjivu wa kaida za kuhesabu wakati hapa ili kueleza kuwa kuipata au kuijua kweli ni kazi inayohitaji kufaulu mitihani na majaribu mengi na mazito yanayoweza kugharimu maisha na hata kutumia muda wote wa maisha yako. Anakazia jambo hili pale EGO, ID na SUPEREGO walipotumwa na serikali kukagua viwanda vilivyokufa na vilivyokuwa vikifanya kazi kwa hasara (*Nagona*, uk. 23). Walikagua viwanda hivyo wakiongozwa na Kizee na kubaini ukweli. Kizee kiliwafunza kuwa ukweli unapatikana kwa njia moja tu, kufikiri. Baada ya kufunzwa kufikiri na kizee na kufahamu chanzo cha hali ngumu ya uchumi katika nchi za ulimwengu wa tatu walijiona wazee wenye mvi. Mwandishi anasema:

Tulitazamana. Kizee kilikuwa kimetufunza jambo moja-kufikiri. Tulishangaa tulipojiona wazee wenye mvi. Kitu gani kilitokea kwetu! Kizee tulikuwa nacho leo tu! Maisha yanakwenda mbio kiasi hicho! (*Nagona*, uk. 23).

Si jambo la kawaida maisha ya siku moja tu mtu kujiona amezeeka na kubaini kuwa tayari ni mzee mwenye mvi. Kezilahabi anazidi kutumia uduara wa wakati kuvunja kaida za kuhesabu wakati kusisitiza kuwa njia pekee ya kuondokana na tatizo la njaa na migogoro ya kiuchumi iliyoikumba dunia hasa nchi za ulimwengu wa tatu ikiwemo Tanzania ni kufikiri. Bila kufikiri matatizo hayo yataidumu kuwepo.

Uduara wa wakati unaonekana tena wazee wawili wachungaji wa ng'ombe yaani Nabii na Mtume wanapomweleza Mwindaji msaka paa kuwa wamekuwa wakimsubiri kwa miaka elfu mbili. Muda huu wa kusubiri ni wa kimazingaombwe kwa sababu umri wa kawaida wa mwanadamu si zaidi ya miaka 120 na Biblia Takatifu inasema kuwa siku za miaka yetu ni miaka sabini au themanini tukiwa na nguvu (Zaburi, 90: 10). La ajabu ni kuwa hawa wazee

wanavunja uhalisia unaofahamika kwa kutumia miaka elfu mbili kwa kumsubiri Mwindaji Msaka Paa. Kizee kinapozungumza na Ego, ID na SUPEREGO anasema imewachukua muda mrefu kufika hapo wakati wao hawana uhakika na muda huo. Kizee kinasema:

Tumekuwa tukiwasubiri, isipokuwa tunashangaa kwa nini imewachukua muda mrefu kufika hapa,...Miaka kumi kufika hapa! Na ingewachukua muda mrefu zaidi kama ndege yenu isingeanguka na kuteketea. Ajali hufanya mambo yawe (*Nagona*, uk. 19).

Pia Kizee kinapomaliza kuwatembeza wataalamu hawa katika baadhi ya viwanda, wataalamu hawa wanashangaa kujiona wazee wenye mvi. Mwandishi anasema: Tulishangaa tulipojiona wazee wenye mvi. Kitu gani kilitokea kwetu! Kizee tulikuwa nacho leo tu! Maisha yanakwenda mbio kiasi hicho! Si rahisi katika maisha ya kawaida kutofahamu kuwa miaka inakwenda na mtu kushtukia amezeeka na kuwa na mvi kichwani akidhani kuwa ni siku moja tu.

Uduara mwingine wa wakati unaonekana Msaka Paa pamoja na wazee wanne walipokuwa kwa mfalme ambaye inaonekana Paa alikuwa amejificha ndani ya milki yake. Kizee anawaambia: Nimekuwa nikiwasubiri. Huu sasa ni mwaka wa milioni na moja. Lakini nilijua mtafika kwa sababu mkisakacho maishani kiko hapa (*Nagona*, uk. 29). Muda huo wa kusubiri ni mrefu mno na hakuna binadamu anayeweza kuishi miaka hiyo yote akisubiri, hivyo muda huo ni wa kimazingaombwe.

Msaka paa pamoja na wazee wanne wakiwa bado wako kwa mfalme ambamo Paa amejificha wanaona kuwa kukaa kwao kwa masaa ndani ya ngome hiyo walipokuwa wakipelekwa sasa na msichana katika bonde la mauti ni kama miaka hamsini. Masaa kuwa miaka na miaka kuwa masaa ni uvunjivu wa kaida ya

kuhesabu wakati ambao hauwezi kuelezeka katika uhalisia wa kawaida. Hata hivyo, kwa kutumia mhimili wa uhalisiamazingaombwe unao sema kuwa wakati na mahali vina uhusiano wa kiduara na si wa kiufuatano hayo yote yanawezekana. Mhimili huo ndio umetumika kuchanganua data katika sehemu hii kama ilivyoelezwa awali. Mhimili huo ni muhimu kwa sababu unasaidia kuhakiki kazi za fasihi zinazoweza kumchanganya msomaji kwa kutumia nyakati zote yaani wakati wa kiufuatano, wakati tuamavu na wakati wa kiduara katika riwaya moja na kwa wakati moja. Hivyo kwa kutumia mhimili huo utafiti umezingatia zaidi ujumbe uliokusudiwa na mwandishi katika uduara, utuamavu na ufuatano huo wa wakati.

Uvunjivu wa kaida ya kuhesabu wakati unaonekana zaidi mhusika wengi katika mmoja anapokwenda kuungama dhambi kwa padri. Wengi katika mmoja anasema aliungama mara ya mwisho karne mbili zilizopita lakini anapoulizwa umri wake anajibu sina. Na anadai kuwa wakati pekee ndio uwezao kulijibu swali hilo (*Nagona*, uk. 47). Ni ajabu kwa mtu aliyeungama mara ya mwisho karne mbili zilizopita kutokuwa na umri hata wa siku moja. Miaka zaidi ya elfu mbili za mtu kuwa miaka sifuri ni hesabu za miaka isiyoelezeka wala kufumbulika kiuhalisia.

Kezilahabi amemtumia mhusika wengi katika mmoja, kwa kuvunja kaida za kuhesabu wakati kuzungumzia matukio ya nyakati tofauti ambayo hayafungwi na wakati fulani maalum katika historia ya maisha ya mwanadamu. Alitaka kueleza juu ya dhambi za wakati uliopita, uliopo na ya wakati ujao. Hivyo kwake umri wa mhusika si kigezo cha kuzingatia bali kuwepo kwa dhambi hizo na madhara yake pamoja na uwezekano wa kusamehewa ndiyo mambo ya kuangalia. Hii ni kwa

sababu wengi katika mmoja si mtu fulani maalum katika kipindi fulani maalum bali ni kiwakilishi tu cha matendo maovu yaliyotendwa wakati uliopita, yanayotendeka sasa na yanayotarajiwa kutendwa.

Kezilahabi ametumia pia uduara wa wakati katika riwaya ya *Mzingile* pale mwandishi anapozungumzia sayari kuzunguka jua, dunia katika mhimili wake na binadamu pia kufikiriwa kuwa ana mhimili wake anaouzunguka. Katika mhimili huo binadamu anajiviringisha mwenyewe akiwa anazunguka jua lake lisilioonekana. Mhimili huo unakaribia kuporomoka kutokana na ukame wa hofu ya kifo, ukame wa wema na upendo, wa fikra na wingi wa uchoyo, kiburi, uonevu, ubinafsi, ubaarakala na maasi (*Mzingile*, uk. 8). Hii ina maana kuwa kila mtu kwa mujibu wa Kezilahabi, amejawa na ubinafsi na hakuna anayemjali mwenzake na hivyo kila mmoja anabeba matatizo yake mwenyewe na hakuna anayefikiria kumsaidia mwingine. Matokeo yake kila mmoja anahesabu muda kivyake bila kuzingatia utaratibu wa kawaida wa masaa au wa siku unaotokana na dunia kuzunguka jua au kujizungusha katika mhimili wake; Jambo hilo linaelekea kumletea binadamu maangamivu makubwa, yaani kuporomoka kwa mhimili wake.

Uduara wa wakati unazidi kuonekana wakati Msimuliaji anapokutana na Kizee pangoni Kizee kikiwa kama mfadhili, Msimuliaji anasema kuwa siku chache zilizopita alikuja kumweleza Kizee habari za mazishi. Kizee kinakanusha na kusema karne nyingi zimepita tangu alipopelekewa habari za mazishi. Hapa kwa Msimuliaji muda unaonekana kwenda kwa namna ya kawaida ya siku yaani kiufuatano lakini kwa Kizee muda unahesabika kwa namna tofauti. Siku

zinazoonekana chache kwa Msimuliaji ni karne nyingi kwa Kizee (*Mzingile*, uk. 57).

Kezilahabi ametumia sana uduara wa wakati kwa sababu katika usasabaadaye kuna mchanganyiko mkubwa sana wa mambo unaoletwa na utandawazi pamoja na maendeleo ya sayansi na teknolojia. Katika utandawazi kuna uwezekano mkubwa wa watu ndani ya nchi moja wakaishi katika nyakati na dunia mbili tofauti ingawa wanakaa pamoja. Kwa sababu ya sayansi na teknolojia ya kisasa kuna uwezekano wa mtu kusafiri na kuyatangulia mabadiliko ya saa yanayotegemea jua. Kwa mfano, Mfuasi kukunjua mguu na mguu huo kukunjuka kwa kasi ya ajabu hadi nchi ya Sibara iliyo umbali wa mwendo wa miaka saba na kurudi na kiko cha mfalme kwa muda mfupi sana (*Nagona*, uk. 33). Kwa namna hiyo Kezilahabi anaziandikia jamii hizo mbili zilizo pamoja yaani; wale wanaoona wakati kama ni wakiufuatano na wale wanaoona wakati kama ni wa duara. Hii ndiyo maana ‘Mimi’ yaani Msimuliaji katika riwaya ya *Mzingile* anapomwambia Mfadhili au Mzee kuwa siku chache zilizopita alimpelekea taarifa za msiba, Mzee anashangaa na kusema kuwa hajasahau kwani tangia apelekewe taarifa za msiba ni karne nyingi zimepita.

Hii ina maana kuwa kama Mzee ni Mungu mwenyewe basi alianza kupelekewa au anazifahamu taarifa za msiba hata kabla ya kuzaliwa Msimuliaji. Pia ‘Mimi’ katika riwaya ya *Nagona* anapoongea na kitu kama kiwiliwili kinachomkaribisha kuingia katika duara ili kutapika na kuongea na roho yake anaambiwa kuwa wamekwisha tumia karibu miaka kumi katika mazungumzo hayo. Anashangaa na kusema kuwa mbona nimefika hapa dakika kumi tu zilizopita.

Wakati Shaaban Robert anapoonekana kuathiriwa na utamaduni wa watu wa pwani na hali ya kushikilia ukale wa Watanganyika wa wakati huo; Kezilahabi ameathiriwa na Biblia katika kutumia uduara wa wakati. Biblia inazungumzia kusimama kwa jua, yaani masaa kutosonga mbele wakati Yoshwa alipokuwa akiwaua Waamori. Pia Biblia inazungumzia jua kurudi nyuma masaa kumi kama ishara ya kuponywa kwa Hezekia katika ugonjwa wa kufisha (Yoshwa, 10: 12-14; Isaya, 38: 7-8).

Kwa kutumia uduara wa wakati kwa kiwango kikubwa katika riwaya za *Nagona* na *Mzingile* ni wazi kuwa Kezilahabi hapa amesai hata namna ya uandishi wake mwenyewe aliokuwa akiutumia katika riwaya zake tangulizi. Hali kama hiyo inapotokea ndiyo inayoitwa kufufuka kwa kazi (Bloom 1975). Hii usababishwa na hali ya msanii fuatishi kuwa na hamu ya kutunga kazi yenye kiwango cha juu kuliko kazi zile za msanii tangulizi.

Kezilahabi kwa sababu ya kuandika kipindi cha usasabaadaye ametumia kwa kiwango kikubwa uduara wa wakati na matukio. Kuna kujirudiarudia kwingi kwa matukio. Wakati una thamani kwa sababu matukio uongozwa na wakati, hivyo hakuna muda wa kupoteza na mambo yanafanyika haraka na kwa muda mfupi. Kwa sababu ya utandawazi unaoambatana na maendeleo ya sayansi na teknolojia mambo mengi na ya tamaduni tofauti huchanganywa na yanaweza kutokea kwa wakati mmoja. Kwa mfano, wakati Kezilahabi anapozungumzia mji wenye watu maskini, wasioongea na wanaoishi kwa matumaini yanayopatikana katika ndoto zao, pamoja na watoto watatu yatima wanaotembea uchi; upande mwingine katika jamii hiyo hiyo kuna wanaofanya majaribio makubwa ya kisayansi ya namna ya kukishinda kifo. Hivyo kwa Kezilahabi kumekuwa na tofauti ya namna

ya kuhesabu muda hata kwa watu wanaoishi kijiji kimoja. Wakati wengine wanapoishi miaka mia iliyopita wengine tayari wanaishi miaka mia mbele katika jamii hiyo hiyo.

Kwa Shaaban Robert, wakati si kitu cha kushughulikia, sio kitu cha muhimu sana. Kinachoangaliwa ni tukio kufanyika, hivyo wakati huweza kuhesabika kulingana na mfululizo wa matukio. Kwa Shaaban Robert wakati ni wa kiufuatano na kwa muda mwingine wakati umekuwa tuli au umetuama. Kwa mfano, wajumbe sita waliotumwa kwenda nchi mbalimbali kujifunza hatua za maendeleo zilizopigwa na nchi hizo ili kuleta maendeleo hayo Kusadikika ni mfano wa wakati uliotuama. Ni wakati uliotuama kwa sababu tangu zama za wajumbe hao wote hakuna mabadiliko yoyote ya kimaendeleo yaliyotokea katika nchi ya Kusadikika. Hivyo tofauti kubwa kati ya Shaaban Robert na Kezilahabi katika kutumia dhana ya wakati ni kuwa Shaaban Robert ametumia wakati wa kiufuatano kwa kiwango kikubwa na wakati uliotuama kwa kiasi kidogo wakati Kezilahabi ametumia uduara wa wakati kwa kiwango kikubwa sana katika riwaya zake teule.

Tofauti ya matumizi ya mbinu ya uchawi na mazingaombwe kati ya kipindi kabla na kipindi cha usasabaadaye katika kuhesabu wakati ni katika thamani ya wakati. Katika kipindi cha usasabaadaye wakati ni mali ya mtu binafsi. Kila mtu anazingatia wakati kivyake na kile apaswacho kukifanya kwa wakati husika. Katika kipindi kabla ya usasabaadaye wakati ni mali ya jamii nzima. Madhara ya kutotumia muda vizuri katika kipindi cha usasabaadaye humwathiri mtu binafsi. Wakati katika kipindi kabla ya usasabaadaye madhara hayo ni kwa jamii nzima.

Umiliki binafsi wa wakati katika kipindi cha usasabaadaye unatumiwa na Kezilahabi kuzua mgongano mkubwa kati ya wahusika katika riwaya zote mbili za *Nagona* na *Mzingile*. Mgongano huo unasababishwa na tofauti ya wahusika katika kuhesabu wakati. Wakati wahusika wengine wanapoona wakati kuwa ni wa kiufuatano wengine wanaona kuwa wakati ni wa kiduara zaidi na kwa wengine wakati unasonga mbele kwa haraka zaidi. Wakati huo huo wengine wanaona ajali kama kisababishi cha wakati kusonga kwa haraka zaidi na kichocheo cha kufanya mambo kuwezekana (*Nagona*, uk. 4,19).

Mgongano wa kuhesabu wakati unatokana na kuwepo kwa watu wenye mielekeo na mitazamo inayokinzana lakini wanaokutana katika shughuli au jambo fulani maalum linalowakutanisha pamoja. Mitazamo hiyo katika kuhesabu wakati inaweza kusababishwa na tofauti za kitamaduni, kielimu, kidini na hata za kiwango cha sayansi na teknolojia. Kwa mfano, Msaka paa anapokutana na Padri katika mji wa watu wasioonekana wala kuongea, wanatofautiana katika kuhesabu wakati. Mwandishi anasema:

“Mimi ni Padri wa mji huu. Hii karne ya nne niko hapa”. Karne ya nne?”
Najua huelewi. Lakini utaelewa siku ikifika (*Nagona*, uk. 4)”.

Hapa kuna mgongano wa kuhesabu wakati. Wakati msimuliaji anapoona kuwa haiwezekani katika uhalisia mtu wa kawaida kuishi karne nne, Padri anamjibu kuwa atafahamu siku ikifika. Hapa inawezekana Kezilahabi ametumia maandiko matakatifu ya Biblia katika kuhesabu wakati. Kezilahabi anataka wasomaji wake wafahamu kuwa jinsi wakati unavyohesabiwa katika Biblia ni tofauti na hesabu za kawaida zilizozoeleka. Biblia mara nyingine imetumia uvunjivu wa kaida katika kuhesabu wakati, kuna uduara na mzunguko usio wa kawaida; kwa mfano, Padri kama kiongozi wa dini ya Kikristo ambao kitabu wakitumiacho ni Biblia,

anaweza kutumia uduara wa wakati wa Kibiblia kuelezea muda mwingi ambao neno la Mungu limeishakaa katika jamii husika. Kwa mfano, katika Biblia inaelezwa hivi:

Maana miaka elfu machoni pako ni kama siku ya jana ikiisha kupita, na kama kesho la usiku...Lakini, wapenzi, msilisahau neno hili, kwamba kwa Bwana siku moja ni kama miaka elfu, na miaka elfu ni kama siku moja (Zaburi, 90: 4; 2Petro, 3: 8).

Hesabu hizo za Kibiblia za wakati ni za kimazingaombwe kwa sababu zinakosa uhalisia kutokana na kuwa za kimzunguko (kiduara). Miaka elfu katika hesabu za kibiblia inaonekana ni muda mfupi sana nayo inaweza kupita haraka na kusahaulika kama jana au kesho la usiku, pia inaweza kuwa sawa na siku moja. Uvunjivu wa kaida katika kuhesabu wakati unakuja pale ambapo tena Biblia inaposema kuwa siku moja inaweza kuwa ndefu sana sawa na miaka elfu za kawaida na tena miaka elfu inaweza kuwa muda mfupi sana kama siku moja. Hii inashadidiwa pia na mgongano wa uduara wa wakati kati ya Kizee na Msimuliaji katika riwaya ya *Mzingile* (uk: 57). Msimuliaji anapojitambulisha kwa Kizee anasema kuwa ni mimi ambaye siku chache zilizopita nilikuja kukueleza habari za msiba. Kizee (yumkini Mungu mwenyewe) kinashangaa na kusema kuwa si siku chache ni karne kadhaa zimepita tangu apelekewe taarifa hizo.

Hesabu hizo za Kibiblia zinaonesha kuwa kwa vile Mungu yuko siku zote, hana mwanzo wala mwisho, kwake wingi au uchache wa siku haufanyi tofauti yoyote wala hauna athari kwake. Hata hivyo kwa mwanadamu ambaye maisha yake yana ukomo siku zina maana zaidi.

Kezilahabi ametumia uduara wa wakati hapa kama kejeli kwa viongozi wa kidini. Padri ambaye ni kiongozi wa kidini, anakiri kuwa ameishakaa katika mji usiotajwa jina kwa karne nne akiwa anakunywa mvinyo tu siku zote (*Nagona*, uk. 4). Hata hivyo ameshindwa kumwongoa mtu hata mmoja. Anasema watu wa mji huo wanamwita kichaa, wanamwona mwendawazimu na wakimwona tu wanakimbia (*Nagona*, uk. 5). Ni jambo la ajabu kwa mtumishi wa Mungu ambaye anatakiwa kutunza na kulisha kondoo (watu wa Mungu) kukimbiwa na wale anaotakiwa kuwatumikia. Hii ni kinyume kabisa na maagizo ya Biblia juu ya mchungaji mwema. Sifa za mchungaji (padri) mwema kwa mujibu wa Biblia ni kuwa: kondoo humsikia sauti yake, huwaita kondoo wake kwa majina yao, huwatangulia na kondoo humfuata, nao waijua sauti yake (Yohana, 10: 3-4). Kinyume chake, Padri analinganishwa na mwizi au mgeni ambaye kondoo hawatamfuata kabisa, bali watamkimbia; kwa sababu hawajui sauti yake (Yohana, 10: 5).

Kezilahabi anasema Padri kama huyo ambaye amemwita kuwa ni padri mlevi, kuungama dhambi zako kwake ni kupoteza muda. Hii ni kwa sababu huwezi kusamehewa hata dhambi moja, kwa sababu Padri kama hao hawasikilizwi. Baraka zao huishia kufukuza tu inzi nyusoni mwao (*Nagona*, uk. 16).

Kezilahabi karibu katika kazi zake nyingi ameonekana kuzungumzia tabia ya baadhi ya viongozi wa kidini zisizoendana na maadili mema yatakiwayo kwa viongozi hao. Kwa mfano, uzinzi wa Padri Madevu na Mama Tinda katika riwaya ya *Gamba la Nyoka* ni mfano mojawapo. Viongozi wengi wa kidini wamekuwa waongo, wazinzi, walawiti, walevi, wafanya biashara haramu, wabinafsi, wezi, wafanya mazingaombwe, wachawi na washirikina.

Ijapokuwa matukio maovu ya viongozi wa kidini yalikuwepo katika jamii miaka ya themanini wakati Kezilahabi alipokuwa akiandika riwaya za *Nagona* na *Mzingile*, lakini kwa sasa uhalisia wa matukio maovu ya viongozi hao yasiyoendana na vitabu vitakatifu, yamezidi na sasa wanayatenda hadharani na kutangazwa katika vyombo vya habari. Kwa mfano, Nabii Tito Onesmo Machibya wa Dodoma nchini Tanzania, alikuwa akinywa na kuwanyweshwa waumini wake pombe, kufanya uasherati pamoja na kuendesha ibada ya kupapasana kanisani usiku taa zikiwa zimezimwa. Alidai kuwa ameagizwa na Mungu kuwa kunywa pombe ni sehemu ya ibada. Alikamatwa na kanisa lake kupigwa marufuku na serikali ya Tanzania mwaka 2014 kwa madai kuwa anadhilisha Ukristo.³⁶

Baadhi ya madhehebu ya Kiprotesti, kwa mfano, Angilikana kuhalalisha ndoa ya jinsia moja na kuwachagua mashoga kuwa viongozi wa makanisa hayo ni jambo la kawaida sasa karibu duniani kote. Kwa mfano, mwaka 2007 kulitokea sitofahamu katika dhehebu la Kiangilikana nchini Tanzania. Sababu ya ugomvi huo ilikuwa ni mjadala uliofanyika jijini Dar es Salaam wa kutaka kuhalalisha ndoa ya jinsia moja katika kanisa hilo.³⁷Kanisa kuingia katika mgogoro wa kutaka kuhalalisha ndoa ya jinsia moja ni dhambi inayokemewa na Biblia kwa sauti kali kabisa. Biblia imeandika wazi (Mwanzo, 18: 20-21) kuwa:

Bwana akasema, kwa kuwa kilio cha Sodoma na Gomora kimezidi, na dhambi zao zimeongezeka sana, basi nitashuka sasa nione kama wanayotenda ni kiasi cha kilio kilichonijia; na kama sivyo nitajua.

Biblia inazidi kudhihirisha wazi kuwa wenyeji wa Sodoma walikusudia kuwalawiti hata malaika waliotumwa kuhakikisha kama kuna uovu katika mji

³⁶ Maelezo hayo yalipakuliwa kutoka internet tarehe 23/12/2017

³⁷ Maelezo hayo yalipakuliwa kutoka internet tarehe 02/06/2019

huo (Mwanzo, 19: 1-11, 23-25). Matokeo yake Sodom na Gomora ziliteketezwa kwa moto.

Kezilahabi ametumia uvunjivu wa kaida ya kuhesabu wakati kwa kumtumia padri aliyekaa katika jamii kwa muda wa karne nne, yaani miaka mia nne, bila kumwongoa hata mtu mmoja, kazi yake kubwa ikiwa ni ulevi; kwa lengo la kukejeli na kuwadhihaki viongozi wa kidini wanaokiuka lengo na maadili ya wito wao. Hapa chini yamenukuliwa mahojiano aliyofanyiwa Mchungaji Antony Lusekelo juu ya unywaji wa pombe katika kipindi cha Kikaangoni cha East Africa Television (EATV). Katika mahojiano hayo Lusekelo alitakiwa kuthibitisha kama pombe ni haramu au la kwa msimamo wa madhehebu ya Kikristo.

Swali: Mchungaji, kuna tuhuma kuwa unatumia pombe

Mchungaji: Hao wanaonituhumu kuwa nakunywa pombe wanapaswa kutoa ushahidi juu ya tuhuma hizo, waeleze ni pombe gani nakunywa, nilikuwa nakunywa wapi na aliyeniona ni nani.

Swali: Je, kunywa bia kiasi bila kulewa ni dhambi au siyo dhambi?

Mchungaji: Siwezi kusema kama ni dhambi au la, maana inategemea na imani ya mtu au makanisa. Biblia haijazuia unywaji pombe. Kuna sehemu nyingine pombe siyo dhambi, dini nyingine mpaka kanisani kuna bar, wakati kwa dini nyingine hata kunywa soda ni dhambi. Dhambi ni makubaliano yenu kwenye dini yenu. Biblia inasema kula kitu chochote hata chakula kupitiliza ni dhambi, hata unywaji wa pombe ukinywa ukapitiliza ni dhambi. Biblia haijaandika moja kwa moja kwamba msinywe pombe, imesema msilewe kwa kuwa ndani ya ulevi mna ufisadi, cha msingi mbadilishe ulevi wenu uwe roho mtakatifu.

Ukiyachunguza mahojiano haya utagundua kuwa Mchungaji Lusekelo anatetea unywaji wa pombe. Anasema kuwa Biblia haijazuia unywaji wa pombe (kileo) na kuwa katika dini nyingine kuna 'bar' mpaka kanisani. Anasema dhambi ni

makubaliano ya waumini wenyewe, wakiamua kuwa kunywa pombe ni dhambi itakuwa dhambi na wakisema kuwa si dhambi haitakuwa dhambi.

Maelezo hayo ya Lusekelo yanazidi kwenda kinyume na Biblia na yanahalalisha mawazo ya Kezilahabi ya upotovu wa maadili kwa viongozi wa kidini. Biblia inaeleza wazi kuwa waasherati, ...wazinzi, walawiti, wevi, walevi, watukanaji wala wanyang'inyi hawataurithi ufalme wa Mungu (1Wakorintho, 6: 9-10). Biblia inasisitiza zaidi kuwa mvinyo hudhahiki, kileo huleta ugomvi na atumiaye vitu hivyo, awe Kuhani au Nabii anakosea katika hukumu kwa sababu vitu hivyo huwafanya wasiwe na hekima kabisa (Mithali, 20: 1; Isaya, 28: 7).

5.3 Kiishilio

Sura hii imechunguza uvunjivu wa kaida katika riwaya teule za Shaaban Robert na Euphrase Kezilahabi. Lengo lilikuwa ni kubainisha athari ya mazingira asilia ya watunzi katika matumizi ya uvunjivu wa kaida katika riwaya teule. Imebainika kuwa watunzi wa riwaya teule wametumia uvunjivu wa kaida katika riwaya zao kwa kuathiriwa na mazingira yao asilia. Shaaban Robert ametumia zaidi: uvunjivu wa kaida ya mahali au mazingira, uvunjivu wa kaida ya mbali na karibu na kaida za kimawasiliano kati ya binadamu na viumbe wengine. Shaaban Robert hakutumia uvunjivu wa kaida kati ya uhai na kifo pia hakutumia ndoto kwa maana halisi ya ndoto bali ndoto ya hila ya Sapa ya kutaka kufahidi bahati ya Salihi. Kinyume chake Kezilahabi ametumia aina zote za uvunjivu wa kaida zilizokuwa zinachunguzwa katika utafiti huu katika riwaya zake zote teule kwa sababu ya athari ya mazingira yake asilia.

Pamoja na athari za mazingira asilia ya watunzi hao katika kutumia uvunjivu wa kaida, usomaji wa masimulizi ya Alfu Lela Ulela pia kumeathiri utunzi wa Shaaban Robert wakati Kezilahabi akiathiriwa na Biblia Takatifu. Imebainika kuwa uvunjivu wa kaida za uhalisia umejumuishwa katika matumizi ya uchawi na mazingaombwe kwa sababu katika uvunjivu wa kaida mhusika anaweza kuingia popote na kufika popote kwa muda mfupi hata kama ni mbali kiasi gani. Anaweza kuzungumza na kiumbe kingine chochote; mfano simba, pundamilia na viumbe wa kufikirika kama malaika, mashetani na majini bila kizuizi cha tofauti za kimaumbile na cha lugha miongoni mwao. Mhusika anaweza kufa na kuishi tena kwa wakati huo huo au kuzungumza na wafu kama na watu walio hai.

Imebainika kuwa Shaaban Robert kwa kutumia uvunjivu wa kaida kwa kuvunja mpaka wa umbali kati ya mbingu na dunia ameelezea imani ya kidini yenye matendo. Kezilahabi kwa upande wake ametumia uvunjivu huu wa mpaka kati ya mbali na karibu kueleza kuwa hakuna kinachoshindikana kama mwanadamu atatumia akili yake katika kufikiri.

Imebainika kuwa Shaaban Robert inawezekana ametumia uvunjivu wa kaida kati ya mbali na karibu na ya mahali kutabiri juu ya maendeleo ya sayansi na teknolojia inayoambatana na utandawazi. Hii ni kwa sababu katika utandawazi dunia inakunjwa na kuwa ndogo kama kiganja cha mkono ambapo mtu anaweza kuona yote na kufika popote katika kiganja hicho kwa muda sifuri. Pia imedhihirika kuwa uchawi na mazingaombwe hubadilika kiwakati na hutofautiana kati ya mtu na mtu na kati ya jamii na jamii kutokana na tofauti kimtazamo na kiwango cha maendeleo ya sayansi na teknolojia ya jamii husika.

Imebanika pia kuwa Shaaban Robert ametumia wakati tuamavu kukemea mila potofu zinazoshikilia ukale ambao hauna faida kwa maendeleo ya jamii. Anahimiza umuhimu wa jamii kubadilika kulingana na wakati kwa kuchukua mazuri yaliyoko katika jamii zingine na kuyatumia kwa maendeleo ya jamii zao. Anahimiza zaidi umuhimu wa kutumia wakati kwa kuzalisha faida. Kuwa hekima na umuhimu wa mtu huhesabiwe kwa kile alichokifanyia jamii na si kwa miaka yake ya kuishi duniani. Kezilahabi kwa upande wake ametumia uduara wa wakati kukemea maovu na uvunjivu wa maadili wa viongozi wa kidini. Viongozi wa kidini wanategemewa kuwa chachu ya matendo mema katika jamii lakini wengi wao wametenda kinyume cha matario ya jamii kwao. Sura inayofuata imechunguza matumizi ya visasili na istiara katika riwaya teule.

SURA YA SITA

ATHARI YA MAZINGIRA ASILIA YA WATUNZI KATIKA MATUMIZI YA VISASILI NA ISTIARA KATIKA RIWAYA TEULE ZA SHAABAN ROBERT NA ZA EUPHRASE KEZILAHABI

6.0 Utangulizi

Sura hii imechunguza matumizi ya visasili na istiara katika riwaya teule za Shaaban Robert na za Euphrase Kezilahabi. Lengo lilikuwa ni kuchunguza athari ya mazingira asilia ya watunzi katika matumizi ya visasili na istiara katika riwaya teule na kulinganisha matumizi ya visasili kati ya Shaaban Robert na Euphrase Kezilahabi. Ili kufaulisha lengo hilo, visasili na istiara za kichawi na za kimazingaombwe zilizoko katika riwaya teule zimebainishwa. Zaidi ya yote matumizi ya visasili na istiara yamelinganishwa kati ya Shaaban Robert na Euphrase Kezilahabi.

Sura hii imegawanyika katika sehemu kuu mbili. Sehemu ya kwanza imefafanua maana ya visasili, imebainisha visasili katika riwaya teule na kulinganisha matumizi ya visasili kati ya Shaaban Robert na Euphrase Kezilahabi katika riwaya teule. Sehemu ya pili imefafanua maana ya istiara, imebainisha na kulinganisha matumizi ya istiara kati ya Shaaban Robert na Euphrase katika riwaya teule.

6.1 Visasili

Kisasili ni hadithi ambayo haihusishwi na mwandishi maalum bali hupatikana katika imani zilizopo katika jamii fulani. Aghalabu visasili huhusisha matukio ya

kiajabu au yasiyotarajiwa katika maisha ya kawaida au hata ya miungu. Huweza kuhusisha pia wahusika wa kishujaa wa kihistoria au wa kuaminika ambao wanatenda matendo yanayokiuka uhalisi wa kawaida. Visasili huakisi muundo wa kitamaduni wa jamii inayohusika. Kwa kuwa kimsingi visasili huhusishwa na hatua ambapo upokezi wa kimdomo unachukua nafasi kubwa, inawezekana kusema visasili huonyesha juhudi za jamii fulani kujaribu kuhifadhi maarifa fulani kujihusu. Hapana lazima ya kisasili kuwa na misingi ya kihistoria inayotambuliwa au inayodhihirika waziwazi (Mulokozi,1996; Wamitila 2003: 91; Method, 2012; Mwangi, 2016). Kisasili kinakuwa cha kichawi na cha kimazingaombwe kama masimulizi au matukio yaliyomo katika kisa husika yanakiuka uhalisia wa kawaida katika maisha halisi.

Uchanganuzi katika sehemu hii umeongozwa na mhimili wa nadharia ya Uhalisiamazingaombwe unaosema kuwa matukio ya kichawi na ya kimazingaombwe yanaonekana ya kawaida lakini yenye hali za kuogofya na kuduwaza.

Shaaban Robert anaeleza kisasili cha mji uliogeuzwa mawe katika riwaya ya *Adili na Nduguze*. Katika mji huo kila kitu kilichokuwepo kiligeuka jiwe. Mji huo uligeuzwa mawe kwa sababu ya mfalme wake, Tukufu, kushikilia ibada ya mizimu na kukataa onyo la bure la Mrefu aliyewataka waachane na ibada hiyo potofu. Mwandishi akieleza jinsi ugunduzi wa mji huo ulivyomtia hofu Adili anasema:

Adili alipotaka kuingia ndani alimwona mtu amesimama mlangoni... Alizidi Kumtazama na kumshika mwilini. Alipofanya hivyo aliona kwamba si mtu ila jiwe lililokuwa halina maisha. Ugunduzi huu ulitia mzizimo wa hofu katika moyo wa Adili lakini alijikaza... Kila alikokwenda alitazama huku na huko. Mabarabara yote yalijaa watu waliosimama, lakini wote walikuwa mawe matupu. Alipofika sokoni aliona umati mkubwa wa watu. Baadhi yao walikuwa wamekaa kitako na wengine walikuwa wamesimama wima. Mbele ya watu waliokaa palikuwa na vikapu vya nafaka iliyogeuka changarawe, unga uliokuwa vumbi, ... na vitu vingine vya biashara vilivyogeuzwa mawe (*Adili na Nduguze*, uk. 21).

Kisasili cha mji uliogeuzwa mawe ni cha ajabu na kinaogopesha. Mwandishi anakiri kuwa ugunduzi wa mji huo unatia hofu na kuvumilia kukaa kwenye mazingira kama hayo kunahitaji moyo mkuu kwa kusema kuwa ugunduzi huu ulitia mzizimo wa hofu katika moyo wa Adili lakini alijikaza. Ingawa kisasili cha mji uliogeuzwa mawe ni cha ajabu na cha kuogofya lakini katika uchawi na mazingaombwe huchukuliwa kama kisa cha kawaida na kinachoweza kutokea katika mazingira halisi katika maisha ya jamii. Hii inashadidiwa na mhimili wa Uhalisiamazingaombwe unatumika kuchanganulia data katika sehemu hii kuwa matukio ya kichawi na ya kimazingaombwe yanaonekana ya kawaida lakini yenye hali za kuogofya na kuduwaza. Merrel (1975) anasisitiza kwa kusema kwamba uchawi na mazingaombwe unatokana na hali mbili za ulimwengu zinazopingana. Merrel hapa anamaanisha kuwa uchawi na mazingaombwe una misingi yake katika uhalisia au ulimwengu ambao tunaufahamu na pia hutuwezesha kuuona uhalisia ambao haufahamiki kwa hali ya kawaida.

Wamitila (2003) anashadidia kwa kusema kuwa uhalisiamazingaombwe hutumika katika fasihi kuchunguza matumizi ya uchawi na mazingaombwe kama matukio ya kawaida yanayotokea katika jamii na kuhusisha matukio hayo na kile yanachokisawiri katika maisha ya kawaida katika jamii husika. Kugeuka mawe

na kuzama kwa miji mingine kulitokana na laana iliyotamkwa na Mrefu. Katika uhalisia si rahisi na hakutegemewi mtu kutamka laana, yaani maneno tu ya kutamkwa kufanya watu na vitu vyote katika mji kugeuka mawe na miji mingine kugharikishwa. Mwandishi anaeleza kuwa, sababu kubwa ya mji huo kugeuzwa mawe pamoja na miji mingine iliyozama kabisa, ni mfalme wake kukataa maonyo ya bure kutoka kwa Mrefu.

Katika historia ya jamii ya Shaaban Robert hakuna kisasili cha miji iliyozama au kugeuka mawe. Hata hivyo kuna kisa cha Mrefu, kiumbe mrefu wa ajabu aliyekuwa kati ya binadamu na jini (taz, uk. 61). Pia kuna kisa cha watu wawili waliokaidi amri ya Jafari Kibwana na kwenda kuvua samaki baharini siku ya Idi. Jafari alisema siku hiyo watu wasifanye kazi yoyote lakini watu hao walikaidi na kwenda kuvua baharini siku hiyo. Matokeo yake walizama na pale walipozama pana mawe mawili yenye sura kamili ya binadamu, moja limesimama na lingine limeinama. Inaaminika kuwa mawe hayo ni watu hao wawili waliokaidi amri ya Jafari Kibwana. La ajabu zaidi ni kuwa kamera haziwezi kuchua picha za sura hizo (taz, uk. 74).

Inawezekana Shaaban Robert kwa kutumia kisasili cha mji wa mawe ameathiriwa pia na kisasili cha gharika ya Nuhu na kuchomwa moto kwa miji ya Sodoma na Gomora katika Biblia (Mwanzo, 6: 5-8, 7: 10-24; 19:12-29). Watu wa wakati wa Nuhu licha ya kuhubiriwa na Nuhu kwa miaka 120, hawakujali wala kutubu dhambi zao. Zaidi ya kuona muujiza wa msururu wa wanyama wakiongozana kuelekea safinani, watu wa wakati wa Nuhu hawakuchukua tahadhari ya kutafuta hifadhi ndani ya safina. Mwisho, kama ilivyokuwa kwa miji mingine ya mfalme

Tukufu waligharikishwa kwa maji. Pia wenyeji wa Sodoma hasa familia ya Lutu licha ya Lutu kuwahimiza watoke Sodoma kwa sababu mji unatarajiwa kuchomwa moto hawakujali. Walimcheka kwa kusema amechanganyikiwa. Mke wa Lutu, licha ya kusikia onyo kali kutoka kwa malaika, alitazama nyuma na kuwa nguzo ya chumvi sawa na wenyeji wa mji wa Fahari walivyokuwa mawe.

Kisasili cha kuzama kwa miji mingine ya mfalme Tukufu na mji wa Fahari kugeuzwa mawe kimekusudiwa kutoa mafunzo na maonyo mengi kwa viongozi na jamii kwa ujumla. Kisa hiki kinaonya kuwa si vizuri kutoa maamuzi ya haraka na kwa hasira bila kufikiri kwanza hasa kwa masuala muhimu na yanayohusu jamii nzima. Pia viongozi wanaonywa kutumia uwezo, nguvu na mamlaka yao kwa uangalifu mkubwa sana. Kinyume cha hapo wanaweza kuleta maangamizi na hasara isiyochukulika kwa jamii au nchi nzima. Mwandishi anasema:

...mfalme ni naibu wa Mungu duniani. Kwa hiyo, ufalme ni amana kubwa. Amana hiyo ilitaka uangalifu mkubwa kwa sababu ni dhima bora iliyowekwa mikononi mwa binadamu. Wajibu wa kwanza wa mfalme ni kuwa mwadilifu katika matendo yake. Kila tendo, jema au baya, ni mfano kwa raia wake (*Adili na Nduguze*, uk. 29).

Shaaban Robert ametumia kisasili hiki cha mji uliogeuzwa mawe kuonya kuwa, hakuna faida yoyote kuendelea kushikilia ukale ambao kulingana na mabadiliko na maendeleo ya sayansi na teknolojia hauna nafasi katika ulimwengu wa sasa. Mwandishi anasisitiza kuwa ibada ya kimizimu ni ukale uliopitwa na wakati. Aidha anawashauri viongozi waliopewa dhamana kubwa ya kuongoza jamii wasishikilie ukale usio na maana, kama kuabudu miti na mizimu, bali wawe wepesi wa kwenda na wakati kwa kupokea mawazo mapya yenye nia ya kujenga na kuendeleza jamii zao.

Kezilahabi naye katika riwaya ya *Nagona* anaelezea kisasili cha mji wenye watu wasiionekana kwa macho, wasioongea na wanaoishi kwa kula matumaini yao yanayopatikana katika ndoto zao. Mimi anaeleza kufika kwake katika mji ambao alisikia kikohozi, vicheko vya watu, kupigwa kofi, kusukumwa na hata kupigwa na yai viza; vyote hivyo na watu wasiionekana. Watu wa mji huo hawali chakula cha kawaida wala hawana maji. Lugha yao ni kimya, chakula chao ni matumaini yao yanayozaliana kila siku kutoka katika kisima cha ndoto zao. Kisima hicho hakiwezi kuonwa na yeyote anayefikiri. Watu wa mji huo wanakishinda kifo kwa kucheka na uhai na kuwepo kwao kunahakikishwa na kukohoa kwao. Mwandishi anasema kuwa asili ya watu wa mji huo kutozungumza, kutokula chakula cha kawaida na watu wa kawaida kutoweza kuwaona ni maasi ya karne nyingi zilizopita (*Nagona*, uk. 6). Hata hivyo hafafanui zaidi kuwa ni maasi gani hayo.

Utokawaida wa tabia, matukio, matendo, mandhari na jinsi watu wanavyoendesha maisha katika mji tajwa ndio hufanya kisasili cha mji huo kuwa wa ajabu, wa kutisha na wa kuogopesha. Watu hao hawaonekani kwa macho, ingawa vicheko na kukohoa kwao kunaweza kusikika, hawaongei na chakula chao ni matumaini yao yanayotokana na ndoto zao. Wanaweza kukupiga bila kuwaona. Mtu wa kawaida akifika katika mazingira ya mji kama huo atayaona kama mazingira ya ajabu, ya kutisha na ya kuogofya. Faustine (2012) anashadidia kwa kusema kuwa:

Uajabu wa mandhari ya mji huu unatokana na kuibuka kwa wahusika wa ajabu ambao ni wa kidhahania. Uajabu wa wahusika hawa unatokana na hali ya kutoonekana kwao, ilihali sauti zao zinasikika wazi na matendo yao kuhisiwa na mhusika Mimi. Kwa namna yoyote ile si rahisi mtu kutembea katika mazingira fulani akasikia sauti au kutendewa vitendo kama hivyo pasipo kumwona mtendaji, na bado akayachukulia mazingira hayo kuwa ni ya kawaida (msisitizo ni wetu).

Kezilahabi ametumia visa vingi vilivyojaza matendo yanayotendwa na watu wasioonekana na vinavyoibua dhana za uchawi na mazingaombwe katika riwaya zake nyingi, *Nagona* na *Mzingile* zikiwemo. Hii inatokana na athari ya mazingira asilia ya kisiwa cha Ukerewe alikozaliwa Kezilahabi. Katika mazingira ya Ukerewe ni jambo la kawaida kuchapwa, kusikia sauti au hata kula pamoja na watu wasioonekana, yaani wachawi. Hata hivyo historia ya kuwepo kwa mji halisi wenye watu wasioonekana katika mazingira ya Ukerewe kama alivyotumia Kezilahabi katika riwaya ya *Nagona* ni suala ambalo halikubaliwi na Wakerewe walio wengi. Hata hivyo inafikiriwa kuwa Kezilahabi ametumia kisasili cha mji wa watu wasioonekana, wasiozungumza na wanaoishi kwa kula matumaini yanayozalishwa katika ndoto zao kutokana na masimulizi ya mji wa Gambosh.

Katika mazimulizi yaliyotapakaa katika mikoa ya kanda ya ziwa nchini Tanzania, iliaininika kuwa Mji wa Gambosh ni mji unaokaliwa na wachawi pekee. Masimulizi yanaeleza kuwa si rahisi kufika au kuona mji huo bila wachawi kukupaka dawa machoni. Ikitokea mtu akafika katika mji huo, atasikia sauti za watu, na hata kupigwa na watu wasioonekana. Inaaminika kuwa baadhi ya watu wanaofikiriwa kuuawa kichawi na kugeuzwa vizuu wamepelekwa Gambosh. Hata hivyo katika uhalisia kuna mji halisi wa Gambosh. Mji huo unaitwa Gambosi na si Gambosh kama ilivyo katika masimulizi. Gambosi iko kilomita 60 kutoka mji wa Bariadi mkoani Simiyu. Maisha ya wenyeji wa kijiji cha Gambosi yanatoa taswira ya mazingira yasiyofikika kirahisi na yasiyo na huduma za elimu, za afya na zile za kiserikali.

Gambosi inaonekana kama ni kijiji cha kufikirika kutokana na masimulizi ya ajabuajabu ya kichawi yanayotia hofu kwa wasio wenyeji. Wenyeji wa Gambosi wanasema wao si wachawi ila wanaheshimu, kulinda, kudumisha na kufuata mila na desturi zao za asili. Hata hivyo wanasisitiza kuwa mtu yeyote anayefika Gambosi kwa nia mbaya, hukiona cha mtema kuni kwa ama kupotea njia na kurandaranda hadi kujikuta amerejea alipotoka au kukipita kijiji hicho bila kuona nyumba wala wenyeji (Gazeti la Mwananchi.co.tz Friday July 7, 2017).

Katika riwaya ya *Mzingile* Kezilahabi anaanza na kisasili cha kuzaliwa Kakulu. Kakulu maana yake ni kakubwa, kazee (*Mzingile*, uk. 2). Maajabu yake yalianza kabla ya kuzaliwa. Alianza kuongea akiwa tumboni. Alizaliwa akiwa na mvi kichwani, ndevu nyingi ndefu, akiwa na meno aliyotumia kukata kitovu chake, alisimama akajipangusa maji ya utelezi na kuwakaripia na kuwafukuza wanawake waliokuwa karibu. Alizaliwa anafahamu methali na aliweza kupanda juu ya mti wa ubuyu siku hiyo hiyo ya kuzaliwa. Mwandishi anasema:

Siku hiyo hiyo aliyozaliwa alimwomba mama yake ubuyu ulioivia mtini. “Siwezi kupanda,” mama yake alimjibu. Basi nipe kigoda changu nikae kwanza.”Kipo cha marehemu baba yako.” “Sitaki kusikia uzushi! Kabla ya mti uliotengeneza kigoda hicho kuwako mimi nilikuwako!” (*Mzingile*, uk. 2).

Kisasili hiki kinadhihirisha kuwa Kezilahabi ametumia visa vya ajabu katika riwaya ya *Mzingile*. Hii ni kwa sababu ni muujiza kumpata mtoto wa kawaida anayeweza kuongea, kutembea, kupanda mti, na hata kuwakemea na kuwafukuza watu siku iyo hiyo ya kuzaliwa kwake. Zaidi ya yote Kakulu anadai kuwa alikwepo kabla ya mti uliotumika kutengeneza kigoda cha baba yake. Hii ina maana kuwa Kakulu alikwepo kabla ya siku ya kuzaliwa kwake.

Kisa hiki cha mtoto kuongea akiwa tumbo, kukwea mti na hata kufahamu methali na misemo mbalimbali ni cha ajabu na cha kuogopesha. Hata hivyo ingawa kisa hicho ni cha ajabu lakini katika uchawi na mazingaombwe inachukuliwa kama kisa cha kawaida chenye uwezekano wa kutokea katika maisha halisi. Hii inathibitishwa na mhimili wa uhalisiamazingaomwe uliotumika hapo awali katika sehemu hii kuwa matukio ya kichawi na ya kimazingaombwe yanaonekana ya kawaida lakini yenye hali za kuogofya na kuduwaza. Mhimili huu umesaidia katika kuchunguza matumizi ya uchawi na mazingaombwe (kama kisasili cha Kakulu) katika riwaya za Shaaban Robert na za Euphrase Kezilahabi kama matukio ya kawaida yanayotokea katika jamii na kuhusisha matukio hayo na kile yanachokisawiri katika maisha ya kawaida katika jamii husika. Gromov, M. (2002) anaungana mawazo hayo kwa kuisitiza kuwa uchawi na mazingaombwe ni njia inayotumika kufinyanga ukweli wa maisha kwa njia tofauti na mbinu za kawaida zilizozoeleka.

Kakulu kwa maneno hayo anafananishwa na Yesu Kristo katika Biblia. Yesu alionekana mwongo au mwenye pepo na Wayahudi wakataka kumpiga kwa mawe kwa sababu ya madai yake kuwa kabla ya kuwepo kwa babu yao Ibrahimu yeye alikuwepo (Yohana, 8: 56-58). Utokawaida wa Kakulu, matendo, na maneno yake ndiyo yaliyomfanya mama yake kugundua kuwa hakumzaa mtoto wa kawaida na hivyo kutokea mlango wa nyuma na kutokomea kusikojulikana.

Kezilahabi, kwa kutumia kisasili cha mji wa watu wasioonekana kwa macho wanaoishi kwa kula matumaini yao yanayozaliana katika kisima cha ndoto zao katika riwaya ya *Nagona* ameathiriwa na kisasili cha mji wa mawe cha Shaaban Robert katika riwaya ya *Adili na Nduguze*. Kezilahabi kama mwandishi fuatishi

ameathiriwa na Shaaban Robert kwa kumwiga lakini si kwa mwigo sisi bali anayaendeleza mawazo ya Shaaban Robert kwa namna nyingine. Hii ni kwa sababu wahusika katika kisasili cha mji wa mawe katika riwaya ya *Adili na Nduguze* ni watu halisi wanaonekana kwa macho lakini hawana uhai ndani mwao. Hata hivyo, mtu akifika katika mji huo bila kuwachunguza watu hao vizuri anaweza akadhani ni watu hai kumbe ni wafu. Kinyume chake wahusika wa mji wa watu wasioonekana kwa macho hawaonekani kwa macho ingawa watu wapo katika mji huo. Mtu akifika katika mji huo bila kufanyiwa kitu chochote na watu hao wasioonekana atafikiria kuwa mji huo hauna watu.

Kinachofanya kisasili cha mji wa watu wasioonekana kifanane na kisasili cha mji wa mawe ni kuwa, jinsi watu wa mji wa mawe wasivyoweza kufanya jambo lolote jipya ingawa wanaonekana kwa macho lakini wamekufa ndivyo walivyo watu wa mji wa watu wasioonekana kwa macho. Watu wa mji wa watu wasioonekana ingawa wanaishi lakini hawana cha maana wanachoweza kufanya kwa sababu wanaishi tu kwa matumaini yanayopatikana katika ndoto zao, yaani matamano yao. Kwa hiyo watu hawa hawana kitu chochote cha maana isipokuwa kwa sababu ya matamano yao (ndoto zao) wanajiona kama wana kila kitu.

Kezilahabi kwa kuiga kisasili cha mji wa mawe ya Shaaban Robert inawezekana anafananisha watu wa mji wa mawe na Waafrika waliokataa mazuri yaliyoletwa na wazungu na hivyo wazungu kuwaacha na tamaduni zao za zamani zenye utajiri mwingi wa asili lakini ambao sasa hauna thamani kwa sababu wenyeji wanaonekana kama watu hai kumbe ni wafu waliosimama ambao hawafahamu kitu chochote wala namna ya kutumia utajiri huo (Wafula,1989). Kama ni hivyo

basi, atakuwa anaendeleza mawazo ya Shaaban Robert kwa namna nyingine katika kutumia mji wa watu wasioonekana katika riwaya ya *Mzingile*.

Watu katika mji wa watu wasioonekana ingawa wako hai na wanafanya mambo mbalimbali lakini nao wanaonekana kama watu waliokufa kiakili. Hii ni kwa sababu wanaishi kwa matumaini yanayopatikana katika ndoto bila kufanya kazi na kuridhika kwa sababu ya ndoto na matamainia yanayotimizwa katika kisima cha ndoto tupu bila matendo. Hivyo, watu wa mji wa watu wasioonekana wanaweza kufananishwa na baadhi ya nchi za Kiafrika ambazo zimepokea utamaduni na rasilimali nyingi za kigeni ambazo ziko ndani ya nchi husika na wenyeji wanaridhika kuwa kuna vitu katika nchi zao lakini vitu vile si vyao kwani vinamilikiwa vyote na wageni. Hivyo, wenyeji wa nchi kama hiyo wako katika nchi zao kama hawako. Kwa hiyo, mtu mwenye ufahamu na mwenye fikra pevu akifika katika nchi hiyo ataona kama hakuna watu. Hii ni kwa sababu vitu na utajiri wote katika nchi hiyo na maamuzi yote hufanywa na wageni. Kwa namna hiyo Kezilahabi atakuwa ameathiriwa kwa kumwiga Shaaban Robert lakini si kwa mwigo sisisi. Kwa kuisitiza hili (Bloom, 1973) anasema kwamba, kwa kumwiga msanii tangulizi, msanii fuatishi huendeleza mada na mawazo ya msanii tangulizi lakini siyo kwa mwigo sisisi bali anayakamilisha kwa namna nyingine inayoonesha kuwa msanii tangulizi inawezekana alishindwa kuyakamilisha.

Katika kisasili cha Kakulu, Kezilahabi kama msanii fuatishi ameonesha upekee na uasilia. Hapa, Kezilahabi hajaathiriwa hata kidogo na Shaaban Robert, bali ameonesha upekee na uasilia kwa kujitenga kabisa na uandishi wa Shaaban Robert (msanii tangulizi) na hata na namna ya uandishi wake yeye mwenyewe.

Hii ina maana kuwa kwa kutumia kisasili cha Kakulu katika riwaya ya *Mzingile*, Kezilahabi ameasi hata namna yake ya utunzi yeye binafsi katika riwaya zake tangulizi alizoandika kabla ya usasabaadaye katika fasihi ya Kiswahili. Lengo la Kezilahabi kufanya hivyo ni kujitenga na aina zote za mabaki (masazo) ya athari za uandishi wa Shaaban Robert na hata athari zake binafsi kwa nia ya kuwa na uhuru kamili na mafanikio binafsi (Bloom, 1925).

6.2 Istiara

Istiara ni kitanzu cha ngano kinachotumika kutoa maadili katika fasihi simulizi. Ni matumizi ya neno kueleza jambo ambalo maana yake ni tofauti na maana ya kawaida ya neno hilo japo kuwa huwa na uhusiano wa namna fulani. Istiara ni hadithi ambayo maana yake ya wazi inawakilisha maana nyingine iliyofichika. Hadithi nzima inakuwa ni kama sitiari. Ni hadithi ambayo huwa na maana mbili; uwazi na ufiche. Ile maana wazi huificha maana ya pili ambayo kueleweka kwake huhitaji ufahamu fulani wa muktadha wa hadithi yenyewe. Wahusika na matukio yaliyopo huwa kama mlinganisho wa hali nyinginezo huwa kama sitiari yaani vinasimamia hali halisi (Khamis na Madumulla, 1989; Mulokozi, 1996; Wamitila, 2003; Masebo na Nyangwine, 2000; Kubo na Wenzake, 2011; Senkoro, 2011).

Uchanganuzi wa data katika sehemu hii uliongozwa na mhimili wa uhalisiamazingaombwe unaotoa kipaumbele kwa mazingira na viumbe wa ajabuajabu kama mazimwi, mashetani, mizuka, majitu, majini pamoja na misitu mikubwa, wanyama, mito na bahari pamoja na matumizi ya baadhi ya tanzu za fasihi simulizi kama visasili, istiara na hurafa kwa kupeleka hadhira katika safari

ya hali na matukio ya kweli na yanayowezekana. Mhimili huu ni faafu kwa sababu ulimwezesha mtafiti kuchungunguza istiaara zilivyotumiwa katika riwaya teule kama visa vya kawaida vinavyowakilisha matukio ya kweli katika mazingira halisi katika jamii husika. Hivyo, kumwezesha mtafiti chunguza na kulinganisha athari ya mazingira asilia ya watunzi katika matumizi ya istiaara katika riwaya teule.

Istiaara imetumiwa kama sehemu ya mazingaombwe katika utafiti huu kwa sababu kile kinachosemwa na kinachoonekana wazi katika hadithi inayosimuliwa sicho kilichokusudiwa na mwandishi au msimuliaji. Kwa hiyo, msomaji anaweza akahadaika na kubakia katika maana ya nje na kutoelewa maana fiche iliyokusudiwa na mwandishi. Kwa mfano, katika riwaya ya *Kusadikika*, Shaaban Robert anapotaka kuzungumzia siasa ya ukandamizaji na wizi wa mali ya Waafrika wakati wa serikali ya kikoloni anatumia istiaara ya ubinafsi, ulafi na uroho wa wenyeji wa nchi ya Majuju na mfalme wao Jeta. Anasema:

Majuju ni taifa lafi na litishalo kabisa. Kila kitu kigumu kijulikanacho duniani kilikuwa laini kama mkate kati ya meno ya Majuju; na kila kilicho kichungu kilikuwa kitamu kama asali katika maonjo yao. Kwa ulafi uliokithiri viumbe hawa, walikuwa hawajui halali wala haramu. Kabuli alipopelekwa mbele ya Jeta alimkuta amekaa kitako midomo wazi. Mto mrefu na mpana ulikuwa ukimiminika katika kinywa chake kikubwa sana. Tone la maji hata moja halikupata nafasi ya kukiepa kinywa hicho. Tani milioni moja za miamba, milioni moja za chuma, milioni moja za magogo, na milioni nyingi za samaki zilimiminika pamoja na mkondo wa maji humo kinywani pia kila dakika tano. Lakini kila dakika moja Jeta alilia: kiu njaa, kiu njaa (*Kusadikika*, uk.23).

Katika hali ya kawaida, wastani wa kiasi cha chakula anachohitajiwa mtu wa kawaida kutumia katika mlo mmoja ni nusu kilo ya aina ya vyakula vyote vikiwekwa pamoja. Na kwa siku moja mtu mzima anatakiwa kula angalau mara

tatu (Taasisi ya Chakula na Lishe Tanzania 2019). Kinyume chake kitendo cha mtu kupanua mdomo na maji ya mto mkubwa, tani za chuma, magogo na samaki kumiminika kinywani na kuendelea kulia muda huo huo kiu njaa, kiu njaa ni hali isiyo ya kawaida na ni muujiza kumpata mtu kama huyo katika ulimwengu wa kawaida.

Kiwango cha ulaji na aina ya vyakula anavyokula Jeta hakuelezeki kwa kutumia nadharia za kisayansi wala za kihalisia bali kwa kutumia uhalisiamazingaombwe. Maelezo hayo yanashadidiwa na mhimili wa uhalisiamazingaombwe unaotumiwa kuchanganulia data katika sehemu hii. Mhimili huo unadai kuwa uchawi na mazingaombwe unatoa kipaumbele kwa mazingira na viumbe wa ajabuajabu kama mazimwi, mashetani, mizuka, majitu, majini pamoja na misitu mikubwa, wanyama, mito na bahari pamoja na matumizi ya baadhi ya tanzu za fasihi simulizi kama visasili, istiara na hurafa kwa kupeleka hadhira katika safari ya hali na matukio ya kweli na yanayowezezana. Mhimili huu ni faafu kwa sababu ulimwezesha mtafiti kuchungunguza istiara kama cha ulafi wa Jeta kama kisa cha kawaida kinachowakilisha matukio ya kweli katika mazingira halisi katika jamii husika. Zamora (2005) anakubaliana na mawazo hayo kwa kusema kuwa, kwa ujumla, uhalisiamazingaombwe hutambulishwa kwa sifa yake ya kuunda maana ya kimazingaombwe kwa kuangalia vitu vya kawaida kwa namna isiyo ya kawaida.

Katika mazingira asilia ya Shaaban Robert kuna visa vya watu waliokuwa walafi, waroho na walioweza kula chakula kingi kupita kawaida ya ulaji wa binadamu. Inaelezwa na Jafari Mhunzi kuwa baadhi ya watu hao walikuwa wamerushiwa uchawi wa majini ya kula kupindukia. La ajabu ni kuwa walikuwa wakila chakula

kingi sana lakini watu waliokuwa wakishuhudia ulaji huo ndio waliokuwa wakivembewa kwa kujaa gesi tupu katika matumbo yao. Mfano wa ulaji uliopitiliza ni kisa cha Nondo mla vyote (taz, uk. 65).

Nondo aliweza kula kilo ishirini za wali, mikungu kumi za ndizi, mbuzi mzima peke yake na kunywa ndoo tano za maji mara moja bila kushiba. Inawezekana kisa hiki ndicho cha mfalme Jeta wa nchi ya Majuju alichokitumia Shaaban Robert katika riwaya ya *Kusadikika* na badala ya kutumia jina la Nondo akamwita Jeta (*Kusadikika*, uk. 23). Kama ni hivyo, itakuwa wazi kuwa Shaaban Robert hapa pia aliathiriwa kwa kiwango kikubwa na mazingira yake asilia katika kutumia istiaru ya mfalme Jeta wa nchi ya Majuju.

Shaaban Robert kutumia istiaru ya ulaji uliopitiza wa mfalme Jeta katika riwaya ya *Kusadikika* kwa sababu ya kuwapo kwa visa vya ajabu kama hivyo katika mazingira yake asilia (ulaji wa Nondo) kunahalalisha mawazo ya Bowers (2004). Bowers akimthibitisha Alejo Carpentier kama mwasisi wa uchawi na mazingaombwe huko Amerika Kusini na kama mwandishi wa riwaya na mhakiki; anasema kwamba Carpentier anaeleza uhalisia kwa uwazi zaidi ambapo vipengele vya uajabu vinajipenyeza kwa namna inayofanya hali ibaki ya kawaida na katika uasilia wake. Anasisitiza kuwa uandishi wa Carpentier ulijitenga kabisa kutoka katika uchoroaji wa Roh. Carpentier alikusudia, kwa kuvutwa na tofauti ya kihistoria, kijiografia, kijamii, kisiasa, kivisasili, na kiimani ya Amerika Kusini inayoonekana si ya wazi pamoja na uajabu wake, kudhihirisha kuwa vitu vya kiajabu vinawezekana. Zaidi ya yote maoni ya Carpentier ni kuwa Amerika Kusini ni bara iliyojaa maajabu, na hivyo kuandika juu ya bara hili huzaa Sanaa ya uhalisiajabu.

Nondo katika mazingira asilia ya Shaaban Robert alikuwa mlafi na mroho wa kupindukia kiasi kwamba watu walikuwa wanaficha chakula wakimwona anakuja la sivyo alikuwa anakula chakula chote na kuwaacha wengine wakiwa na njaa (taz, uk. 65). Kwa hiyo inawezekana Shaaban Robert ametumia ulafi na uroho wa Jeta ili kuelezea matendo ya viongozi waroho, walafi, wenye tamaa na wasiotosheka. Hawa viongozi hawaridhiki hata kama watachukua mali yote ya nchi kwa faida yao binafsi. Mwandishi anasema:

Mfalme alitaka kumla Kabuli bila kugawana na wawinda waliomkamata. Choyo chake kikubwa kiliwaudhi wawinda, pakatokea vita kati ya majeshi ya mfalme na raia. Kwa vita hivyo kila kitukilichokuwa na uhai kiliangamizwa (*Kusadikika*, uk. 23).

Katika uhalisia wa maisha ni ajabu na ni muujiza kupata taifa lenye watu wenye meno yanayoweza kutafuta kitu kigumu zaidi duniani, lenye mfalme mwenye kinywa kipana cha kuhimili kupitisha maji ya mto mkubwa na mrefu wenye maji yanayotiririka pamoja na tani milioni za miamba, chuma, magogo na samaki kwa dakika tano na kulia kiu njaa, kiu njaa, kila baada ya dakika moja. Msomaji wa kawaida anaweza kuhadaika kwa kuishia kucheka kwa kushangaa ulafi huo bila kuchunguza maana ya ndani iliyokusudiwa na mwandishi.

Swali la kujiuliza ni kwa nini Shaaban Robert atumie istiara ya uroho wa Majuju na ulafi wa mfalme wao Jeta badala ya kutumia lugha ya wazi bila kucha mawazo yake? Ili kulijibu swali hilo ni vyema kufahamu hali ya siasa katika nchi za Afrika Mashariki wakati wa utunzi wa riwaya ya *Kusadikika*.

Omary (2011) akielezea maana ya siasa anahitimisha kwa kusema kuwa siasa ya jamii husika ndiyo huamua aina ya mfumo wa maisha ambayo itafuatwa na

wanajamii wake. Katika siasa ndipo sera, mipango, bajeti na maamuzi kuhusu miradi ya maendeleo hutolewa na kuletwa mbele ya wananchi kwa ajili ya utekelezaji. Hii ni sawa na kusema kuwa masuala ya kisiasa ndiyo huongoza masuala ya uchumi, utamaduni na ya kijamii kwa kiasi kikubwa. Uongozi na mfumo wa utawala katika jamii hujengwa na kusimamiwa na siasa. Mfumo wa utawala katika jamii unapokuwa wa kitabaka, watunzi wa kazi za fasihi katika jamii hiyo wanatakiwa kuandika kazi zinazosifia au kuikosoa tabaka fulani katika jamii hiyo. Hii ni kwa sababu fasihi ni mali ya jamii na jamii inapokuwa na matabaka kazi ya fasihi lazima iwe mali ya tabaka mojawapo kati ya matabaka yanayojitokeza katika jamii hiyo. Kwa hiyo tabaka tawala litataka lisifiwe na kuenziwa katika kazi za fasihi hata kama linafanya mabaya kiasi gani. Kinyume cha hapo kazi hizo zitakumbana na rungu la udhibiti. Hivyo basi kama mtunzi anakusudia kuzungumzia makosa ya tabaka tawala atalazimika kutumia lugha ya mficho ili kukwepa rungu la udhibiti.

Shaaban Robert aliandika riwaya za mwanzo kama *Maisha Yangu na Baada ya Miaka Hamsini* (1936-1946) wakati wa utawala wa serikali ya kikoloni ya Mjerumani. Katika riwaya hiyo alieleza mabaya ya serikali hiyo kwa lugha ya wazi jambo ambalo wakoloni hao hawakulifurahia. Masawe (2014: 73) akichunguza masuala ya kisiasa katika riwaya za Shaaban Robert anasema:

Kimsingi, serikali ya kikoloni iliwakataza kufanyika kwa mambo ambayo walidhani kuwa yatahatarisha uwepo wa serikali yao. Kwa mfano, walikataza uandishi wa kazi za fasihi ambazo zilionesha kutokukubaliana na matendo ya serikali hiyo.

Kwa maoni hayo ya Masawe, Shaaban Robert kuandika kwa lugha ya wazi mabaya ya wakoloni na kuikosoa serikali yao ilikuwa ni kwa hatari ya usalama

wa maisha yake. Serikali nyingi duniani hazipendi kukosolewa pale zinapofanya kinyume cha matarajio ya wananchi waliowachagua na kuwaweka madarakani. Hivyo, watunzi wa kazi za fasihi katika serikali za namna hiyo wanaogopa kuelezea hisia, manjozi, hasira na machungu ya wananchi kwa lugha ya wazi. Huu ni udhaifu mkubwa sana unaofanywa na watu waliopewa madaraka makubwa katika kuongoza nchi zao. Hii ndiyo maana Shaaban Robert kwa kumtumia Mrefu katika riwaya ya *Adili na Nduguze* anasema kuwa ufalme au uongozi ni amana kubwa inayotaka uangalifu mkubwa kwa sababu ni dhima bora iliyowekwa mikononi mwa binadamu. Wajibu wa kwanza wa kiongozi ni kuwa mwadilifu katika matendo yake. Kila tendo, jema au baya, ni mfano kwa raia wake.

Katika mahojiano yaliyofanyika kwa njia ya simu kati ya mtafiti na Ikibali, mtoto wa Shaaban Robert, katika kujibu swali kuwa anafikiri ni kwa nini Shaaban Robert hakutumia lugha ya wazi katika riwaya za *Adili na Nduguze*, na *Kusadikika* na *Kufikirika*.

Alijibu kuwa:

Baba yangu aliwahi kuniambia sababu ya kuandika kazi zake kwa mtindo wa kimazingaombwe. Alisema kuwa katika kipindi cha utawala wa serikali ya Kikoloni ya Kijerumani aliandika riwaya ya *Maisha Yangu na Baada ya Miaka Hamsini*. Mambo aliyoyaeleza humo yalikuwa yanakosoa utawala huo kwa lugha ya wazi. Ndipo watawala hao walipomwingiza katika daftari la watu hatari na kutaka kumuua. Kwa bahati Ujerumani ilinyang'anywa makoloni yake na Tanganyika kuwekwa chini ya utawala wa Waingereza na hivyo kusalimika kuuawa kwa Baba yangu. Kwa hiyo, akaona ni vema aandike kazi zake zilizofuatia kwa lugha ya mficho na ya kimazingaombwe ili serikali ya Kiingereza nayo isije ikakusudia kumuua.

Maelezo hayo ya Ikibali yanaonesha kuwa serikali ya kikoloni haikuwa tayari kukubali kukosolewa kwa jambo lolote ambalo ilifanya kinyume na matakwa ya

wananchi. Hivyo walifanya kila njia kuhakikisha kuwa wanazuia ukosolewaji wa aina yoyote ile dhidi yao. Wale walioonekana kuisema vibaya serikali ya kikoloni waziwazi au kwa maandishi maisha yao yalikuwa hatarini. Kwa mfano, Osale Otango (taz, uk. 77) kwa sababu ya kutetea haki ya wanyonge alikamatwa mkoani Tanga mwaka 1958 na kuswekwa gerezani na utawala wa kikoloni ya Mwingereza kwa lengo la kunyamazisha sauti ya Waafrika kutetea haki zao. Kwa maana hiyo, ili kukwepa uthibiti wa tabaka tawala, Shaaban Robert alitumia istiara kama namna au mtindo wa uandishi wa mficho ili kueleza ukweli kwa namna inayoifanya tabaka tawala kutong'amua kwa urahisi kuwa inasemwa au inashutumiwa kwa matendo yake maovu kwa wananchi wanyonge.

Senkoro (1995) anakiri mawazo hayo kwa kusema kuwa:

Ilimlazimu Shaaban Robert kutumia (istiara) mficho wa kitashititi kupitia kejeli na dhihaka pamoja na mambo ya ajabuajabu ili kukwepa udhibiti ambao ungeweza kuzifanya zipigwe marufuku riwaya zake zilizoeleza mabaya ya utawala wa serikali ya kikoloni (msisitizo ni wetu).

Ili kuelewa vizuri kile anachokimaanisha Senkoro katika maelezo yake hapo juu ni vyema maana ya kejeli na dhihaka zinapotumika katika mambo ya ajabuajabu ikawekwa bayana.

Msokile (1992: 227) anaeleza kejeli kuwa ni tamathali inayokusudiwa kuleta maana iliyo kinyume na ile iliyokusudiwa au kinyume na ukweli ulivyo. Lengo hasa ni kutaka kuzuia matatizo na migongano pindi itumikapo kwa lengo maalumu la kufundisha na kuasa. Wakati mwingine kejeli ina maana ya kuchekelea mtu, kumdharau, na kumchusha kwa mzaha. Ni usemi ambao maana yake ya ndani ni kinyume chake, na inabeua maana yake halisi. Ni kebehi ambapo kismwacho sicho kikusudiwacho.

Dhahaka nayo imeelezwa na Kuhenga (1975) kama aina ya tamathali ya dharau yenye lengo la kumweka mtu katika hali duni kupita kiasi, lakini kwa mbinu za kimafumbo. Mara nyingine mtu anayedharauliwa hujifahamu, lakini mara nyingi huwa hajifahamu. Wanaomsema kwa kawaida hujua bezu zote juu ya mtu huyo. Senkoro (2011: 13) anashadidia maana hiyo ya Kuhenga kwa kusema:

Dhahaka ni tamathali yenye ubeuzi mkali, jahili unaopenya kweli kweli. Hutoa maneno ambayo kijuujuu yanasikika vizuri sana masikioni kwani yamejaa utani, mzaha na masihara, lakini maneno hayo hayo huwa yamekusudiwa yatoe maana iliyo kinyume chayo kabisa.

Kwa maelezo hayo ya Msokile, Kuhenga na Senkoro inaweza ikasemwa kuwa Senkoro anamaanisha kuwa, kwa kuogopa kudhibitiwa na serikali ya kikoloni ya Mwingereza, Shaaban Robert aliamua kutumia istihara kama mtindo wa sanaa ya lugha kuyasema maovu ya mkoloni bila serikali hiyo kumaizi kuwa inasemwa. Kwa mawazo ya Senkoro, Shaaban Robert ametumia ulafi, uroho na ubinafsi wa Mfalme Jeta ili kuicheka, kuonyesha dharau, kukebehi na kuidunisha kupita kiasi serikali ya kikoloni.

Shaaban Robert kwa kutumia mhusika wa kimazingaombwe, Mfalme Jeta, amesema serikali ya kikoloni bila serikali hiyo kutambua kuwa inasemwa. Kinyume chake Waafrika waliokuwa wanakandamizwa na ambao kila walichokuwa wakikizalisha kilikuwa kinachukuliwa na wakoloni walafi na wasiotosheka, ilikuwa rahisi kwao kung'amua kuwa Shaaban Robert anazungumzia maovu na ulafi wa serikali ya kikoloni iliyokuwa inasomba mali na kila kitu kilichokuwa kinapatikana Afrika bila kutosheka. Zaidi ya yote Shaaban Robert alikuwa anaibezwa, kuicheka na kuidunisha kupita kiasi serikali hiyo, yaani serikali lafi, isiyotosheka na isiyochagua halali wala haramu: chuma,

mwamba, magogo na samaki vyote kwa mamilioni ya tani pamoja na mkondo wa maji hubugiwa kila dakika tano na mtu mmoja, mkoloni, bila kuchambua. Mwisho anaikebehi kuwa licha ya kusomba kila kitu kutoka Afrika lakini haishibi, haitosheki wala kuridhika. Kila dakika moja, baada ya kumeza tani zote hizo, Jeta analia kiu njaa, kiu njaa (*Kusadikika*, uk. 23).

Kezilahabi badala ya kutumia istihara moja kwa moja katika riwaya za *Nagona* na *Mzingile* anamwamisha msomaji kutoka katika mazingira ya kawaida ya ulimwengu unaojulikana hadi katika ulimwengu wa kimazingaombwe, ulimwengu wa kuzimuni, ulimwengu wa nusu kuwa macho na nusu kuwa ndotoni, ulimwengu wa kindoto baina ya uhai na kifo (Mbatih, 1988). Kwa mfano, anapozungumzia athari za mwingiliano kati ya utamaduni wa Kiafrika na wa nchi za Magharibi, anatumia ndoto ya utamaduni wa Mwafrika. Ndoto kama ilivyokwishaelezwa kuwa ni sehemu ya uchawi na mazingaombwe kwa sababu katika ndoto mambo yote yanawezekana na mhusika anakuwa na nafsi mbili. Nafsi tulivu na nafsi inayotembea ndotoni kichawi na kimazingaombwe. Katika ndoto hii, msichana anayewakilisha utamaduni wa Kiafrika anajitokeza kama mhubiri akihutubia wanawake na mara anakamtwa na kupelekwa katika jengo la Olympus. Katika jengo hili muziki unachezwa na wachezaji ni wasichana, wakati wengi wa watazamaji ni watu mashuhuri na wenye heshima katika jamii kulingana na nafasi zao. Mwandishi anasema:

Katika mstari wa mbele walikuwa wamekaa wanasiasa mashuhuri kutoka nchi mbalimbali, ... Nyuma yao walifuata viongozi wa dini mbalimbali... Wakuu wa dini walifuatiwa na maprofesa wa vyuo vikuu na walimu wa vyuo vidogo...(*Mzingile*, uk. 68).

Kezilahabi amezungumzia ndoto hii kufaulisha kuzungumzia mwingiliano wa utamaduni wa Kiafrika na utamaduni wa Kimagharibi. Anazungumzia jinsi wasomi, wanasiasa na viongozi wa dini wanaotarajiwa kusimamia maadili ya jamii na kukemea maovu wanavyofurahia muziki ya uchi inayodhalilisha utamaduni wa Mwafrika kwa kigezo tu kwamba biashara hiyo inasimamiwa na watu kutoka nchi za Ulaya bila kufikiria madhara yake kwa nchi zao. Kucheza uchi katika muziki wa ‘Olympus’ ni mfano mojawapo wa biashara isiyokubaliana na utamaduni wa Kiafrika. Ni udhalilishaji wa utu wa mwanamke pamoja na kuchukua rasilimali za Afrika kwa kutumia biashara haramu na ya kufedhehesha. La ajabu ni kuwa wale wanaojaribu kutetea utamaduni wa Kiafrika wanaonekana washamba waliopitwa na wakati na wasiotetewa hata na Waafrika wenzao. Hii ni kwa sababu msichana yule aliyetetea utu na utamaduni wa Kiafrika kwa kukataa kucheza uji mbele za watu aliitwa mshamba na kuuawa na Waafrika wenzake wanaopenda kulamba makombo ya Wazungu.

Mwandishi anasema:

Meneja...akaenda jukwaani kutoa tangazo. “Samahani wateja wapenzi. Ni juzi tu tumemleta toka msituni. Bado sijamwingiza katika muundo wa uchumi wa ulimwengu, na hajazoea mwanga wa aina hii! Lakini nitamfundisha ustaarabu!...Walimfunga wakampeleka chumbani kwa meneja. Baada ya kumpiga viboko walimfungua. Alianza tena kupigana nao. Walimuua akipigana. Walimnajisi amekufa (*Mzingile*, uk. 75).

Ni muundo gani wa uchumi wa ulimwengu ambao meneja anauzungumzia ambao msichana huyu anaukataa, kama sio kupata pesa kwa kuuza utu wao kwa kucheza uchi na kumwingizia meneja pesa nyingi sana na wale wasichana kupata kwa siku moja pesa inayozidi mshahara wa profesa kwa mwezi? Kinachoshangaza ni viongozi wanaotakiwa kukemea na kutokomeza machafu na uozo kama huo ndio wa kwanza kuushangilia na hivyo kuufumbia macho.

Kezilahabi ametumia istiaara ya ndoto ya utamaduni wa Mwafrika kama lugha ya mficho kuwasema viongozi wa Kiafrika wanaofurahia rasilimali za nchi zao kuchukuliwa na wageni bila wao kujali, huku matendo na biashara ovu zinazoendeshwa na wageni zikionekana kama burudani kwao. Hata hivyo, kufa kwa msichana huyo akipigana kunawakilisha baadhi ya Waafrika waliodhamiria na ambao wako tayari kutetea utu na utamaduni wao mpaka tone la mwisho la damu. Kifo hicho pia kinaonesha kwa kiasi fulani kushindwa kwa utamaduni wa Mwafrika dhidi ya machafu yote yanayoletwa na utamaduni wa Kimagharibi kwa kigezo cha maendeleo ya kiuchumi yanayoambatishwa katika soko huria.

Swali la kujiuliza ni kwa nini Kezilahabi atumie istiaara kwa namna ya ndoto na mandhari ya kuzimuni zaidi katika *Nagona* na *Mzingile* tofauti na uandishi wake katika riwaya zake tangulizi?

Mbatiah (1998) ameupa uandishi wa Kezilahabi wa *Nagona* na *Mzingile* anuani “Mienendo Mipya Katika Uandishi wa Kezilahabi”. Anasema Kezilahabi ameulasi uandishi wake wa awali wa uhalisia alioutumia katika riwaya zake za kipindi cha kwanza ambazo ni *Rosa Mistika* (1971), *Kichwamaji* (1974), *Dunia Uwanja wa Fujo* (1975) na *Gamba la Nyoka* (1979). Kubadilika kwa uandishi wa Kezilahabi una historia yake katika nyuso za udhibiti wa kazi za fasihi nchini Tanzania. Kezilahabi aliandika riwaya ya *Rosa Mistika* (1971) miaka minne baada ya kutangazwa kwa Azimio la Arusha nchini Tanzania.

Senkoro (1993) anasema kuwa kutangazwa kwa Azimio la Arusha kulileta matumaini mapya kwa wananchi kutokana na maadili na ahadi zilizokuipo ndani ya azimio hilo. Hata hivyo maadili yaliyotangazwa na wanasisa jukwaani yalikuwa kinyume kabisa na matendo yao. Kezilahabi kwa kuona hili akaandika

Rosa Mistika kukemea maovu hayo. Matokeo yake kitabu kilipigwa marufuku na Wizara ya Elimu kwa madai kuwa kilikiuka maadili ya jamii kwa kueleza mambo ya aibu kwa wazi. Sababu kubwa haikuwa kueleza mambo ya aibu kwa wazi, bali ilikuwa kusema mambo hayo ya aibu yanafanywa na nani. Mambo hayo ya aibu yalikuwa yakifanywa na baadhi ya viongozi ambao wamepewa dhamana kubwa ya kusimamia utekelezaji wa maadili mema katika jamii. Hatua hii ya kupigwa marufuku kwa *Rosa Mistika* ni kinyume kabisa na mawazo ya Nyerere (1968) anayesema kuwa:

Kila mmoja ana uwezo wa kusema kwa uhuru kabisa, na maneno ya kila mtu sharti yasikilizwe hata kama mawazo ya mtu huyo yamepotoka kiasi gani au hayapendwi kiasi gani.

Mawazo haya ya Nyerere ni ya muhimu kabisa. Hii ni kwa sababu kutumia mamlaka uliyopewa kuzuia au kuzima mawazo ya mtu mwingine kwa sababu tu hayaendani na matakwa yako binafsi au matendo yako maovu ni kuwanyima watu uhuru wa kuzungumza. Katika wiki ya kumbukizi ya miaka ishiriki ya kifo cha Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, Rais wa kwanza wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Oktoba, 2019; Rais Mstahafu wa awamu ya nne, Jakaya Mrisho Kikwete, aliyashadidia maneno hayo ya Nyerere kwa kusema maneno yafuatayo:

“Dhamana ya uongozi haikufanyi uwe mtu zaidi ya raia mwingine yeyote, haikufanyi wewe uwe na haki zaidi kuliko mtu ambaye si kiongozi. Kujishusha hakukufanyi usiwe kiongozi, kujifanya mwamba wala hakukufanyi uwe kiongozi zaidi... unapokuwa na binadamu wenzako fahamu kuwa nao ni binadamu kama wewe. Mawazo hayapigwi rungu, mawazo yanashindwa na mawazo yaliyo bora zaidi (Gazeti la Mtanzania, Oktoba 9, 2019, uk. 4)”.

Mawazo hayo ya Nyerere yaliyosisitizwa na Kikwete yanatokana na ushauri alioishautoa Shaaban Robert kwa watawala katika riwaya ya *Adili na Nduguze* kama ilivyokwisha dondolewa kuwa:

...mfalme ni naibu wa Mungu duniani. Kwa hiyo, ufalme ni amana kubwa. Amana hiyo ilitaka uangalifu mkubwa kwa sababu ni dhima bora iliyowekwa mikononi mwa binadamu. Wajibu wa kwanza wa mfalme ni kuwa mwadilifu katika matendo yake. Kila tendo, jema au baya, ni mfano kwa raia wake (*Adili na Nduguze*, uk. 29).

Kwa maelezo hayo watawala wanatakiwa kuongoza kwa kufuata maadili mema, kwa uadilifu mkubwa, kwa kujiona sawa na raia wengine wa kawaida, kwa kuwapa wananchi pamoja na waandishi nafasi ya kutoa mawazo yao kwa uhuru kabisa ili wawe mfano bora kwa raia wao.

Serikali nyingi zimeshindwa kutimiza mambo hayo na badala yake sheria zinatungwa ili kulinda maslahi ya watawala huku zikiwanyima waandishi wa kazi za fasihi kutoa mawazo yao kwa uhuru kabisa. Kwa mfano, kitendo cha Adili kuwaombea ndugu zake wasiuawe na jini, Huria binti Kisasi, ingawa walifanya maovu yanayostahili kifo kunaonesha udhaifu katika mahakama zetu. Hii inasisitizwa na Adili na Huria. Adili anasema kuwa jaribu la jinai halikutosha kuhalalisha adhabu ya kifo duniani. Kinyume chake Huria anasisitiza kuwa jaribu na jinai lilitosha kuhalalisha adhabu ya kifo ujinini. Huria anashangazwa na sheria za wanadamu zinazoonekana kutatiza na hivyo akahitimisha kuwa wanadamu watakuwa hatarini milele (*Adili na Nduguze*, uk. 40).

Hali ya kutatiza kwa sheria inajitokeza pia katika mahakama ya Kusadikika amabapo mashtaka mengi yalikubaliwa bila ya swali wala kiapo. Kama mashtaka yaliletwa mbele ya baraza na wafalme, watoto wao, matajiri, au watu wengine

maarufu nguvu ya desturi hii ilifanywa mara dufu. Hapana shaka kuwa salama ya watu wadogo ilikuwa kidogo sana katika nchi hii (*Kusadikika*, uk. 7).

Sengo (1992: 58) anasisitiza kuwa ili kuwatendea haki wananchi, sheria inastahili uhuru wa kujitetea. Anakazia kwa kusema:

Ni jambo linalosikitisha kuona kwamba baadhi ya sheria zinatungwa katika baadhi ya nchi kuwakandamiza baadhi ya watu. Kinachosikitisha zaidi ni kile kitu kinachopunguza hadhi ya haki ya watu hao. Ubora wa sheria ni kutobagua. Sheria ikishatungwa kwa ajili ya watu, ni lazima ifuatwe na watu wote. Ikiwa kutakuwa na ubaguzi wa aina yoyote, masazo ya watu wataanza kuikebehi na kutofautiana na sheria ipasavyo. Na hali ikiwa hivyo, usalama wa nchi utapungua na mahala pake vurugu na dhuluma zitashika nafasi hiyo.

Hii ndiyo maana Karl Marx (1962) aliwahi kusema kuwa Sheria inaniruhusu kuandika lakini kwa sharti moja kuwa niandike kwa mtindo usio wangu. Ninayo haki ya kuonyesha undani wa mambo, lakini nalazimishwa niuonyeshe undani huo kwa kupitia kauli isiyo yangu. Mimi ni mcheshi lakini sheria inaniumrisha niandike bila mzaha wowote; mimi hupenda kusema mambo bila kuficha, lakini sheria hainitaki niandike hivyo. Kwa mawazo hayo ya Karl Marx inaweza kusemwa kuwa mbali na sababu zingine, Shaaban Robert na Euphrase Kezilahabi wametumia istiara katika riwaya zao teule kwa kulazimishwa, yaani kwa kuogopa rungu la dola. Hii ina maana kuwa ili kazi zao zisidhibitiwe wamelazimika kuandika kwa mtindo usio wao, wameonyesha undani wa mambo kwa kauli zisizo zao na kuandika kwa kuficha ukweli wa mambo kinyume cha matashi yao.

Kutoa habari hizi kama ndoto ni namna ya kukwepa udhibiti kwa sababu ndoto haihukumiwi. Kezilahabi ametumia mbinu hii ya ndoto kwa kuathiriwa na Biblia. Katika Biblia watu mbalimbali na manabii wameota au kutafsiri ndoto yenye kuonesha makosa ya wafalme bila kuchukuliwa hatua yoyote. Hii ni kwa sababu

wanadai kuwa ni ndoto tu na si mawazo binafsi ya mwotaji au mfasiri. Ndoto katika Biblia inachukuliwa kama inatokana na nguvu fulani iliyo nje ya mwotaji na hata kwa yule ambaye ndoto inamhusu (Biblia Takatifu: Mwanzo, 20: 6, 31: 24; Danieli, 4: 9-28). Kezilahabi kama ilivyo kwa Shaaban Robert ametumia istiara hapa kukwepa lugha ya wazi kama ilivyokuwa katika riwaya ya *Rosa Mistika* na kusababisha riwaya hiyo kufungiwa kwa muda. Kwa hiyo, sababu kubwa ya Kezilahabi kutumia istiara ni kukwepa udhibiti kutoka kwa tabaka tawala.

Tatizo linaloweza kutokea kwa mwandishi kulazimishwa kuandika kinyume cha matashi yake na ambalo limejitokeza katika *Nagona* na *Mzingile* ni kutoeleweka kwa kazi ya fasihi kwa hadhira lengwa. Riwaya za *Nagona* na *Mzingile* zimewatatanisha hata wahakiki wa kazi za fasihi na hivyo jamii kutoupata moja kwa moja ujumbe uliokusudiwa na mwandishi. Tatizo lingine ni kuwa waandishi wanaweza kuandika kikasuku kwa kuisifu tabaka tawala, na hivyo, kutoshughulikia mambo muhimu yanayozikabili jamii zao.

6.3 Kiishilio

Sura hii imechunguza matumizi ya visasili na istiara katika riwaya teule za Shaaban Robert na za Euphrase Kezilahabi. Wote, Shaaban Robert na Kezilahabi wametumia visasili katika utunzi wao. Shaaban Robert ametumia kisasili kimoja tu cha Fahari, mji uliogezwa mawe katika riwaya ya *Adili na Nduguze*. Kezilahabi kwa upande wake katika riwaya ya *Nagona* ametumia kisasili kimoja cha mji wenye watu wasioonekana kwa macho na wanaoshi kwa kula matumaini

yao yanayopatikana katika ndoto zao; na kisasili cha kuzaliwa kwa Kakulu katika riwaya ya *Mzingile*.

Shaaban Robert ametumia kisasili cha mji wa Fahari kuelezea madhara yanayoweza kuletwa na viongozi kwa raia wao kwa kushikilia ukale usiofaa, hasa mila na tamaduni za kuabudu mizimu, miti pamoja na mawe. Kezilahabi naye ametumia kisasili cha Kakulu kuzungumzia dini ya Ukristo akimlinganisha Kakulu na Yesu Kristo katika Biblia Takatifu.

Kufanana kati ya Shaaban Robert na Kezilahabi katika matumizi ya visasili ni kuwa; visa vyote ni vya ajabu visivyotarajiwa kutokea katika maisha ya kawaida. Kezilahabi kwa kiwango fulani katika riwaya ya *Nagona* anamwiga Shaaban Robert kwa kutohusisha wahusika wa kishujaa wa kihistoria au wa kuaminika ambao wanatenda matendo yanayokiuka uhalisi wa kawaida kama inavyotarajiwa katika visasili vingi. Kinyume chake katika riwaya ya *Mzingile* Kezilahabi amemtumia Kakulu mhusika shujaa wa kihistoria na wa kuaminika anayetenda mambo yanayokiuka uhalisi wa kawaida. Hii ni tofauti na Shaaban Robert ambaye hakutumia mhusika shujaa katika kisasili cha mji wa mawe katika riwaya ya *Adili na Nduguze*.

Imedhihirika kuwa Shaaban Robert ametumia istihara ya ulafi wa Jeta mfalme wa nchi ya Majuju katika riwaya ya *Kusadikika* kama sehemu ya mazingaombwe katika utafiti huu ili kuficha maana ya ujumbe aliokusudia kufahamika kwa urahisi kwa tabaka tawala. Kusudi lake lilikuwa kukwepa rungu la uthibiti kutoka kwa utawala kandamizi la kikoloni ya Mwingereza. Kezilahabi naye badala ya kutumia istihara moja kwa moja ametumia mandhari ya masimulizi ya ulimwengu

wa kuzimuni na visa vya ajabuajabu katika riwaya za *Nagona* na *Mzingile*. Lengo lake pia likiwa ni kukwepa udhibiti kutoka kwa tabaka tawala.

Sura inayofuata ndio sura ya mwisho katika utafiti huu. Majumuisho ya mambo yote yaliyofanyika katika utafiti huu yamefanywa kwa muhtasari. Matatizo, maoni na mapendekezo kwa ajili ya tafiti za baadaye yametolewa katika sura hiyo.

SURA YA SABA

MUHTASARI, MATOKEO NA MAPENDEKEZO

7.0 Utangulizi

Sura hii inatoa muhtasari wa utafiti mzima kutoka sura ya kwanza hadi ya sita. Katika sura hii matokeo ya utafiti juu ya matumizi ya uchawi na mazingaombwe katika riwaya za Shaaban Robert na za Euphrase Kezilahabi yamewasilishwa. Dhamira kuu ya utafiti huu ilikuwa ni kuchunguza athari ya mazingira asilia ya mtunzi katika matumizi ya mbinu ya uchawi na mazingaombwe katika riwaya za Shaaban Robert na za Euphrase Kezilahabi. Zaidi ya hayo pia majibu ya maswali yaliyosukuma kufanyika kwa utafiti huu yametolewa kwa kifupi baada ya uchunguzi wa kina kwa kila lengo la utafiti kufanyika. Yafuatayo ni malengo yaliyokusudiwa kufanikishwa katika utafiti huu.

- i. Kubainisha uchawi na mazingaombwe katika mazingira asilia ya watunzi wa riwaya teule.
- ii. Kuchunguza athari ya mazingira asilia ya watunzi katika matumizi ya mbinu ya uchawi na mazingaombwe katika riwaya teule.
- iii. Kulinganisha matumizi ya mbinu ya uchawi na mazingaombwe kati ya watunzi Shaaban Robert na Euphrase Kezilahabi.

Malengo hayo yamechunguzwa kwa kutumia misingi ya nadharia ya Uhalisiamazingaombwe na Kiwewe cha Kuathiriwa ambazo ndizo zilipendekezwa kuongoza utafiti huu. Sura hii inamalizia kwa kutoa maoni na mapendekezo kwa ajili ya tafiti zaidi.

7.1 Muhtasari wa Utafiti

Utafiti huu umechunguza matumizi ya uchawi na mazingaombwe katika riwaya za *Adili na Nduguze*, *Kusadikika* na *Kufikirika* za Shaaban Robert pamoja na *Nagona* na *Mzingile* za Euphrase Kezilahabi. Matumizi ya uchawi na mazingaombwe yaliyochunguzwa katika riwaya hizo ni wahusika wa ajabu, matukio ya ajabuajabu, uvujivu wa kaida za uhasilia pamoja na matumizi ya visasili na istiaru. Matumizi hayo ya uchawi na mazingaombwe yalilinganishwa kati ya Shaaban Robert na Euphrase Kezilahabi kwa kuyahusisha na uwepo wake katika mazingira asilia ya watunzi hao. Utafiti huu umegawanyika katika sura sita.

Sura ya kwanza imechunguza vipengele muhimu vinavyohalalisha kufanyika kwa utafiti huu. Vipengele hivyo ni pamoja na usuli wa utafiti ambapo maana ya uchawi na mazingaombwe imewekwa bayana. Vipengele vingine ni suala la utafiti, maswali na malengo ya utafiti, sababu za kuchaguliwa kwa mada, upeo na mipaka ya utafiti na yaliyoandikwa kuhusu mada. Si hivyo tu, pia sura hiyo imefafanua misingi ya nadharia pamoja na mbinu za utafiti ambapo nadharia mbili zimetumika. Nadharia hizo ni nadharia ya Uhalisiamazingaombwe iliyoasisiwa na Franz Roh (1925) na Kiwewe cha Kuathiriwa iliyoasisiwa na Harold Bloom (1973).

Sura ya pili imechunguza uwepo wa matumizi ya uchawi na mazingaombwe katika mazingira asilia ya watunzi wa riwaya teule. Lengo lilikuwa ni kuthibitisha kama kuna matumizi ya uchawi na mazingaombwe katika mazingira asilia ya watunzi hao. Imebainika wazi kuwa kuna visa na matukio mengi sana ya uchawi

na mazingaombwe katika mazingira asilia ya watunzi wa riwaya tajwa. Matukio na visa hivyo vya uchawi na mazingaombwe vilivyoko katika mazingira asilia ya watunzi vimetumiwa kama rejea za uchanganuzi katika sura zilizofuata (sura ya 3 hadi ya 6) kuthibitisha kama watunzi wa riwaya tajwa wametumia uchawi na mazingaombwe kwa sababu ya kuathiriwa na mazingira yao asilia au la.

Sura ya tatu imechunguza athari ya mazingira asilia ya watunzi katika usawiri wa wahusika wa ajabu katika riwaya teule za Shaaban Robert na za Euphrase Kezilahabi. Lengo lilikuwa ni kuchunguza athari ya mazingira asili ya watunzi katika matumizi ya mbinu ya uchawi na mazingaombwe katika riwaya teule na kulinganisha matumizi ya uchawi na mazingaombwe kati ya Shaaban Robert na Euphrase Kezilahabi. Imebainika kuwa wote Shaaban Robert na Euphrase Kezilahabi wameathiriwa na mazingira yao asilia katika kutumia kwao wahusika wa ajabu katika riwaya teule. Zaidi ya kuathiriwa na mazingira asilia Shaaban Robert ameathiriwa kwa kiasi fulani na masimulizi ya Alfu Lela Ulela wakati Euphrase Kezilahabi ameathiriwa na Maandiko Matakatifu ya Biblia pamoja na lugha ya Kilatini aliyojifunza katika seminari ya Kikatoliki.

Imebainika kuwa wote Shaaban Robert na Euphrase Kezilahabi wametumia wahusika wa kisaikolojia kama wanyama, ndege, majini, majitu, mashetani na malaika lakini matendo na tabia ya wahusika wa Shaaban Robert yanakaribiana na matendo ya watu wa kawaida wanaofanya mambo ya ajabu katika maisha hali. Kinyume chake wahusika wa ajabu wa Kezilahabi uhalisia wao haupambanuliki vizuri. Wakati Shaaban Robert anapotumia mbinu za kijadi au nduni za fasihi simulizi kwa kiwango kikubwa katika kuwapambanua wahusika; Kezilahabi

anatumia wahusika wengi batili ambao kwa kiwango kikubwa ni wahusika wa kiusasabaadaye.

Shaaban Robert amewatumia wahusika wa ajabu kuelezea umuhimu wa kutenda mema na kuisisitiza kuwa kila mmoja hulipwa kadri ya matendo yake. Anasisitiza mabadiliko kwa kuhimiza jamii kuachana na mila potofu na ukale usio na faida kama vile ibada ya kimizimu. Kezilahabi kwa upande wake ametumia wahusika wa ajabu kujaribu kueleza umuhimu wa kufikiri. Amewatumia pia wahusika hao kutaka kumweleza Mungu kuwa ni nani, suala ambalo ameshindwa kupata uvumbuzi wake. Zaidi ya yote amewatumia wahusika hao kujaribu kutaka kufumbua fumbo la maisha baada ya kifo. Suala ambalo bado pia limekuwa ni kitendawili ambacho jibu lake bado halijapatikana. Hata hivyo anahimiza kuwa ili kupata majibu hayo kinachotakiwa ni kufikiri.

Sura ya nne imechunguza matumizi ya matukio ya ajabuajabu katika riwaya teule za Shaaban Robert na za Euphrase Kezilahabi. Lengo lilikuwa kuchunguza athari ya mazingira asilia ya watunzi katika matumizi ya matukio ya ajabuajabu katika riwaya teule. Imebainika kuwa watunzi wote wawili wametumia kwa kiwango kikubwa matukio ya ajabuajabu katika riwaya zao teule ingawa kwa viwango tofauti kwa kila riwaya. Pia kuna viwango mbalimbali vya kufanana na kutofautiana kati ya waandishi hao katika kutumia kwao matukio ya ajabuajabu. Matukio mengi ya ajabuajabu katika riwaya za Shaaban Robert yameelezwa kama visa, na kwa kutumia nduni za fasihi simulizi. Sababu za kutokea kwake zimeelezwa wazi na watendaji, watendewa na watendwa wote wanaonekana kwa macho na mara nyingine wamehusishwa hata na washuhudiaji au watazamaji.

Kinyume chake katika riwaya za Kezilahabi matukio mengi ya ajabuajabu yameelezwa kwa muhtasari na kwa mfululizo wa taswira au jazanda. Watendaji wengi wa matukio hayo haowaonekani ingawa matokeo ya matendo yao ni bayana.

Sura ya tano imechunguza matumizi ya uvunjivu wa kaida za uhalisia katika riwaya teule za Shaaban Robert na za Euphrase Kezilahabi. Lengo lilikuwa kuthibitisha kama uvunjivu wa kaida uliomo katika riwaya teule umetokana na athari ya mazingira asilia ya watunzi wa riwaya hizo au la. Hili kufaulisha lengo hilo, uvunjivu wa kaida uliomo katika riwaya teule ulibainishwa na kuchunguzwa uwepo wake katika mazingira asilia ya watunzi hao. Imebainika kuwa mazingira asilia ya watunzi yameathiri kwa kiwango kikubwa matumizi ya uvunjivu wa kaida za uhalisia katika riwaya teule.

Wote Shaaban Robert na Euphrase Kezilahabi wametumia sana uvunjivu wa kaida za mahali au mazingira, uvunjivu wa kaida ya mbali na karibu na uvunjivu wa kaida za kimawasiliano kati ya binadamu na viumbe wengine. Shaaban Robert hakutumia kabisa uvunjivu wa kaida kati ya uhai na kifo. Pia hakutumia ndoto kwa maana halisi ya ndoto na zaidi ya yote ametumia uvunjivu wa kaida za wakati katika riwaya ya *Kusadikika* pekee. Kinyume chake Kezilahabi licha ya kutumia sana ndoto na uhalisia na uvunjivu wa kaida za kuhesabu wakati pia ametumia uvunjivu wa kaida kati ya uhai na kifo.

Sura ya sita imechunguza matumizi ya visasili na istiara katika riwaya teule za Shaaban Robert na za Euphrase Kezilahabi. Lengo lilikuwa kubainisha athari ya

mazingira asilia ya watunzi katika matumizi ya visasili na istiara katika riwaya teule.

Wote, Shaaban Robert na Kezilahabi wametumia visasili katika utunzi wao. Shaaban Robert ametumia kisasili cha Fahari, mji uliogeuzwa mawe kuelezea madhara yanayoweza kuletwa na viongozi kwa raia wao kwa kushikilia ukale usiofaa, hasa mila na tamaduni za kuabudu mizimu, miti pamoja na mawe. Mila kama hizi zimepitwa na wakati. Badala yake Shaaban Robert anapendekeza kuwa jamii za Kiafrika zipokee imani ya dini ya Kikristo na Uislamu badala ya kushikilia umizimu usio na faida yoyote.

Mwisho kabisa katika sura ya saba kuna muhtasari wa sura zote za utafiti huu na matatizo yaliyojitokeza na namna yalivyokabiliwa pamoja na maoni, mapendekezo na mchango wa utafiti.

7.2 Matokeo ya Utafiti

Utafiti huu umeshughulikia malengo matatu. lengo la kwanza lilikusudia kubainisha matumizi ya uchawi na mazingaombwe katika mazingira asilia ya watunzi wa riwaya teule. Matokeo yamedhihirisha kuwa uchawi na mazingaombwe ilikuwepo na bado hata sasa inatumika sana katika mazingira asilia ya watunzi wa riwaya teule. Katika mazingira asilia ya Shaaban Robert, kwa mfano, kuna mwingiliano mkubwa sana kati ya wanadamu na majini. Mwingiliano huo umesababisha matumizi mengine ya uchawi na mazingaombwe yaliyochunguzwa kwa upande wa Shaaban Robert kuwa na mwingiliano mkubwa na uwepo wa majini.

Tofauti na mazingira asilia ya Shaaban Robert, katika mazingira asilia ya Kezilahabi kuna matumizi mengi ya kuvunjwa kwa kaida kati ya uhai na kifo. Hii imesababisha matumizi mengine ya uchawi na mazingaombwe kwa upande wa Kezilahabi kuhusishwa au kufanywa na watu wasioonekana, kuongea na watu wanaohisiwa kuwa wamekufa lakini wanarudi na kufanya baadhi ya matukio yanayofanywa na watu walio hai; misitu, meli au mitumbwi inayotembea au kuongea lakini inatoweka ghafla kusikojulikana. Kwa ufupi mazingira asilia ya Kezilahabi yamegubikwa na maluelue mengi kati ya uhai na kifo au kati ya kuwapo na kutokuwapo.

Lengo la pili lilikuwa ni kuchunguza athari ya mazingira asilia ya watunzi katika matumizi ya uchawi na mazingaombwe katika riwaya teule. Matumizi ya uchawi na mazingaombwe yaliyochunguzwa ni wahusika wa ajabu, matukio ya ajabuajabu, uvunjivu wa kaida pamoja na visasili na istihara. Matokeo yanaonesha kuwa wote Shaaban Robert na Euphrase Kezilahabi wametumia wahusika wa ajabu katika riwaya zote tano kwa kuathiriwa kwa kiasi kikubwa na mazingira yao asilia. Hata hivyo, namna na kiwango cha matumizi ya wahusika hao hutofautiana kwa kila riwaya. Shaaban Robert ametumia wahusika wa ajabu wengi zaidi katika riwaya ya *Adili na Nduguze*. Wengi wa wahusika hao wakiwa ni majini wanaoweza kubadilika katika umbo au sura tofauti, wanaoweza kuingia na kufika popote na pia kuwasiliana na binadamu bila kizuizi chochote. Riwaya za *Kusadikika* na *Kufikirika* zina wahusika wachache wa ajabu ukilinganisha na *Adili na Nduguze*. Hata hivyo wahusika hao wamebeba ujumbe muhimu uliokusudiwa na mtunzi kwa jamii husika.

Matokeo yameonesha kuwa Kezilahabi ametumia katika riwaya za *Nagona* na *Mzingile* wahusika wa ajabu wengi sana kuliko Shaaban Robert katika riwaya za *Adili na Nduguze*, na *Kusadikika* na *Kufikirika*. Karibu wahusika wote waliotumiwa na Kezilahabi katika riwaya hizi ni wa ajabu. Hii ni kwa sababu wanakosa sifa za kuwa binadamu wa kawaida. Kuna: wanaoishi kati ya uhai na kifo, wenye miguu mirefu isiyonekana miisho yake, wenye uwezo wa kubeba milima, kunywa maji yote ya mto, wenye nafsi nyingi, wenye mamilioni ya miaka ya kuishi, walioanza kuishi kabla wazazi wao hawajazaliwa, wenye miili inayotoa mwanga, wenye uwezo wa kubadilika sura mbalimbali na wenye uwezo wa kutapika na kusafisha roho zao.

Imebainika kuwa wote Shaaban Robert na Euphrase Kezilahabi wametumia matukio ya ajabuajabu katika riwaya zao kwa kuathiriwa na mazingira yao asilia ingawa kwa kiwango na kwa namna tofauti. Matokeo yanaonesha kuwa athari za kimazingira ya kijamii, kisiasa, kidini na ya kitamaduni, yamechangia kwa kiwango kikubwa kwa Shaaban Robert na Euphrase Kezilahabi kutumia visasili na istihara katika riwaya teule.

Lengo la tatu lilikuwa kulinganisha matumizi ya mbinu ya uchawi na mazingaombwe kati ya watunzi Shaaban Robert na Euphrase Kezilahabi. Matokeo ya utafiti yamebainisha kuwa tofauti mojawapo kati ya Shaaban Robert na Euphrase Kezilahabi ni kuwa Kezilahabi amechanganya sifa za usasabaadaye na nduni za fasihi simulizi katika kuwasawiri wahusika wa ajabu. Kinyume chake wahusika wa Shaaban Robert ingawa ni wa ajabu lakini wanaonesha uhalisia na uwezekano wa kupatikana katika mazingira halisi ya mtunzi. Kwa maana hiyo

riwaya teule za Shaaban Robert zinaonesha uhalisia na kuweza kuaminika na kueleweka kwa urahisi zaidi ya riwaya teule za Kezilahabi.

Matokeo yanaonesha kwamba kutumia matukio ya ajabuajabu kumemwezesha Shaaban Robert kueleza matukio halisi na ya kweli yanayotokea katika jamii. Kinyume chake matokeo yanaonesha kwamba Kezilahabi ametumia matukio ya ajabuajabu mfululilo ili kujenga katika akili ya msomaji taswira na picha ya uhalisia wa matukio hayo katika jamii.

Matokeo yanaonesha kuwa Kezilahabi ametumia kisasili cha mji wa watu wasioonekana kwa macho, wanaoishi kwa matumaini yanayozaliana katika ndoto zao kwa kuathiriwa na kisasili cha mji wa mawe cha Shaaban Robert ingawa si kwa mwigo sisisi. Kinyume chake Kezilahabi kama mwandishi fuatishi ametumia upekee na uasilia katika kisasili cha Kakulu na hivyo kujitenga na athari za kazi za Shaaban Robert na hata athari zake yeye mwenyewe katika riwaya zake tangulizi.

Matokeo yanaonesha kuwa vipengele vya uvunjivu wa kaida vilivyokuwa vinatafitiwa vimetumika katika riwaya teule ingawa kwa viwango tofauti. Jedwali lifuatalo limebainisha matumizi ya vipengele vya uvunjivu wa kaida na riwaya zilizotumia vipengele hivyo.

Jedwali na. 7.1 Uwiano wa Matumizi ya Uvunjivu wa Kaida katika Riwaya**Teule**

RIWAYA HUSIKA						
Na	AINA YA UVUNJIVU WA KAIDA	ADILI NA NDUGUZE	KUSADIKIKA	KUFIKIRIKA	NAGONA	MZINGILE
1	Mahali au mazingira	X	X	x	x	x
2	Mbali na karibu	x	x		x	x
3	Mawasiliano na viumbe wengine	x	x		x	x
4	Ndoto na uhalisia		x		x	x
5	Uhai na kifo				x	x
6	Wakati		x		x	x
	JUMLA	4	5	1	7	7

Jedwali linaonesha kuwa Kezilahabi ametumia vipengele vyote vya uvunjivu wa kaida zilizokuwa zinachunguzwa katika riwaya za *Nagona* na *Mzingile*. Shabaan Robert kwa upande wake hakutumia uvunjivu wa kaida kati ya ndoto na uhalisia, wakati pamoja na uhai na kifo katika riwaya ya *Adili na Nduguze*. Pia hakutumia uvunjivu wa kaida kati ya uhai na kifo na kujibadilisha kimazingaombwe katika riwaya ya *Kusadikika*. Katika riwaya ya *Kufikirika* Shaaban Robert ametumia uvunjivu wa kaida za mahali au mazingira pekee.

7.3 Mchango wa Utafiti

Kazi hii imechangia kwa kiasi kikubwa hasa upande wa nadharia kuwa nadharia ya uhalisiamazingaombwe ni mwafaka wa kuchambua kazi za fasihi zilizoandikwa kwa kuegemea mtindo wa uchawi na mazingaombwe.

Mchango mwingine ni kuwa tasnifu hii imefafanua na kuelekeza kuwa kazi za Shaaban Robert na za Euphrase Kezilahabi zinaweza kusomwa na kuhakikiwa kwa urahisi kwa kuyahusisha na mazingira asilia ya watunzi hao. Kuwa kwa kutumia mtindo wa uchawi na mazingaombwe msomaji na mhakiki wanaweza kusoma na kuelewa kazi za fasihi ya Kiswahili kwa urahisi, kwa kina na kwa upana zaidi.

Mchango wa tatu ni juu ya aina au mbinu za uchawi na mazingaombwe ambazo zimetumiwa katika tasnifu hii. Mbinu hizo hazikudhihirishwa moja kwa moja, hata hivyo zimejitokeza katika usawiri wa wahusika, matukio ya ajabuajabu pamoja na uvunjivu wa kaida za uhalisia. Mbinu hizo ni pamoja na kujibadilisha kimazingaombwe. Kuingia kwa namna ya ajabu bila kizuizi mahali au katika mazingira yoyote, kwa mfano, kuingia ndani ya nyumba kutokea ardhini kwa kupitia sakafu kupasuka. Kuona na kufika kwa muda mfupi sana sehemu yoyote hata ikiwa mbali kiasi gani ikiwa ni pamoja na kuona mambo yanayofanyika mbali katika mazingira mengine bila kuwepo mahali hapo. Kufanya viumbe vya asili kama miti, mawe na nyota kuongea pamoja na kuwasiliana na viumbe wengine, kwa mfano, punda, kwa kutumia lugha ya kutamkwa. Kufahamu mawazo yaliyobanwa katika akili ya mtu na kufahamu matukio yote yatakayotokea katika maisha ya mtu mpaka mwisho kwa kumtazama tu. Kuishi

kati ya uhai na kifo pamoja na kuhesabu wakati kimazingaombwe. Watunzi wa kazi za fasihi zenye mwelekeo wa mtindo wa uchawi na mazingaombwe wanaweza kutumia baadhi ya mbinu hizo katika utunzi wao katika kazi za fasihi.

Mchango wa nne ni kuwa tasnifu hii inatoa mwelekeo mpya juu ya mtazamo wa jamii na hata wasomaji na wahakiki wa kazi za fasihi kuhusu dhana za uchawi na mazingaombwe. Watu wengi wamekuwa na mtazamo hasi dhana hizi zinapotajwa na hivyo kupelekea ugumu hata wa kufanyika kwa utafiti wa kina nyanjani juu ya matumizi ya mbinu ya uchawi na mazingaombwe katika fasihi ya Kiswahili. Uchawi na mazingaombwe zimekuwa zikihusishwa kwa sehemu kubwa katika ulozi, kudhuru watu, kuua na hata kuhafifisha maendeleo. Kwa maana hiyo, wale wanaojihusisha na uchawi na mazingaombwe kuonekana kama adui wa jamii na kutazamwa kwa jicho baya na sehemu kubwa ya watu katika jamii. Utafiti huu umebaini kuwa uchawi na mazingaombwe ni dhana zilizobeba maana nyingi ndani yake, dhana hasi na chanya.

Utafiti umebaini kuwa kwa mtazamo chanya, uchawi na mazingaombwe Unaweza kutumiwa kurahisisha usafirishaji, kurahisisha mawasiliano, kutumiwa kama sehemu ya maabara kugundua aina ya magonjwa, kutibu wagonjwa bila kusafiri kwenda kwa mganga na kufahamu matatizo ya jamii na kutafuta namna ya kuyazuia kabla hayajatokea. Hivyo watunzi wa kazi ya fasihi kutokana na utafiti huu wanaweza sasa kutunga kazi zinazoegemea mtazamo chanya wa matumizi ya uchawi na mazingaombwe na hivyo kusaidia katika kubadilisha mawazo ya wasomaji na jamii kutoka katika mawazo hasi na ya kizamani juu ya matumizi ya uchawi na mazingaombwe.

Mchango wa tano ni maelezo kwa watafiti wanaotarajia kutumia nadharia ya uhalisiamazingaombwe katika kufanya tafiti zinazohusiana na athari za mazingira asilia ya mtunzi katika utunzi wa kazi ya fasihi kama ulivyo katika utafiti huu. Ni matumaini ya mtafiti kuwa mawazo yaliyotolewa katika tasnifu hii yatafungua na kuonyesha njia kwa watafiti hao ambao tafiti zao zina mwelekeo wa kichawi na kimazingaombwe.

7.4 Matatizo

Yapo matatizo au changamoto mbalimbali zilizojitokeza katika utafiti huu. Tatizo mojawapo lilikuwa ni kutofautisha dhana za uchawi na mazingaombwe. Pia istilahi nyingi zinazohusishwa na nadharia ya uhalisiamazingaombwe zimeandikwa kwa lugha ya Kiingereza na Kijerumani na zinaingiliana sana kiasi cha kupata ugumu kuzitofautisha. Ingawa baada ya masahihisho mengi na kwa uongozi wa wasimamizi tatizo hilo limetatuliwa lakini muda mwingi sana ulitumika katika kutafsiri na kuhusianisha istilahi hizo na mazingira halisi ya fasihi ya Kiswahili.

Upatikanaji wa wazee wenye umri wa miaka 60 na kuendelea ili kuwahoji kuhusu jinsi wanavyomfahamu Shaaban Robert ilileta changamoto kwa kiasi fulani kwa sababu katika ukoo wa Shaaban Robert wazee hao ni wachache sana. Zaidi ya yote wazee wenye miaka 60 na kuendelea waliopatikana wengi wanatokea Machui Hospitalini, na ingawa walitoa habari nyingi za majini na matukio ya ajabuajabu, lakini hawakuwa na habari za moja kwa moja kumhusu Shaaban Robert. Hata hivyo, data zilizotolewa na wenye umri wa miaka 60 kurudi nyuma zilitosheleza kwa ajili ya uchambuzi.

7.5 Mapendekezo

Hapa chini yametolewa mapendekezo mbalimbali hasa kuhusu masuala ambayo utafiti huu haukuyakabili ili yafanyiwe uchunguzi zaidi. Pia mapendekezo mbalimbali yametolewa kwa taasisi zinazohusika na utungaji wa sera ili zichukue hatua stahiki zinazolingana na mapendekezo hayo.

7.5.1 Mapendekezo kwa Ajili ya Tafiti Zaidi

Imebaini kuwa wakati wahakiki wengi wa kazi za fasihi wanapokubaliana kuwa kazi yoyote ile ya kubuni lazima iathiriwe na mazingira asilia ya mtunzi, wako baadhi wanaodai kuwa mazingira asilia hayana mchango wowote katika ubunaji na uundaji wa kazi ya fasihi. Wanasisitiza kuwa matini ya kifasihi inajitosheleza yenyewe na wala haitegemei kitu chochote kilichoko nje yake. Kwa kuwa utafiti huu umechunguza na kubaini kuwa mazingira asilia ya mtunzi yamechangia pakubwa katika matumizi ya mbinu ya uchawi na mazingaombwe katika riwaya teule na hivyo kuhitimisha kuwa hakuna kazi ya fasihi inayoweza kukwepa athari ya mazingira asilia ya mtunzi. Hivyo, utafiti zaidi unahitajika ili kuchunguza uhalali wa mawazo ya wahakiki wa kundi la pili kuwa mazingira yaliyomlea na kumkuza mwandishi hayana nafasi katika kazi ya fasihi wala hayana athari kwa mtunzi wa kazi husika.

Kuna haja ya kufanyika uchunguzi zaidi juu ya matumizi ya mbinu ya uchawi na mazingaombwe katika tanzu zote za fasihi ili kupanua zaidi uelewa juu ya uchawi na mazingambwe. Utafiti huu umeshughulikia riwaya teule za Shaaban Robert na za Euphrase Kezilahabi pekee. Utafiti zaidi unahitajika ili kupanua matumizi ya uchawi na mazingaombwe katika tanzu za ushairi na tamthilia.

Kezilahabi ametumia sana uduara wa wakati katika riwaya za *Nagona* na *Mzingile*. Matumizi hayo yamechangiwa kwa kiwango kikubwa sana na Biblia. Ingawa utafiti huu umegusia kwa kiasi kidogo nafasi ya Biblia katika matumizi ya uchawi na mazingaombwe, hata hivyo, kuna haja ya kufanyika utafiti wa kina juu ya athari za Biblia katika matumizi ya uduara wa wakati katika nathari za Kiswahili.

Imedhihirika katika utafiti huu kuwa kuna kuingiliana kwa kiasi fulani kati ya dini na uchawi na mazingaombwe. Na kuwa baadhi ya matumizi ya uchawi na mazingaombwe yaliyotumiwa na waandishi wa riwaya teule yametokana na imani zao katika dini zao, au usomaji wao wa Kurani Tukufu na Biblia Takatifu kama vitabu vitakatifu vya dini (Ukristo na Uislamu). Hivyo basi kuna haja ya kufanyika kwa utafiti wa kina juu ya athari za dini katika matumizi ya uchawi na mazingaombwe katika nathari za Kiswahili.

Kumekuwa na utata kwa kiasi fulani katika matumizi ya istilahi uhalisiamazingaombwe na uhalisiajabu katika utafiti huu. Kuna wataalamu wa fasihi ya Kiswahili wanaodai kuwa ni maneno mawili yenye maana moja (Senkoro, 2007; Walibora, 2010; Mohamed, 2012) na kuna wanaodai kuwa ni maneno yenye maana tofauti na pia ni nadharia tofauti ingawa zinakaribiana (Faustine, 2012 na 2017). Kwa hiyo kunahitajika utafiti zaidi kuchunguza mipaka kati ya uhalisiamazingaombwe na uhalisiajabu kama nadharia za fasihi katika nathari za Kiswahili.

Kazi hii imechunguza matumizi ya mbinu ya uchawi na mazingaombwe kwa jumla. Utafiti zaidi unahitajika juu ya athari ya mazingira asilia ya mtunzi katika

matumizi ya uchawi na mazingaombwe katika nathari za Kiswahili kwa kuzingatia tofauti za kijinsia. Hii itasaidia kubaini kuwa nani anaathirika zaidi na matumizi ya uchawi na nani anathirika zaidi na matumizi ya mazingaombwe kati ya mwanamke na mwanaume katika nathari za Kiswahili.

7.5.2 Mapendekezo kwa Wasomaji na Wahakiki wa Kazi za Fasihi

Kwa kuwa imethibitika kuwa waandishi wa riwaya teule wametumia mbinu ya uchawi na mazingaombwe kwa kuathiriwa kwa kiasi kikubwa na mazingira asilia ya jamii zao; Inapendekezwa kuwa ili kufahamu vizuri na kuhakiki kwa usahihi riwaya hizo, wasomaji na wahakiki wanapaswa kusoma na kuzihakiki riwaya hizo kwa kuzingatia muktadha wa uhalisia wa maisha katika mazingira asilia katika jamii ya watunzi wa riwaya teule.

7.5.3 Mapendekezo kwa Watunga Sera

Vyombo vinavyosimamia udhibiti vichaguliwe kwa makini, viwe na kanuni imara zinazoziongoza na zilizo wazi ili wasimamie maadili kwa uhuru kabisa bila kuingiliwa na chombo kingine chochote. Pia riwaya za Shaaban Robert zitumike kama vitabu vya kiada katika shule za upili hasa katika nchini za Afrika Mashariki. Hii ni kwa sababu vinafundisha maadili mema kwa vijana na jamii kwa ujumla.

Kwa vile jamii mbalimbali zinahesabu muda kwa namna zinazotofautiana, na hata kwa sababu kuna kutofautiana katika kuhesabu muda kwa watu walioko katika jamii moja; maoni yetu kuhusu wakati ni kuwa wakati hutumiwe vizuri ili uzalishe faida. Miaka ihesabike si kwa wingi wa siku za kuishi duniani bali kwa

yale yaliyofanyika katika miaka hiyo. Hii ina maana kuwa heshima ya mtu itokane kwanza na yale anayoyafanya na ndipo wingi wa miaka ya kuishi duniani ifuatie nyuma. Kwa mfano, kupandishwa madaraja kazini kutokane mara nyingi na kile ulichokifanyia shirika au taasisi na si kwa miaka ya kukaa kazini. Hii itakuwa sawa na maneno ya Shaaban Robert katika riwaya ya *Kusadikika* kuwa, ‘Zamani heshima ya mtu ilitokana na wingi wa mvi kichwani (miaka mingi ya kuishi) lakini sasa heshima itokane na busara ya mtu na kile anachokitendea dunia.

MAREJELEO

- Adam, A. O. (2014). "Kuchunguza Dhamira za Kijamii na Kiutamaduni Katika Riwaya ya Kiswahili: Mifano Kutoka *Kuli* na *Vuta N'Kuvute*", .Tasnifu ya Uzamivu Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.
- Allende, I. (1985). *The House of the Spirits*. London: Anchor Brendon Ltd.
- Ayiera, E. A, Ontieri, J.O Na Ayodi, N. (2017). Mchango wa Mazingira ya Mwandishi Katika Matumizi ya Mafumbo, Katika International Journal of Arts and Education 1 (1): 1-7: Serial Publishers.
- Amisah, A. B. (2005). "An Exploratory Study on the Self-concept and Spiritual Well-being of Commercial Sex Workers." Manila: De La Salle University. Thesis.
- Bloom, H. (1973). *The Anxiety of Influence*. New York: OUP.
- Bowers, M.A. (2004). *Magical Realism*. New York: Routledge.
- Brecht, B. (1964). *Brecht on Theatre: The Development of an Aesthetic*..[1st ed New York: Hill and Wang.
- Bronowski, J. (1978). *Magic Science and Civilization*. New York: Columbia University Press.
- Burton, R. F. S. (1962), *Alfu Lela Ulela*, Kitabu cha 1, 2, 3 & 4. (Edwin, W. Brenn, mfasiri). Nairobi, Kenya: Longhorn.
- Calvin, S. Hall (1947). "Diagnosing Personality by the Analysis of Dream," *Journal of Abnormal and Social Psychology*, 42, 68-79.
- Carpentier, A. (1949). *On The Marvelous Real in America*, the Introduction to His Novel *The Kingdom of This World*. Duke University Press.
- Chully (2017). Tofauti Kati ya Lugha ya Binadamu na Mawasiliano ya Wanyama. Kutoka internet Tarehe 15/05/2017.
- Clemence, J. N. (2020). *Power of Words in Human Life*. Independently Published.
- Coker, S. C. (1990), "An Endless Forest of Terrible Creatures", In *Magical Realism in West African Fiction*. New York: Routledge.
- Cooper, B. (1998). *Magical Realism in West African Fiction*. New York: Routledge.
- Croucher, S. L. (2004). *Globalization and Belonging: The Politics of Identity a Changing World*. Lenhem: Rowman & Littlefield.

- Derrida, J. (1981). *The Death of Roland Barthes*. Chicago and London: University of Chicago Press.
- D’Haen, T.L.(2005). “Magical Realism and Postmodernism”. *Decentering Priviledged Centers.*” In *Magical Realism: Theory, History, Community*, Zamora, Lois Parkinson and Wendy B. Faris, eds., Durban and London: Duke University Press.
- Durkheim, E. (1912). *The Elementary Forms of Religious Life*, Dover Publication, Inc. Mineola, New York.
- Edwin, W. Brenn, mfasiri (1928), *Alfu Lela Ulela*, Kitabu cha 1, 2, 3 & 4. Dar es Salaam: Longman Tanzania.
- Farady, A. (1972). *Dream Power*. London: Hodder and Stoughton.
- Faustine, S. (2012). “Matumizi ya Mtindo wa Uhalisiamazingaombwe katika Riwaya Teule za Euphrase Kezilahabi: Dhima na Athari zake kwa Hadhira”. *Tasnifu ya Digrii ya Uzamili Katika Fasihi ya Kiswahili*. Chuo Kikuu cha Dodoma, (Haijachapishwa).
- Faustine, S. (2017). “Falsafa ya Waafrika na Ujenzi wa Mtindo wa Uhalisiajabu katika Riwaya ya Kiswahili”.*Tasnifu ya Shahada ya Uzamivu Katika Fasihi ya Kiswahili*. Chuo Kikuu cha Dodoma, (Haijachapishwa).
- Faustine, S. (2019). “Falsafa ya Waafrika kama Kijenzi cha Mtindo wa Uhalisiajabu katika Riwaya za Kiswahili”. *Katika Koja la Taaluma za Insia*. Karljamer Publisher Limited, Dar es Salaam Tanzania.
- Flores, A. (1988). *Magical Realism Strategies: The Suppliment of Realism*.*Twentieth Century Literature* 34 (2).
- Freud, S. (1965). *The Interpretation of Dreams*, Stachey, J.Trans. Newyork: Avon.
- Gibbe, A. G. (1978). *Shaaban Robert Mshairi*, Dar es Salaam: Taasisi ya Chunguzi wa Kiswahili
- Gromov, M. (2002). *Post Modernist Element in Recent Swahili Novels*. Nairobi: The Jomo Kenyatta Foundation.
- Gromov, M. (2004). *Post- Modernistic Elements in Recent Swahili Novels*. *Nairobi Journal of Literature*, Tol. 2 (uk.28-36).
- Haji, A. V. (2018). *Kutathmini Mbinu za Usawiri wa Wahusika Katika Riwaya ya Dunia Uwanja wa Fujo na Asali Chungu: Utafiti Linganishi*. *Tasnifu ya Uzamili: Chuo Kikuu Uria cha Tanzania*

- Hegerfeld, A. (2005). *Contentious Contributions: Magical Realism Goes British*. Pg 62-81 (found in Internet)
- Hirsch, E.D. (1967). *Validity in Interpretation*, New Haven and London: Yale University Press.
- Jumane, A. (2016). Mabadiliko ya Vionjo vya Kiuandishi Katika Riwaya ya Kiswahili: Ulinganisho wa Riwaya za Shaaban Robert na Said A. Mohamed.
- Jung, C. G. (1974). *Dreams*, Princeton: Princeton University Press.
- Kalegeya, T. (2013). "Utandawazi na Riwaya ya Kiswahili: Uchunguzi Kifani wa Makuadi wa Soko Huria na Almasi za Bandia", *Tasnifu ya Uzamili*, Chuo Kikuu cha Dar es salaam.
- Kevogo, A.U (2017). Taswira ya Utandawazi Katika Riwaya Mpya ya Kiswahili. Mfano wa Riwaya ya *Dunia Yao*. Kioo cha Lugha vol. 15 Na.1(108-126)
- Kezilahabi, E. (1971). *Rosa Mistika*. Nairobi: E.A.L.B
- Kezilahabi, E. (1974). *Kichwa Maji*. Dar es Salaam: E.A.L.B.
- Kezilahabi, E. (1975). *Dunia Uwanja wa Fujo*. Dar es Salaam: E.A.L.B
- Kezilahabi, E. (1978). *Gamba la Nyoka*. Nairobi: E.A.L.B.
- Kezilahabi, E. (1985). "African Philosophy and the Problem of Literary Interpretation." PhD.Thesis: University of Wisconsin- Madison. (Haijachapishwa).
- Kezilahabi, E. (1990). *Nagona*. Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.
- Kezilahabi, E. (1991). *Mzingile*. Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.
- Khamis, S. (2007). Vionjo vya Riwaya Mpya ya Kiswahili Katika *Kioo cha Lugha* Na.5, Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.
- King'ei, K. (1999). Historia na Maendeleo ya Kiswahili, Katika *Chemichemi: International Journal of Arts and Social Sciences*, Vol. 1: Kenyatta University.
- Kombo, D. and D. Tromp (2006). *Proposal and Thesis Writing: An Introduction*. Nairobi Paulines Publication Africa.
- Kubo na Wenzake (2011). *Mwangaza wa Fasihi Simulizi*. Nairobi: The National Education Services.

- Kuhenga, C. (1975). *Tamathali za Usemi*. Dar es Salaam: EALB.
- Kurani Tukufu. Nukuu zimetoka Tafsiiri ya Mohamed Marmaduke ya Kurani Tukufu Nakala iliyofanywa mwaka (1930).
- Kwaka, M. A (2018). Uhakiki wa Wakati na Uwasilishaji Usemi Kama Vipengee vya Usimulizi Katika *Utenzi wa Nabii Isa*. Tasnifu ya Uzamili Chuo Kikuu cha Nairobi.
- Leal, L. (2009). *Magical Realism in Spanish American*. From MR: Theory, History, Community PP. 120.
- Levinson C. S. (1983). *Pragmatics*. Cambridge: Cambridge University Press.
- Lure, H. (2010). *Perspective in Social Research Methods and Analysis*. Thousands Oak Sage Publication Inc.
- Madumulla, J.S. (2009). *Riwaya ya Kiswahili, Historia na Misingi ya Uchambuzi*, Nairobi: Sitima Printers and Stationary.
- Magaju, J.K. (2004). Uhalisiajabu Katika Riwaya za Babu Alipofufuka S.A. Mohamed (2001) na Bina-Adamu! (2002) K.W.Wamitila. Tasnifu ya Shahada ya Uzamili: Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa)
- Maggati, C. N. na Wenzake. (2021). Athari ya Mazingira Asilia ya Mtunzi katika Matumizi ya Kujibadilisha Kimazingaombwe: Uchunguzi wa Riwaya Teule za S. Robert na Euphrase Kezilahabi. Katika Mulika Na. 40(2).
- Makulla, S. A. (2012). Athari za Uhalisiamazingaombwe kwa Msomaji katika Kuzielewa Kazi za Fasihi za Said Ahmed Mohamed, Tasnifu ya Uzamili Chuo Kikuu cha Dodoma. (Haijachapishwa).
- Malinowski, B. (1974). *Magic, Science and Religion and Other Essay*. London: Souvenir.
- Malugu, A. (2016). Nafasi ya Fasihi Katika Kusawiri Swala la Dini, Katika Kiswahili Juzuu Na.79, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.
- Marquez, G.G. (1967). *One Hundred Years of Solitude*. London: Pan Books Ltd.
- Marquez, G.G. (1983). *Chronicle of Death Foretold*. London: Picador Ltd.
- Marwick, M. (1970). *Witchcraft and Sorcery*. Harmondsworth: UK.
- Marx. K. (1962). Modern Continental Literary Criticism. Kutoka Katika O. B. Hardison, JR. Appleton-Century-Crofts-New York, Uk. 120.

- Masawe, B.A. (2014). Kuchunguza Masuala ya Kisiasa Katika Riwaya za Shaaban Robert. Mfano wa *Kusadikika* na *Kufikirika*. Tasnifu ya Uzamili: Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.
- Masebo na Nyangwine (2000). Nadharia ya Fasihi Kidato cha 5 na 6. Nyambari Nyangwine Publishers: Dar es Salaam, Tanzania.
- Massamba na Wenzake (1999). Sarufi na Miundo ya Kiswahili Sanifu. Dar es Salaam: Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili.
- Mathooko, J.M na Wenzake (2007). *Academic Proposal Writing*. Nakuru, Amu Press.
- Matinde, S.R. (2012). Dafina ya Lugha, Isimu na Nadharia. Mwanza: Serengeti Educational Publishers (T) Ltd.
- Mbatiah, M. (1997). Commitment in the Swahili Novel: An Appraisal of the Works of Said Ahmed Mohamed in Massamba, D.P.B and M. M. Mulokozi (eds.) Kiswahili Vol. 60. Dar es Salaam: TUKI.
- Mbatiah, M. (1997). Mienendo Mipya Katika Uandishi wa Kezilahabi. *Mulika Nambari 24*. Dar es Salaam: Kiswahili Vol.60. Dar es Salaam: TUKI.
- Mbiti, J.S. (2011). *African Religion and Philosophy*. Kampala: East African Educational Publishers Ltd.
- Mbogo, E. (2008). *Ngoma ya Ng'wanamalundi*, Nyambari Nyangwine Publishers. Dar es Salaam.
- Mdee, J.S, K. Njogu na A. Shafi. (2011). Kamusi ya Kiswahili ya Karne ya 21, Longhorn Publishers (T) Ltd Dar es Salaam Tanzania.
- Merriam-Webster's Learner's Dictionary*. (2006). G & C. Merriam Co: Springfield Massachusetts.
- Mesaki, S. (1993). "Witchcraft and Witch-killings in Tanzania". Ph.D Dissertation, University of Minnesota.
- Method, S. (2012). *Hadithi Fupi: Nadharia Mbinu na Mifano*. Iringa: Kasenyenda Tanzania.
- Mihanjo, A. (2004). Falsafa na Usanifu wa Hoja-Kutoka Wayunani Hadi Watanzania (Waafrika). Salvatorian Institute of Philosophy and Theology. Morogoro: Tanzania.
- Mkumbwa, A. (2012). "Ujitokezaji wa Visasili na Visakale katika Riwaya ya Kiswahili ya Kimajaribio." Tasnifu ya Digrii ya Umahiri. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. (Haijchapishwa).

- Mohamed, S. A. na J. S Madumulla (1989). Mulika no: 21. TUKI. Dar es Salaam.
- Mohamed, S.A. (1995). *Kunga za Nathari ya Kiswahili: Riwaya, Tamthiliya na Hadithi fupi*. Nairobi: East African Education Publishers.
- Mohamed, S.A. (2001). *Babu Alipofufuka*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.
- Mohamed S.A (2003). Fragmentation, Orality and Magical Realism in Kezilahabi's Novel *Nagona*. Nordic Journal of African Studies 12 (1). 78-91.
- Mohamed, S.A. (2005). Signs of New Features in the Swahili Novels. Research in African Literature 36/: 92-108.
- Moh. F.C. (2002). *Ben Okri, An Introduction to his Early Fiction*. Enungu: Fourth Dimensions.
- Momanyi, J. (1991). *Matumizi ya Taswira Kama Kielelezo cha Uhalisi Katika Utenzi wa Al-Inkishafi*. Tasnifu ya M. A. Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa)
- Mpalanzi, L. (2018). 'Mpaka Kati ya Uganga na Uchawi: Uchunguzi Kutoka Riwaya za Kiethnografia za Kiswahili'. *Mulika Nambari 37*. Taasisi ya Taaluma za Kiswahili. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Uk 149
- Msokile, M. (1992). *Misingi ya Hadithi Fupi*. Dar es Salaam University Press.
- Mturo, N. J. (2018). Jiniuchawi na Ushirikina Kama Mkakati wa Uchimuzi Katika Riwaya Teule za Maundu Mwingizi. Tasnifu ya Uzamifu. Chuo Kikuu cha Nairobi.
- Mugwika, F. (2012). "Dhana ya Uchimuzi Katika Uendelezaji wa Riwaya ya Kimajaribio ya Mafamba". Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa).
- Mulokozi, M. M na Kahigi, K. K. (1979). *Kunga za Ushairi na Diwani yetu*. Dar es Salaam. Tanzania Publishing House.
- Mulokozi, M. M (1996). *Fasihi ya Kiswahili*. Chuo Kikuu Huria cha Tanzania: Dar es Salaam.
- Mulokozi, M. M (2017). *Utangulizi wa Fasihi ya Kiswahili*. Dar es Salaam. KAUTTU.
- Mung'ong'o, C.G. (1977). *Mirathi ya Hatari*. Dar es Salaam: E.A.L.B.
- Murithi, J. J. (2017). "Itikadi Katika Riwaya za Said Ahmed Mohamed". Tasnifu ya Uzamifu. Chuo Kikuu cha Kenyatta.

- Ndulute, C. (1994). *The poetry of Shaaban Robert*, Dar es salaam. Dar es Salaam. Dar es Salaam Universitr Press.
- Newton, K.M. (1997). *Twentieth Century Literary Theory* (2nd edition). New York: St. Martina Press.
- Ngugi, B. (2008). *Tathmini ya Mtaala wa Isimu Jamii Nchini Kenya*. Tasnifu ya Uzamili:Chuo Kikuu cha Kenyatta, Nairobi. (Haijachapishwa).
- Njogu, K. na Rocha. C (1999). *Ufundishaji wa Fasihi: Nadharia na Mbinu*. Nairobi, JKF.
- Njoroge, A. W. (2014). *Viongozi Kama Visababishi vya Mabadiliko Katika Riwaya za Mwenda Mbatiah: Vipanya vya Maabara Majira ya Tufani*. Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Nairobi.
- Ntarangwi, M. (2004). *Uhakiki wa Kazi za Fasihi*, Augustana College, Rock Island.
- Nyabunga, V.A. (2005). *Uhakiki wa Bina-Adamu! (2002) na Musa Leo (2004) na Wamitila, K.W.* Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa).
- Nyerere, J. K. (1968). *Uhuru na Maendeleo*. Government Printer. Dar es Salaam.
- Ohly, R. (1981). *Aggressive Prose: A case Study in Kiswahili Prose of the Seventies*. TUKI: Dar es Salaam.
- Okri, B. (1991). *The Famished Road*. London; Vintage.
- Olali, T. (2010). *Structure and Anti-Structure of a Swahili New Novel: A Stylistic Analysis of Babu Alipofufuka*.
- Onchwati, S. J. (2016). *Uhalisiajabu Unavyojitokeza Katika Ukawafi wa Miiraji na Utenzi wa Fumo Liyongo*. Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Nairobi.
- Onoda, F. (2017). *Circular motifs and Structure in Euphrase Kezilahabi's Nagona and Mzingile and an Ongoing Buddhistic Study*. Swahili Forum 23 (2016): 76-97
- Osore, M.K. (2008). "Defamiliarization in the Novels of Euphrase Kezilahabi and Said Ahmed Mohamed". PhD. Thesis: Kenyatta University. (Haijachapishwa)
- Oxford English Dictionary (2021). United Kingdom: Oxford University Press.
- Pinker, S. (1994). *The Language Instinct*. New York. William Morrow and Company, Inc.

- Ponera, A.S. (2014). "Ufutuhi Katika Nathari za Kiswahili Ulinganisho wa Nathari za Shaaban Robert na za Euphrase Kezilahabi." Tasnifu ya Shahada ya Uzamivu: Chuo Kikuu cha Dodoma.
- Ponera, A. S na S. Mkwama (2019). Utanzuaji Vibandiko kama Mkakati wa Kuzielewa Riwaya za Kifalsafa: Mfano wa Riwaya ya *Nagona*. Katika Koja la Taaluma za Insia. Dar es Salaam: Karljamer Publishers Limited.
- Ramadhani, S. K. (2013). "Usawiri wa Mwanamke Katika Taarab za Mipasho: Mfano Kutoka Nyimbo za Yusuf Mzee". Tasnifu ya M. A. Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.
- Rettova, A. (2004). "Afrophone Philisophies-Possibilities and Practice.The Reflexion of Philosophical Influences in Euphrase Kezilahabi's *Nagona* and *Mzingile*". In *Swahili Forum 11*. (Pg: 45-68).
- Rimon, K. S. (2002). Narrative Fiction Contemporary Poetics. London: Routledge and Co.Ltd.
- Rio, F. (2002). Magical Realism: Definitions: (Found in the Internet, hajachapishwa).
- Robert, S. (1946). *Kufikirika*. Nairobi: Oxford University Press.
- Robert, S. (1951). *Kusadikika*. Nairobi: Evans Brothers, Kenya Ltd.
- Robert, S. (1952). *Adili na Nduguze*. London and Basingstone: Macmillan Publishers.
- Robert, S. (1958). *Wasifu wa Siti Binti Saad*. Nairobi: East African Swahili Committee.
- Robert, S. (1960). *Maisha Yangu na Baada ya Miaka Hamsini*. Nairobi: Nelson.
- Robert, S. (1968). *Kielelezo cha Fasili*. Nairobi: Nelson.
- Robert, S. (1968). *Siku ya Watenzi Wote*. Surrey: Nelson.
- Robert, S. (1968). *Utubora Mkulima*. Nairobi: Nelson.
- Roh, F. (1925). *Magic Realism: Post –Expressionism. Magical Realism, Theory, History, Community*. Ed. Zamora and W. B. Faris. Durham: Duke University Press. Pg 15-32.
- Rushdie, S. (1981). *The Midnight's Children*. London: Bulter and Tanner Ltd.
- Safari, A.J. (1993). Uchawi Katika Riwaya za Kiswahili, Katika Fasihi Uandishi na Uchapishaji: Dar es Salaam University Press. Dar es Salaam.

- Scott, R.M. (2010). *Birth Death and Feminity: Philosophes of Embodiment*. Bloomington: Indiana University Press.
- Sean, B. (2010). *The Death and Return of the Author: Criticism and Subjective in Barthes, Foucault, aand Derrida (ed.)*. Edinburgh University Press.
- Sengo, T.S. (1975). *Shaaban Robert: Uhakiki wa Maandishi yake*. Nairobi, Longman Tanzania limited.
- Senkoro, F.E.M.K, (1987). *Fasihi na Jamii*. Dar es Salaam: Press and Publicity Centre.
- Senkoro, F.E.M.K. (1995). E. Kezilahabi: Shaaban Robert wa Pili. *Kioo cha Lugha*, 1 (1),61- 68. University of Dar es Salaam: TUKI.
- Senkoro, F.E.M.K. (1995). Sanaa, Ubunifu na Jamii, Katika Kioo cha Lugha, Juzuu 1, Na.2.
- Senkoro, F.E.M.K. (2006). Fasihi ya Kiswahili ya Majaribio: Makutano ya Fasihi Simulizi na Fasihi Andishi. Katika F.E.M.K. Senkoro & K.K. Kahigi (wahariri), *Kioo cha Lugha*, 4, 2238. University of Dar es Salaam: Tuki.
- Senkoro, F.E.M.K. (2007). Uhalisiamazingaombwe Katika Fasihi ya Kiswahili: istilahi mpya, mtindo mkongwe. Katika F.E.M.K Senkoro& K.K.
- Kahigi(wahariri), *Kioo cha Lugha*, 5, 111. University of Dar es Salaam: TUKI.
- Senkoro, F.E.M.K. (2011). *Fasihi, Mfululizo wa Lugha na Fasihi*. KAUTTU. Dar esSalaam.
- Shorter, A. (1998). *African Culture and the Christian Church*. London: G. Chapman.
- Spindler, W. (1993). *Magic Realism. A Typology*: Forum for Modern Language Studies Vol. xxxix No.1.
- Strassberg, B. (2005). *Magic, Science, Religion, Technology and Ethics in the Post-Modern World*. In Zygon Vol. 40 No. 2. Gladstone: The Joint Publication (1994) Board of Zygon.
- Strecher, M. (1999: 267). "Magical Realism and Search for Identity in the Fiction Murakami Haruki" *Journal of Japanese Studies*, Juzuu 25/2.
- Swahili Oxford Living Dictionary* (2017). United Kingdom: Oxford University Press
- Syambo, B na A Mazrui. (1992). *Uchambuzi wa Fasihi*. Nairobi: East African Educational Publishers

- The New Century Dictionary of the English Language* (1957). Appleton-Century-Standard Publishing; 6th Edition.
- Thonya, L.M. (1974). *Imani za Ushirikina na Uchawi*. East Africa Literature Bureau: Nairobi.
- Topan, F. (1970). *Aliyeonja Pepo*. Dar es Salaam: Tanzania Publishing House Ltd.
- TUKI (2000). *English-Swahili Dictionary*. Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.
- TUKI (1981). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam: Oxford University Press.
- United Bible Societies. (1952). Maandiko Matakatiifu ya Mungu Yaitwayo Biblia.
- Vutagwa, F.L. (2013). “Sifa za Kiuhalisiajabu na Umuhimu Wake Katika Utenzi wa Mwana Fatuma”. *Tasnifu ya Uzamili*: Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa).
- Wafula, R.M. (1989). “The Use of Allegory in Shaaban Robert’s Prose Works”. M.A. Thesis University of Nairobi.
- Walibora, K.W. (2010). Uhalisiamazingaombwe. Mshabaha kati ya *Dunia Yao* na the *Tin Drum*. *Swahili Forum* 17: 143-157.
- Wamitila, K.W. (1991). *Nagona na Mzingile Kezilahabi’s Metaphysics*. Katika Jarida la *Kiswahili Na. 54*. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam: TUKI.
- Wamitila, K.W. (1991). *Nagona na Mzingile Kezilahabi’s Metaphysics*. Katika Jarida la *Kiswahili Na. 54*. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam: TUKI.
- Wamitila, K.W. (1997). Contemptus Mundi and Carpe Diem Motifs in Kezilahabi’s Works. *Kiswahili: Juzuu Na. 60*. Dar es Salaam: TUKI.
- Wamitila, K.W. (2002). *Uhakiki wa Fasihi, Misingi na Vipengele Vyake*. Nairobi: Phoenix Publishers.
- Wamitila, K.W. (2003). *Bina-Adamu!* Nairobi: Phoenix Publishers.
- Wamitila, K.W. (2003). *Kamusi ya Fasihi Istilahi na Nadharia*. Nairobi: Focus Book.
- Wamitila, K.W. (2004). *Kichocheo cha Fasihi Simulizi na Fasihi Andishi*. English Press Nairobi.

- Wanjiru, M.J. (2013). “Uhalisia na Uhalisiajabu Katika Riwaya Mpya. *Babu Alipofufuka* (Said Ahamed Mohamed) na *Watu wa Gehenna* (Tom Olali)”. Tasnifu ya Uzamili: Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa).
- Warren, A. (1949). *Theory of Literature*, Harmondsworth: Penguin Books Limited.
- Waruguru, K.J. (2013). Usawiri wa Ndoa Katika Riwaya ya *Unaitwa Nani?* Tasnifu ya Uzamili: Chuo Kikuu cha Nairobi.
- Webster’s Revised Unabridged Dictionary. (2003). Barnes & Noble: Random House.
- White, E. G. (1955). *S. D. A Bible Commentary Vol. 4*. Ellen G. White Estate, Inc.
- WiLDAF Tanzania. (2011). Ulinzi wa Wanawake Dhidi ya Ukatili wa Kijinsia Tanzania. WiLDAF. Mikocheni: Dar es Salaam.
- Williams. R. (1995). *The Postmodern Novel in Latin America: Politics, Culture, and the Crisis of Truth*. New York: St. Martin’s.
- Wimsatt, W. and M.C. Beardsley. (1946). *The Intentional Fallacy*. *Sewanee Review*, Vol.54 (pg, 468-488).
- Zamora, P.L. and B.W, Faris (1995:191-208). *Magical Realism Theory, History Community*. London: Duke University Press.

VIAMBATISHO

KIAMBATISHO A: Mwongozo wa Usaili, Mjadala na Ushuhudiaji kwa

Wenyeji wa Tanga/Ukerewe

Utafiti huu unahusu matumizi ya mbinu ya uchawi na mazingaombwe katika riwaya za Shaaban Robert na za Euphrase Kezilahabi. Lengo la utafiti ni kuchunguza athari ya mazingira asilia ya watunzi, Shaaban Robert na Euphrase Kezilahabi katika matumizi ya mbinu ya uchawi na mazingaombwe katika riwaya zao teule.

- i. Unaombwa kutaja jina na umri wako
- ii. Je, amewahi kutokea mtu anayefanya mambo ya ajabuajabu yaani yasiyoweza kufanywa na watu wa kawaida katika jamii yenu? Kama jibu ni ndiyo, unaweza kuelezea baadhi ya mambo aliyowahi kuyafanya?
- iii. Elezea visa vya kichawi na vya kimazingaombwe vilivyowahi kutokea katika jamii yenu.
- iv. Ni matukio gani ya ajabuajabu yaliyowahi kutokea au yanayotokea katika jamii yenu unayoweza kueleza?
- v. Matukio hayo yanatendwa na watu gani? Na unayahusisha na nini?
- vi. Kuna mawasiliano ya aina yoyote kati ya walio hai na wafu katika jamii yenu?
- vii. Unaweza kuelezea matukio ya watu walio na uwezo wa kujigeuza sura zao na kuwa kitu kingine au kumbadili mtu mwingine sura na kumfanya kuwa kitu kingine katika jamii yenu?
- viii. Unaweza kuelezea visa vyovyote vya uhusiano kati ya majini na watu katika jamii yenu?

- ix. Je, katika jamii yenu kumewahi kuwepo watu wenye uwezo wa kuingia popote, na wenye uwezo wa kufika mahali popote kwa muda mfupi hata kama ni mbali kiasi gani?
- x. Je, wamewahi kutokea katika jamii yenu watu wenye uwezo wa kuwasiliana na viumbe wengine bila kizuizi cha tofauti za namna za mawasiliano miongoni mwao?
- xi. Unaweza kuelezea visa vyovyote vya uhusiano kati ya watu waliofikiriwa kuwa wamekufa na watu walio hai katika jamii yenu?
- xii. Unaweza kuelezea kutokea kwa matukio yanayohusiana na miji, watu, au vitu vinavyojitokeza na kupotea ghafla katika jamii yenu?
- xiii. Unaweza kusimulia matukio yanayotokea katika jamii yenu yanayotendwa na viumbe/watu wasioonekana? Na kwa maoni yako unafikiri matukio hayo yanafanywa na viumbe/watu wa namna gani?
- xiv. Unaweza kuelezea kwa ufupi unavyomfahamu Shaaban Robert/Euphrase Kezilahabi?
- xv. Unaweza kuelezea kuwepo au kutokwepo kwa uhusiano kati ya Shaaban Robert/Euphrase Kezilahabi na utamaduni wa jamii yenu?
- xvi. Kuna visa vyovyote vya matumizi ya uchawi na mazingaombwe unavyovifahamu vilivyowahi kufanywa au vilivyowahi kuhusishwa na Shaaban Robert/Euphrase Kezilahabi katika jamii yenu?
- xvii. Kuna visa vyovyote zaidi vya asili ya jamii yenu unavyoweza kusimulia?

KIAMBATISHO B: Vibali vya kufanya utafiti

KENYATTA UNIVERSITY
GRADUATE SCHOOL

E-mail: dean-graduate@ku.ac.ke

Website: www.ku.ac.ke

OUR REF: I84/32256/15

P.O. Box 43844, 00100
NAIROBI, KENYA
Tel. 8710901 Ext. 57530

Date: 5th February, 2018

The Director General
National Commission for Science,
Technology & Innovation
P.O. Box 30623-00100,
NAIROBI

Dear Sir/Madam,


RE: RESEARCH AUTHORIZATION FOR MAGGATI C. NYANDURU REG.NO. C82/27820/13

I write to introduce **Nyanduru** who is a Postgraduate Student of this University. The student is registered for Ph.D. Degree programme in the Department of Chemistry in the School of Pure & Applied Sciences.

Nyanduru intends to conduct research for a Ph.D. thesis entitled, "Mada: Matumizi ya Uchawi na Mazingaombwe Katika Riwaya za Shaaban Robert na za Euphrase Kezilahabi"

Any assistance given will be highly appreciated.

Yours faithfully,


MRS. LUCY N. MBAABU
FOR: DEAN, GRADUATE SCHOOL

AM/cao

UNIVERSITY OF DAR-ES-SALAAM
OFFICE OF THE VICE CHANCELLOR
P. O. BOX 35091 ♦ DAR ES SALAAM ♦ TANZANIA

General: +255 22 2410500-8 ext. 2001
 Direct: +255 22 2410700
 Telefax: +255 22 2410078



Telegraphic Address: UNIVERSITY OF DAR ES SALAAM
 E-mail: vc@admin.udsm.ac.tz
 Website address: www.udsm.ac.tz

Ref. No: AB3/12(B)

Date: 23rd July 2018

Regional Administrative Secretary
Tanga Region

RE: REQUEST FOR RESEARCH CLEARANCE

The purpose of this letter is to introduce to you **Mr. Charles Nyanduru Maggati** who is a bonafide staff member of the University of Dar es Salaam and a PhD Student at Kenyatta University. Mr. Nyanduru is required to conduct research as part of his PhD studies.

In accordance with government circular letter Ref. No. MPEC/R/10/1 dated 4th July 1980, the Vice Chancellor of the University of Dar es Salaam is empowered to issue research clearances to staff members and students of the University of Dar es Salaam on behalf of the government and the Tanzania Commission for Science and Technology (COSTECH). I am pleased to inform you that I have granted a research clearance to **Mr. Maggati**.


I therefore, kindly request you to grant him any help that may enable him achieve his research objectives. Specifically we request your permission for him to meet and talk to the leaders and other relevant stakeholders in your region in connection with his research.

The title of the research is '**Matumizi ya Uchawi na Mazingaombwe Katika Riwaya za Shaaban Robert na za Euphrase Kezilahabi**'.

The period of the research is from **July 2018 to April 2019** and the research will cover **Tanga Region**.

Should there be any restriction, you are kindly requested to advise us accordingly. In case you may require further information, please do not hesitate to contact us through the Directorate of Research and Publication, Tel. +255 22 2410500-8 Ext. 2084 or 2410727 and E-mail: research@udsm.ac.tz.

Yours sincerely,


 VICE CHANCELLOR
 UNIVERSITY OF DAR ES SALAAM
 P.O. Box 35091
 DAR ES SALAAM

Prof. William A. L. Anangisye
VICE CHANCELLOR

UNIVERSITY OF DAR-ES-SALAAM
OFFICE OF THE VICE CHANCELLOR
P. O. BOX 35091 ♦ DAR ES SALAAM ♦ TANZANIA

General: +255 22 2410500-8 ext. 2001
 Direct: +255 22 2410700
 Telefax: +255 22 2410078



Telegraphic Address: UNIVERSITY OF DAR ES SALAAM
 E-mail: vc@admin.udsm.ac.tz
 Website address: www.udsm.ac.tz

Ref. No: AB3/12(B)

Date: 23rd July 2018

District Executive Director
 Ukerewe District Council
Mwanza Region

RE: REQUEST FOR RESEARCH CLEARANCE

The purpose of this letter is to introduce to you **Mr. Charles Nyanduru Maggati** who is a bonafide staff member of the University of Dar es Salaam and a PhD Student at Kenyatta University. Mr. Nyanduru is required to conduct research as part of his PhD studies.

In accordance with government circular letter Ref. No. MPEC/R/10/1 dated 4th July 1980, the Vice Chancellor of the University of Dar es Salaam is empowered to issue research clearances to staff members and students of the University of Dar es Salaam on behalf of the government and the Tanzania Commission for Science and Technology (COSTECH). I am pleased to inform you that I have granted a research clearance to **Mr. Maggati**.


I therefore, kindly request you to grant him any help that may enable him achieve his research objectives. Specifically we request your permission for him to meet and talk to the leaders and other relevant stakeholders in your district in connection with his research.

The title of the research is '**Matumizi ya Uchawi na Mazingaombwe Katika Riwaya za Shaaban Robert na za Euphrase Kezilahabi**'.

The period of the research is from **July 2018 to April 2019** and the research will cover **Ukerewe District**.

Should there be any restriction, you are kindly requested to advise us accordingly. In case you may require further information, please do not hesitate to contact us through the Directorate of Research and Publication, Tel. +255 22 2410500-8 Ext. 2084 or 2410727 and E-mail: research@udsm.ac.tz.

Yours sincerely,


 VICE CHANCELLOR
 UNIVERSITY OF DAR-ES-SALAAM
 P.O. Box 35091
 DAR-ES-SALAAM

Prof. William A. L. Anangisye
VICE CHANCELLOR

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
 TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

MKOA WA MWANZA:
 Anuani ya Simu: "ADMIN"
 Simu Nambari: 028-2515056
 Tovuti: www.mwanza.go.tz
 Barua Pepe: das.ukerewe@mwanza.go.tz



OFISI YA MKUU WA WILAYA,
 S.L.P.02,
 NANSIO/UKEREWE.

Unapojibu Tafadhali Taja:

Kumb. Na.AB.297/367/03/9

15/3/2019.

Mkurugenzi Mtendaji,
 Halmashauri ya Wilaya,
 S.L.P. 41,
 UKEREWE

YAH:UTAMBULISHO WA BW.CHARLES NYANDURU MAGATI.

Tafadhali rejea mada tajwa hapo juu.

Namtambulisha kwako Bw. Charles Nyanduru Magati kutoka chuo kikuu cha Dares salaam .Anakusudia kufanya utafiti kuhusu "*Matumizi ya uchawi na Mazingaombwe katika riwaya na Shaban Robbert na za Euphrase Kezilahabi*".

Muda wa utafiti ni Julai hadi April 2019 .Apewe ushirikiano unaohitajika.

Asante kwa ushirikiano.

Josephat K. Mazula
 Kny: KATIBU TAWALA WA WILAYA
 UKEREWE
 K.N.Y. KATIBU TAWALA CINDI
 UKEREWE

Nakala: Mkuu wa wilaya
 UKEREWE – Aione ndani ya jalada

"Bw.Charles Nyanduru Magati"

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
PRESIDENT'S OFFICE
REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT

REGION: MWANZA

Address : "REGCOM"
 Tel. No. 028 – 2500690-2500686
 Fax:028-2501057/2541242
 E-Mail rasmwanza @pmoralg.go.tz.
 In reply please:



REGIONAL COMMISSIONER'S OFFICE,
 P.O. BOX 119,
 MWANZA

Ref. No. DA.277/333/01/61

11 March, 2019

District Administrative Secretary,
 Ukerewe District,

RE: RESEARCH PERMIT FOR CHARLES NYANDURU MAGGATI

Refer to the above title.

The above mentioned has been allowed to conduct research on the "Matumizi ya Uchawi na Mazingaombwe katika Riwaya za Shaaban Robert na za Euphrase Kezilahabi". The period of his research is from July to April, 2019.

You're sincerely

W. James
 W. James

For REGIONAL ADMINISTRATIVE SECRETARY
 MWANZA

K. N. Y. KATIBU TAWALA (M)
 MKOA WA MWANZA (3)

C.C. Vice Chancellor
 UNIVERSITY OF DAR ES SALAAM

To Mr Charles Nyanduru Maggati,
 Student of Dar es Salaam University,